

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Thelathini na Sita – Tarehe 27 Mei, 2019

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawaomba tukae. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mkutano wetu wa 15, leo ni Kikao cha 36.

Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA NISHATI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

NAIBU WAZIRI WA MADINI:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE - K.n.y. MWENYEKITI WA
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI)**

Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini Kuhusu utekelezaji na Majukumu ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**MHE. TUNZA I. MALAPO - K.n.y. MSEMADI MKUU WA
KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA
MADINI:**

Taarifa ya Msemadi Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni juu ya Wizara ya Madini kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Tunza Malapo, tunakushukuru.

Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Tunaanza na TAMISEMI, swali la kwanza litaulizwa na Mheshimiwa Azza Hilal, Mbunge wa Viti Maalum - Shinyanga.

Na. 297

Hitaji la Mabweni Shule za Sekondari-Shinyanga

MHE. AZZA H. HAMAD aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga Mabweni katika shule za sekondari zilizoanzishwa Kitarafa ili kuwasaidia watoto wa kike waweze kupata elimu iliyo bora Mkoani Shinyanga?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Selemiani Saidi Jafo, tafadhalii.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Azza Hilal Hamad, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa shule za sekondari kuwa na mabweni ili kuboresha elimu. Kwa sasa mpango wa Serikali ni kuziboresha shule za sekondari zilizopo ambapo kipaumbele ni katika ujenzi wa miundombinu muhimu wa vyumba vya madarasa, vyoo mabweni na maabara ili kuboresha mazingira ya kufundishi na kujifunzia. Ukarabati wa shule hizo unahusisha miundombinu ya mabweni hasa kwa watoto wa kike ili kuweza kupata elimu iliyobora. Hadi sasa, shule za sekondari 1241 zimejengewa mabweni kati ya shule za sekondari 3634 zinazotumia ruzuku ya Serikali Kuu, mapato ya ndani ya Halmashauri na mchango wa jamii. Serikali itaendelea kujenga mabweni na kushirikisha wadau mbalimbali wa maendeleo kwa kadiri bajeti itakavyoruhusu.

SPIKA: Mheshimiwa Azza Hillal swali la nyongeza tafadhalii.

MHE. AZZA H. HAMAD: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza maswali ya nyongeza. Awali ya yote niipongeze sana Serikali kwa kazi kubwa ambayo inaifanya katika kuhakikisha inaboresha miundombinu katika shule zetu. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; Je, Serikali iko tayari sasa kuhakikisha inajenga mabweni katika shule zetu zilizoanzishwa kimkakati zaidi katika shule ya sekondari Samuye, Kizumbi, Isagenhe na Ukenyenge zilizopo katika

Mkoa wa Shinyanga kwa sababu Wanafunzi wamekuwa wakitembea umbali mrefu na hivyo kukumbana na vishawishi vingi barabarani na kupelekea kupanga mitaani?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Je, Serikali hamuoni sasa ni wakati muafaka wa kuweza kufikiria kutokuwapangia shule zilizoko mbali wanafunzi hawa kwa kila Kata sasa hivi ina shule?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Jafo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA

NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nikiri, Mheshimiwa Azza takribani wiki mbili au tatu zilizopita alikuwa akinijulisha suala zima la changamoto ya miundombinu ya elimu katika Mkoa ule wa Shinyanga na nilimuhakikisha kwamba Serikali tutafanya kila liwezekanalo, lile linalowezekana tutaenda kulifanyia kazi alichanganye pamoja na ajenda hiyo ya elimu pamoja na ajenda ya afya.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo naomba niseme kwamba Serikali tutaangalia kila kinachowezekana katika maeneo uliyoyaainisha lile litakalowezekana kwa sasa tutaweza kulifanyia. Lakini ni azma ya Serikali kuhakikisha tunapambana miundombinu inaimarika kama tulivyofanya pale sekondari ya Tinde ambapo Mbunge tumeenda wote pamoja pale kwa ajili ya kuona eneo gani lazima tufanye hilo.

Mheshimiwa Spika, suala la kutowapangia mbali kwa vile kila Kata sasa ina shule, jambo hili ndiyo kielelezo chetu ni kwamba kama katika Kata hasa zile zetu ambapo kama kuna vijana wamefaulu katika eneo lile ni vyema sasa watoto wakapangiwa kwa karibu zaidi kuepusha usumbufu huo mabao Mheshimiwa Mbunge ulizungumza. Kwa hiyo,

tumelichukua Serikali na tutalitolea maelekezo katika maeneo mbalimbali.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Waziri kivuli wa Elimu.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, pamoja na juhudhi za Serikali kuhakikisha kwamba wanajenga mabweni, utakubaliana nami kwamba baadhi ya mabweni hayo yamekuwa yakiungua mara kwa mara na hivi karibuni shule ya Ashira mabweni yake mawili ya wasichana yameungua.

Je, Serikali mna utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba kunakuwa na ulinzi katika shule hizo ili hii rasilimali kubwa ambayo imeshatumika ya fedha kujenga mabweni hayo iweze kulindwa?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Pole sana kwa sekondari ya Ashira. Majibu Mheshimiwa Waziri wa Nchi, tafadhalii.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Dada yangu Susan.

Mheshimiwa Spika, ni kweli na niwape pole Wananchi wote wa Tanzania kwa sababu watoto wale, juzi nilikuwepo Ashira ile shule wkeli imeungua lakini ukija kuangalia taarifa ya awali inaonyesha kwamba ni hujuma tu kwa sababu yale mabweni mawili hayaungani na siyo kwamba kulikuwa na *short* ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni kweli inawezekana maeneo mengine kuna hujuma na nawaomba niwaeleze Serikali juzi nilisha-*deploy* timu yangu ya Mainjinia iko pale tokea jana inafanyakazi na leo hii haraka iwezekanavyo ndani ya wiki mbili, tatu tuanze ukarabati wa yale majengo kwa sababu siyo muda mrefu vijana wa *form five* wengine tutawaingiza katika maeneo yale. Kwa hiyo, tutafanya

ukarabati wa shule ile yote kwa ujumla wake kuhakikisha inarudi Ashira katika hali yake ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo ni maelekezo yetu sasa kipaumbele suala zima la walinzi na hasa kuangalia usalama wa shule zetu nini kifanyike kwa sababu tunatumia fedha nydingi sana, haiwezekani watu wenye nia mbaya wakahujumu juhudhi hii kubwa ya Serikali na Wananchi wake kwa ujumla.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda, naomba tuendelee na Viwanda na Biashara swali la Mheshimiwa Maria Ndila Kangoye. Mheshimiwa Maria

Na. 298

Sekta Binafsi Kuanzisha Viwanda Vikubwa na vya Katil

MHE. MARIA N. KANGOYE aliuliza:-

Serikali iliahidi kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha viwanda vikubwa na vya katil na kuweka utaratibu wa kuvilinda dhidi ya viwanda vya nje.

(a) Je, Serikali imefikia wapi katika zma hii ambayo ni mwelekeo wa kufikia uchumi wa katil na utoaji ajira hasa kwa vijana?

(b) Je, Serikali imeweka mkakati upi ili kuweza kujenga mazingira rafiki yatakayowezesha kupunguza gharama za uwekezaji na uendeshaji wa viwanda?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ndila

Kangoye Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jukumu la Serikali kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha viwanda vikubwa na vya katи ni la msingi na endelevu. Serikali imeendelea kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika viwanda kuitia kituo cha uwekezaji Tanzania yaani *TIC* na mamlaka ya kuendeleza maeneo huru ya uzalishaji kwa ajili ya kuuza nje yaani *EPZA*. Uhamashajihу unaambatana na kutoa vivutio mbalimbali ikiwemo misamaha ya kodi katika mitambo na mshire zinazotumika kwneye uzalishaji. Aidha, Shirika la kuhudumia viwanda vidogo vidogo (*SIDO*) limekuwa likihamasisha na kusaidia uanzishwaji wa viwanda vidogo na vya katи ambavyo ni msingi wa maendeleo ya viwanda vikubwa kuitia mafunzo na uvezeshaji wa kiufundi na mitaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na niliyoeleza katika swalı namba 4404 liliojibиwa tarehe 07 Mei, 2019, ili kulinda viwanda vya ndani dhidi ya ushidani usio wa haki, Serikali kuitia Tume ya Ushindani (*FCC*) na Shirika la viwango Tanzania yaani *TBS* na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) vimikuwa vikidhibiti uingizaji wa bidhaa hafifu, bandia na zinazoingia kwa njia zisizo rasmi bila kulipiwa kodi. Vilevile Serikali imikuwa ikitoa misamaha ya kodi kwa baadhi ya bidhaa za ndani na kutozwa zaidi baadhi ya bidhaa zinazoingizwa kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa mazingira bora ya biashara na uwekezaji ni kichocheo muhimu kwa maendeleo ya viwanda Nchini. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali imeendelea kutenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa viwanda na biashara na kuyawekea miundombinu muhimu na kuanzisha kongano za viwanda yaani *clusters* ili kuwezesha wanaviwanda kupata huduma na kuendeleza viwanda vyao kwa urahisi.

SPIKA: Mheshimiwa Maria nimekuona.

MHE. MARIA N. KANGOYE: Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya kutoka Wizarani

kwanza nianze kwa kumkumbusha kwamba naitwa Maria Ndila Kangoye siyo kama hivyo alivyonitaja. Nitauliza swali moja la nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni katika ya Nchi zinazoongoza katika ufugaji Barani Afrika hususani ufugaji wa Ng'ombe, lakini licha ya hivyo tumekuwa nyuma sana katika biashara ya mazao ya mifugo. Ningependa kujua ni nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba inakabiliana na upungufu mkubwa wa viwanda vya kuchakata nyama na maziwa nchini?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Mifugo tafadhali. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la nyongeza pamoja pia na kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na mkakati mkubwa na mzuri sana wa kuhakikisha tunapata viwanda vya uchakataji wa mifugo Nchini. Kwa kuanzia kwa haraka haraka hivi sasa, tunavyo viwanda takribani vitatu tunavyovijenga katika Nchi. Kiko kiwanda pale Mkoani Arusha, Wilayani Longido, tunacho kiwanda pale Mkoani Pwani katika Wilaya ya Kibaha, tuna kiwanda kikubwa ambacho tunakitarajja tulichoingia mkataba na Taifa la Misri kitakachojengwa katika Ranch yetu ya Ruvu pale Kibaha pia. Sambamba na kuchakata nyama, tunavyo viwanda ambavyo vinachakata mazao mengine ya mifugo kama vile maziwa.

Mheshimiwa Soika, Serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi katika kuwekeza kwenye viwanda na mazingira ya uwekezaji katika viwanda hivi vya uchakataji wa mifugo yako mazuri na tunawakaribisha kwa ajili ya kufanya kazi hii.

SPIKA: Tunaendelea na Maliasili na Utalii, swali linaulizwa na Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, Mbunge wa Chambani.

Na. 299

Utalii wa Bahari Kupitia *Diving*

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN aliuliza:-

Utalii wa Baharini kupitia “*diving*” unakua kwa kasi sana Duniani kote hali ambayo inaongeza soko la ajira katika sekta hiyo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na changamoto za soko la ajira kwa vijana wa Kitanzania?

(b) Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha usalama wa watalii wanapokuwa chini ya maji hasa kutokana na uvuvi haramu wa kutumia mabomu?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, Mbunge wa Chambani lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utalii wa kuzamia (*diving*) ni moja kati ya shughuli za kitalii ambazo zinafanyika hapa Nchini katika bahari ya Hindi kwenye meeneo ya hifadhi ya bahari ya maeneo tengefu. Idadi ya watalii wanaotembelea maeneo hayo imekuwa ikiongezeka ambapo hadi hivi sasa idadi imefikia watalii 46000. Aidha, kutokana na idadi hiyo ya watalii na uwekezaji unaofanyika katika maeneo hayo, ajira nyingi zinaendelea kuzalishwa na kipato kuongezeka kwa Wananchi na Taifa kwa ujumla. Vilevile Serikali kupitia

uongozi wa maeneo hayo imekuwa ukihamasisha vijana kuijunga na mafunzo ya uzamiaji na kuongoza watalii ili wawzeze kunufaika na ajira katika sekta husika.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa mafunzo ya utalii wa kuzamia yanatolewa katika vituo vya uzamiaji vya *diving centres* vinavyotambuliwa Kisheria katika maeneo ya hifadhi ya bahari ya maeneo tengefu ya Mafia vituo vinne, Dar es salaam vituo viwili na Tanga vituo viwili. Mafunzo hayo yanatolewa kwa vijana wanaoishi katika maeneo jirani na hifadhi ya bahari ya maeneo tengefu ili kuwajengea uwezo utakaowawezesha kupata ajira katika sekta husika.

Mheshimiwa Spika, utalii wa kuzamia ni taaluma ambayo hupatikana baada ya mtu kupata mfunzo ya kuzamia ambapo huambatana na mafunzo ya usalama na uokoaji. Aidha, kwa mujibu wa taratibu za Kimataifa, wazamiaji hupaswa kuwa na Bima ya Maisha ambayo husaidia kutoa fidia na matibabu endapo ataumia na kupata ajali wakati za uzamiaji.

Vilevile wazamiaji huhimizwa kutumia vifaa vyenye ubora ili kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza wakati wa uzamiaji. Vifaa hivyo ni pamoja na Mitungi ya gesi, *Boyance control device, Regulator, Mask, Fins, Wet or Dry suit, Dive computer* na Snorkel na vifaa vingine muhimu.

Mheshimiwa Spika, maeneo yanayotumika kwa ajili ya shughuli za uzamiaji katika hifadhi yameainishwa na kuhakikishwa kuwa uvuvi haramu na vilipuzi havipo. Hata hivyo Serikali imeendelea na jitihada za kudhibiti uvuvi haramu ikiwemo matumizi ya vilipuzi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Hadi sasa uvuvi huo umedhibitiwa kwa kiwango kikubwa katika maeneo yote ya bahari ya Hindi na hivyo kufanya maeneo hayo kuwa salama kwa watalii wanaozamia.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Mbunge wa Chambani swali la nyongeza.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawli ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, ametaja vituo vya Mafia, Dar es Salaam na Tanga ambavyo vinatoa mafunzo ya elimu hii; nilikuwa nataka kujua vinatoa mafunzo kwa kiwango gani? Wanatoka Ma-diving instructor, diver masters au wanafunzi wa kiwango gani wanaotoka katika vituo hivyo vya kufundishia?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; siyo tu kwamba ile mitetemo wanapolipua wale wavuvi inawatisha na inawasumbua wale Ma-divers wanapokuwa chini ya maji lakini pia eneo ambalo limepigwa lile bomu huwa linaathirika sana na kupoteza ule uhalisia wake kiasi kwamba mpaka rangi ya eneo lile huwa inabadilika. Je, Serikali ina mpango wowote wa kufanya utafiti kuona ule uoto wa asili unarudi pale yale Matumbawe yaliyoharibiwa kwa muda wa miaka mingapi?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kimsingi kwa mujibu wa swali lake la kwanza, mpaka sasa hatuna vyuo ambavyo vinatoa vyeti maalum lakini tuna vituo ambavyo vinatoa mafunzo kwa ajili ya kusindikiza watalii wanaokuja kwa ajili ya uzamiaji. Katika vyuo vyetu vyote vya Mbegani na wapi hatuna *certificate* maalum kwa ajili ya divers au *snorkel* au nini ambayo inatolewa katika maeneo hayo. Wanapata uzoefu kutokana na wale ambao wamekuwa waki-practice kwa muda mrefu kwahiyio vituo hivyo ndiyo nimevitaja katika jibu langu la msingi.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili amesema kuna utafiti gani unafanyika kujua athari zinzaotokana na ulipuzi; ni kweli kwamba milipuko inapolipuka ndani ya maji uharibu kabisa maumbile ya Dunia ndani maji na hasa Matumbawe ambayo ndiyo kivutio kikubwa cha wazamiaji na maeneo yote

baharini na kimsingi maeneo haya ambayo yamekuwa ukifanyika uzamiaji yamekuwa ni maeneo yanayolindwa na kwa mfano, ukienda kule Mafia kuna kikosi maalum ambacho kinalinda maeneo hayo na kina *patrol* maalum. Kwa hiyo, uzoefu wa maeneo hayo kushambuliwa na wazamiaji haupo, kwa hiyo nimuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika maeneo ambapo tunapeleka watalii kwa ajili ya shughuli hii ni maeneo ambayo yanalindwa na kusimamiwa vizuri na hakuna uwezekano wa matumizi ya mabomu.

SPIKA: Naomba tuendelee na Wizara ya Madini kuna nyongeza ya majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba tena ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kuongezea kujibu swali la Mheshimiwa la Mheshimiwa Yussuf kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza vilevile Mvuu mwenzangu Mheshimiwa Kanyasu kwa majibu yake yale ya awali. Lakini pia nieleze tu kuwa katika chuo Kikuu cha Dar es Saalam katika kozi ya *Aquatic Science* moja ya jambo la msingi kabisa kwenye kozi ile watu wanafundishwa kitu kinachoitwa *swimming and snorkeling*.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, *swimming and snorkeling* mtu anayekwenda kupata shahada ya *swimming* mathalani mimi mwenyewe hapa ni lazima unafundishwa namna ya kuweza kuogelea na kuweza kuingia kwenye maji kwa muda mrefu na ndipo upate *degree* yako. Lakini kama haitoshi alivyosema Mheshimiwa Kanyasu kuwa Ndegani wanao utaratibu ambao wanashirikiana hasa na Mamlaka ya Bahari Kuu ambapo wanafundishwa pale kwa muda mfupi nakupewa udhoefu. Wataalam wetu ambao wanakwenda kuwa *observer's* watazamaji katika meli hawa pia wanafundishwa namna hata ya ku-*dive*.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili la Matumbawe ni *conservation*, Matumbawe yanachukua si pungufu ya miaka

50 hadi 100 yale ambayo yamevunjwa na mabomu, kwa hivyo kitu pekee ambacho sisi wataalam wa Sayansi ya Majini tunachokifanya ni kuhakikisha kuwa maeneo yaliyoharibiwa namna hiyo yanakwenda kuhifadhiwa tumefanya jitihada kubwa kwa kupitia mradi wetu mkubwa unaitwa *sea offish* ukanda wa Pwani ambapo kuanzia Tanga kule MOA mpaka Mtwara maeneo ya Mtwara mwishoni kule tumekuwa na huo mradi ambao tunadhibiti na kuyalinda maeneo yetu ya miamba na tumeonesha mafanikio makubwa sana katika Wilaya ya Kilwa, hivi sasa hata mazao yanayopatikana katika miamba ile kwa maana ya Matumbawe yameongezeka kwa kiasi kikubwa sana.

SPIKA: Nakushukuru sana tunahamia Wizara ya Madini swali la Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza.

Na. 300

Fidia kwa Wananchi wa Mtaa wa Mgusu Kupisha Mgodi

MHE. UPENDO F. PENEZA aliuliza:-

Wananchi wa Mtaa wa Mgusu wanaoishi ndani ya mipaka ya Mgodi wa *Geita Gold Mine* wanaathirika sana na uchafuzi wa mazingira unaotokana na takazinazomwagwa katika maeneo karibu na wananchi.

Je, ni lini Serikali itatoa agizo kwa *Geita Gold Mine* kulipa wananchi fidia ili watoke katika eneo liliomililikishwa Mgodi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Madini Mheshimiwa Nyongo tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini naomba nijibu swali la Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nijibu kama swali liliyoulizwa na kama ni marekebisho hayo anayoyasema Mheshimiwa Mbunge basi tunaomba arudishe swali alete jingine jipya tutamjibu kwa lile eneo lakini hapa tumemjibu kadri liliyoulizwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mtaa wa Mgusu uko kilomita 4.5 kutoka eneo la uchimbaji la Nyamulilima *Star and Comment* la *GGM* ambapo kwa sasa uchimbaji unaendeshwa kwa niia ya chini kwa chini yaani *Underground Mining Operations*. Mawe ya Dhahabu yanayozalishwa katika eneo hilo hupelekwa kwenye eneo maalum la uchenjuaji yaani *Processing plant* ambalo lipo umbali wa kilomita 19 kutoka Mtaa wa Mgusu. Kwa umbali huo ni wazi kuwa ni vigumu kwa taka ngumu kufika katika Mtaa huo. Hata hivyo ukingo wa miamba isyo na madini yaani *Waste Rocks* umewekwa ili kuzuia miamba hiyo kutoka nje ya eneo la uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, Kifungu cha 96(1) na 97(1)(a) na (b) vinaeleza kuwa, fidia inapaswa kulipwa kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi katika hatua ambapo muwekezaji anataka kuanza kuchimba madini baada ya kushauriana na Mamlaka ya Serikali za Mtaa husika na kujiridisha juu ya madhara yanayoweza kusababishwa na uchimbaji huo.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mtaa wa Mgusu wengi wao wanajishughulisha na uchimbaji mdogo wa madini. Hata hivyo tathimini ya mazingira iliyofanywa na mgodi wa *GGM* haionyeshi uwepo wa madhara yanayohitaji kuhamishwa kwa wananchi wa Kitongoji hicho. Aidha, Wizara kupitia Ofisi ya Madini Mkoa wa Geita itaendelea kusimamia na kukagua eneo hilo.

SPIKA: Mheshimiwa Upendo Peneza nimekuona swali la nyongeza.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa bahati mbaya swali langu lilinukuliwa tofauti na nilivyowasilisha. Lakini kwa faida ya wananchi wa Nyakabale

ninaomba kujua kwamba sehemu ya Nyakabale ni eneo limekuwa likipata shida kubwa kutokana na mgodi wa Geita *Gold Mine* kwa maana ya kimatatizo ya kimazingira lakini hata wananchi wenyewe kuzuia kufanya shughuli mbalimbali za kimaendeleo ya kwamba itabidi wapishe shughuli za mgodi.

Mheshimiwa Spika, Iakini ni miaka sasa hawawaondoi katika eneo hilo. Sasa ninaomba kujua tuliahidiwa na Mheshimiwa Waziri Kalemani kwamba wale wananchi wangeondolewa Iakini mpaka leo hawajaondolewa. Je, Serikali inatupa leo kauli gani wananchi wa Geita hasa wananchi wa Nyakabale kuhusu kulipwa fidia ama kuruhusiwa kwamba waendelee na shughuli zao za kimaendeleo katika eneo hilo la Nyakabale?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili linahusu katika upande huo wa ulipwajji fidia, sheria yetu imeruhusu haya makampuni kuweza kutumia wathamini binafsi kwenda kuhesabu mali za wananchi na hatimaye kuweza kulipwa na hili limeleta malalamiko kwa maana ya wananchi wengine kuona kwamba wanapunjwa na kampuni hizo kutetea maslahi zaidi za makampuni hayo ya uwekezaji. Sasa Je, Serikali leo inatoa kauli gani kuhakikisha ya kwamba maslahi ya wananchi katika maeneo husika yanalindwa ahsante? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili Mheshimiwa Naibu Waziri Madini Mheshimiwa Nyongo tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba maeneo ya Nyakabale yako ndani ya leseni ya uchimbaji yaani leseni ambayo ni *special mining license* ya mgodi huu wa *GGM* ndani ya zile kilomita 290 za mgodi huo.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba sheria inasema kwamba ni lazima mtu ambaye anataka kuwekeza kuchimba maeneo yale watu wanaoishi maeneo yale ni lazima awalipe fidia waondoke ili aweze kufanya *operation* zake.

Mheshimiwa Spika, lakini eneo la Nyakabale liko nyuma ya mgodi huo na kweli kuna wakati fulani mimi mwenyewe niliweza kutembelea pale nikakuta kuna maeneo mengine ambayo wananchi walizuiliwa wasiendeleze yale maeneo yao au wasiendelee kujenga kwa sababu wako ndani ya leseni na mimi niliweza kuwapa nilitoa tamko kwa mgodi kwamba wawalipe wananchi hao na kuondoka kama wananchi hao wanaathirika na uchimbaji huo. Lakini vilevile ni kwamba mgodi walisema wako tayari wataweza kuwaonda wale wote ambao wanaonekana wanaathirika na shughuli za mgodi.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile katika swalii la pili kuhusu fidia ya yale maeneo ambayo yanazunguka mgodi ambayo yapo karibu na Mji wa Geita hapa tunavyozungumza ni kwamba uthaminishaji ulikuwa unaendelea na uthaminishaji ule ulikuwa unafanywa na kampuni binafsi lakini chini ya usimamizi wa *Chef Valuer* wa Serikali ambapo mpaka sasa hivi tumekwishakuona kwamba ni watu wangapi ambao wanatakiwa walipwe uthaminishaji umeshakubaliana waliothaminiwa na wathaminishaji wote wameshakubaliana na toka Jumatatu tayari fidia hizo zimeanza kulipwa na kampuni ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana jamani leo ni Bajeti ya Wizara ya Madini, kwa hiyo mtapata nafasi baadaye lakini pia tuna maonyesho hapo nje na *GGM* wapo wanaweza wakaendelea kujibu mambo haya kadri hali inavyoendelea, basi Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante wananchi wangu wa Epanko tangu wafanyiwe tathimini ni miaka miwili mpaka sasa hivi hawajalipwa, na Mheshimiwa Waziri alishafika huko na anajua shida, sasa sheria inasema mtu akifanyiwa uthamini baada ya miezi sita anatakiwa alipwe na ikizidi hapo analipwa fidia na uthamini ukizidi miaka miwili unakuwa *cancelled* unafanywa upya, nataka kusikia kauli Serikali. Je, hawa wananchi waliofanyiwa uthamini wao lini watalipwa ni miaka miwili imeshapita?

SPIKA: Wanalipwa lini Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, ni kweli uzuri kwenye sheria ya uthaminishaji na kulipa fidia iko wazi tunataka makampuni yote yakishafanya uthamini walipe ndani ya muda uliokubaliwa, mtu ambaye hatalipa ndani ya miezi sita sheria inasema atalipa lakini atalipa na *interest* yaani kwa maana ya usumbufu na asipolipa ndani ya miaka miwili, sheria inasema kwamba tayari ule uthaminishaji una-expire kwa mujibu wa sheria kwa hiyo ni lazima mrudi mfanye uthaminishaji upya.

Mheshimiwa Spika, nipende kutoa tu wito kwa makampuni yote walipe kwa muda ambao umepangwa wasipofanya hivyo inaleta mtafaruku, mfano mzuri uko kule Mara Tarime, kuna watu ambao hawakulipa ndani ya muda matokeo yalivyokuja kuonekana ni kwamba sasa wale wenye zile nyumba waliona kwamba baadaye wataonekana watakuja kuondolewa wakawa wanajenga nyumba za kutegesha, nyumba za gharama nafuu ili waje walipwe fedha nyingi. Sasa hii imetokea maeneo mengi, kwa hiyo tunaomba sana makampuni yote tunawahasa mkishafanya uthaminishaji lipeni kadri ya sheria inavyosema usipofanya hivyo inaleta mtafaruku. Nashukuru sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Heche ndio mlikuwa mnajenga upya nyinyi, swali la nyongeza tafadhali fupi.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri aliambie Bunge na awaambie Watanzania kwa mujibu wa Sera ya Madini ya Mwaka 2009 kampuni inatakiwa kulipa fidia ifanye *relocation* na ifanye *resettlement* kama inahamisha watu. Lakini hawajawahi kuhamisha mtu wala kumfanya *relocation* na licha ya hivyo mpaka sasa kwa mfano wananchi wa Tarime waliofanyiwa uthamini maeneo ya Nyamongo kuanzia mwaka 2009 mpaka leo tunavyozungumza hawajawahi kulipwa. Juzi Mheshimiwa Waziri wa Madini alikuwa pale ametoa kauli lakini mgodi

unakiuka hausikilizi, kwa hiyo, nataka Mheshimiwa Waziri ni lini hasa watu hawa wanaoendelea kuteseka kwa zaidi ya miaka 10 au 15 watalipwa sasa ahsante? (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Madini Mheshimiwa Dotto Biteko majibu.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini naomba njibui swali la nyongeza la Mheshimiwa John Heche Mbunge wa Tarime kwa kifupi tu na kwa sababu leo ni bajeti yetu tutaeleza kwa kina hayo yote.

Mheshimiwa Spika, nieleze kwamba ni kweli kulikuwa na changamoto ya muda mrefu toka mwaka 2012 kwenye fidia za maeneo ya mgodi wa *North Mara* huko Nyamongo. Lakini kama Serikali tumechukua hatua kubwa sana kwa sababu kuna maeneo mengine ambapo kwa kweli tungekimbia tu wananchi walipwe fidia walikuwa wamepunjwa sana, kwa mfano awamu ya 47 wananchi 66 ambaao walikuwa wanadai fedha walithaminiwa kiasi cha shilingi milioni 224 peke yake, tumekwenda kule tumeangalia tumekuta wale wananchi walikuwa wamepunjwa sana tumeagiza uthamini huo ufanyike upya ili wananchi walipwe stahiki yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Heche anafahamu Awamu ya 24 na Awamu ya 34 wananchi hawa walikwenda mahakamani na kwa kuwa wamekwenda mahakamani tuliwashauri kwamba wamalize shauri lao mahakamani wakishakumaliza sisi kama Serikali huku tutasimamia utaratibu wao wa kulipwa. Lakini Awamu ya 30, 32 (a) na (b) ambazo mgodi hauhitaji hayo maeneo *Chief Valuer* ameelekeza mgodi uwalipe kifuta jasho wananchi hao.

Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Heche kwamba jambo hili tumelifanya pamoja na kwenye bajeti tutalieleza kwa kina awe na subira tusiharakishe shughuli za Bunge ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Nishati swali la Mheshimiwa Saul Henry Hamon Mbunge wa Rungwe kwa niaba yake ataulizwa na pacha wake Mheshimiwa Dkt.Tulia Ackson. (*Makof*)

Na. 301

Hitaji la Umeme vijiji vya Unyamwanga, Kisondela na Mpuga

MHE. DKT. TULIA ACKSON (K.n.y. MHE. SAUL H. AMON)
aliuliza:-

Umeme wa REA umepita katika vijiji vya Unyamwanga, Kisonidzela na Mpuga lakini wananchi wa maeneo hayo hawajaunganishiwa huduma ya umeme.

Je, ni lini wananchi hao wataunganishiwa huduma ya umeme?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati, Mheshimiwa Subira tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saul Henry Amon Mbunge wa Rungwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ni mionganini mwa halmashauri zilizonufaika na utekelezaji wa mradi wa *REA* // uliotekelvezwa na mkandarasi kampuni ya *SINOTEC Ltd.* kutoka nchini China ambapo vijiji vya Unyamwanga na Kisonidzela ni mionganini mwa vijiji vilivyopatiwa huduma ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kuititia utekelezaji wa mradi wa *REA* // mzunguko wa kwanza unaoendelea kutekelezwa na Mkandarasi *STEG International Services* jumla ya vijiji 26 katika Wilaya ya Rungwe vitafikishiwa umeme ikiwemo kijiji cha Mpuga.

Mheshimiwa Spika, kazi za mradi zinahusisha ujenzi wa kilomita 20 za njia ya umeme wa msongo kilovoti 33, kilomita 42 za njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4, ufungaji wa transfoma 25 na kuunganisha wateja wa awali 1,195. Gharama ya mradi ni shilingi bilioni 2.25

Mheshimiwa Spika, baadhi ya vitongoji ambavyo havikufikiwa na umeme katika utekelezaji wa REA II katika vijiji vya Unyamwanga na Kisonidzela vitapatiwa umeme kupitia mradi wa ujazilizi Awamu ya II *Densification II* utakaoanza na kutekelezwa kuanzia mwezi Julai, 2019 ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson nilikuona.

MHE. DKT. TULIA ACKSON: Mheshimiwa Spika, nakushuru kwa fursa pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza Kata ya Lupepo haina umeme kabisa na hivyo shule ya Sekondari Lupepo haina huduma hiyo na pia zahanati ya Lupepo watu wanajifungulia gizani, ni lini kwenye Kata hii tutaletewa umeme wa REA? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Waziri alipokuja Jiji la Mbeya alitoa ahadi kwa Kata ya Usalaga na Kata ya Iduda kwamba wananchi wa maeneo haya watawekewa umeme kwa shilingi 27,000. Lakini kuna Kata zingine za Jiji la Mbeya ambazo pia hazina umeme na ningependa kusikia msimamo wa Serikali kuhusu bei ya umeme kwenye kata hizi, na kata hizi ni Kata ya Itende, Kata ya Iziwa, Kata ya Nsoho, Kata ya Iwambi, Kata ya Mwasanga, Kata ya Itezi, Kata ya Mwansekwa, Kata ya Nsalaga na Kata ya Idunda na Kata ya Itagala? Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati Dkt. Kalemani majibu tafadhali.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa

majibu mazuri katika swalii la msingi la msingi la Mheshimiwa Naibu Spika kwa niaba ya Mheshimiwa Mbunge wa Rungwe.

Mheshimiwa Spika, napenda nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Naibu Spika kwa niaba ya Mheshimiwa Mbunge wa Rungwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kabisa katika shule ya sekondari katika Kata la Lupepo pamoja na kituo cha afya havijapatiwa umeme, lakini nilipotembelea Rungwe niliwaomba sana Mkurugenzi na Mwenyekiti wa Halmashauri waweze kulipia ili shule pamoja na zahanati zipelekewe umeme. Niombe tu Mkurugenzi wakandarasi wetu wako *site* na wamemfuatilia mpaka wiki iliyopita alipe ili shule ya sekondari na zahanati zote zipatiwe umeme ikiwezekano wiki ijayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili kweli nilitembelea Mbeya Mjini na maeneo mengine na katika maeneo ambayo nilitembelea nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Spika kwa niaba ya Mbunge na Wabunge wengine wa Mbeya kwa kufuatilia ipasavyo sana katika kupeleka umeme katika vijiji vya Mbeya Mjini.

Mheshimiwa Spika, nilipotembea Mbeya Mjini kwanza aliomba maeneo saba yapelekewe umeme ikiwemo eneo la Kitunda, Msalaga na maeneo mengine yote yameshapelekewa umeme nakupongeza Mheshimiwa Naibu Spika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini ameendelea kuomba maeneo mengine 14 katika Jiji la Mbeya ili nayo yapelekewe umeme kwa shilingi 27,000, tumeanza kuyapelekea kuanzia mwezi huu Kata zote za Msalaga mpaka Relini zitapelekewa umeme wa 27,000, nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Spika. (*Makofii/ vigelegele*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri niliona Mheshimiwa Msigwa na Mheshimiwa Selasini wanahangaika sana. Sijui kwa nini kwa kweli haya tuende

upande wa CUF uliza swali lako na Mheshimiwa Semuguruka pia.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nataka nipate tu maelezo ya Serikali ni lini mtapeleka umeme katika vile vijiji ambavyo vilishapitishwa kwenye mradi wa REA II vijiji vya Ruvu na Dimba katika Jimbo la Mchinga?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Mchinga hako huko umeme unaenda au bado, majibu tafadhalii Mheshimiwa Subira.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ameulizia vijiji vyake viwili ambavyo viko kwenye mpango wa kupelekewa umeme katika *REA* / / mzungunguko wa kwanza, nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge na tulikutana Lindi nikamuahidi baada ya Bunge hili la Bajeti tutatembelea Jimbo lake na Mkandarasi *State Grid* kupitia ziara ambayo alifanya Mheshimiwa Waziri katika Wilaya ya Luwangwa, Wilaya ya Nachingwea na Jimbo la Mtama Lindi vijijini ameonesha kupata kasi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilitaka nimtaarifu tu kwamba kazi inaendelea katika vijiji alivyovitaja na baada ya Bunge hili kwa ruksa ya Mheshimiwa Waziri tutaambatana naye tukague na tuwashe umeme katika vijiji vyake asiwe na wasiwasi ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Oliver Semuguruka.

MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona niweze kuuliza swali la nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kabla ya kuuliza swali naomba kutoa pole nyangi kwa Wananchi wa Mkoa wa Kagera kwa mafuriko kwa ajili ya mvua nyangi zinazoendelea kunyesha. Mimi Mbunge wao na Serikali tuko pamoja, nawapa pole sana Ndugu zangu wa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, sasa swalii la nyongeza, changamoto iliyopo Rungwe inafanana kabisa na changamoto iliyopo Wilaya ya Ngara katika Kata ya Mlusagamba, Kata ya Bukiriro na Mganza. Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika kata hizo?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbunge Oliver na kumpongeza, hii ni mara yake ya tatu anasimama ndani ya Bunge hili kuulizia masuala ya nishati katika Jimbo la Ngara. Hizo kata alizozitaja ikiwemo Msagamba, nataka nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwa miradi ya *REA* inayoendelea kata hizi zimeingia kwenye *REA* Awamu ya Tatoo, Mzunguko wa Pili, ambaa unaanza tarehe 01Julai, 2019, tuko katika hatua za kuandaa makabrasha ya zabuni. Kwa hiyo, nimtoe hofu tu kwamba, na Wananchi wakazi wa Ngara kwamba, Serikali yetu ya Awamu ya Tano imedhamiria ifikapo 2020/21 maeneo yote, vijiji vyote vikiwemo vijiji vya Wilaya ya Ngara viwe vimewaka umeme. Kwa hiyo, nimtoe tu wasi Mheshimiwa Mbunge aendeleee kushirikiana na sisi katika kufuatilia hayo maeneo yake, asante sana.

SPIKA: Tuendelee, bado tuna maswali mengine Wizara hii. Mheshimiwa Mbunge wa Busanda, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba anauliza swalii. Kwa niaba yake, nimekuona Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe.

Na. 302

Hitaji la Umeme wa *REA* /// Busanda

MHE. AUGUSTINO M. MASELE (K.n.y. MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA) aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme wa *REA* /// katika Kata za Bujula, Nyamalimbe, Kamena, Nyalwanzaka,

Nyakamwaga, Busanda Kaseme, Magenge, Butindwe na Nyaruyeye?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati. Mheshimiwa Subira Hamisi Mgusu, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la mhesimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inapeleka umeme katika Jimbo la Busanda kupitia Mradi wa *REA III* Mzunguko wa Kwanza ambapo Kata ya Nyaruyeye itapatiwa umeme kupitia Mkandarasi Kampuni ya *JV White City International Contractors*. Na kazi ya kupeleka umeme katika Kata ya Nyaruyeye itakamilika mwishoni mwa Mwezi Mei, 2019 ambayo ni wiki hii.

Mheshimiwa Spika, katika Kata nyingine za Nyalwanzaja, Kamena, Busanda na Nyakamwaga zitapata umeme kupitia utekelezaji wa mradi wa kusambaza umeme katika vijiji vinavyopitiwa na mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa Gridi ya Taifa ya Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Bulyanhulu hadi Geita. Hadi mwezi Mei, 2019 mkandarasi amekamilisha kazi za kufanya *survey* na kazi za ujenzi wa mradi zinatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2019 na kukamilika mwezi Januari, 2021. Katika Kata zilizobaki za Magenge, Nyamalimbe, Bujula na Kaseme zitapatiwa umeme kupitia Mradi wa *REA III* Mzunguko wa Pili unaotarajiwa kuanza Mwezi Julai, 2019.

SPIKA: Mheshimiwa Masele nimekuona. Swali la nyongeza tafadhali.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza ni kwamba, mkandarasi wa Awamu hii ya III wa REA katika Mkoa wa Geita anaonekana anaenda anasusua katika utekelezaji wake. Sasa ni nini hatua zinazochukuliwa na Serikali, ili kuhakikisha kwamba, maeneo ya utekelezaji wa mradi huu REA III unakamilika kwa mujibu wa ratiba?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; katika Wilaya ya Mbogwe kuna vijiji vilivyoachwa kwenye Awamu hii ya REA Phase III ikiwemo Kata Mpya ya Bonigonzi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba, vijiji vyote vya Wilaya ya Mbogwe vinapatiwa nishati hii ya umeme? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Nishati. Mheshimiwa Dkt. Kalemani, tafadhali.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge Masele, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ya mzingi:-

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Masele katika kuliza swalii la msingi. Kwanza ni kweli Jimbo la Mbogwe lina vijiji 86 na katii ya vijiji hivyo ni vijiji 23 havijapata umeme, ikiwemo Kata Mpya ya Bonigonze. Lakini pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Masele na ufuatiliaji wake Kata Mpya ya Nyabunigonza ambayo inapitia Kijiji cha Lunguya kwenda Kijiji cha Chibutwe, umbali wa kilomate mbili na iko katikati imeshaanza kushushiwa umeme tangu jana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni matumaini yetu kwamba, kata nzima na vijiji vyake vitano itapelekewa umeme kuanzia mwezi huu hadi mwezi Septemba mwaka huu.

Nimpe tu taarifa Mheshimiwa Mbunge, nimefuatilia kazi hizi na kumpongeza sana kwenye wilaya yake itabakiza vijiji vitano ambavyo tunaanza kuvipelekea umeme kuanzia mwezi ujao na vitakamilika mwezi Disemba mwaka huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni lini mkandarasi, *White City*, atamaliza kazi katika Mkoa mzima wa Geita:-

Mheshimiwa Spika, kwanza mkandarasi huyu ameshafikia *average* ya asilimia 52 na muda wake wa kumaliza kazi kimsingi ni mwezi Juni mwakani, lakini tunamtaka amalize kazi mwezi Disemba mwaka huu, ilibaki kazi ndogondogo za kuunga wateja, hasa ambao watachelewa kulipa. Kwa hiyo, nimpe taarifa na kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuuliza maendeleo ya mkandarasi katika Mkoa mzima wa Geita, lakini nimhakikishie kwamba, utakamilika ndani ya muda. (*Makofii*)

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Malocha, Mheshimiwa Selasini atafuatia.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nashukuru sana:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ile ya Awamu ya Pili ilipeleka umeme katika Mji Mdogo wa Laela, lakini haikushusha umeme katika sekondari ya Lusaka na Sekondari ya Kaengesa. Je, ni lini Serikali itashusha umeme katika sekondari hizo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, tafadhalii, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Subira Khamisi Mgatu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Malocha amejielekeza kwenye utekelezaji wa REA // ambapo Mji wa Raela nao ulifikiwa, lakini ameeleza Sekondari za Kaengesa kwamba, hazijapatiwa umeme. Nataka nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwanza nimpongeze kwa kazi nzuri, tuliambatana kwenye ziara katika jimbo lake mpaka Kilyamatundu, lakini tulitoa maelekezo kwamba, Mradi wa Ujazilizi Awamu ya // ambao unaanza tarehe 01Julai, 2019 na tuko hatua za mwisho za kuwapata wakandarasi maeneo ya Raela na hususan vitongoji ambavyo havijafikiwa na hizi sekondari.

Mheshimiwa Spika, namuagiza Meneja *TANESCO* wa Mkao ahakikishe maeneo haya yanaingizwa kwenye Mradi wa Ujazilizi Awamu ya Pili, ili waendelee kusambaziwa umeme na maeneo menginebya taasisi za umma katika Mkao wa Rukwa kwa kuwa upo katika orodha ya mikoa 26 ambayo itafikiwa na Mradi wa Ujazilizi Awamu ya II. Asante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Kitandula, swali la mwisho Wizara hii ya nishati, uliza.

Ooh! kabla ya Mheshimiwa Kitandula, nilikwishamtaja Mheshimiwa Selasini, subiri kidogo Mheshimiwa Kitandula.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa jinsi Waziri na Naibu wake wanavyojibu haya maswali inaonekana kwamba, kazi yao ni nzuri, wanazunguka sana kwenye hii nchi na wana *data* za kutosha. Nawapongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa katika Jimbo la Rombo kuna Kata za Reha, Nanjara, Kitirima, Mraokerio, Kwandele, ambazo vijiji kadhaa bado havijapata huduma ya umeme na mradi wa ujazilizi bado haujaanza kufanya kazi vizuri. Je, ni lini kata hizi na vijiji vyake sasa mradi wa kuapelekea umeme utakamilika? Asante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana na yeye pia kwenye jimbo lake tumewahi kufanya ziara, lakini kwa kweli, nikiri katika Mkao wa Kilimanjaro kulikuwa na changamoto ya utekelezaji wa mradi wa *REA* // na Serikali ilichukua hatua na ikaitangaza ile kazi tena na mkandarasi yuko *site* anaendelea. Katika maeneo aliyoyataja ikiwemo Kata ya Nachara na vijiji ambavyo havijapatiwa miundombinu ya umeme Mheshimiwa Mbunge ameulizia masuala ya mradi wa ujazilizi:-

Mheshimiwa Spika, nataka nimtaarifu Mkao wa Kilimanjaro ni miongoni mwa mikoa 9 ya ujazilizi ambayo

itapata mradi wa ujazilizi Awamu ya II, mzunguko wa kwanza. Kwa hiyo, nataka nimtaarifu kwa kweli, vitongoji vyote vilivyosalia katika Mkoa wa Kilimanjaro vitapate umeme na huo mradi kama nilivyo sema kwenye maswali ya awali kwamba, uko hatua za kuwapata wakandarasi. Asante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Kitandula, tafadhalii.

Na. 303

Kupeleka Umeme wa REA III – Mkinga

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme wa *REA III* katika Kijiji cha Hemsambia na Vitongoji vyake vyote?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati, bado tuko kwako.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Vijiji vya Hemsambia na Kindundui ni miongoni mwa Vijiji vya Kata ya Kigongoi, Wilaya ya Mkinga vilivyofaidika na Awamu ya Tatu ya utekelezaji wa Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini, *REA III*, mzunguko wa kwanza. Mkandarasi Kampuni ya Ubia ya *JV Radi Service Limited*, *Njarita Contractor Limited* na *Aquila Contractor Limited* yuko site anaendelea na kazi ya kusambaza umeme katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, kazi za kupeleka umeme katika Vijiji vya hemsambia na Kindundui imejumuisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometra 2.1, njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometra mbili, ufungaji wa transfoma mbili za KVA 50 pamoja

na kuwaunganishia umeme wateja wa awali 62. Gharama ya mradi ni shilingi milioni 184.23.

Mheshimiwa Spika, vijiji vingine vya Kata ya Kigongoi vya Vuga, Kwekuyu, Kindundai, Mgambo Shashui na Bombo Mbuyuni vitapatiwa umeme kuititia Mradi wa REA III Mzunguko wa Kwanza unaoendelea kutekelezwa Wilayani Mkinga na kukamilika mwezi Juni, 2020. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Kitandula nimekuona.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Wizara ambayo yanatupa matumaini, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *survey* iliyofanyika Hemsambia illifanyika kwa vitongoji viwili na kuacha vitongoji vingine vitano. Je, Waziri anatuthibitishia kwamba, kwa azma ile ya kuhakikisha kwamba, kila kijiji kinapofikiwa lazima kijiji chote kipate umeme; Je, vitongoji hivi vitajumuishwa kwenye kupatiwa umeme?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wakati tunapeleka umeme kwenye Kata ya Bosha maeneo ya Vitongoji vya Miyongwe, Kwemsakazi, Kwashemwaondwa na Kibago B yalirukwa, lini maeneo haya yatapatiwa umeme?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Waziri mwenyewe.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya swali la msingi la Mheshimiwa Kitandula, lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga na pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, katika maswali yake mawili ya nyongeza kwanza ni kweli, kwenye Kijiji cha Hemsambia tulifanya *surveyvitongoji* viwili na tukabakiza vitongoji vitano ambavyo tayari wakandarasi tumeshaviingiza kwenye

marekebisho na yanafanyiwa kazi. Na hivi sasa Mheshimiwa Mbunge, pamoja na kupongeza, tulipokuwa katika jimbo lako wiki iliyopita tulitoa maelekezo na wakandarasi wameshaanza kuyafanya kazi. Kwa hiyo, niwape taarifa tu Wananchi wa vitongoji vitano vya Kijiji cha Msambia kwamba, vitongoji vyote katika kijiji hicho vitafanyiwa kazi na vitakamilika mwezi Septemba mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, katika swali la msingi la pili la Mheshimiwa Mbunge, ni kweli tunazo kata tano muhimu sana kwa Mheshimiwa Mbunge, lakini Kata ya Bosha yenye vijiji vinne vikiwemo Kijiji cha Kwashemhonda, pamoja na Kwesekazi, pamoja na Kibango vimeshaanza kufanyiwa kazi na Shirika la Umeme – *TANESCO* kwa sababu, sasa hivi bei ni ileile 27,000/= . Na jana tumewasiliana na Mheshimiwa Mbunge alikuwa kufuatilia na *TANESCO* pamoja na wataalamu wameshaingia *site* kuanzia leo. Kwa hiyo, ni matumaini yetu Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Mkinga muwe na matumaini kwamba, Kata na Vijiji vyote vya Bosha vinakwenda kupatiwa umeme mwisho wa mwezi Disemba mwaka huu.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Esther Matiko. Swali la nyongeza tafadhalii na Mbunge wa Nyanghwale utamalizia.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Mji wa Tarime kwa hadhi ya kuwa mji ulitakiwa kuwa na umeme kwa zaidi ya asilimia 90, lakini maeneo yenye umeme ni chini ya asilimia 40. Na kwa sababu, Waziri wakati anajibu baadhi ya maswali hapa amehakikisha kwamba, na akatoa *instructions* kwamba, vituo vya afya, zahanati, shule kama sekondari vihakikishwe vinapewa umeme.

Mheshimiwa Spika, kwenye Jimbo langu Kata ya Nkende kuna kituo cha afya, kuna sekondari na kuna shule za msingi, lakini hazina umeme. Kata ya Kenyamanyori ina shule ya sejkontari, ina shule za msingi, ina kituo cha afya hakina umeme na Kata ya Kitale kuna Sekondari ya nkongole na Mogabili na vituo vya afya pale, zahanati hazina umeme, vilevile na Kata ya Nyandoto.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua sasa ni lini, na nimekuwa nikiuliza haya maswali, ni lini huu umeme wa *REA* utaweza kufika kwenye hayo maeneo ambayo hayana umeme kabisa, ili sasa hizo zahanati, vituo vya afya, sekondari na shule za msingi ziweze kupata umeme, pamoja na Wananchi? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Kalemani, majibu tafadhali.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, kwanza pamoja na kuwapongeza Wananchi wa Tarime kwa kupelekewa umeme katika vijiji vyote iko changamoto katika kata ambazo amezitaja, hasa Kata ya Nkende pamoja na Kenyamanyori na Kitale. Nimeshazungumza mpaka na Mkurugenzi alipie zahanati na shule zipelekewe umeme kwa sababu, vijiji na vitongoji vya maeneo hayo vina umeme. Kwa hiyo, nikupongeze Mheshimiwa kwa kufuatilia, lakini nikuombe uwasiliane na Mheshimiwa Mkurugenzi na Halmashauri ya Kijiji cha Nkende pamoja na Kijiji cha Kitale na Kenyamanyori waweze kulipia ili shule na zahanati zipelekewe umeme.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, nyongeza ya hilo, nitapenda nitembelee mimi mwenyewe ili nikatoe maelekezo kwa wakurugenzi waweze kulipia. Mheshimiwa Esther hata akibaki nitakwenda mwenyewe ili kusudi maeneo hayo na zahanati ziweze kupatiwa umeme, ahsante sana. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Uende naye. (*Makofi/kicheko*)

SPIKA: Eeh, jibu hilo ni zuri, Mheshimiwa Waziri nenda mwenyewe bwana. (*Kicheko*)

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, uliniita.

SPIKA: Uliza swali lako Mheshimiwa Mama Nagu.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, uliniita.

SPIKA: Aah! Nyanghwale kweli, Mbunge wa Nyanghwale, Mheshimiwa Amar.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swalii la nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Nyanghwale ina vijiji 62 na mpaka kufikia leo hii ni vijiji saba tu ambavyo vimeshawashwa umeme na vijiji 13 tayari nguzo zimeshasimama. Nimeongea na mkandarasi kwa nini hajawasha vile vijiji 12 akadai kwamba, kuna upungufu wa nyaya.

Je, Waziri anatuambia nini kuhusu upungufu huo wa nyaya?

SPIKA: Eeh! Mheshimiwa Waziri, isaidie Nyanghwale rafiki yangu, majibu tafadhalii.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, kwanza kwa taarifa hiyo nashukuru kuipokea, kwanza umenipa jukumu la kufuatilia, nikuhakikishie nitalifuatilia hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusiana na upungufu wa nyaya naomba nitoe taarifa kuititia Bunge lako Tukufu na kwa Watanzania hivi sasa hapa nchini hatuna shida na nyaya wala nguzo wala mita, changamoto inaweza ikawa ni utaratibu wa wakandarasi wenyewe namna ya kuhifadhi hivyo vifaa.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii Mheshimiwa Mbunge nimfuatilie mkandarasi tumfuatilie tujue changamoto ni nini, lakini tunachomuagiza kuititia Bunge lako Tukufu, napenda nichukue nafasi hii kumuagiza Mkandarasi wa *White City* anayetekeleza Mradi wa *REA* katika Mkoa mzima wa Geita, ikiwemo na Nyanghwale, achukue hatua za kuhakikisha vifaa vyote vinapatikana *site* na kazi ikamilike ndani ya wakati.

SPIKA: Ahsante, tuelekee kilimo Waheshimiwa Wabunge; Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu uliza swali lako.

Na. 304

Kupunguza Bei ya Mbegu za Mahindi na Pembejeo

MHE. DKT. MARY M. NAGU aliuliza:-

Serikali iliondoa kodi kwenye mbegu za mahindi mwaka 2017 – 2018:-

Je, ni lini Serikali itasimamia upunguzwaji wa bei kubwa ya mbegu za mahindi na pembejeo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA) alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu, Mbunge wa Hanang, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua ambazo zinzaidia kupunguza bei za pembejeo ikiwa ni pamoja na kufuta ada na tozo zilizokuwa zinatozwa na taasisi za udhibiti wa pembejeo za kilimo. Katika kipindi cha mwaka 2017 na 2018 Serikali imefuta ada na tozo 12 katika tasnia ya mbegu kwa lengo la kupunguza gharama za uzalishaji na bei ya mbegu.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Februari, 2019 Serikali imekutana na wadau wa pembejeo za kilimo kwa lengo la kujadili maendeleo ya pembejeo za kilimo, ikiwemo kujadili suala la bei ya mbegu. Katika kikao hicho wadau walikubaliana kufanya utafiti wa kuhusisha taasisi ya udhibiti wa mbegu Tanzania (*TOSCI*) na Chama cha

Wafanyabiashara wa Mbegu (*TASTA*) ili kutathmini gharama za uzalishaji na usambazaji. Jitihada zinazoendelea ni kutafuta vyanzo vya fedha ili kumuwezesha mshauri elekezi kufanya tathmini hiyo. Matokeo ya tathmini hiyo yatawezesha upangaji wa bei ya mbegu ambayo itamnufaisha mkulima na mzalishaji. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Nagu, uliza swali lako la nyongeza.

MHE. Dkt. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Naibu Waziri kujibu swali. Baada ya kutoa kodi na tozo 12, mategemeo yetu ilikuwa bei ya mbegu kuwa chini au kuteremka kutoka shilingi 9000/10,000 zimepanda bei mpaka 12,500. Je, kuna uhusiano gani sasa tulipiga kelele huku kuondoa tozo na kodi lakini bado bei ya mbegu imeongezeka. Naomba Mheshimiwa Waziri atuambie pamoja na kwamba tathmini haijaisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mbegu ni suala muhimu sana katika kilimo, sasa yeye amesema mnatafuta fedha na mnategemea kufanya tathmini, hamuoni tumechelewa kufanya hivyo wakati kilimo kinaendelea kila msimu. Naomba uniambie fedha zitapatikana lini na tathmini itafanywa lini ili bei mbegu ithibitiwe na iteremke? Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Kushusha bei ya mbegu tafadhali majibu Mheshimiwa Innocent Bashungwa, tatizo la mbegu ni kubwa sana nchini upatikanaji wake.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA): Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu kwa namna anavyofuatilia changamoto za wakulima wake katika Wilaya ya Hanang na napenda kujibu maswali yake mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu amesema kwamba pamoja na jitihada za Serikali kuondoa kodi na tozo, bado bei ya mbegu haijashuka na mkakati wa

Serikali katika hili ni kwamba tumetambua kwamba mkulima na mzalisha mbegu wamekuwa wote wakitegemea msimu wa mvua, badala ya mzalisha mbegu kuzalisha mbegu za kutosha wakati wa kiangazi ili aweze kumpatia mkulima mvua zinavyoanza mkulima huyu aweze kupanda.

Mheshimiwa Spika, sasa mkakati wa Serikali ni kwamba kwanza nimpongeze Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli amesaidia Serikali kuingia makubaliano na *EFAD*. Tumeingia makubaliano tumepeata bilioni 127.3 na fedha hizi asilimia kubwa itaenda kwenye taasisi za uzalishaji wa mbegu. Na nimuhakikishie Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Wilaya ya Hanang hatutawasahau katika hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa swali la pili, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu alikuwa anazungumzia kuchelewa kufanyika kwa tathmini lakini Serikali haljachelewa kama nilivyosema, tayari Serikali imeshapata dawa fedha zimepatikana, sasa tunaenda kwenye utekelezaji. Asante sana

SPIKA: Ahsante, swali la mwisho kwa siku ya leo, Mheshimiwa Saed Kubenea, badala yake Mheshimiwa Tunza.

Na. 305

Ujenzi wa Kiwanda na Bandari ya Samaki

MHE. TUNZA I. MALAPO (K.n.y. MHE. SAED A. KUBNEA)
aliuliza:-

Uvuvi katika nchi yetu ni shughuli inayohusu wakazi wengi sana ikiwa ni ya pili kutoka kwenye kilimo kwa kutoa ajira kwa Watanzania wengi:-

(a) Je, ni lini na ni wapi kiwanda cha samaki kwa ukanda wa Pwani kitajengwa?

(b) Je, mpango wa ujenzi wa Bandari ya Samaki umefikia wapi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Uvuvi, Mheshimiwa Abdalla Ulega tafadhali, Mifugo na Uvuvi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea, Mbunge wa Ubungo lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika Sekta ya Uvuvi kwa kuweka mazingira mazuri ikiwemo uwepo wa malighafi kwa viwanda vya kusindika mazao ya uvuvi. Hadi sasa kuna viwanda vitano vya kusindika mazao ya uvuvi katika Ukanda wa Pwani. Vilevile, Serikali inatarajia kupitia Shirika la Uvuvi Tanzania (*TAFICO*) kujenga viwanda vya kusindika mazao ya uvuvi nchini ikiwa ni moja ya mikakati yake.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imeingia mkataba na mshauri elekezi Kampuni ya *Sering Ingegneria* kutoka Italia kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari ya uvuvi katika mwambao wa Pwani ya Bahari ya Hindi. Kampuni hii ilianza kazi tarehe 2 Agosti, 2018 na tayari imekabidhi taarifa ya awali (*inception report*) na kazi inaendelea ambapo hatua ya pili ya ukusanyaji wa taarifa muhimu (*interim report*) inaendelea. Aidha, upembuzi huo utakapokamiliika utawezesha kutambua maeneo yanayofaa kwa ujenzi wa bandari na gharama za ujenzi wa bandari ya uvuvi.

SPIKA: Mheshimiwa Tunza, nilikuona.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri swali hili umepewa siku nyingi na hili swali limeuliza ni lini na ni wapi, umejibu kwa ujumla naomba nifahamu hivyo viwanda vitano vya kuchakata samaki katika ukanda wa Pwani viko maeneo gani, kama na sisi watu wa Mtwara vinatuhusu viro huko kwetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari umesema utakapokamilika, nataka uwe *specific* unakamilika lini ili hiyo bandari ipatikane kwa maendeleo ya wavuvi na nchi yetu kwa ujumla, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Eeh! Tunza leo umekuwa mkali, Mheshimiwa Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, majibu tafadhali; lini, wapi?

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ni wapi viwanda hivyo vipo; viwanda hivyo katika Mkoa wa Dar es salaam, Mkoa wa Pwani na Mkoa wa Tanga. Mkoa wa Dar es salaam tunacho kiwanda cha *Alfa Cluster, Bahari Food, Pugu Road* lakini vilevile Mkoa wa Pwani tunacho Kiwanda cha Abajuko kilichopo pale Vikindu Madafu, Mkuranga na vilevile tunacho kiwanda cha *Alfa Cluster*, Tanga Jiji ambacho kinafanya kazi ya kuchakata samaki aina ya pweza.

Mheshimiwa Spika, swalı lake la pillı, ni lini hasa tutamaliza hii kazi ya upembuzi yakinifu ya ujenzi wa bandari ya uvuvi, tutamaliza. Mkandarasi amepewa muda wa mwaka mmoja kwa hivyo bado yupo ndani ya muda wa kukamilisha kazi yake na hatimaye atuletee ile ripoti ambayo itakuwa na ushauri wa mahala kuzuri zaidi tutakapoweza kuweka bandari yetu lakini na gharama zake za ujenzi wa ile bandari yenyewe. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge muda haupo upande wetu. Sasa nitambulisse wageni waliopo katika Jukwaa la Spika, wageni wanne wa Mheshimiwa Spika kutoka Shirika la Ndege la Tanzania (*ATCL*) ambao wamekuja kutoa huduma kwa Waheshimiwa Wabunge. Mkurugenzi wa Mauzo Ndugu Edward Nkwabi, karibu sana. Meneja Ndugu Salome Sedoyeka, hawapo *ATCL* eeh? *ATCL* naona hawapo lakini kwa ujumla tunataka tufanye utaratibu ambao *ATCL* wakati Bunge linapokuwepo hapa wawe na ofisi ndogo hapa hapa katika maeneo ya Bunge ili Wabunge muweze kupata huduma za haraka. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Naibu Spika ambaye ni mama mzazi wa Mheshimiwa Mariam Ditopile, Bi. Asila Suleiman Ditopile, ahsante sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Dotto Biteko, Waziri wa Madini ambao ni watumishi kutoka Wizara ya Madini ni pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini, Profesa Simon Msanjila, ahsante sana, karibu sana Katibu Mkuu. Kamishna wa Madini, Ndugu David Mlabwa, karibu Kamishna. Mwenyekiti wa Tume ya Madini, Profesa Idris Kikula, karibu sana Profesa. Mwenyekiti wa Bodi ya *STAMICO* Meja Jenerali Mstaafu Michael Isamuhyo, karibu *General*. (*Makofi*)

Mwenyekiti wa Bodi ya *GST* Profesa Jastinian Ikingura, karibu. Mwenyekiti wa Bodi ya *TEIT* ni Ndugu Ludovic Utouh, karibu sana. Kamishna wa Tume ya Madini Profesa Abdulkarim Mruma, karibu sana Mruma. Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Madini (*MRI*) Profesa Hudson Nkotagu, Kamishna wa Tume ya Madini Dkt. Athanas Macheyeki, Mtendaji Mkuu wa Tume ya Madini Profesa Shukrani Manya, Mtendaji Mkuu wa *STAMICO* Kanali Sylvester Ghuliku, Kaimu Mtendaji Mkuu wa *GST* Ndugu Yokbeth Myumbilwa, Kaimu Mkuu wa Chuo cha *MRI* Ndg. Fredrick Mangasini, Mratibu wa Kituo *TGC* Ndugu Eric Mpesa, Kaimu Katibu Mtendaji wa *TEIT* Ndugu Mariam Mgaya, karibu sana. (*Makofi*)

Tuna wageni 10 wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ambao ni Kamishna na *Chief Executive Officer of The Workers Compensation Fund Control Board of Zambia*, Dkt. Elizabeth Nkumbula, karibu sana wageni wetu kutoka Lusaka. (*Makofi*)

Director of Legal Services from the same organization in Zambia Mrs Priscilla Bwembya, you are welcome. Director of Occupational Health and Safety from the same organization, Ndugu Kingsley Kangwa, karibu. Head of Communication and Customer Services, Ndugu Maybin Nkolombwa, karibu. Director General Ndugu Masha Mshomba, you are welcome. Director of Finance Planning

and Investment Ndugu Basil Ewala, ahsante. Director of Assessment Services Dkt. Abdulssalaam Omary, Head of Public Relations Unit Ndugu Laura Kunenge, Head of Legal Services Unit, Ndugu Abraham Siyovelwa, Plan and Research Manager Ndugu Patric Ngwila, ahsante karibuni sana wageni wetu wote. (Makofi)

Wageni wengine wa Mheshimiwa Dotto Biteko ni pamoja na wageni 14 wa Mheshimiwa Biteko ambaeo ni Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi, Wilaya ya Bukombe wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya, Ndugu Daniel Machongo, karibuni sana ndugu zangu kutoka kule Bukombe, Ushirombo, eeh! Leo mmuone Mbunge wenu anavyofanya mambo yake hapa, karibuni sana. Ila huku magari mengi nyie Wasukuma msije mkagongwa na magari Dodoma, muwe mnaangalia angalia vizuri, siyo mnatoka Ushirombo kule mnakuu mbiombio hapa. (Makofi)

Pia wapo Madiwani 27 wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe, Madiwani ooh! Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani, karibuni mjifunze namna ambavyo Bunge linaendesha mambo yake na hongereni sana kwa kazi nzuri mnayofanya kule Bukombe, Wilaya inakimbia taarifa zenu tunazipata, hongereni sana. (Makofi)

Wageni kutoka Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Wadogo wa Madini Tanzania (*FEMATA*) wakiongozwa na Rais wa *FEMATA* Ndugu John Bina, karibuni sana *FEMATA*. (Makofi)

Wageni kutoka Chemba ya Migodi Tanzania (*Tanzania Chamber of Mines*) wakiongozwa na Rais wa Chemba Ndugu Gerald Mturi, karibuni sana. (Makofi)

Wageni kutoka Umoja wa Wafanyabiashara wa Madini (*TAMIDA*) wakiongozwa na Mwenyekiti wa *TAMIDA* Taifa Ndugu Sammy Mollel, wale kule karibuni sana. (Makofi)

Wageni kutoka Chama cha Wanawake Wachimbaji Madini (*TAWOMA*) wakiongozwa na Mwenyekiti wa *TAWOMA* Ndugu Eunice Negele. Wabunge wakinamama wenzenu

hawa wanachimba madini, wanaonyesha/ wanathibitisha kwamba inawezekana hata kuingia katika Sekta ya Madini kwa wakinamama inawezekana na ushahidi ni huo hapo. (*Makof/ Vigelegele*)

Pia wapo wageni kutoka Mtandao wa AZAKI wa Uchechemuzi, Kiswahili hiki; Uchechemuzi katika Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi wanaitwa (HakiRasilimali) wakiongozwa na mratibu wao Ndg. Rachel Chagonja, wachechemuzi wale hao hapo, ahsante sana. (*Makof*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Naibu Waziri wa Madini ambao ni wapiga kura wake wakiongozwa na Ndg. Zubeda Haroun, karibuni sana popote pale mlipo, wale pale, karibuni sana. (*Makof*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Prof. Joyce Ndalichako, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ambao ni viongozi wa *NACTE*. Mwenyekiti wa Bodi ya *NACTE* Prof. John Kondoro, karibu sana Profesa na Katibu Mtendaji wa *NACTE* Dkt. Adolf Rutayuga, karibu sana Katibu wa *NACTE*. (*Makof*)

Wageni 12 wa Mheshimiwa Dkt. David Mathayo (Mb), ambao ni wataalam kutoka Kampuni ya *SHANTA MINING* ya Mkoa wa Songwe wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu, Ndugu Honest Mrema, karibuni sana ninyi kutoka Mkoa wa Songwe. (*Makof*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Venance Mwamoto kutoka Taasisi ya utoaji wa Elimu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa watu wenye uoni hafifu ya Jijini Dar es salaam, karibuni wageni wa Mwamoto, wengine wapo kule. (*Makof*)

Mgeni wa Mheshimiwa Oliver Semuguruka ambaye ni mdogo wake kutoka Dar es Salaam, Ndugu Oscar Nyerere, karibu sana Oscar. (*Makof*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Josephine Genzabuke ambao ni Madiwani wa Viti Maalum kutoka Wilaya ya

Kibondo, Mkoani Kigoma ambaye ni Mwanne Kihemo na Jane Rulanyaga, karibuni sana Waheshimiwa Madiwani. (*Makofii*)

Kwa ajili ya mafunzo tuna wanafunzi 70 na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari ya Mtumba ya hapa Jijini Dodoma, wanafunzi wa Mtumba Sekondari, karibuni sana, mmependeza kwelikweli. Hii Mtumba Sekondari ipo karibu na Makao Makuu ya Serikali kule katika eneo lile ambalo wote tunalifahamu sasa. (*Makofii*)

Matangazo mawili Mheshimiwa William Ngeleja Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba juzi *Bunge Sports Club (Ndugai Boys)* walipata bao mbili *Dodoma Veterans* bao moja katika mechi illyochezwa juzi na goli lillifungwa na Mheshimiwa Cosato Chumi, mchezaji wetu mahiri sana na Mheshimiwa Yussuf Kaiza alikuwa ndiyo nyota wa mchezo ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Haonga pia. (*Makofii*)

Mpira wa pete *Bunge Queens* iliwagalagaza bila ya huruma *Dodoma Veterans* kwa magoli 23 kwa 8, dhahama hiyo ya magoli ya Bunge ilifanywa na Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata na Mheshimiwa Esther Matiko ambaye pia ndiyo alikuwa nyota wa mchezo. Shukrani wa Waheshimiwa Wabunge wote, wananchi na Waheshimiwa Wabunge mloliojitekeza kushangilia Timu yetu ya *Bunge Queens* na *Bunge Sports Club* kwa ujumla. (*Makofii*)

Ofisi ya Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sanyansi na Teknolojia, inawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, anawatangazia kwamba Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundı (*NACTE*) limeandaa maonesho ya elimu ya ufundı na mafunzo yatakayofanyika hapa Jiji la Dodoma katika Uwanja wa Jamhuri kuanzia leo, tarehe 27 hadi tarehe 31 Mei, 2019. Kauli mbiu ni elimu ya ufundı na mafunzo kwa maendeleo ya uchumi wa viwanda Tanzania.

Washiriki wa maonesho hayo ni vyuo na taasisi mbalimbali za Umma na binafsi zinazotoa elimu na mafunzo ya elimu ya kati. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kwenda kuona mambo yatakayofanyika kwenye vyuo vya taasisi zenu zinazotoa elimu ya mafunzo ya ufundi lakini pia kujifunza kuhusu fursa zilizopo kwenye vyuo mbalimbali na taasisi hizo.

Huduma zitakazotolewa wakati wa siku za maonesho ni pamoa na ushauri wa namna ya kuanzisha vyuo kwa fani mbalimbali, kuelimisha Umma juu ya vyuo vilivyosajiliwa na baraza na fani mbalimbali, lakini pia kutoa elimu kwa Umma ya jinsi mwanachuo anavyoweza kupata taarifa zake katika mfumo kuititia tovuti za baraza.

Lakini pia Waheshimiwa Wabunge, tuna maonesho mbalimbali ya wadau wa Sekta ya Madini ambayo Mheshimiwa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Doto Biteko, na timu yake yote ya Wizara, wameyaandaa hapa ambapo mara nyingi tunaandaa futari katika viwanja vyetu vya Bunge. Tunawaomba mnapotoka kwa chai kidogo au kunyoosha miguu basi mteremke hapo muwatemebelee wadau wa madini.

Wamekuja hapa na kwa kweli mimi nilishiriki jana kuyafungua maonesho hayo, wamejiantaa vizuri, yana *information* nyingi na wanawatarajia Waheshimiwa Wabunge kwamba mtawatemebelea ili muweze kuona na kuchukua *pamphlets* mbalimbali, majarida, muweze kujisomea na kuelewa zaidi kuhusu masuala yanayohusiana na masuala ya madini katika nchi yetu.

Kwa hiyo nawaomba mtembelee maonesho hayo, yako hapahapa katika Uwanja wa Bunge, na myakumbuke na haya ambayo yako Jamhuri – yatakuwepo kwa siku ngapi ya Jamhuri? – kwa siku tatu mfululizo; leo, kesho na keshokutwa. Ahsante sana.

Katibu!

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Katibu!

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE: Hoja za Serikali.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mwongozo wa Spika.

NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Madini

SPIKA: Ahsante sana. Leo ni Wizara ya siku moja, na mambo ya madini mnajua watu wengi, Wabunge wangependa kuelewa mambo mengi na siku moja, tukipoteza muda tunakula muda wa wachangiaji bila sababu za msingi. Kwa hiyo naomba tuendelee; Mheshimiwa Waziri wa Madini tafadhali. (*Makofii*)

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyelekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, ambayo imechambua bajeti ya Wizara ya Madini, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kuitisha Taarifa ya utekelezaji wa majukumu kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Madini pamoja na Taasisi zake kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia nchi yetu amani na utulivu na kutuwezesha kushiriki katika Mkutano huu wa 15 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, kwa unyenyekevu namshukuru Mwenyezi Mungu kwa

kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa mara ya kwanza nikiwa Waziri wa Madini na kwamba ni mara yangu ya kwanza kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kawaida na ya Maendeleo kwa Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nitumie fursa hii pia kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunitfea kuwa Waziri wa Madini, Wizara ambayo ikisimamiwa vizuri na kwa ufanisi itatoa mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tumsikilize Mheshimiwa Waziri, tupunguze sauti.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, aidha, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuipa kipaumbele Sekta hii ya Madini kwa miongozo, maelekezo na maagizo mbalimbali anayoyatoa. Napenda kumuahidi kwa niaba ya wenzangu Wizarani pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba sisi Wizara ya Madini tutasimamia Wizara hii ili iweze kuongeza tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, nipende pia vilevile kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maelekezo na miongozo thabiti anayotupatia hapa Wizarani. Vilevile, napenda kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake makini, ushauri na maelekezo anayoyatua katika kufanikisha utendaji kazi wa Wizara ya Madini kwa nia ya kuhakikisha kwamba rasilimali za madini zinawanufaisha Watanzania na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii vilevile kukupongeza wewe mwenyewe pamoja na Naibu Spika kwa namna mnavyolismamia na kuliendesha Bunge letu Tukufu. Kwa hakika sisi wote ni mashahidi wa namna uongozi wenu ulivyokuwa na ueledi, umakini na wenye kutanguliza mbele

maslahi ya Taifa. Kimsingi nipende kusema kuwa tunajivunia kuwa na viongozi wa mfano wa kuigwa kama ninyi. Nipende kuwashukuru pia Wenyevit wa Bunge kwa ujumla kwa namna ambavyo wanakusaidia wewe mwenyewe kuendesha shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, chini ya uongozi wa Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Dustan Luka Kitandula (Mbunge), na Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, kwa ushirikiano na ushauri mzuri wanaoutoa katika kipindi chote cha mwaka 2018/2019 ikiwa ni pamoja na kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Mwaka 2019/2020. Vilevile, nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati wote pamoja na Wabunge wote kwa ujumla wao kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutupatia ushauri kwa nyakati tofauti kwani hiyo ndiyo dhana halisi ya kuwawakilisha wananchi wao.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kuchukua fursa hii kuwasilisha Hotuba ya Wizara ya Madini ambayo inatoa Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2018/2019; Kazi zilizotekelze na taasisi zilizo chini ya Wizara kwa Mwaka 2018/2019 pamoja na Mpango, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kutokana na marekebisho yaliyofanyika Mwezi Oktoba, 2017 kupitia Hati Idhini Na.144 ya tarehe 22 Aprili, 2016, Wizara ya Madini ilipewa majukumu yafuatayo;

- (i) Kubuni, kuandaa na kusimamia Sera, Mikakati na Mipango ya kuendeleza Sekta ya Madini;
- (ii) Kusimamia migodi na kuhamasisha shughuli za uchimbaji pamoja na utafutaji wa madini kwa kutumia tafiti za kijofizikia na kijiolojia;

- (iii) Kuratibu na kusimamia uongezaji thamani madini kwenye biashara ya madini;
- (iv) Kukuza ushiriki wa wazawa kwenye shughuli za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini nchini;
- (v) Kusimamia na kuratibu shughuli na maendeleo ya uchimbaji kwa wachimbaji wadogo;
- (vi) Kusimamia taasisi na mamlaka zilizoko chini ya Wizara; na
- (vii) Kuratibu na kusimamia maendeleo na utekelezaji majukumu kwa watumishi wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, kulingana na Mpango Mkakati wa Wizara wa Mwaka 2019/2020 hadi 2023/2024, Malengo Makuu ya Wizara ya Madini ni haya yafuatayo;

- (i) Ni kupunguza maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na magonjwa yasiyoambukiza na kutoa huduma kwa waathirika wa Virusi vya UKIMWI;
- (ii) Kuimarisha na kuendeleza utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa;
- (iii) Kuboresha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali madini;
- (iv) Kuboresha Sekta ndogo ya Uchimbaji Madini;
- (v) Kuimarisha usimamizi wa mazingira katika Sekta ya Madini; na
- (vi) Kuboresha uwezo wa Wizara katika utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2020/2025, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa kipindi cha Mwaka 2015 – 2020, Sera ya Madini ya Mwaka 2009 na Sheria ya Madini ya mwaka

2010 kama ilivyorekebishwa mwaka 2017; pamoja na maagizo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia ilizingatia maeneo ya kipaumbele iliyojipangia katika kutekeleza majukumu yake ikiwemo kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali yanayotokana na rasilimali madini, kuwaendeleza wachimbaji wadogo na wa kati wa madini, kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini, kuimarisha ufuutiliaji na ukaguzi wa usalama, afya, mazingira na uzalishaji wa madini katika migodi midogo, ya kati na mikubwa; kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini na kuendelea kuboresha mazingira ya uwezeshaji wananchi kufaidika na rasilimali za madini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2018/2019, Wizara ya Madini ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi bilioni 310.6 ambapo shilingi bilioni 310.32 zilipangwa kukusanya na Tume ya Madini na shilingi 278,003,000 zilipangwa kukusanya na Wizara chini ya Chuo cha Madini. Hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2019, Wizara ilifanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 244.25 sawa na asilimia 78.64 ya lengo la mwaka. Ni matarajio ya Wizara kwamba kufikia Juni 30, 2019 lengo la makusanyo hayo litavushwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Madini ilitengewa jumla ya shilingi billioni 58.9. Kati ya fedha hizo, jumla ya shilingi billioni 39.29 zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, sawa na asilimia 66.69 ya bajeti ya Wizara na shilingi billioni 19.62 sawa na asilimia 33.3 zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, shilingi billioni 20.95 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi billioni 18.33 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara pamoja na taasisi zake. Vilevile, kati ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa, shilingi billioni 16.8 sawa na asilimia 85.62 ni fedha za ndani na shilingi billioni 2.8 sawa na asilimia 14.38 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2019 Wizara ilipokea jumla ya shilingi billioni 26 kutoka Wizara ya

Fedha na Mipango. Kati ya Fedha hizo, shilingi bilioni 25.92 zilipokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 100,000,000 ambazo ni fedha za ndani zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katи ya fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa, shilingi bilioni 15.4 zilikuwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 10.52 zilikuwa ni matumizi ya mishahara kwa watumishi wa Wizara na taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa umeendelea kuimarika na kufikia asilimia 5.07 kwa mwaka 2018. Mchango huo ulitokana na kuongezeka kwa uelewa kwa wadau wa madini kuhusu umuhimu wa uwazi na kutii Sheria ya Madini. Kufanikiwa kwa uhamasishaji kuhusu ukujali wa sekta na kuimarisha usilmamizi wa shughuli za madini kwa kudhibiti utoroshwaji wa madini, pia kuimarisha ukaguzi katika sehemu za uzalishaji madini na biashara ya madini; kuongezeka kwa viwango vya mrabaha ulioanzishwa kwa ada ya ukaguzi wa madini kuptitia Marekebisho ya Sheria ya Madini Sura ya 123 yaliyofanyika mwaka 2017.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa changamoto za Sekta ya Madini zinapatiwa ufumbuzi na hivyo kuwafanya wadau kufanya shughuli zao za uchimbaji na biashara ya madini katika mazingira ya kibiashara yanayovutia, Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliiitisha mkutano na wadau na wafanyabiashara madini tarehe 22 hadi tarehe 23 Januari, 2019 Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya mkutano huo ilikuwa ni pamoa na kusikiliza na kupokea changamoto na kero mbalimbali zinazowakabili wachimbaji, wafanyabiashara na wadau wa Sekta ya Madini. Katika mkutano huo Serikali ilipokea kero na hoja mbalimbali zikiwemo; kupunguzwa kwa kodi na tozo zinazotozwa kwa wachimbaji wadogo wa madini, kufutwa kwa maeneo ya

leseni za madini zisizoendelezwa, kuwekwa kwa maafisa madini kwenye maeneo ya machimbo ya madini, kudhibiti utoroshwaji wa madini, kuimarisha utunzaji wa mazingira katika maeneo ya uchimbaji madini, ukosefu wa miundombinu na tozo na ada kulipwa kwa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa wachimbaji wa madini wanapata masoko rasmi na kuhakikisha kwamba Serikali inaratibu shughuli zao, Serikali ilianzisha mchakato wa kuanzishwa kwa masoko kwa ajili ya wachimbaji. Serikali imeanzisha mfumo huu katika mikoa yote nchini. Na ninaomba kutoa taarifa tu kwamba wakuu wote wa mikoa nchini wameagizwa kutekeleza agizo hili na soko la kwanza lilizinduliwa Mkoani Geita tarehe 17 Machi, 2019.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana viongozi wote wa mikoa, wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya kwa utayari wao wa haraka wa kuanzisha masoko haya. Na masoko haya yamefunguliwa maeneo mbalimbali yakiwemo Geita, Kahama, Namanga, Singida, Chunya, Ruvuma, Shinyanga, Katavi, Dodoma, Kigoma, Tabora, Mara na Iringa. Naomba nitoe wito kwa viongozi wote wa mikoa na wilaya ambazo bado hawajatekeleza maagizo hayo ya Serikali kuharakisha taratibu za uanzishwaji wa masoko hayo katika maeneo yao mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kukamilika kwa Ukuta wa Mirerani mwezi Aprili, 2018 udhibiti wa madini ya Tanzanite umeimarika na hivyo kuongeza ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na madini hayo. Wachimbaji wa madini Mirerani wameitikia wito huo vizuri kwa kulipa kodi na sasa wanalipa kodi kuliko kipindi chochote kwenye historia ya uzalishaji wa eneo hilo. Wachimbaji wadogo Mirerani walikuwa wanachangia kwa asilimia 6 hadi 10 ya mapato yote ya Mirerani; kiasi kikubwa kilikuwa kikichangiwa na Mgodi wa *TML*. Kwa mfano katika Mwaka 2017 kiasi cha shilingi bilioni 1.9 kilikusanywa, kati ya fedha hizo shilingi 930,094,043 zilikusanywa kutoka katika Mgodi wa *TML* kama mrabaha na ada ya ukaguzi ikiwa sawa na asilimia 85 ya mapato yatokanayo na uzalishaji wa Tanzanite na shilingi

164,134,243.88 sawa na asilimia 15 zilikusanywa kutokana na wachimbaji wadogo. Kwa mwaka 2018, wachimbaji wadogo pekee kwa sasa wanachangia zaidi ya bilioni 1.4 na uzalishaji umeongezeka kutoka kilo za Tanzanite 147.7 hadi kilo 781.2 kwa mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa mafanikio haya yanakuwa endelevu, Wizara imekwishakujenga jengo la wafanyabiashara wa madini yaani *brokers house* na inaendelea na ujenzi wa Kituo cha Pamoja (*One Stop Centre*) ndani ya ukuta unaozunguka machimbo ya tanzanite katika eneo la Mirerani. Wizara vilevile inaendelea kufunga *CCTV cameras* katika eneo hilo. Kwa sasa Wizara imeweka miundombinu ya umeme kuzunguka eneo la ukuta Mirerani. Uwekezaji huo wa Serikali utagharimu shilingi bilioni 4.2. Lengo la uwekezaji huo ni kuhakikisha kuwa shughuli zote zinazohusu biashara ya madini zinafanyika ndani ya ukuta, kulmarisha upatikanaji wa takwimu na kudhibiti utoroshaji wa madini ya Tanzanite.

Mheshimiwa Spika, kazi nydingine iliyotekelizwa na Wizara katika mwaka wa fedha 2018/2019 ni kukamilisha uandaaji wa Mwongozo wa Uongezaji Thamani Madini na Miamba, 2019, Tangazo la Serikali Na. 60/2019 liliotolewa tarehe 25 Januari. Lengo la mwongozo wake ilikuwa ni kuainisha viwango vya uongezaji thamani wa madini katika madini na miamba kabla ya kuruhusiwa kuyasafirisha nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madini inaendelea kusimamia vilevile udhibiti wa matumizi ya baruti ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa watumiaji wa baruti wanaingiza, wanatumia na kutunza baruti kwa usahihi ambapo vibali 146 vya kuingiza baruti nchini na leseni 6 za maghala ya kuhifadhiya baruti katika maeneo ya Geita na Lugoba vimetolewa. Aidha, jumla ya tani 32,398 za baruti zilitengenezwa migodini na vipande 3,725,645 vya fataki viliiingizwa nchini kwa ajili ya shughuli za uchimbaji na ulipuaji madini.

Mheshimiwa Spika, katika kuvutia uwekezaji, Wizara imeendelea kushiriki katika maonesho mbalimbali ya ndani na nje ya nchi. Mwezi Septemba, 2018, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Geita na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (*TanTrade*), ilishiriki kuandaa na kufanikisha maonesho ya kwanza ya teknolojia ya uchimbaji na uchenjuaji wa madini ya dhahabu yaliyofanyika Mkoani Geita. Maonesho hayo yalishirikisha kampuni 250 kutoka maeneo mbalimbali hapa nchini ambayo yalikuwa ni makampuni ya wachimbaji wakubwa na wachimbaji wadogo na wachenjuaji wa madini pamoja na wafanyabiashara wa madini. Maonesho hayo, pamoja na mambo mengine, yalilenga kuwawezesha wadau kutambua fursa za uwekezaji zillizopo katika Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, Wizara vilevile imeendelea kufanya mapitio ya Sera ya Madini ya Mwaka 2009 kwa lengo la kuihuisha ili iendane na mazingira ya sasa. Aidha, kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara ilifanikiwa kurekebisha Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali zikiwemo;

- (a) Sheria ya Madini Sura ya 123 (*Revised Edition 2018*);
- (b) Marekebisho ya Sheria ya Uwazi na Uwajikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia ya Mwaka, 2015; na
- (c) Miongozo wa Kuhakiki Uongezaji Thamani Madini au Miamba Nchini kabla ya Madini Kusafirishwa Nje ya Nchi, 2019 kwa Tangazo la Serikali Na.60/2019.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia ilifanya marekebisho katika Kanuni mbalimbali za Madini chini ya Sheria ya Madini Sura ya 123 kama ifuatavyo; Marekebisho ya Kanuni za Madini (Biashara ya Madini na Makinikia) 2018, Tangazo la Serikali Na. 138/2019; Marekebisho ya Kanuni za Madini (Ushirikishwaji wa Huduma na Bidhaa za Watanzania) 2018, Tangazo la Serikali Na. 139/2019; Marekebisho ya Kanuni za Madini (Uongezaji Thamani Madini) 2018, Tangazo la Serikali Na. 136/

2019. Vilevile, Wizara imetafsiri katika Lugha ya Kiswahili Kanuni za Utunzaji Mazingira kwa Wachimbaji Wadogo za Mwaka 2010, Tangazo la Serikali Na. 403/2010. Aidha, Wizara imekamilisha Rasimu za Kanuni za Masoko ya Madini, 2019 na Kanuni za Madini (Cheti cha Uasilia), 2019 ambapo rasimu hizi tayari zimekwishakuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kufanyiwa upekuzi na hatimaye kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, vilevile, mwezi Februari, 2019 Wizara kwa kushirkiana na Wizara ya Fedha na Mipango ilipitia Sheria mbalimbali zilizokuwa zinahusiana na masuala ya kodi

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka 2018/2019, Wizara imepokea na kukamilisha taratibu za ajira mpya kwa watumishi 14 kupitia Sekretarleti ya Ajira katika Utumishi wa Umma na watumishi watano kwa utaratibu wa uhamisho. Aidha, jumla ya watumishi 230 wamehama Wizara ya Madini kutoka iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini na watumishi 31 wamehamishiwa Tume ya Madini hivyo mpaka mwezi Machi, 2019, Wizara ya Madini ilikuwa na jumla ya watumishi 199.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kuwajenega uwezo watumishi wake katika fani mbalimbali ikiwemo Jiolojia, Uhandisi Migodi, Jemolojia, Utunzaji wa Kumbukumbu na Utafutaji wa Madini. Jumla ya watumishi 41 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu. Kati ya hao, watumishi 14 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu katika ngazi za: Astashahada, Shahada pamoja na Shahada za Uzamivu na watumishi 27 wamepata mafunzo ya muda mfupi kwenye fani za Jemolojia, Jiolojia, Uhandisi Migodi na Utunzaji Kumbukumbu.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa huduma ya lishe na chakula kwa watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI, ili kutekelezaji Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 2 wa mwaka 2006 na Mwongozo wa Kudhibiti UKIMWI katika

Utumishi wa Umma wa Mwaka 2007, pia Wizara imetoe elimu kuhusu Magonjwa Sugu yasiyoambukizwa.

Mheshimiwa Spika, moja ya malengo makuu ya Wizara ni kuimarisha na kuendeleza Mikakati wa Taifa na Mpango wa Kupambana na Rushwa. Katika kutekeleza lengo hilo, Wizara ilikamilisha uandaaji wa Mkakati wa Kupambana na Rushwa katika kipindi cha 2017/2022.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizotekeliza na Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini lengo kuu la utekelezaji wa mradi wa SMMRP kwa Awamu ya II ilikuwa ni kuboresha shughuli za uchimbaji madini nchini na kuhakikisha kwamba uzalishaji wa madini unakuwa wa tija kuchochea kasi ya ukuaji wa maendeleo na kupunguza umaskini. Katika kutekeleza lengo hilo, Wizara kupitia mradi huu imetekeliza shughuli zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, ukarabati Ofisi za Madini moja ya kazi zilizotekeliza na mradi huu ilikuwa ni ukarabati wa Ofisi za Madini. Ukarabati huu ulifanyika katika Ofisi za Madini Moshi na Nachingwea. Ukarabati katika Ofisi ya Madini Moshi na wa Ofisi ya Madini Nachingwea umekamilika kwa asilimia 100. Kukamilika kwa ukarabati katika Ofisi hizi kumeondoa uhaba wa nafasi za kufanya kazi kwa watumishi wa umma na kuongeza tija katika utoaji huduma kwa wateja. Wizara pia kupitia kupitia Mradi wa huu ilitekeleza ujenzi wa Vituo vya Umahiri saba ambavyo ni Bariadi, Musoma, Bukoba, Mpanda, Chunya na Handeni. Vituo hivi vyote viko katika hatua mbalimbali ya ujenzi ambapo kati ya hivyo vituo vya Bariadi, Musoma, Bukoba, Handeni na Jengo la Chuo cha Madini (Dodoma) umekamilika na ujenzi wa vituo vya Mpanda, Chunya na Songea upo katika hatua za mbalimbali za ukamilishaji.

Mheshimiwa Spika, lengo la vituo hivyo pamoja na mambo mengine, ni kutoa mafunzo yanayohusu madini kwa wachimbaji wadogo vilevile vitatumika kufanya maonesho ya madini na vifaa vitakavyotumika katika shughuli za uchimbaji madini. Aidha, kukamilika kwa ujenzi wa vituo hivyo

kutaleta faida mbalimbali ikiwemo uwepo wa takwimu za wachimbaji wadogo katika maeneo husika na upatikanaji wa taarifa sahihi za utoaji mafunzo na maarifa kwa Wachimbaji wadogo kupitia wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, vituo hivi pia vitakuwa na manufaa makubwa kwa wachimbaji wadogo wanaozunguka maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwapatia ajira vituo hivi vinatarajia kutoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu kuhusu maswali yanayohusu uchimbaji, uchenjuaji, biashara ya madini afya, usalama migodini, utunzaji wa mazingira, masuala ya kijamii pamoja na masuala mtambuka pia vituo hivi vitatoa huduma ya uchenjuaji wa madini kwa bei ndogo na nafuu na ambayo ni himilivu kwa wachimbaji wadogo. Ni kuwawezesha vile vile wachimbaji wadogo waweze kujifunza kwa vitendo ili baadaye na wao waweze kuwekeza kwa kusimika mitambo kama hii ambayo badala ya kutumia mitambo inayotumia zebaki katika uchenjuaji wa madini. Aidha, Serikali ya Tanzania ikiwa ni Mwanachama wa *Minemata Convention* ipo katika mchakato wa mwisho wa kupunguza ama kuzuia kabisa matumizi ya kemikali ya zebaki katika uchenjuaji wa madini ya dhahabu kwa kuwa kwa kiasi kikubwa kemikali hizi zimekuwa na athari mbaya kwa afya ya binadamu na mazingira kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kituo cha Lwamgasa ambacho pia kimejengwa mgodi wa mfano, wananchi wataweza kujifunza kwa vitendo namna bora ya uchimbaji wa kisasa ikiwa ni pamoja na utengenezaji wa mashimo ya uchimbaji madini *mining shaft and drift* bila kutumia magogo. Teknolojia hii itakuwa na manufaa yafuatayo:-

- (i) kupunguza kwa kiasi kikubwa ajali migodini kwa kutumia simenti kuimarisha ukuta;
- (ii) kurahisisha utoaji wa mbale mgodini;
- (iii) kuongeza maisha ya mgodi;

(iv) kupunguza athari za kimazingira kwa kutokukata miti hovyo; na

(v) kurahisisha ufungaji wa migodi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, vile vile vituo hivi ili viwe na tija, ufanisi pamoja na kufikia malengo yaliyokusudiwa, Wizara imeingia makubaliano na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) namna bora ya uendeshaji na usimamizi wa vituo hivi ikiwa ni pamoja na kutoza gharama nafuu kwa wachimbaji wadogo watakao waleta mbale ya madini ya dhahabu kwa ajili ya uchenjuaji. Kupitia wachenjuaji hao wadogo wa eneo husika, Serikali itaweza kujua kwa uhakika ni kiasi gani cha dhahabu iliyopatikana na hivyo kuweza kupata kodi na mrabaha halisi kutokana na wachimbaji wadogo hao. Aidha, mafunzo yatakayokuwa yanatolewa katika kituo hiki yataboresha namna ya uchimbaji na uchenjuaji wa kitaalam na kuongeza kipato cha wananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mradi wa SMMRP imenunua mtambo wa kuchoronga miamba (*Multipurpose Air Rotary Rig*) ambao umegharimu Dola za Marekani 1,128,947. Mtambo huo umekabidhiwa kwa STAMICO mwezi Desemba, 2018 kwa ajili ya matumizi ya biashara pamoja na kuwasaidia wachimbaji wadogo. Mtambo huu utatumika katika kufanya utafiti wa kina wa Kijiolojia. Utafiti huu utahusisha uchorongaji wa miamba ambapo taarifa zake zitatumika kujua wingi wa mashapo kwenye eneo husika, viwango vya mbale, ukubwa na umbali kutoka usawa wa ardhi kwa mashapo. Huduma hii itatolewa na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kwa bei nafuu kwa Wachimbaji Wadogo ambapo taarifa hizo zitawawezesha kujua kiasi gani cha mashapo kilichopo katika leseni zao.

Mheshimiwa Spika, kupitia kazi zitakazofanywa na mtambo huu, Serikali itanufaika kwa mambo yafuatayo:-

(i) kupata mapato kupitia kutoa huduma ya Uchorongaji;

- (ii) Kufanya Tafiti za kina kwa manufaa ya Taifa kupitia STAMICO;
- (iii) Kuongeza kipato kwa kiasi kikubwa kwa Wachimbaji Madini watakaopata huduma ya mtambo huu;
- (iv) Kuongeza pato la Taifa kutokana na Makusanyo yatakayotokana na Wachimbaji wanaofanya utafiti wa Kina.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia kupitia Mradi huo ilinunua magari yaliyogharimu Yen 14,722,940 sawa na fedha za Kitanzania 302,799,486 kwa ajili ya usimamizi wa shughuli za madini.

Mheshimiwa Spika, shughuli nyingine zilizotekelezwa na mradi ni pamoja na kugharamia uandaaji wa Mpango Mkakati wa Wizara wa kuendeleza Kituo cha Jemolojia Tanzania ambapo jumla ya shilingi 185,859,000 zilitumika; ununuvi wa Vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya Ofisi za Madini uligharimu shilingi 423,860,150.06 uandaaji wa Mwongozo wa Mazingira uliogharimu shilingi 176,000,000.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2018/2019 Wizara ilianda na kukamilisha Mpango Mkakati (*Strategic Plan*). Lengo la Mpango huo ni kutoa dira na mwelekeo wa Wizara kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2019/2020 hadi 2023/2024. Mpango huo ndio uliotumika katika kuandaa Mpango na Bajeti wa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizotekelezwa na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini. Wizara ya Madini inasimamia Taasisi ya Tume ya Madini; Taasisi ya Jiolojia ya Utafiti Madini Tanzania (GST), Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI); Chuo cha Madini (MRI), na Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC)

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la kuundwa kwa Tume ya Madini ni pamoja na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali yatokanayo na rasilimali madini kuimarisha ufuatiliaji

wa ukaguzi wa usalama, afya, mazingira, uzalishaji na biashara ya madini katika migodi midogo, ya kati na mikubwa, kudhibiti utoroshaji wa madini na kuendelea kuboresha mazingira ya uwezeshaji wananchi katika kunufaika na sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kinachoishia mwezi Machi, 2019 jumla ya kilo 27,550.9 za dhahabu zilizalishwa na kusafirishwa nje ya nchi kutoka katika Migodi Mikubwa na ya Kati. Migodi hiyo ni *Geita Gold Mining Ltd*, *North Mara Gold Mine Ltd*, *Pangea Gold Mine Ltd* (Buzwagi), Bulyanhulu Gold Mine Ltd, Shanta Mining Ltd (New Luika) na STAMIGOLD Biharamulo Mine. Aidha, kilo 2,214.9 za dhahabu zilizalishwa na wachimbaji wadogo, wachenjuaji na wafanyabiashara wa madini nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi tajwa karati 309,303.85 za madini ya almasi kilizalishwa katika Mgodi wa almasi wa Mwadui karati 3,352.9 katika Mgodi wa El Hilal na karati 4,747.45 kutoka katika wafanyabiashara wa almasi (*Dealers*). Pia, wachimbaji wadogo wa madini ya tanzanite wamezalisha tanzanite ghafi jumla ya kilo 768.75 tanzanite zilizokuwa zilizokatwa na kusafirishwa kiasi cha karati 87,389.02 na magonga kiasi cha kilo 13,146.07. Aidha, madini mengine ya vito kiasi cha kilo 534,728.48 kilizalishwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa makaa ya mawe jumla ya tani 603,325.40 zilizalishwa kwenye Mgodi wa Ngaka Kambas *Mining Investment* mkoani Ruvuma tani 7,370.69 katika Mgodi wa Kabulo – Songwe, tani 7,696.96 katika Mgodi wa Edenville. Aidha, tani 13,087,435.48 za madini ya ujenzi na tani 5,351,227 za madini mengine ya viwandani zilizalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kudhibiti Utoroshaji wa Madini Tume ya Madini kuitia Ofisi zake za mikoa na Maafisa Migodi Wakazi kwenye migodi ina wajibu wa kusimamia uzalishaji na mauzo ya madini nchi nzima. Utekelezaji wa wajibu huu unasaidia kuimarisha udhibiti wa utoroshaji na biashara

haramu ya madini. Katika kuhakikisha kuwa rasilimali madini ambayo tumejaliwa kuwa nayo inakuwa na manufaa kwa Watanzania wote, Tume ya Madini kwa kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama pia imekuwa ikifanya udhibiti wa utoroshaji wa madini.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Februari, 2019 jumla ya karati 66.60 za madini ya almasi yenye thamani ya Dola za Marekani 34,782 Jijini Dodoma; gramu 77.20 za madini ya dhahabu zenye thamani ya shilingi 6,363,995.90 mkoani Tabora; kilo 75,957 za madini ya vito yenye thamani ya Dola za Marekani 1,795,687.8 Jijini Dar es Salaam, na kilo tano za madini ya dhahabu yenye thamani ya shilingi 389,789,712 mkoani Geita, gramu 11,445.52 za madini ghafi na karati 1,351 ya vito jumla ya shilingi 206,576,346.05 mkoani Arusha, tani 3.7 za madini ya aina ya *rhodelite* zenye thamani ya Dola za Marekani 50,162.46, mkoani Morogoro; kilo 319.594 za madini ya dhahabu yenye thamani ya Dola za Marekani 11,731,814 mkoani Mwanza yote haya yalikamatwa kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, madini yaliyokamatwa katika Mikoa ya Dodoma, Tabora, Mwanza na Dar es Salaam yalitafishwa na Serikali. Aidha, Madini yaliyokamatwa Mikoa ya Arusha, Morogoro na Geita yapo katika hatua mbalimbali za uchunguzi. Mpaka mwezi Machi 2019, madini ambayo yalikwishatafishwa yaliwu na thamani ya jumla ya shilingi 6,363,995.95 na Dola za Marekani 13,562,284.59.

Mheshimiwa Spika, vilevile kudhibiti utoroshaji wa madini nchini, ulinzi umeimarishwa katika maeneo yote ya uzalishaji wenye migodi mikubwa ya kat i kwa kuweka Maafisa Madini Wakazi yaani *Mines Residents Officer (MRO)*. Lengo la kuweka Maafisa hawa ni kusimamia na kuwasilisha taarifa sahihi za uzalishaji wa madini na kudhibiti mianya ya utoroshaji wa madini. Aidha, katika maeneo ya viwanja vya ndege na mipakani wamewekwa wasimamizi maalum kwa ajili ya kusimamia utoroshaji wa madini usiweze kuendelea. Nitoe wito kwa Watanzania wote kufanya shughuli za madini kwa kuzingatia Sheria za nchi kwa kuzingatia kanuni za nchi. Lakini

nitoe wito vilevile kwa wachimbaji wadogo watambue kuwa rasilimali hizi ni zetu wote na wao wawe sehemu ya udhibiti wa utoroshaji madini

Mheshimiwa Spika, siku za hivi karibuni kumekuwepo na matukio ya watumishi wasiokuwa waaminifu kwa kushirikiana na wachimbaji na wafanyabiashara ya madini wasio waaminifu kushiriki katika kuibia Serikali mapato kupitia kuwasilisha taarifa zisizosahihi za uzalishaji wa madini. Katika kuhakikisha kuwa tunatokomeza tabia hii isiyo ya Kizalendo ya Serikali kupoteza mapato, Serikali imeendelea kuchukua hatua thabiti za kinidhamu ikiwemo kuwasimamisha kazi ili kupisha uchunguzi na kuwfakisha mahakamani wale wanaobainika kukiuka sheria.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Madini vile vile iliendelea na utoaji wa leseni mbalimbali za madini ambapo hadi kufikia Machi, 2019 jumla ya leseni 13,180 ziliidhinishwa kwa ajili ya kupewa leseni za utafutaji madini, uchimbaji mdogo, uchimbaji wa kati, uchenjuaji madini na biashara ya madini. Kati ya maombi hayo, maombi ya leseni za uchimbaji wa kati wa madini zilikuwa leseni 74 utafutaji wa madini leseni 866, uchimbaji mdogo leseni 9,728; uchenjuaji wa madini leseni 39; leseni kubwa ya biashara madini 736; na leseni ndogo ya biashara ya madini 1,734. Kati ya maombi hayo yaliyoidhinishwa, jumla ya leseni 4,831 zimekwishakutolewa katika mchanganuo wa leseni nillioutaja hapo juu.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Madini vile vile imeendelea na zoezi la kuhuisha taarifa kuhusu leseni na kubaini leseni zenyе mapungufu pamoja na kuandaa Hati za Makosa kwa leseni zilizobainika kuwa na mapungufu. Mchanganuo wa Leseni zilizofanywa mapitio ni kama ifuatavyo: Leseni za Uchimbaji Mkubwa leseni 07 ambapo zimeandaliwa Hati za Makosa; na Leseni za uchimbaji wa Kati leseni 271 nazo zimeandaliwa hati za makosa ambapo 66 tayari zimekwishaandikiwa Hati za Makosa; Leseni za Utafutaji wa Madini leseni 1,509 ambapo 200 zimeandikiwa Hati za Makosa na Leseni za Uchimbaji Mdogo 16,356 na kati yake 863 zimeandikiwa Hati za Makosa. Maeneo yote

yatakayofutwa yatabaki wazi kwa ajili ya uwekezaji wenye utayari na uwezo wa kuyaendeleza ikiwemo wachimbaji wadogo. Nipende kutoa wito kwa wamiliki wote wenye leseni za madini hapa nchini kuzingatia Sheria ya madini Kanuni na taratibu zinazosimamia Sekta ya Madini na shughuli zao ili kuondoa usumbufo usiokuwa wa lazima wa kunyang' anywa maeneo kwa kufutiwa leseni zao.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Tume ya Madini ilifanya ukaguzi katika migodi ya Sekenke *One*, Nabii Eliya VAT *Leaching Plant* iliyoko mkoa wa Singida; migodi ya Pamoja Mining, Nyarugusu Mining iliyoko Geita; mgodi wa zamani wa *Resolute Tanzania Limited*, eneo la uchimbaji madini la wachimbaji wadogo Mahene mkoani Tabora; Maeneo ya Uchenjuaji wa dhahabu mkoani Tabora, na mgodi wa dhahabu wa chini ya ardhi (*Underground Mine*) wa Bulyanhulu. Kaguzi hizi zote zilibaini upungufu katika kusimamia masuala ya kiusalama, afya na mazingira na kuwepo kwa mashimo na maeneo hatarishi yenye kemikali ambazo ni hatarishi kwa afya za watu.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mapungufu mbalimbali yaliyobainika, Tume ya Madini ilitoa maelekezo ya kufanyika kwa marekebisho katika migodi hiyo kama ifuatavyo: kufukiwa kwa kuweka vizuizi katika mashimo ya wazi na yasiyotumika; kuzuia wachimbaji kuhifadhi na kuuza baruti bila ya kuwa na vibali; kuhakikisha kuwa wafanyakazi wote katika maeneo ya uzalishaji madini wanatumia Vifaa Kinga *Protection gears* ambazo zitawasaidia kujikinga na madhara.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Madini pia iliendelea kusimamia na kuhakikisha kuwa kampuni za uwekezaji katika Sekta ya Madini zinatumia bidhaa zinazozalishwa na huduma zinazopatikana hapa nchini Katika kufanikisha sharti hili, waombaji wote wenye leseni kubwa na za katil za uchimbaji wa madini (*Special Mining License -SML* na *Mining License - ML*) walitakiwa kuwasilisha Mipango ya kuhusu kutumia bidhaa zinazozalishwa na kutumia huduma zinazotolewa na makampuni ya kitanzania (*Local Content Plan*) kwa Tume ya Madini kama kigezo muhimu cha kupata leseni.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2018/2019 Tume ya Madini ilipitia Mipango 55 ya waombaji wa leseni za utafutaji, uchimbaji na uchenjuaji wa madini ili kuona kama mipango hiyo inakidhi matakwa ya Sheria. Kat i ya Mipango hiyo, Mipango 42 iliidhinishwa. Mipango 13 ilibainika kuwa dosari na mapungufu na ilirejeshwa ili wahusika waweze kufanya maboresho ili waweze kukidhi mahitaji husika.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Utafiti wa Madini Tanzania (GST), jukumu kubwa la Taasisi ya (GST) ni kufanya tafiti za jiosayansi kwa lengo la kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Madini. Kupitia tafiti hizi taarifa mbalimbali za jiolojia na uwepo wa madini nchini zinaandalowi, kwa lengo la kuhamasisha uanzishwaji wa migodi hapa nchini unakuwa wenyе tija. GSTina jukumu la kuratibu majanga asili ya jiolojia kama matetemeko ya ardhi, milipuko ya volkano pamoja na maporomoko ya udongo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, *GST* ilikadiriwa kukusanya maduhuli ya shilingi 371,000,000 kutoka kwenye vyanzo vyake ambavyo ni tozo za ramani na machapisho ya jiosayansi, tozo za huduma za maabara, na ada za ushauri elekezi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 jumla ya shilingi milioni 432.2 zilikusanya. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 117.06 ya lengo lillokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, *GST* ilikamilisha ugani wa jiolojia na jioskemia katika QDS 202 iliyopo Kibaha mkoani Pwani na QDS 49 iliyopo katika katika Wilaya ya Maswa, pamoja na ramani zipo katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji. Matokeo ya awali ya utafiti huo yanaonesha kuwa kwenye QDS 202 kuna madini ya chokaa hasa katika maeneo ya Mkulazi yenyе ubora wa asilimia 15 hadi 39. Aidha, katika QDS 49 kuna viashiria vya uwepo wa madini ya dhahabu katika eneo la Buhangija, madini ya vito *amethyst* katika maeneo ya Chuli, Sayusayu, Masanwa na Sulu, madini ya Opal na chokaa katika eneo la Isagenghe.

Mheshimiwa Spika, *GST* kwa kushirikiana na Taasisi ya Jiolojia ya China, *China Geological Survey – CGS* ilikamilisha

utafiti wa jikemia kwa skeli kubwa katika Mkoa wa Mbeya na skeli ndogo katika nchi nzima. Utafiti huu ulipelekea kutengenezwa kwa atlasi ya nchi nzima na ya Mkoa wa Mbeya. Atlasi na taarifa hizi zitasaidia kuongeza uelewa juu ya madini yanayopatikana katika eneo lilihofanyiwa utafiti. Taarifa hizi pia zinaweza kutumika katika sekta za kilimo, maji, mazingira na masuala ya mipango mijii.

Mheshimiwa Spika, vilevile GST kwa kushirikiana na Taasisi ya Jiosayansi na Rasilimali Madini ya Jamhuri ya Watu wa Kenya ilikamilisha utafiti wa jiolojia katika maeneo ya QDS 257, 312, 313, 319 na 320 yaliyoko katika Wilaya za Momba, Songwe na Tunduru. Aidha, kupitia ushirikiano huo, GST ilikamilisha utafiti wa jiofizikia kwa kutumia ndege (*High-resolution airborne geophysical survey*) katika maeneo ya QDS 312 na 313. Uchunguzi wa sampuli katika maabara, uchakataji wa taarifa na uchoraji wa ramani na taarifa zake unatarajiwa kukamilika mwaka wa fedha ujao.

Mheshimiwa Spika, tafiti maalum *GST* ilifanya tafiti maalum ikiwemo utafiti wa jiolojia ili kubaini sababu za kutitia na kutokea kwa mashimo makubwa katika eneo la Kitopeni, Itigi mkoani Singida. Utafiti ulibaini uwepo wa uwazi uliosababishwa na kuyeyukwa kwa miamba iliyoundwa na madini ya jasi na na udongo wa eneo hilo ni tifutifu ambao umechangia kubomoka kiraishi baada ya kunyonyolewa maji mengi ya mvua.

Mheshimiwa Spika, GST ilikamilisha ukusanyaji na uchakataji wa takwimu za kutoka maeneo mbalimbali katika kila mkoa na kuchora ramani zinazoonesha madini katika mikoa na wilaya zote za Tanzania Bara. Lengo la zoezi hilo lilikuwa ni kuboresha Kanzidata ya Taifa ya Madini na Kitabu cha Madini yanayopatikana Tanzania na matumizi yake.

Mheshimiwa Spika, GST pia imeendelea na Huduma za Maabara na kuratibu majanga ya asilia hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la STAM/CO imeendelea kutekeleza majukumu yake kama

yalivyoainishwa katika Hati ya Kurekebisha Uanzishwaji wake. Majukumu hayo ni pamoja na kuwekeza kwenye shughuli za uchimbaji na utafutaji madini, kuwekeza katika uchenjuaji, uongezaji thamani na uuzaaji madini, na kutoa huduma na ushauri wa kitaalam na kiufundi katika Sekta ya Madini ikiwemo wachimbaji wadogo kwenye nyanja za jiolojia, uhandisi, mazingira na uchorongaji miamba.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Makaa ya Mawe Kabulo, Shirika linaendelea na uchimbaji na uuzaaji wa makaa ya mawe katika mradi wa Kabulo uliopo mkoani Songwe. Kwa sasa uzalishaji unafanyika katika eneo la Kabulo na ulianza mwezi Novemba, 2018. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2019, *STAMICO* imefanikiwa kuchimba jumla ya tani 22,119 za makaa ya mawe ambapo tani 7,664.8 zimeuzwa katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, *STAMIGOLD* ni kampuni tanzu ya Shirika la Madini nchini na inayomilikiwa na *STAMICO* na Msajili wa Hazina. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2019 mgodi wa *STAMIGOLD* umezalisha wakia 9,879.8 za madini ya dhahabu na wakia 1,346.92 za madini ya fedha yenye jumla ya Dola za Marekani 12,353,394.4 sawa na shilingi bilioni 28.267. Mauzo hayo yameuwezesha mgodi kulipa mrabaha wa shilingi bilioni 1.7 na ada ya ukaguzi ya shilingi milioni 282.7 kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2018/2019, Shirika lilipata mafanikio kukamilika ukarabati wa kinu cha kusagia makaa ya mawe kwa lengo la kuongeza thamani ya makaa yanayochimbwa katika Mgodi wa Kabulo ili kukidhi mahitaji ya soko, kupata zabuni ya uchorongaji miamba kwa kutumia mtambo kwenye Mgodi wa dhahabu wa *Buckreef* kiasi cha mita 1,719 na kukamilikaa ukarabati wa nyumba nne za makazi katika Mradi wa Kiwira pamoja na matengenezo ya magari mawili ya mizigo yatakayotumika kubeba makaa ya mawe kutoka mgodini hadi eneo la kuuzia.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 shirika limefanikiwa kufanya biashara na kupata faida ya shilingi bilioni 1 ikiwa ni miaka mingi tangu shirika lianzesha.

kujijendesha kibiashara. Gawio hilo limetokana na mapato ya vyanzo vyake nya ndani pamoja na mapato ya kampuni tanzu ya Shirika ya kuchimba dhahabu ya Biharamulo STAMIGOLD ambapo kwa mwaka 2018 shirika liliweza kutengeneza faida na hivyo kutoa gawio kwa Serikali..

Mheshimiwa Spika, nipende kuwahakikishia watanzania kuwa shirika litaendelea kutoa gawio kwa Serikali kwa kuongeza wigo wa vyanzo vyake nya mapato. Aidha, ni matumaini ya Wizara kuwa kufuatia hatua zinazoendelea kuchukuliwa, STAMICO itaendelea kuimarika na kuwa Shirika la Umma litakaloendesha miradi yake kwa weledi na kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Madini lengo kubwa la kuanzishwa Chuo cha Madidi Dodoma ni kutoa mafunzo ya Ufundji Sanifu katika Sekta ya Madini ili kuzalisha wataalam wa kada ya kati. Chuo kina kampasi mbili ambazo ni kampasi ya Dodoma na kampasi ya Nzega. Mafunzo yatolewayo na Chuo cha Madini Dodoma yamegawanyika katika aina kuu tatu. Mafunzo ya muda mrefu, mafunzo ya muda mfupi pamoja na mafunzo maalum yanayoandaliiwa kulingana na mahitaji ya wadau.

Mheshimiwa Spika, fani zinazofundishwa na Chuo cha Madini ni pamoja na Jiolojia na Utafiti wa Madini, Sayansi za Mafuta na Gesi, Uhandisi Uchimbaji Madini, Uhandisi Uchenjuaji Madini, Uhandisi wa Mazingira na Usimamizi wa Migodi; na Upimaji Ardhi na Migodi. Mafunzo haya yanatolewa kwa mfumo wa umahiri ambapo msisitizo mkubwa ni kutekeleza mafunzo kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, chuo kwa mwaka wa fedha 2018/2019, kimedahili jumla ya wanafunzi 600 kwa kampasi zote Dodoma na Nzega sawa na ongezeko la asilimia 11.9 ikilinganishwa na wanafunzi 536 waliodahiliwa mwaka 2017/2018. Kati ya hao, wanafunzi 503 walidahiliwa kampasi ya Dodoma na 97 kampasi ya Nzega. Wanafunzi 91 waliodahiliwa katika fani za Jiolojia na Utafutaji Madini, 99 katika Uhandisi Uchimbaji Madini, 144 katika usimamizi wa

migodi, wanafunzi 99 katika Sayansi za Mafuta na Gesi na 104 katika upimaji wa Ardhi na Migodi.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2018/19, Chuo cha Madini kilikadiriwa kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 268,000,000. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2019 chuo kilikuwa kimekusanya jumla ya shilingi 242,603,540 sawa na asilimia 90.52 ya lengo. Makusanyo haya yalitokana na ada ya mafunzo, usajili na malazi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2018/2019 hadi tarehe 31 Machi, 2019, Chuo kimeendelea kuboresha miundombinu yake ikiwemo ukarabati wa majengo na mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Ukarabati umefanyika katika majengo ya madarasa, mabweni, nyumba za watumishi, pamoja na jengo la utawala ikihusisha pia kufanya ukarabati katika mifumo ya umeme, maji safi na maji takatika Kampasi ya Nzega.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Chuo kilifanikiwa kupata usajili kamili wa kampasi ya Nzega kwenye Baraza la Taifa la Mafunzo ya Ufundji NACTE na kupewa namba ya usajili REG/SAT/041. Usajili huu umekifanya Chuo cha Madini kampasi ya Nzega sasa kutambuliwa na NACTE kama kituo cha kutolea mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika fani za Madini, Mafuta na Gesi.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Jemolojia Tanzania, majukumu ya Kituo cha Jemolojia Tanzania ni pamoja na kutoa mafunzo ya muda mrefu stashahada katika fani za usanifu wa madini ya vito na teknolojia ya kutengeneza vito, utambuzi, ukataji na kutengeneza vito, na kutoa huduma za kusanifu madini ya vito, miamba, utengenezaji wa bidhaa za mapambo na urembo pamoja na kutoa mafunzo ya muda mfupi katika fani ya ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 chuo kilidahili jumla ya wanafunzi 26 katika fani za usanifu wa madini ya vito, utambuzi wa madini ya vito na usonara. Aidha, katika kipindi husika jumla ya wanafunzi 23

wamehitimu mafunzo ya ukataji na ung'arishaji madini ya vito kwa ngazi ya cheti. Kituo pia kilizalisha bidhaa zitokanazo na miamba, madini ya vito na usonara kama ifuatavyo; vinyago 64, hereni 72, vikuku 40, miti ya mawe 15, mikufu 24, vidani 50, *beads* kilo 21 na vito vilivyokatwa karati 35.35, pamona na vinyago vinavyotokana na miamba.

Mheshimiwa Spika, Mpango na Makadirio na Matumizi ya mwaka wa fedha 2019/2020. Uandaaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2019/2020 umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2020/2025. Mpango wa pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano mwaka 2020/2025, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa mwaka 2015 na 2020, Sera ya Madini ya Mwaka 2009, Sheria ya Madini, maagizo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa, muongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2019.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2019/2020, Wizara imejiwekea maeneo yafuatayo ya kipaumbele; kuimarishe ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali yatokanayo na rasilimali madini, pili uanzishwaji na usimamizi wa Masoko ya Madini, kudhibiti utoroshwaji wa madini, kuendeleza uchimbaji mdogo na wa kati wa madini, kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini, kuimarishe ufuatiliaji na ukaguzi wa usalama, mazingira na uzalishaji wa madini katika migodi midogo ya kati na mikubwa, kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini, kuboresha mazingira ya kuwawezesha wananchi kunufaika na rasilimali za madini; na kuendeleza rasilimali watu na kuboresha mazingira ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara inapanga kukusanya shilingi 473,814,268,992 ikilinganishwa na shilingi 310,598,007,000 kwa Mwaka 2018/2019 ongezeko hili ni sawa na asilimia 52.6. Mikakati itakayotumika kufika lengo hilo ni pamoja na kusimamia masoko ya madini, kuimarishe ukaguzi wa migodi mikubwa, ya kati na midogo ili kupata taarifa sahihi za uwekezaji, uzalishaji, mauzo, tozo na kodi mbalimbali. Kudhibiti utoroshwaji wa madini katika maeneo yote nchini kuimarishe ukaguzi wa madini ya ujenzi na

viwandani, kufuatilia taarifa za ununuzi na uuzaji kwa wafanyabiashara wa madini na kufuatilia wadaiwa wa tozo mbalimbali za madini kwa mujibu wa Sheria kwa wakati pia kudhibiti uchimbaji na uchenjuaji haramu wa madini, na kuboresha na kuimarisha Mfumo wa utoaji wa leseni na utunza wa taarifa zake.

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa masoko na usimamizi wa masoko ya nchini. Ili kuhakikisha kuwa wachimbaji wadogo wananaufaika na shughuli za uchimbaji madini, Wizara kwa kushirikiana na ofisi za wakuu wa mikoa kote nchini imeanzisha na inaendelea zoezi la kuanzisha masoko na minada ya Madini kote nchini. Jitihada hizi ni kutatua tatizo la muda mrefu la ukosefu wa masoko ya madini hapa nchini. Vilevile, masoko hayo yatarahisisha upatikanaji wa takwimu sahihi za madini yanayouzwa katika masoko na ukusanyaji wa tozo za Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti utoroshaji wa madini nchini, Wizara itaendelea kuimarisha ulinzi na usimamizi katika maeneo yote ya uzalishaji. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine zenyeye dhamana ya ulinzi na usalama itaendelea kuhakikisha kuwa katika maeneo ya viwanja vya ndege, bandari na mipakani na maeneo yote ambao ni watu wanaweza kusafiri nje ya nchi usimamaizi madhubuti ili kudhibiti mianya ya utoroshaji.

Mheshimiwa Spika, uendeleza wa wachimbaji wadogo, katika jitihada za kuwaendeleza wachimbaji wadogo wa madini nchini, Wizara itafanya yafuatayo. Kwanza kuwapatia maeneo yanayofaa wachimbajii, kutoa huduma nafuu za kitaalam kwa wachimbaji wadogo ikiwa ni pamoja na kuwafahamisha kuhusu uwepo wa mashapo, kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo kuhusu uchimbaji wa madini wenye tija kuititia Vituo vya Umahiri na vituo vya Mfano vinavyojengwa, na kuendelea kuwapatia elimu na kuwakumbusha umuhimu wa kufanya shughuli zao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu zinazosimamia Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza thamani madini, Wizara itahamasisha uwekaji na uwekezaji wa ndani na nje kujenga viwanda vya kuchakata madini hapa nchini kama vile viwanda vya uchenjuaji na uyeyushaji wa madini ya metali yaani *Smelters & Refineries*. Itasaidia pia kuongeza mapato na ajira kwa Watanzania na kukuza kwa matumizi ya teknolojia.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa shughuli za uchimbaji wa madini hapa nchini zinafanyika kwa kuzingatia taratibu za usalama, afya, na utunzaji wa mazingira, Wizara itaendelea kuimarisha na kutekeleza mikakati mbalimbali iliyojivekea. Katika mikakati hiyo ni pamoja na kufanya kaguzi za mara kwa mara na kufuatilia utekelezaji wa kasoro za kiusalama, afya na mazingira zitakazobainika wakati wa ukaguzi, kuhakikisha kuwa migodi mikubwa na ya kati inaweka Hati Fungani ya Uhifadhi wa Mazingira, kusimamia mipango ya ufungaji migodi, kuhakikisha kuwa migodi yote ya uchimbaji mdogo inakuwa na Mpango wa Utunzaji Mazingira na ambayo inakidhi matakwa ya kisheria, kusimamia utekelezaji wa Mkataba wa Minamata wa kupunguza na kuzuia matumizi ya zebaki katika uchenjuaji wa madini kwa kusimamia matumizi ya teknolojia rafiki yanayozalisha na migodi mikubwa, ya kati na midogo. Aidha, vilevile Wizara itaimarisha ushirikiano na Taasisi nyingine za Serikali kwa kuhusisha usimamizi wa masuala ya afya na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya madini, Tanzania ni moja ya nchi iliyobarikiwa kuwa na madini mengi na yenye thamani. Uwepo wa utajiri wa madini haya unatoa fursa mbalimbali za uwekezaji. Fursa hizo zinapatikana katika mnyororo mzima wa madini huhusisha shughuli za utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji na biashara ya madini. Katika kuhamasisha na kutangaza fursa hizi, Wizara itaendelea kushirikiana na Balozi zetu zote duniani zilizopo nchi mbalimbali pamoja na Kituo cha Uwekezaji Tanzania T/C. Wizara pia itashiriki kwenye makongamano na mikutano mbalimbali inayohusu shughuli za madini ndani na nje ya nchi.

Wizara Vilevile, itahakikisha upatikanaji wa taarifa za kijiosayansi kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, Ushiriki wa Watanzania katika shughuli za Madini (*Local Content*) Wizara itaendelea kusimamia na kuhakikisha kuwa kampuni za uwekezaji katika Sekta ya Madini zinafuata Sheria ya Madini ambayo inaelekeza kampuni zote zinazoomba leseni za utafutaji na uchimbaji wa madini nchini kuwa na mpango wa matumizi ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini. Lengo la takwa hilo la kisheria ni kuhakikisha kuwa kampuni hizo zinatumia malighafi na bidhaa zinazozalishwa hapa nchini na huduma mbalimbali zinazotolewa na watanzania pamoja na kampuni.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu ipasavyo, Wizara itahakikisha inajenga ujuzi wa watumishi kwenye nyanja mbalimbali zikiwemo Uhandisi Migodi, na uongezaji thamani madini ili kuongeza tija na ufanisi katika utendaji kazi wao. Vilevile, Wizara itaboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kununua vitendea kazi mbalimbali pamoja na kuboresha ustawi wa watumishi. Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu juu ya afya bora hususan kwa watumishi wanaoishi na virusi vya ugonjwa wa UKIMWI waliojitokeza. Wizara pia itaendelea kutoa elimu mahali pa kazi ili kuzuia maambukizi mapya ya ugonjwa wa UKIMWI na Magonjwa Sugu yasiyoambukiza. Aidha, elimu itatolewa kuhusu rushwa na madhara yake katika utendaji wa kazi wake. Pia, kutohana na upungufu wa watumishi uliopo kwenye kada mbalimbali, Wizara itaendelea kufuatilia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kupata watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, sambamba na vipaumbele vya Wizara iliyojiveke, Wizara itaendelea kutekeleza Mradi wa usimamizi endelevu wa rasilimali madini ili kutimiza lengo lake la kuboresha manufaa kijamii na kiuchumi yatokanayo na uchimbaji wa madini kwa kuimarisha zaidi sehemu ya miradi ya kiuchumi na hivyo kuhakikisha ukuaji wa uchumi kwa maendeleo ya nchi yetu unakuwa wenye tija.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2019/2020 Tume ya Madini itatekeleza shughuli zifuatazo, kuimarisha shughuli za ukusanyaji wa mapato ya Serikali yatokanayo na rasilimali madini, kuimarisha ukaguzi wa usalama, afya, mazingira na uzalishaji wa madini katika migodi midogo, ya kati na mikubwa na kusimamia shughuli za uzalishaji katika mitambo ya uchenjuaji wa madini; kuendelea kuboresha mazingira ya kuwawezesha wananchi kunufaika na rasilimali madini, kuimarisha udhibiti wa utoroshwaji wa madini, kuimarisha usimamizi wa biashara ya madini na kushughulikia migogoro inayotokana na shughuli za madini.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Madini itaboresha mfumo wa kielektroniki wa kutoa wa leseni pamoja na taarifa zake.

Mheshimiwa Spika, shukrani, mafaniko yaliyofikiwa katika kuendeleza sekta ya madini yantokana na michango inayoendelea kutolewa na wadau mbalimbali. Kipekee nimshukuru Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo Mbunge na Naibu Waziri Madini kwa namna anavyonipa ushirikiano katika kusimamia Sekta ya Madini. Hakika nikiri kuwa tangu tulivyochaguliwa wote kama Manaibu Waziri wa Wizara hii, na kwa sasa kama Naibu Waziri wangu, amekuwa na mchango mkubwa sana katika kusimamia Sekta hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba nimshukuru sana Prof. Simon Samwel Msanjila, Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini kwa namna anavyosimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, niwashukuru Wenyezeti wa Tume ya Madini Profesa Idriss Kikula, Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini Profesa Shukrani Manya na Makamishina wote wa Tume kwa kusimamia kwa umakini uendeshaji wa Tume.

Kipekee, nawashukuru sana Wakuu wa Vitengo; Wenyezeti wa Bodi zilizo chini ya Wizara, Viongozi na Taasisi na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Madini kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia na kujituma kwao katika kuhakikisha kuwa jukumu la Wizara ya Madini na lengo lake linafikiwa bila vikwazo vyovyote.

Mheshimiwa Spika, vilevile, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru washirika wetu wote wa maendeleo, wamekuwa bega kwa bega pamoja nasi kutekeleza mipango yetu ya Sekta ya Madini. Washirika hao wa maendeleo wanajumuisha; Benki ya Dunia, Serikali za Jamuhuri ya Watu wa China, Serikali ya Jamuhuri ya Watu wa Korea ya Kusini, Misri na Australia. Serikali itaendelea kushirikiana na wadau hawa katika kutekeleza majukumu haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukrani zangu za pekee na za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Bukombe ambao kwa muda wote wameendelea kuniamini na kunipa ushirikiano wakati natekeleza majukumu haya. Napenda niwaahidi watu wema hawa wa Bukombe kuwa nitatumia kipaji nilichopewa na Mwenyezi Mungu, nitatumia nguvu zangu nilizonazo kuwatumi kwa nguvu zangu zote na kamwe sitawaangusha na ninawaomba tuungane tujenge Bukombe yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitamshukuru kwa dhati kabisa mke wangu mpenzi Benadetha Clement Biteko pamoja na watoto wangu Elshadai, Elvin, Elis, Abigael, Amon, Abishai na Amos kwa kunivumilia, kuniunga mkono na kuniombea kwa Mwenyezi Mungu ili niweze kutekeleza majukumu niliyopewa na Mheshimiwa Rais katika kujenga na kutetea maslahi ya Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu ya Wizara ya Madini Mwaka 2019/2020, naomba Bunge lako Tukufu liridhie na kuitisha makadirio ya Jumla ya shilingi bilioni 49,466,898,200 kwa ajili ya Matumizi ya Wizara na Taasisi zake Mwaka 2019/2020 kwa mchanganuo wa Bajeti kama ifuatavyo:-

(i) Bajeti ya Maendeleo ni shilingi bilioni 7,039,810,200 ambazo ni fedha za ndani.

(ii) Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ni shilingi bilioni 42,427,088,000, ambapo shilingi bilioni 16,473,825,000 ni kwa

ajili ya mishahara na shilingi bilioni 25,953,263,000 ni Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi, Naibu Spika, Wenye viti wa Bunge na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, kabla sijahitimisha, kwa kuwa nilichosoma ni muhtasari naomba hotuba nzima inakiliwe kwenye kumbukumbu za Bunge (*Hansard*) kama ilivyowasilishwa kwenye hati ya kuweka mezani. Hotuba nzima pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara ya Madini ya “www.madini.go.tz”

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa hotuba nzuri na kwa kutumia muda wako vizuri. Sasa namuomba nimuite Mheshimiwa Mwenye viti wa Kamati ya Nishati na Madini, kwa niaba yake Mheshimiwa Mariam Ditopile karibu una si zaidi ya nusu saa.

MHE. MARIAM D. MZUZURI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:

Mheshimiwa Spika, nashukuru, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenye viti Mungu, mwangi wa rehema kwa kujaalia amani, utulivu na upendo wa Nchi yetu lakini binafsi kunijaalia uzima, uhai na afya kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa niaba ya Kamati yangu na kuwasilisha taarifa hii. Naomba taarifa hii yote iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 99 (9) na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Kuhusu

Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matakwa ya kanuni, Kamati ilifanya kazi kuu mbili ambazo ni:

- (i) Kutembelea na Kukagua Utekelezaji wa Miradi iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa fedha 2018/2019 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016 na
- (ii) Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii imagawanyika katika sehemu tatu; sehemu ya kwanza ni utangulizi, ya pili inahusu uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na sehemu ya tatu inahusu Maoni na Ushauri wa Kamati pamoja na hitimisho.

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2018/2019; kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayotekelvezwa chini ya Wizara ya Madini. Ziara hizo zilifanyika katika Mikoa ya Dodoma na Ruvuma. Lengo la ziara ikiwa ni kujionea Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, miradi iliyokaguliwa ni ifuatayo:-

- (i) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Utawala katika Chuo cha Madini Dodoma (*MR*);

(ii) Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Madini katika eneo la Mtumba-Dodoma; na

(iii) Mradi wa Ujenzi wa kituo cha Umahiri Songea kwa maana ya Songea *Centre of Excellence*.

Mheshimiwa Spika, Maelezo na Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ni kama inavyoonekana katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; kufuatia hali halisi wakati wa ukaguzi wa miradi, kamati inatoa ushauri kwamba, Mikataba ya Ujenzi wa majengo ya Wizara ya Madini na Taasisi zake unapaswa kuzingatia ubora wa majengo pamoja na hali halisi ya utekelezaji wa miradi kwani Kamati imebaini kuwa Serikali inatoa muda mfupi sana kwa wakandarasi na kusababisha mikataba kuongezwa muda wa utekelezaji mara kwa mara hivyo kuathiri utekelezaji, ufanisi na ubora wa kazi za ujenzi wa miradi. Pia Serikali inapaswa kuendelea kuwasimamia wakandarasi wanaopewa kutekeleza miradi mbalimbali ipasavyo kwani baadhi ya wakandarasi hawana nguvu kazi ya kutosha hivyo kusababisha kuzorota kwa utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara ichukue hatua za haraka kuanisha maeneo yanayofaa kuzalisha kokoto katika Mji wa Songea na kutoa leseni kwa sekta binafsi ili kuwezesha ukuaji wa sekta ya ujenzi katika Mji huo. Kamati ilijiuliza ikiwa Wizara ilikosa kokoto kipindi cha ujenzi, Je hali ikoje kwa wananchi wa kawaida? Hivyo ni Rai ya Kamati kuwa Wizara iharakishe kutatua changamoto hiyo katika Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti pamoja na maoni na ushauri wa kamati kwa mwaka wa fedha 2018/2019; Tume ya Madini imeendelea na usimamizi wa uzalishaji na biashara ya madini nchini. Kwa kipindi cha Mwezi Julai, 2018 hadi Februari 2019, Tume ilikusanya jumla ya Shilingi bilioni 218.45 sawa na asilimia 106 ya lengo la miezi nane (8) kutokana na vyanzo mbalimbali

vya maduhuli. Kati ya makusanyo hayo Shilingi 172.2 zilitokana na makusanyo ya mrabaha; na Shilingi bilioni 28.47 zilitokana na ada ya ukaguzi wa madini. Mchanganuo wa makusanyo kwa baadhi ya madini yanayozalishwa nchini ni kama ulivyoonyeshwa katika majedwali yaliyomo katika Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kamati inaamini kwamba ikiwa Tume ya Madini itaongezewa Wafanyakazi na kuzingatia majukumu iliyonayo sambamba na vitendea kazi itakuwa imeongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake na hivyo kuwezesha kuongezeka kwa mchango wa sekta ya madini katika uchumi wa Nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kushughulikia mambo mengi ya kibajeti ya Wizara ya Madini, Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 katika maeneo yafuatayo:-

- (i) Makusanyo ya Maduhuli;
- (ii) Hali ya upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina; na
- (iii) Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara ya Madini ilipanga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi bilioni 310.59 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2019 maduhuli yaliyokusanya ni jumla ya shilingi bilioni 218.65 sawa na asilimia 105.6 ya lengo la miezi nane (8).

Mheshimiwa Spika; Kamati inapenda kuipongeza Serikali kupitia Wizara ya Madini na Tume ya Madini katika kuhakikisha wanadhibiti utoroshaji wa madini Nchini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ni matarajio ya Kamati kuwa Wizara itaendelea kudhibiti utoroshaji wa madini ili Sekta ya Madini iweze kutoa mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa kama inavyotarajiwa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Taarifa ya hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; Katika mwaka wa fedha wa 2018/19 Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania liliidhinisha Bajeti ya jumla ya shilingi bilioni 58.9 kwa Wizara ya Madini. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 19.6 sawa na asilimia 33.3 ya Bajeti yote ya Wizara zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Shilingi bilioni 39.2 sawa na asilimia 66.7 ya Bajeti yote ya Wizara zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, shilingi bilioni 20.9 sawa na asilimia 53.3 zilitengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi bilioni 18.3 sawa na asilimia 46.7 zilikadiriwa kutumika kulipa Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zilizopo chini yake.

Mheshimiwa Spika, Vilevile, kati ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa, shilingi bilioni 16.8 sawa na asilimia 85.62 ya bajeti ya maendeleo ni fedha za ndani na shilingi bilioni 2.82 sawa na asilimia 14.38 ya bajeti hiyo ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Februari 2019, Jumla ya shilingi bilioni 23.4 zilipokelewa na Wizara kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Fedha hizi ni sawa na asilimia 59.59 ya lengo la Mwaka la shilingi bilioni 39.28. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 14.07 ni fedha za Matumizi Mengineyo ambayo ni sawa na asilimia 60.13 ya fedha zilizopokelewa na shilingi bilioni 9.3 sawa na asilimia 39.87 zilipokelewa kwa ajili ya kulipa Mishahara.

Mheshimiwa Spika, Kiasi cha shilingi milioni 100 fedha za ndani zimepokelewa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Februari, 2019. Aidha, Wizara ilipokea shilingi bilioni moja kwa ajili ya Ujenzi wa Ofisi za Wizara eneo la Mtumba-Dodoma. Fedha hizo zilitoka Wizara ya Fedha na Mipango. Kiasi cha shilingi milioni 100 za maendeleo ni sawa na asilimia 0.5 ya bajeti yote ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2018/2019 ambayo ni shilingi bilioni 19.62.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia kwa kifupi TEITI ina kazi kubwa ya kutoa taarifa ya uwazi na uwajibikaji juu ya matumizi ya mapato ya Halmashauri yanayotokana na tozo kutoka Kampuni za uchimbaji wa madini, mafuta na gesi asilia. Hivyo, katika kipindi cha Julai 2018 hadi Februari 2019 Taasisi ya TEITI imepokea shilingi milioni 135.9 kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 55.8 ya bajeti ya matumizi mengineyo kwa Mwaka 2018/2019 na hadi kipindi taarifa zinawasilishwa katika kamati, hakuna fedha ya maendeleo iliopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za TEITI. Kukosekana kwa Fedha kwa Taasisi hii, kunakwamisha sana Utekelezaji wa majukumu kwa Taasisi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa msisitizo; Kamati inasikitishwa na utolewaji wa fedha za miradi usioridhisha kwani Fedha za maendeleo zimepokelewa kwa kiasi kidogo sana ambacho ni chini ya asilimia moja ya fedha zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ni ukweli kwamba utolewaji wa fedha chini ya asilimia moja unasababisha ucheleweshwaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na miradi mingine kutotekelezeka kabisa.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika eneo hili Kamati inafahamu kuwa kiasi cha Shilingi bilioni 8.6 kilitengwa kwa ajili ya uchenjuaji wa visusu vya dhahabu katika mgodi wa Buhemba na kwamba sasa kiasi hicho kinakusudiwa kutumika katika mtaji wa *STAMICO* pindi mazungumzo na majadiliano ya ubia kati ya mwekezaji na *STAMICO* yatakapokamilika. Kamati inaona kuwa mazungumzo haya yamechukua muda mrefu na jambo ambalo linaweza kuleta athari katika uwekezaji huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha majadiliano ili mradi huu uweze kutekelezeka. Hivyo basi, ni rai ya Kamati kuwa, Serikali izingatie utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo kama zinavyoidhinishwa na Bunge ili kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa wakati kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, uzingatiaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka 2018/2019; wakati wa uchambuzi wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo kuhusu utekelezaji wa Bajeti pamoja na usimamizi wa Miradi ya maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa mwaka husika. Hata hivyo kwa kiasi kikubwa maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa na baadhi bado haujafanyiwa kazi na Serikali kama ifuatavyo:-

- (a) Serikali kutopeleka fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwenye miradi ya maendeleo na hivyo kusababisha kukwamisha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa;
- (b) Mkakati wa Wizara ya Madini kuhusu uwekezaji kwa ajili ya kuendeleza Mradi wa Madini ya Bati kwa kuwa taarifa za Benki ya Dunia zinaonesha kuimarika kwa bei na soko la madini hayo Duniani;

Mheshimiwa Spika, pamoja na mapungufu machache yaliyoanishwa hapo juu, Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa kuboresha mazingira ya biashara ya madini hususani kwa kuwafutia wachimbaji wadogo kodi ya ongezeko la thamani ya VAT asilimia 18% na kodi ya zuiro (*withholding tax*) ya asilimia 5%.

Mheshimiwa Spika, napenda kurudia; pamoja na mapungufu machache yaliyoanishwa hapo juu, Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa kuboresha mazingira ya biashara ya madini hususani kwa kuwafutia wachimbaji wadogo kodi ya ongezeko la thamani asilimia 18% na kodi ya zuiro asilimia 5%. Ni imani ya kamati kuwa wachimbaji wadogo wataunga mkono juhudii za Serikali kwa kulipa kodi na tozo mbalimbali ili Serikali iweze kukusanya mapato bila usumbufu.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Mpango na Makadirio na Matumizi kwa Wizara ya Madini (Fungu 100) kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Mapitio ya Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; Katika uchambuzi wa

Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Kamati ilibaini kuwa Mpango na Bajeti wa Mwaka 2019/2020 umezingatia azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujielekeza katika uchumi wa viwanda ambapo shilingi bilioni sita sawa na asilimia 85.23 ya Bajeti ya Maendeleo ya shilingi bilioni 7.03 ya Wizara imeelekezwa katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati kwa maana ya *strategic project* ya kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kamati inaridhishwa na malengo ya wizara kwa Mwaka 2019/2020, hata hivyo kamati inatambua kwamba kuwa na malengo ni jambo moja na kufanya juhudui au kutekeleza mikakati kufikia malengo hayo ni jambo lingine. Hivyo kamati inaa mini kuwa Serikali itatekeleza mikakati iliyonayo kwa ufanisi na uhoodari ili kufikia malengo ilijojiwekea kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato. Kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara ya Madini inakadiria kukusanya jumla ya Shilingi 476.3 ikililinganishwa na Shilingi 312.6 zilizokadiriwa kwa Mwaka 2018/2019, sawa na ongezeko la asilimia 52.36. Kati ya kiwango kilichopangwa kukusanywa Mwaka 2019/2020 Shilingi 470.89 sawa na asilimia 98.85 zitakusanywa na kuwasilishwa Hazina; na Shilingi 5.48 sawa na asilimia 1.15 zitakusanywa na kutumika na taasisi na wakala zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kamati ina maoni kuwa mpango wa kukusanya maduhuli kwa makisio makubwa yaende sambamba na uwekezaji wa Serikali katika sekta hiyo ili kuleta manufaa zaidi kwa nchi. Hivyo ni Rai ya Kamati kuwa ili Wizara iweze kukusanya maduhuli ya Serikali kulingana na malengo ya ukusanyaji waliyowekewa; Wizara inapaswa kuwa na wafanyakazi na vitendea kazi vya kutosha vitakavyowezesha kuimarisha ufuatiliaji, usimamizi na ukaguzi endelevu wa shughuli za sekta ya madini. Vilevile Wizara inapaswa kuimarisha na kusimamia vyema minada ya mauzo ya madini nchini ili kuvutia wafanyabiashara wengi wa kimataifa na wa ndani ya nchi kushiriki katika minada hiyo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi. Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara ya Madini inakadiria kutumia jumla ya Shilingi 49.46 ikilinganishwa na Shilingi 58.9 zilizopitishwa na Bunge katika mwaka wa fedha 2018/2019 sawa na upungufu wa asilimia 16.03. Kupungua kwa Bajeti hiyo kumetokana na kupungua kwa fedha za mishahara na miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara imetengewa kiasi cha Shilingi 7.03 ikiwa ni Bajeti ya Miradi ya Maendeleo ikilinganishwa na Shilingi 19.62 zilizotengwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, sawa na upungufu wa asilimia 64.12. Aidha, bajeti ya maendeleo ni asilimia 14.23 ya Bajeti yote ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/20 ambazo ni fedha za ndani. Hata hivyo, shilingi 6,000,000,000 sawa na asilimia 85.23 ya Bajeti yote ya Maendeleo zimeelekezwa kwenye Miradi ya klmkakati, yaani Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini na Mradi wa Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia.

Mheshimiwa Spika, Wizara inakadiria kutumia jumla ya Shilingi 42.42 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Bajeti hii inajumuisha Shilingi 25.95 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo kwa Wizara na Taasisi zake ambayo ni sawa na asilimia 61.17 ya bajeti ya matumizi ya kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Aidha, Wizara imetenga Shilingi 16.47 kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na taasisi zake ambayo ni asilimia 38.83 ya bajeti ya Wizara ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati. Kamati yako imetekeleza majukumu yake ya msingi yaliyoainishwa katika Kanuni ya 98 (1) na (2) pamoja na kanuni ya 117(11)(a) ya Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016. Hivyo basi, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao kwa Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi na Ukusanyaji wa Maduhuli. Matarajio ya makusanyo ya maduhuli

yasiyoendana na ikama ya wafanyakazi na vitendea kazi muhimu kwa Tume ya Madini ni changamoto kubwa kwa ufanisi wa kazi na ufkiaji malengo. Hivyo, kamati inaishauri Serikali kuajiri wafanyakazi wakutosha na kupeleka vitendea kazi ili kuimarisha ufuatilaji, usimamizi na uratibu wa shughuli za uendeshaji wa masoko ya madini nchini na hatimaye kuongeza ufanisi na tija katika ukusanyaji wa maduhuli.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi, Uratibu na Uendeshaji wa Masoko ya Madini. Kuanzishwa kwa masoko ya madini kunahitaji kuende sambamba na wafanyakazi wa kutosha kwenye masoko hayo. Bila ya kuwa na idadi stahiki ya wafanyakazi masoko hayo yanaweza kuwa kero kwa wafanyakazi na uchochoro au kichaka cha rushwa. Kamati inaishauri kuimarisha na kusimamia minada ya mauzo ya madini nchini na kuhakikisha kuwa masoko hayo yanakuwa na wafanyakazi wa kutosha wenyewe weledi wa masuala ya madini na masoko ili kuvutia wafanyakazi na wengi wa kimataifa na wa ndani ya nchi na kushiriki katika minada ya madini;

Mheshimiwa Spika, Utoroshaji wa Madini. Utoroshaji wa madini hasa Tanzanite na dhahabu kwa muda mrefu umeikosesha Serikali mapato na hivyo kusababisha nchi kushindwa kunufaika ipasavyo na rasilimali hizi. Licha ya Serikali kudhibiti utoroshwaji wa madini kuliko vipindi vingine, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuweka mikakati endelevu na mbinu za kisasa ili kudhibiti kikamilifu utoroshaji wa madini na biashara isiyo rasmi ya madini ili Serikali iweze kukusanya mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, Ajira kwa Watumishi wa Wizara na Taasisi Zake. Taasisi nyingi zilizo chini ya wizara zinakabiliwa na uhaba wa watendaji, hivyo kuathiri usimamizi na utendaji katika shughuli mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutoa vibali nya kuajiri watumishi kwa mujibu wa ikama ya taasisi hizo ili kuleta ufanisi na kuziwezesha taasisi kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa masoko ya madini nchini; Kamati inatambua umuhimu wa kuanzisha masoko ya madini nchini na kwamba yatawezesha Serikali kudhibiti biashara ya madini, kukusanya kodi na maduhuli kwa uwazi na kuvutia wauza madini wa ndani na nje ya nchi.

Hivyo, katika ujenzi wa masoko ya madini nchini, Kamati inaishauri Serikali kuzingatia uwepo wa masoko yenye tija kwa kujenga masoko maeneo ambayo madini yanapatikana kwa wingi ili kuleta tija na matumizi mazuri ya rasilimali.

Mheshimiwa Spika, Uwazi wa Mikataba na Makusanyo Yatokanayo na Sekta ya Madini. Uwazi na uwajibikaji katika sekta ya madini utawezesha nchi kunufaika zaidi na rasilimali zake kwa kila kitu kitakuwa wazi kwa wananchi. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuboresha uwazi na uwajibikaji katika sekta ya madini ikiwa ni pamoja na kuiwezesha Taasisi ya TEIT kifedha ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ikiwemo kutoa taarifa juu ya mikataba pamoja na mapato ya makusanyo yatokanayo na biashara ya madini.

Mheshimiwa Spika, Ukamilishaji wa Utengenezaji wa Kanuni. Uwepo wa kanuni za madini utarahisha utekelezaji wa Sheria ya Madini sura ya 123 kwa ukamilifu wake. Mpaka sasa Serikali hajjakamilisha utengenezaji wa kanuni zote chini ya Sheria hiyo. Kamati inaishauri Serikali Kuharakisha utengenezaji wa kanuni za Sheria ya Madini Sura ya 123 ili kutoa ufanuzi juu ya masharti ya sheria hiyo kuhusu uchimbaji wa rasilimali ya madini.

Mheshimiwa Spika, Uendelezaji wa Wataalamu Katika Masuala ya Jiolojia. Kwakuwa Wakala wa Jiolojia nchini unakabiliwa na changamoto ya upungufu wa wataalamu wenye taaluma stahiki kama vile wakemia, wajiolojia, wahandisi wa jiolojia; Kamati inaishauri Serikali kuwekeza kwa kutoa fursa za masomo kwa wananchi na watumishi mbalimbali katika taaluma hizo ili kuweza kupata wataalamu. Aidha, Serikali iboreshe maslahi ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, Elimu kwa Wafanyabiashara wa Madini Kuhusu Sheria ya Madini. Kamati imebaini kwamba kuna uelewa mdogo wa Sheria ya Madini kwa wafanyabiashara wa madini pamoja na wachimbaji ambao unasababisha migogoro na hivyo kusababisha kutokulipwa kwa baadhi ya tozo. Kutokana na hali hiyo Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutoa elimu kwa wafanyabiashara wa madini juu ya Sheria ya Madini ili kupunguza migogoro mbalimbali kwa wafanyabiashara na wachimbaji wa madini nchini.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho, ningependa kurudia tena kwa niaba ya kamati kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwanza kwa uamuzi wake wa kukutana na wachimbji wadogo wote nchini na kusikiliza kero zao; pia kwa uamuzi wake wa kizalendo wa kuanzisha masoko ya madini katikak ngazi ya mikoa na wilaya. Huu ni mwendelezo wake wa kuhakikisha rasilimali za nchi zinawanufaisha Watanzania wote. Ni maoni yetu sasa Shirika la STAMICO nalo watakuwa wameshaelewa nini Serikali ya Mheshimiwa Rais inataka kuhusu usimamizi wa rasilimali na ukusanyaji wa mapato kama mashirika mengine ya umma yanavyofanya. Ni matumaini kwamba STAMICO nayo itanoga kama TTCL na tutaona kwamba wanatoa gawio kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe mwenyewe kaka yangu, mshauri wangu Mhe. Job Yustino Ndugai Mbunge wa Kongwa na kule nyumbani tumezoea kukuita Sembuche, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; kwa kweli nakushukuru sana mimi binafsi kwenye uongozi wako umeweza kuniona mimi na kuweza kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati, nakushukuru sana. Pia nimshukuru Dr. Tulia Akson Mbunge wa Mbeya mtarajiwa na Naibu Spika, pia na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuliongoza Bunge hili kwa weledi mkubwa. Tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu afya njema na uzima katika kuendelea kutekeleza majukumu mliyopewa.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini;

Iakini kipekee nipende kumshukuru Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Mwenyekiti. Pia niwashukuru sana Wajumbe pamoja na ufupi wangu pamoja na kuwa na umri mdogo iakini bado wanani pa ushirikiano kutekeleza majukumu yangu kama Makamu Mwenyekiti wao na nikitoa maagizo kwa kweli yanatekelezeka. Mungu awabariki wanakamatii kwani hii Kamati itabaki kuwa kwenye historia kwa sababu tunasaidia nchi yetu kuleta mapinduzi makubwa sana katika sekta ya madini. Pia naomba kwamba majina yao yote yaingie katika kumbukumbu Rasmi za Bunge. Lakini nisiwe mchoyo wa fadhila nipende kumshukuru pia Mheshimiwa Catherine Magige kwani ni yeye ndiye aliona kwamba nafaa kuwa nafasi ya Makamu Mwenyekiti na alishiriki sana kunipigia debe mshenga huyu ili niweze kushika nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa niaba ya wajumbe wa Kamati kwa Mheshimiwa Dotto Mashaka Biteko, Waziri wa Madini, Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo Naibu Waziri wa Madini; ama kweli hawa wanatembea kinadharia sifa kwamba vijana tukiaminika tunaweza. Mimi huwa napenda kuwapa jina kwamba hawa ni *the fantastic double*, kwa kweli Mungu awabariki na muendelee kuchapa kazi sana. Bila kusahau watendaji wote wa wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Profesa Saimon Nsanjila kwa ushirikiano wao mkubwa kwa kamati yetu muda wote.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Steven Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi, Ndg. Michael Chikokoto pamoja na Makatibu wa Kamati Ndg. Felister Mgonya na Ndg. Omary Magwinza kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ulitaja wageni leo, kwa namna ya kipekee lazima nitakuwa sijakamilisha dhamira yangu kama sitomshukuru mama yangu kipenzi kwa kunizaa na kunilea katika maadili yanayomwongoza Mwenyezi Mungu na kwa kweli amekuwa akinipa moyo katika kazi hii ya siasa. Mama

nikwambie neno moja nakupenda sana na sitokuangusha mama yangu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 100 Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambayo ni Shilingi Bilioni 49,466,898,200.

Mheshimiwa Spika, Naunga mkono hoja na Naomba kuwasilisha.(*Makofi*)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA
MADINI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA
MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 PAMOJA NA
MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 – KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 99 (9) na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Fasili ya 6(9) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati inao wajibu wa kusimamia majukumu yote ya kisera yanayotekelawa na Wizara hii. Aidha, majukumu ya Kamati kuhusiana na Uchambuzi wa bajeti ya kila mwaka ya Wizara inazozisimamia yameelekezwa katika Fasili ya 7(1). Kamati imetekeliza ipasavyo majukumu hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matakwa ya kanuni, Kamati ilifanya kazi kuu mbili ambazo ni:

- a) Kutembelea na Kukagua Utekelezaji wa Miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2018/2019 [*Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016*]; na
- b) Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 [*Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016*].

1.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2018/2019

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayotekelawa chini ya Wizara ya Madini. Ziara hizo zilifanyika katika Mikoa ya Dodoma na Ruvuma (Songea). Lengo la ziara likiwa ni kujionea Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, miradi iliyokaguliwa ni ifuatayo:-

- (i) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Utawala katika Chuo cha Madini Dodoma (MRI);
- (ii) Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Madini (Ihumwa Dodoma);na
- (iii) Mradi wa Ujenzi wa kituo cha Umahiri Songea (Songea Centre of Excellence).

1.3 Maelezo na Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

1.3.1 Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Utawala katika Chuo cha Madini Dodoma (MRI);

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Jengo la Utawala katika Chuo cha Madini Dodoma pamoja na ujenzi wa Vituo Saba (7)

vya umahiri (*Centers of Excellence*) katika maeneo ya Bariadi, Bukoba, Musoma, Handeni, Mpanda, Chunya na Songea upo chini ya Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali Madini Awamu ya Pili (*Sustainable Management of Mineral Resources Project-SMMRP II*) ambao unaghanimu jumla ya Dola za Marekani **milioni 50** ambazo katika hizo **Dola milioni 45** ni mkopo kutoka Benki ya Dunia na **Dola milioni 5** zinatolewa na Serikali ya Tanzania. Aidha, Mradi huu unatekelezwa ndani ya miaka mitatu kuanzia mwezi Septemba, 2015 hadi Disemba, 2018 ambapo kwa sasa upo katika hatua za mwisho za ufungaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la mradi wa SSMRP ni kuweka/kuboresha mazingira wezeshi yatakayosaidia sekta ya madini kuwa na faida na mchango mkubwa zaidi kijamii na kiuchumi kwa manufaa ya watanzania na taifa kwa ujumla kwa kuimarisha zaidi sehemu ya miradi ya kiuchumi na kijamii iliyokuwa inatekelezwa na mradi wa Awamu ya Kwanza.

Mheshimiwa Spika, kutohana na malengo hayo, mradi wa ujenzi wa Jengo la Taaluma la Chuo cha Madini ulianza kutekelezwa kwa mfuko wa *SMMRP*. Wizara ilimkabidhi Mkandarasi SUMA JKT eneo la ujenzi mnamo tarehe 14 Julai, 2018 na kazi ya ujenzi ilianza rasmi tarehe 30 Julai, 2018. Ujenzi wa Jengo hilo utagharimu jumla ya takribani **Shilingi bilioni 2.86**.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine, jengo hilo linatarajiwaa kuwa na Ofisi kwa ajili ya Chama cha Wachimbaji Madini Wanawake Tanzania. Mpaka wakati kamati inatembelea mradi, ujenzi ulikuwa umefikia **asilimia 65** ambapo hadi kufikia tarehe 31 Januari, 2019 jumla ya takribani **Shilingi bilioni 1.91** sawa na **asilimia 67** zimelipwa kwa Mkandarasi. Aidha, hadi sasa mradi huu ujenzi umefikia asilimia 80.

Mheshimiwa Spika, Jengo hilo linatarajiwaa kuwa na manufaa yafuatayo:-

- a) Uwepo wa ofisi za wachimbaji madini wadogo wanawake (TAWOMA) ambazo zitasaidia kuratibu mafunzo yatakayowaendeleza akina mama wachimbaji wa Madini;
- b) Kumaliza tatizo la ukosefu wa ofisi kwa Wakufunzi;
- c) Kupunguza tatizo la ukosefu wa vyumba vyaa madarasa na kutoa fursa kwa chuo kuongeza nafasi za udahili na hivyo kusaidia Kuongezeka kwa idadi ya wataalamu wenye weledi wa masuala ya madini.

1.3.2 Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Madini (Ihumwa- Dodoma);

Mheshimiwa Spika, Wizara ilipokea Fedha zipatazo **Shilingi Bilioni 1 mnamo tarehe 5 Novemba, 2018** kutoka Wizara ya Fedha na Mipango. Fedha hizo zilitolewa kwa ajili ya Ujenzi wa Ofisi za Wizara katika Mji wa Serikali Dodoma eneo la Ihumwa. Mara baada ya kupokea Fedha hizo, Wizara ilipata mkandarasi ambaye ni Kampuni ya ujenzi ya Mzinga Holding Co. Ltd na kusaini nayo mkataba wenye thamani ya takribani **Shilingi Milioni 975** pamoja na **VAT**. Kazi ya ujenzi ilianza rasmi tarehe 4 Disemba, 2018 na kutakiwa kukamilika tarehe 28 Februari, 2018 kama ilivyo kwenye mkataba wa nyongeza (*addendum contract*).

Hata hivyo hadi wakati kamati inatembelea mradi huo tarehe 13 Machi, 2019 ujenzi ulikuwa umekamilika kwa **asilimia 80**.

Mheshimiwa Spika, ziara ya kamati katika mradi wa ujenzi wa ofisi za wizara ya madini ilibaini changamoto zifuatazo:-

- a) Muda mfupi wa utekelezaji wa mkataba. Kwa mujibu wa mkataba mkandarasi alipaswa amalize mradi huo ndani ya mwezi mmoja ambao ultimia mwezi Januari, 2019. Hata hivyo mkandarasi ameshindwa kumaliza ndani ya mwezi mmoja na hivyo kupewa mkataba wa nyongeza kila mwezi (*addendum contract*);
- b) Mvua zilizonyesha kati ya mwezi Disemba na Januari zimepelekea mradi kutokamilika kwa wakati.

Hatahivyo, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukamilisha mradi huu kwa hatua za awali ambazo zimewezesha Wizara ya Madini kuhamishia ofisi zake katika katika mji wa Serikali, Ihumwa.

1.3.3 Mradi wa Ujenzi wa kituo cha Umahiri Songea

Mheshimiwa Spika, Eneo la Mradi wa kituo cha Umahiri kwa ajili ya wachimbaji wadogo lipo katika kiwanja Namba 86 Angoni Arms - Manispaa ya Songea. Mkandarasi SUMA JKT alikabidhiwa rasmi eneo la ujenzi tarehe 15 Julai, 2018 na mnamo tarehe 24 Julai, 2018 kazi ya ujenzi ilianza. Ujenzi wa kituo hicho utagharimu kiasi cha takribani **Shilingi bilioni 1.27**.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mradi huo ulichelewa kuanza kutokana na kukosekana kwa kibali cha kuruhusu kubomoa jengo la zamani. Hadi wakati Kamati inatembelea mradi huo ujenzi ulikuwa umekamilika kwa **asilimia 40** ambapo hadi kufikia tarehe 31 Januari, 2019 kiasi cha **Shilingi milioni 373.99** zilikuwa zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho. Aidha, kwa mujibu wa mkataba wa Ujenzi wa jengo hilo, ujenzi ultarajiwu kukamilika ifikapo mwezi Aprili, 2019. **Hatahivyo, mpaka sasa mradi huu ujenzi umefikia asilimia 50 wakati ulipaswa ukamiliwe mwezi Aprili, 2019.**

Mheshimiwa Spika, ziara ya kamati katika mradi huu ilibaini changamoto zifuatazo:

- a) Kukosekana kwa kibali cha kuvunja jengo la zamani hivyo kusababisha ujenzi kuchelewa kuanza;
- b) Mkandarasi kukosa wafanyakazi wa kutosha na hivyo ujenzi kwenda kwa kusuasua;
- c) Changamoto ya upatikanaji kokoto katika Mji wa Songea ulisababisha ujenzi wa mradi kusimama mara kwa mara.

1.4 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

Mheshimiwa Spika, kufuatia hali halisi wakati wa ukaguzi wa miradi, kamati inatoa ushauri kwamba;

a) Mikataba ya Ujenzi wa majengo ya Wizara ya Madini na Taasisi zake unapaswa kuzingatia ubora wa majengo pamoja na hali halisi ya utekelezaji wa miradi kwani Kamati imebaini kuwa Serikali inatoa muda mfupi sana kwa wakandarasi na kusababisha mikataba kuongezwa muda wa utekelezaji mara kwa mara hivyo kuathiri utekelezaji, ufanisi na ubora wa kazi za ujenzi wa miradi;

b) Serikali inapaswa kuendelea kuwasimamia wakandarasi wanaopewa kutekeleza miradi mbalimbali ipasavyo kwani baadhi ya wakandarasi hawana nguvu kazi ya kutosha hivyo kusababisha kuzorota kwa utekelezaji wa miradi.

c) Wizara ichukue hatua za haraka kuanisha maeneo yanayofaa kuzalisha kokoto katika mji wa Songea na kutoa leseni kwa sekta binafsi ili kuwezesha ukuaji wa sekta ya ujenzi katika mji huo. Kamati ilijiuliza ikiwa Wizara ilikosa kokoto je hali ikoje kwa wananchi wa kawaida, Hivyo ni Rai ya Kamati kuwa Wizara iharakishe kutatua changamoto hiyo katika mkoa wa Ruvuma.

SEHEMU YA PILI

**2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI
PAMOJA NA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA
MWAKA WA FEDHA 2018/2019;**

Mheshimiwa Spika, Jukumu la msingi la Wizara ya Madini ni kusimamia maendeleo ya Sekta ya Madini nchini kwa kuweka mifumo thabiti ya utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini. Kazi zilizotekelze wa Wizara ya Madini katika kipindi cha kuanzia Julai 2018 hadi Februari, 2019 zilikuwa ni kuimarisha usimamizi na udhibiti wa rasilimali madini kwa lengo la kuongeza makusanyo ya Maduhuli kwa Serikali. Katika

kufanikisha haya, Tume ya Madini imekuwa kiungo muhimu katika kuhakikisha ukaguzi na usimamizi wa biashara ya madini nchini unafanyika kikamilifu. Kazi zinazofanywa na Tume ya Madini ni pamoja na kudhibiti utoroshaji wa madini; kusimamia shughuli zote za uthaminishaji madini nchini na kushiriki minada ya madini; kuandaa bei elekezi; usimamizi wa shughuli za maabara; na kusimamia utekelezaji wa kanuni za uwezeshaji wananchi kiuchumi (*local content*) katika Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Madini imeendelea na usimamizi wa uzalishaji na biashara ya madini nchini. Kwa kipindi cha Mwezi Julai, 2018 hadi Februari 2019, Tume ilikusanya jumla ya **Shilingi 218,450,606,094** sawa na **asilimia 106** ya lengo la miezi nane (8) kutohana na vyanzo mbalimbali vya maduhuli. Kati ya makusanyo hayo **Shilingi 172,212,495,009.56** zilitokana na makusanyo ya mrabaha; na **Shilingi 28,476,013,756.24** zilitokana na ada ya ukaguzi wa madini. Mchanganuo wa makusanyo kwa baadhi ya madini yanayozalishwa nchini ni kama ulivyooneshwa kwenye Jedwali lifuatato;


Mchanganuo wa makusanyo ya Mrabaha na Ada ya Ukaguzi

Aina ya Madini	Kipimo cha Uzito	Uzito	Thamani (TZS)	Mrabaha (TZS)	Ada ya Ukaguzi (TZS)
Dhababu	Kg	26,735.13	2,467,491,051,477.92	148,049,463,088.68	24,674,910,514.78
Feeda (Silver)	Kg	8,627.53	9,790,459,946.29	587,427,596.78	97,904,599.46
Almasi	Karati	267,001.99	138,276,005,749.48	8,296,560,344.97	1,382,760,057.49
Tanzanite	Kg	522.68	16,775,739,408.51	705,643,679.79	167,757,394.09
Makaaya Mawe	Tani	223,385.58	28,407,248,496.71	852,217,454.90	284,072,484.97
Madri Uenzi	Tani	8,072,703.02	125,509,989,822.09	3,765,299,694.66	1,209,276,026.95
Madini Mengineyo	Tani			9,955,883,149.78	659,332,678.50
Jumla				172,212,495,009.56	28,476,013,756.24

Chanzo; Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti wa Tume ya Madini kwa mwaka 2018/2019

Mheshimiwa Spika, Kulingana na mchanganuo huo, madini ya dhahabu yamechangia kwa **asilimia 86.07** kiwango ambacho ni kikubwa ikilinganishwa na aina nyingine za madini. Mchango wa madini mengine ni kama ifuatavyo: almasi **asilimia 4.82**, madini ujenzi **asilimia 2.48**; makaa ya mawe **asilimia 0.57**; tanzanite **asilimia 0.44**; fedha **asilimia 0.34** pamoja na madini mengineyo yaliyochangia **asilimia 5.29**.


Mchango wa aina mbalimbali za madini kwenye maduhuli ya Serikali.



Chanzo; Taarifa ya Tume ya Madini kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2018/2019

Mheshimiwa Spika, Kati ya mchango wa **asilimia 86.07** zilizotokana na madini ya dhahabu, **asilimia 7.73** zilitokana na ushiriki wa wachimbaji wadogo wafanyabiashara wa dhahabu pamoja na mitambo ya uchenjuaji; na **asilimia 78.33** zilitokana na wachimbaji wakubwa. Ufanuzi wa mchango wao ni kama unavyoonekana katika kielelezo kifuatacho;

Mchango wa wachimbaji wadogo, wafanyabiashara na mitambo ya uchenjuaji dhahabu kwenye maduhuli ya Serikali.



Chanzo: Taarifa ya Tume ya Madini kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2018/2019

Mheshimiwa Spika, kamati inaamini kwamba ikiwa Tume ya Madini itaongezewa Wafanyakazi kwa kuzingatia majukumu iliyonayo sambamba na vitendea kazi itakuwa imeongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake na hivyo kuwesheha kuongezeka kwa mchango wa sekta ya madini katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kushughulikia mambo mengi ya kibajeti ya Wizara ya Madini, Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 katika maeneo yafuatayo:-

- Makusanyo ya Maduhuli;
- Hali ya upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina; pamoja na
- Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati.

2.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara ya Madini ilipanga kukusanya maduhuli ya jumla ya **shilingi 310,598,007,000** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2019 maduhuli yaliyokusanya wa

ni jumla ya **shilingi 218,650,392,234** sawa na **asilimia 105.6** ya lengo la miezi nane (8).

Mheshimiwa Spika, Wizara imeweza kuvuka lengo la ukusanyaji maduhuli kwa kipindi cha miezi nane (8) kuanzia Julai 2018 hadi Februari, 2019 kutokana na sababu zifuatazo:-

- (i) Usimamizi mzuri wa Sheria, Kanuni na taratibu zinazosimamia Sekta ya Madini;
- (ii) Kusitisha uagizaji wa makaa ya mawe kutoka nje ya nchi ambao ulisababisha kuongezeka kwa matumizi na uzalishaji wa makaa ya mawe nchini;
- (iii) kudhibiti utoroshwaji wa madini; na
- (iv) Kuongezeka kwa mapato ya madini ya Tanzanite kutokana na kuongezeka kwa udhibiti kufuatia kujengwa kwa Ukuta; ambao unasaidia kudhibiti biashara holela na magendo .

Mheshimiwa spika, Kamati inapenda kuipongeza Serikali kupitia Wizara ya Madini na Tume ya Madini katika kuhakikisha wanadhibiti utoroshaji wa madini nchini. **Ni matarajio ya Kamati kuwa Wizara itaendelea kudhibiti utoroshaji wa madini ili Sekta ya Madini iweze kutoa mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa kama inavyotarajiwa na Wananchi.**

2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya hali ya upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha wa 2018/19 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliidhinisha Bajeti ya jumla ya **shilingi 58,908,481,992** kwa Wizara ya Madini. Kati ya fedha hizo, **shilingi 19,620,964,000** sawa na **asilimia 33.3** ya Bajeti yote ya Wizara zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, **Shilingi 39,287,517,992** sawa na **asilimia 66.7** ya Bajeti yote ya Wizara zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, **shilingi 20,953,262,992** sawa na **asilimia 53.3** zilitengwa kwa

ajili ya Matumizi Mengineyo na **shilingi 18,334,255,000** sawa na **asilimia 46.7** zilikadiriwa kutumika kulipa Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zilizopo chini yake. Villevile, kati ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa, **shilingi 16,800,000,000** sawa na **asilimia 85.62** ya bajeti ya maendeleo ni fedha za ndani na **shilingi 2,820,964,000** sawa na **asilimia 14.38** ya bajeti hiyo ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Februari 2019, Jumla ya **shilingi 23,412,070,873.43** zilipokelewa na Wizara kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Fedha hizi ni sawa na **asilimia 59.59** ya lengo la Mwaka la **shilingi 39,287,517,992**. Kati ya fedha hizo **shilingi 14,078,672,637.43** ni fedha za Matumizi Mengineyo (O.C) ambayo ni sawa na **asilimia 60.13** ya fedha zilizopokelewa. Na **shilingi 9,333,398,236** sawa na **asilimia 39.87** zilipokelewa kwa ajili ya kulipa Mishahara.

Mheshimiwa Spika, Kiasi cha **shilingi 100,000,000** fedha za ndani zimepokelewa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Februari, 2019. Aidha, Wizara ilipokea **shilingi 1,000,000,000** kwa ajili ya Ujenzi wa Ofisi za Wizara eneo la Ihumwa, Dodoma. Fedha hizo zilitoka Wizara ya Fedha na Mipango. Kiasi cha **shilingi 100,000,000** za maendeleo ni sawa na **asilimia 0.5** ya bajeti yote ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2018/19 ambayo ni **shilingi 19,620,964,000**.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI) ina kazi kubwa ya kutoa taarifa ya uwazi na uwajibikaji juu ya matumizi ya mapato ya Halmashauri yanayotokana na tozo kutoka Kampuni za uchimbaji wa madini, mafuta na gesi asilia, hatahivyo, katika kipindi cha Julai 2018 hadi Februari 2019 Taasisi ya TEITI imepokea **Shilingi 135,909,500** kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) sawa na **asilimia 55.8** ya bajeti ya matumizi mengineyo kwa mwaka 2018/19 na hadi kipindi taarifa zinawasilishwa katika kamati, hakuna fedha ya maendeleo iliyopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za TEITI. Kukosekana kwa Fedha kwa Taasisi hii, kunakwamisha sana Utekelezaji wa majukumu kwa Taasisi hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na utolewaji wa fedha za miradi usioridhisha kwani Fedha za maendeleo zimepokelewa kwa kiasi kidogo sana ambacho ni chini ya asilimia 1 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ni ukweli kwamba utolewaji wa fedha chini ya asilimia 1 unasababisha ucheleweshwaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na miradi mingine kutotekelezwa kabisa.

Aidha, katika eneo hili Kamati inafahamu kuwa kiasi cha Shilingi bilioni 8,600,000,000 kilitengwa kwajaili ya uchenjuaji wa visusu vya dhahabu katika mgodi wa Buhemba na kwamba sasa kiasi hicho kinakusudiwa kutumika kama mtaji wa STAMICO pindi mazungumzo na majadiliano ya ubia kati ya muwekezaji na STAMICO yatakapokamilika. Kamati inaona kuwa mazungumzo haya yamechukua mda mrefu na jambo ambalo linaweza kuleta athari katika uwekezaji huu. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha majadiliano ili mradi huu uweze kutekelezeka.

Hivybasi, ni rai ya Kamati kuwa, Serikali izingatie utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo kama zinavyoidhinishwa na Bunge ili kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa wakati kama ilivyokusudiwa.

2.3 Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka 2018/2019

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchambuzi wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/19, Kamati ilioa Maoni, Ushauri na Mapendekezo kuhusu utekelezaji wa Bajeti pamoja na usimamizi wa Miradi ya maendeleo iliyoidhinishwa fedha kwa mwaka husika. Hatahivyo kwa kiasi kikubwa maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa na baadhi bado haujafanyiwa kazi na Serikali kama ifuatavyo:-

- a) Serikali kutopeleka fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwenye miradi ya maendeleo na hivyo kusababisha kukwamisha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa;

b) Mkakati wa Wizara ya Madini kuhusu uwekezaji kwa ajili ya kuendeleza Mradi wa Madini ya Bati kwa kuwa taarifa za Benki ya Dunia zinaonesha kuimarika kwa bei na soko la madini hayo Duniani;

Mheshimiwa Spika, pamoja na mapungufu machache yaliyoanishwa hapo juu, Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa kuboresha mazingira ya biashara ya madini hususan kwa kuwafutia wachimbaji wadogo kodi ya ongezeko la thamani (VAT 18%), na kodi ya zuio (withholding tax 5%). Ni imani ya kamati kuwa wachimbaji wadogo wataunga mkono juhudzi za Serikali kwa kulipa kodi na tozo mbalimbali ili Serikali iweze kukusanya mapato bila usumbufu.

2.4 Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Madini (Fungu 100) kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

2.4.1 Mapitio ya Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi wa Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Kamati ilibaini kuwa Mpango na Bajeti wa Mwaka 2019/2020 umezingatia azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujielekeza katika uchumi wa viwanda ambapo **shilingi 6,000,000,000** sawa na **asilimia 85.23** ya Bajeti ya Maendeleo ya **shilingi 7,039,810,177** ya Wizara imeelekezwa katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati (*strategic projects*) ya kuongeza mapato ya Serikali.

Hivyo, Maeneo yaliyopewa kipaumbele kwa mwaka 2019/2020 katika Sekta ya Madini na kuzingatiwa katika bajeti ni kuimarisha ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali yatokanayo na rasilimali za madini; uanzishwaji na Usimamizi wa Masoko ya Madini; kudhibiti utoroshwaji wa madini; kuendeleza Wachimbaji Wadogo na wa kati wa madini; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; kuimarisha ufuutiliaji na ukaguzi wa usalama, mazingira na uzalishaji wa madini katika migodi midogo, ya kati na mikubwa; kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini; kuendelea

Kuboresha Mazingira ya kuwawezesha Wananchi Kufaidika na Rasilimali Madini; na kuendeleza rasilimali watu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza majukumu yake, Wizara ina malengo yafuatayo:-

- a) Kuboresha utoaji huduma kwa Wadau wa Sekta ya Madini;
- b) Kuongeza Mchango wa sekta ya Madini kijamii na kiuchumi;
- c) Kuwaimarisha Wachimbaji wadogo wadogo wa Madini nchini;
- d) Kuimarisha mifumo ya ukaguzi na usimamizi wa migodi
- e) Kuimarisha na kuendeleza Mkakati wa Taifa na Mpango wa kupambana na Rushwa; na
- f) Kuboresha huduma kwa waathirika na kupunguza maambukizi ya Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kamati inaridhishwa na malengo ya wizara kwa mwaka 2019/2020, hata hivyo kamati inatambua kwamba kuwa na malengo ni jambo moja na kufanya juhudui au kutekeleza mikakati kufikia malengo hayo ni jambo lingine. Hivyo kamati inaamini kuwa Serikali itatekeleza mikakati iliyonayo kwa ufanisi ili kufikia malengo ilijojiwekea kwa manufaa ya Taifa.

2.4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

Mheshimiwa Spika, Kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara ya Madini inakadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 476,380,613,492** ikilinganishwa na **Shilingi 312,672,507,000** zilizokadiriwa kwa Mwaka 2018/2019 sawa na ongezeko la **asilimia 52.36**. Kati ya kiwango kilichopangwa kukusanya wa Mwaka 2019/2020 **Shilingi 470,897,011,000** sawa na **asilimia 98.85** zitakusanya na kuwasilishwa Hazina; na **Shilingi**

5,483,602,492 sawa na **asilimia 1.15** zitakusanya na kutumika na Taasisi na Wakala zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kamati ina maoni kuwa mpango wa kukusanya maduhuli kwa makisio makubwa yaende sambamba na uwekezaji wa Serikali katika sekta hiyo ili kuleta manufaa zaidi kwa nchi. Hivyo ni Rai ya Kamati kuwa ili Wizara iweze kukusanya maduhuli ya Serikali kulingana na malengo ya ukusanyaji waliyowekewa; Wizara inapaswa kuwa na wafanyakazi na vitendea kazi vya kutosha vitakavyowezesha kuimarisha ufuutiliaji, usimamizi na ukaguzi endelevu wa shughuli za Sekta ya Madini. Vilevile wizara inapaswa kuimarisha na kusimamia vyema minada ya mauzo ya madini nchini ili kuvutia wafanyabiashara wengi wa kimataifa na wa ndani ya nchi kushiriki katika minada ya madini.

2.4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara ya Madini inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 49,466,898,200** ikilinganishwa na **Shilingi 58,908,481,992** zilizopitishwa na Bunge katika Mwaka wa Fedha 2018/19 sawa na upungufu wa **asilimia 16.03**. Kupungua kwa Bajeti hiyo kumetokana na kupungua kwa fedha za mishahara na miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara imetengewa kiasi cha **Shilingi 7,039,810,200** ikiwa ni Bajeti ya Miradi ya Maendeleo ikilinganishwa na **Shilingi 19,620,964,000** zilizotengwa Mwaka wa Fedha 2018/19, sawa na upungufu wa **asilimia 64.12**. Aidha, Bajeti ya Maendeleo ni **asilimia 14.23** ya Bajeti yote ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 ambazo ni fedha za ndani. Hatahivyo, **Shilingi 6,000,000,000** sawa na **asilimia 85.23** ya Bajeti yote ya Maendeleo zimeelekezwa kwenye Miradi ya kimkakati, yaani Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini na Mradi wa Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI).

Mheshimiwa Spika, Wizara inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 42,427,088,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Bajeti hii inajumuisha **Shilingi 25,953,263,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) kwa Wizara na Taasisi zake ambayo ni sawa na **asilimia 61.17** ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Aidha, Wizara imetenga **Shilingi 16,473,825,000** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake ambayo ni **asilimia 38.83** ya bajeti ya Wizara ya Matumizi ya Kawaida.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Kamati yako imetekeleza majukumu yake ya msingi yaliyoainishwa katika Kanuni ya 98 (1) na (2) pamoja na kanuni ya 117(11a) ya Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016. Hivyo basi, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao kwa Wizara ya Madini;

3.1 Usimamizi na Ukusanyaji wa Maduhuli

Matarajio ya makusanyo ya maduhuli yasiyoendana na ikama ya wafanyakazi na vitendea kazi muhimu kwa Tume ya Madini ni changamoto kubwa kwa ufanisi wa kazi na ufikiaji malengo. Hivyo, kamati inaishauri Serikali kuajiri wafanyakazi wakutosha na kupeleka vitendea kazi ili kuimarisha Ufutiliaji, usimamizi na uratibu wa shughuli za uendeshaji wa masoko ya madini nchini na hatimaye kuongeza ufanisi na tija katika ukusanyaji wa maduhuli;

3.2 Usimamizi, Uratibu na Uendeshaji wa masoko ya Madini

Kuanzishwa kwa masoko ya madini kunahitaji kuende sambamba na wafanyakazi wa kutosha kwenye masoko hayo, bila ya kuwa na idadi stahiki ya wafanyakazi masoko hayo yanaweza kuwa kero kwa wafanyabiashara na uchochoro au kichaka cha rushwa. Kamati inashauri Serikali

kuimarisha na kusimamia minada ya mauzo ya madini nchini na kuhakikisha kuwa masoko hayo yanakuwa na wafanyakazi wa kutosha wenye weledi wa masuala ya madini na masoko ili kuvutia wafanyabiashara wengi wa kimataifa na wa ndani ya nchi na kushiriki katika minada ya madini;

3.3 Utoroshaji wa Madini

Utoroshaji wa madini hasa Tanzanite na dhahabu kwa muda mrefu umeikosesha Serikali mapato na hivyo kusababisha nchi kushindwa kunufaika ipasavyo na rasilimali hizi. Licha ya Serikali kudhibiti utoroshwaji wa madini kuliko vipindi vingine; Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuweka mikakati endelevu na mbinu za kisasa ili kudhibiti kikamilifu utoroshaji wa madini na biashara isiyo rasmi ya madini ili Serikali iweze kukusanya mapato ya kutosha;

3.4 Ajira kwa Watumishi wa Wizara na Taasisi zake

Taasisi nyingi zilizo chini ya wizara zinakabiliwa na uhaba wa watendaji hivyo kuathiri usimamizi na utendaji katika shughuli mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo; hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutoa vibali vya kuajiri watumishi kwa mujibu wa ikama ya taasisi hizo ili kuleta ufanisi na kuziwezesha taasisi kutekeleza majukumu yake ipasavyo;

3.5 Ujenzi wa Masoko ya Madini nchini

Kamati inatambua umuhimu wa kuanzisha masoko ya madini nchini na kwamba yatawezesha Serikali kudhibiti biashara ya madini, kukusanya kodi na maduhuli kwa uwazi na kuvutia wauza madini wa ndani na nje ya nchi. Hivyo, Katika ujenzi wa masoko ya madini nchini, Kamati inaishauri Serikali kuzingatia uwepo wa masoko yenye tija kwa kujenga masoko maeneo ambayo yanapatikana madini kwa wingi ili kuleta tija na matumizi mazuri ya rasilimali;

3.6 Uwazi wa mikataba na makusanyo yatokanayo na Sekta ya Madini

Uwazi na uwajibikaji katika sekta ya madini utawezesha nchi kunufaika zaidi na rasilimali zake kwa kuwa kila kitakuwa wazi kwa wananchi. Hivyobasi, Kamati inaishauri Serikali

kuendelea kuboresha uwazi na uwajibikaji katika sekta ya madini ikiwa ni pamoja na kuiwezesha Taasisi ya TEITI kifedha, ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ikiwemo kutoa taarifa juu ya mikataba pamoja na mapato ya makusanyo yatokanayo na biashara ya Madini;

3.7 *Ukamilishaji wa utengenezaji wa kanuni*

Uwepo wa kanuni za madini utarahisha utekelezaji wa Sheria ya Madini ya Sura ya 123 kwa ukamilifu wake. Mpaka sasa Serikali hajakamilisha utengenezaji wa Kanuni zote chini ya Sheria hiyo. Kamati inaishauri Serikali Kuharakisha utengenezaji wa kanuni za Sheria ya Madini Sura ya 123 ili kutoa ufanuzi zaidi juu ya masharti ya sheria hiyo kuhusu uchimbaji wa rasilimali ya madini;

3.8 *Uendelezaji wa wataalamu katika masuala ya Jiolojia*

Kwakuwa Wakala wa Jiolojia nchini (GST) unakabiliwa na changamoto ya upungufu wa wataalamu wenyewe taaluma stahiki kama vile wakemia, wajiolojia, wahandisi wa jiolojia; Kamati inaishauri Serikali kuwekeza kwa kutoa fursa za masomo kwa wananchi na watumishi mbalimbali katika taaluma hizo ili kuweza kupata wataalamu. Aidha, Serikali iboreshe maslahi ya watumishi wenyewe taaluma hizo kwani kazi wanazofanya ni kubwa na zina manufaa makubwa kwa nchi;

3.9 *Upatikanaji wa Pesa kwa Wakala wa Jiolojia (GST)*

Wakala wa Jiolojia (GST) ni muhimu sana katika maendeleo ya sekta ya madini hivyo kuna umuhimu wa Wakala huu kuwezesha kifedha ili kuweza kutekeleza kazi zake kwa ufanisi. Kamati inaishauri Serikali kupeleka fedha kwa Wakala wa Jiolojia (GST) kwani taasisi hii ina majukumu makubwa na muhimu hasa ikizingatiwa kuwa imeongezewa majukumu mapya kuititia marekebisho ya Sheria ya Madini ya mwaka 2017. Vilevile Serikali inapaswa kuongeza vitendea kazi

hususan magari na vifaa vingine vya ugani ili taasisi hii iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

3.10 Elimu kwa wafanyabiashara wa madini kuhusu Sheria ya Madini

Kamati imebaini kwamba kuna uelewa mdogo wa Sheria ya Madini kwa wafanyabiashara wa madini pamoja na wachimbaji ambao unasababisha migogoro na hivyo kusababisha kutokulipwa kwa baadhi ya tozo; kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutoa elimu kwa wafanyabiashara wa madini juu ya sheria ya madini ili kupunguza migogoro mbalimbali kwa wafanyabiashara na wachimbaji wa madini nchini.

4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe mwenyewe Mhe. Job Yustino Ndugai (Mb) Spika, Dr. Tulia Akson (Mb) Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuliongoza Bunge hili kwa weledi mkubwa. Tunawaombea afya njema na uzima katika kuendelea kutekeleza majukumu mliyopewa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa ushirikiano wao wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati yako. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo:-

- | | |
|--|-----------------------|
| 1. Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb | - Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb | - M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Mohamed Juma Khatib, Mb | - Mjumbe |
| 4. Mhe. Ally Mohamed Keissy, Mb | - Mjumbe |
| 5. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb | - Mjumbe |
| 6. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb | - Mjumbe |
| 7. Mhe. Bahati Ali Abeid, Mb | - Mjumbe |
| 8. Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb | - Mjumbe |
| 9. Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb | - Mjumbe |

- | | |
|--|----------|
| 10. Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mb | - Mjumbe |
| 11. Mhe. John Wegesa Heche, Mb | - Mjumbe |
| 12. Mhe. Hamoud Abuu Jumaa, Mb | - Mjumbe |
| 13. Mhe. Msukuma Joseph Kasheku, Mb | - Mjumbe |
| 14. Mhe. Jesca David Kishoa, Mb | - Mjumbe |
| 15. Mhe. Rashid Ajari Akbar, Mb | - Mjumbe |
| 16. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb | - Mjumbe |
| 17. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb | - Mjumbe |
| 18. Mhe. Yosepher Ferdinand Komba, Mb | - Mjumbe |
| 19. Mhe. James Kinyasi Millya, Mb | - Mjumbe |
| 20. Mhe. Lameck Okumbo Airo, Mb | - Mjumbe |
| 21. Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb | - Mjumbe |
| 22. Mhe. Zubeda Hassan Sakuru, Mb | - Mjumbe |
| 23. Mhe. Hamida Mohamed Abdallah, Mb | - Mjumbe |
| 24. Mhe. Kiza Hussein Mayeye, Mb | - Mjumbe |
| 25. Mhe. Frank George Mwakajoka, Mb | - Mjumbe |
| 26. Mhe. Abdallah Ally Mtalea, Mb | - Mjumbe |

Mheshimiwa Spika, nitoe pia shukrani zangu za dhati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati kwa Mhe. Doto Mashaka Biteko(Mb) – Waziri wa Madini, Mhe. Stanslaus Haroun Nyongo(Mb) - Naibu Waziri wa Madini pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Profesa Simon Msanjila kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati yetu wakati wote.

Mheshimiwa Spika, Kwa namna ya kipekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Steven Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi, Ndg. Michael Chikokoto pamoja na Makatibu wa Kamati Ndg. Felister Mgonya na Ndg. Omary Magwinza kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha Taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 100 Wizara ya Madini kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 ambayo ni **Shilingi Bilioni 49,466,898,200**.

Mheshimiwa Spika, Naunga mkono hoja na Naomba kuwasilisha.

Dunstan Luka Kitandula

MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI

27 Mei, 2019

SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Mariam Ditopile, tunakushukuru. Sana sasa naomba nimwite Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Madini. Mheshimiwa Heche una nusu saa, sasa polepole Mura, taratibu. (*Kicheko*)

MHE. JOHN W. HECHE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MADINI:
Mheshimiwa Spika, napenda kuwasilisha Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, Utangulizi. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia uhai, afya njema na kunipa nguvu na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako tukufu ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Madini pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Hati Idhini Na.144 ya tarehe 22 Aprili, 2016 iliyofanyiwa marekebisho tarehe 15 Oktoba, 2017 majukumu ya Wizara ya Madini ni kubuni, kuandaa na kusimamia Sera, Mikakati na Mipango ya kuendeleza sekta ya Madini, kusimamia migodi na kuhamasisha shughuli za uchimbaji pamoja na utafutaji wa madini kwa kutumia tafiti za kijiofizikia na kijiolojia. Kuratibu na kusimamia uongezaji thamani madini kwenye biashara ya madini, kukuza ushiriki wa wazawa kwenye shughuli za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini nichini, kusimamia na kuratibu shughuli na maendeleo ya wachimbaji wadogo,

kusimamia taasisi na mamlaka zilizoko chini ya Wizara pamoja na kuratibu na kusimamia maendeleo na utekelezaji majukumu kwa watumishi wa Wizara. Wizara pia inasimamia taasisi sita ambazo ni Tume ya Madini Tanzania, Chuo cha Madini, Kituo cha Jiemolojia Tanzania, na Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (*Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative-TEITI*).

Mheshimiwa Spika, napenda pia kurejea Sera mbadala za CHADEMA, Toleo la Julai, 2018 kuhusu usimamizi madhubuti na endelevu wa Sekta ya Madini. Ili kuhakikisha sekta ya Madini inasimamiwa kwa maslahi mapana ya taifa na wananchi, CHADEMA tutahakikisha tunarekebisha sheria zote zinazosimamia madini, tutahakikisha tunakuwepo na fursa za mikopo kwa wachimbaji wadogo na wa kati, pamoja na kurudisha mazingira katika hali yake ya kawaida baada ya shughuli za uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kwamba madini ni kwa ajili ya vizazi vyote vya sasa na vijavyo, itahakikisha kwamba uwepo wa madini unatumika kama dhamana kwa ajili ya Serikali kupata fedha za kuwekeza kwenye miradi ya maendeleo ambayo ni endelevu, na hivyo CHADEMA hatutashindwa kupeleka fedha za miradi ya maendeleo kwa ajili ya kuendeleza madini.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Wizara katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 ilidhinishiwa jumla ya shilingi bil. 58,908,481,992. Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 19,620,964,000 zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli miradi ya maendeleo na shilingi 20,958,262,992 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, Fedha za Maendeleo Zilizopelekwa; katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara iliomba na kuidhinishiwa jumla ya shilingi Bilioni 19,620,964,000

hadi kufikia Februari, 2019 Wizara ilikuwa imeshapokea jumla ya shilingi milioni 100 tu, sawa na 0.5% ya bajeti yote ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Ina maana katika kipindi hicho fedha pekee zilizopelekwa ni shilingi milioni 100 kwa ajili ya wizara nzima kufanya shughuli za maendeleo. Kwa uwezo huu wa Serikali kushindwa kutoa hata asilimia moja ya fedha za miradi ya maendeleo, ni kushindwa kwa Serikali hii kutekeleza miradi ya maendeleo. Kwa maneno mengine Serikali imefikia kikomo cha uwezo wa kugharamia miradi ya maendeleo, na ushahidi wake ni namna ambavyo Serikali inaweza kukusanya na kutumia fedha. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujuu sababu za Serikali kutoa fedha ambazo hazifiki hata 1% ya bajeti ya maendeleo ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, ukimya na ufisadi wa *TANCO*. *National Development Cooperation* wallingia ubia na kampuni ya *pacific cooperation East African Limited* kwa kifupi *PCEA* ya Australia mnamo tarehe 03 Aprili mwaka 2008 kwa umiliki wa asilimia 30 Tanzania na asilimia 70 *PCEA* kwenye kampuni ya *TANCO Energy Ltd* kwa malengo ya kuendeleza uchimbaji wa makaa ya mawe, uzalishaji na usambazaji wa umeme katika mradi wa muhukuru Ndaka Kusini mwa Tanzania. Hata hivyo mnamo taehe 28 Aprili 2011 Kampuni ya *PCEA* ilibadili jina na kuwa *Inter-energy cooperation* ya Australia. Kampuni hiyo ndio inamiliki hisa za kampuni *inter- energy Tanzania Limited*.

Mheshimiwa Spika, taarifa zinaonesha kwamba *TANCOAL Energy Limited* kampuni msimamizi wa ubia haikutekeleza majukumu ya uendeshaji wa ubia huo kulingana na matakwa ya mkataba. Gharama kubwa za ukodishaji wa magari, mitambo mgodini zilizotokana na *TANCOAL* kushindwa kuwekeza kiasi cha dola milioni 20.49 kwa ajili ya ununuzi wa mitambo na kiasi cha Dola za Marekani milioni 1.41 kwa ajili ya ununuzi wa magari. Kushindwa huko kwa *TANCOAL* kumesababisha Kampuni hiyo kutumia dola za Kimarekani milioni 42.07 kwa ajili ya kukodisha mitambo na magari, gharama ambazo ni mara mbili zaidi ya kiasi kilichotakiwa kuwekezwa kwenye ununuzi wa

mitambo na magari kati ya mwaka 2012 na 2016. Jambo hili linaongeza gharama ya uendeshaji na kutia Serikali hasara. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Kampuni hii pia imeshindwa kujenga barabara ya kwenda mgodini kwa kiasi cha dola za Marekani milioni 14.49 kati ya mwaka 2012 hadi mwaka 2016, hivyo kuongeza gharama za uzalishaji. Gharama hizo ziliongezeka baada ya kampuni kutumia jumla ya dola za Marekani milioni 2.843 kwa ajili ya kukodi magari kutoka mgodini hadi sehemu ya mauzo umbali wa kilometra 40. Kutojengwa kwa barabara hiyo kumeongeza gharama za uendeshaji na kuondoa fursa ya kampuni kupata faida ambayo ndio chanzo cha Serikali kupata gawio. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nchi yetu sasa imekuwa ni shamba la bibi, taarifa za fedha za *TANCOAL* kwa miaka sita kati ya mwaka 2011 hadi 2016 zinaonesha kuwa gharama za utafutaji madini za shilingi bilioni 6.5 zilijumuisha shilingi milioni 880.07 isivyostahili. Gharama hizo ziliainishwa katika taarifa za fedha za mwaka 2013 hadi 2016 isivyostahili kwani utafiti wa madini ulikuwa umekamilika tangu mwaka 2012. Kuingizwa kwa gharama hizo katika taarifa za fedha za *TANCOAL* kuliathiri upatikanaji wa faida na kuonesha hasara ambapo Serikali haikuweza kupokea gawio wala kukusanya kodi stahiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2014 hadi 2016, *TANCOAL* walitumia jumla ya shilingi milioni 940.03 kwa shughuli zisizohusiana na uchimbaji wa madini kinyume na mkataba wa ubia. Hali kadhalika, jumla ya dola za Marekani milioni 3.3 zililipwa kama gharama za shughuli za madini kwa kampuni Tanzu ya *Intra Energy* inayojulikana kama *TANZCOAL* ya nchini Malawi. Yaani fedha zinavunwa Tanzania zinakwenda kulipwa Malawi kwa ajili ya shughuli za kampuni hiyo ambayo iko Malawi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, matumizi hayo tajwa ni kinyume cha mkataba na yamesababisha *TANCOAL* kutoripoti faida hivyo kushindwa kutoa gawio kwa mbia ambaye ni Serikali

pia kutolipa kodi stahiki kwa Serikali. Mapitio ya taarifa za *TANCOAL* kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2014 yalionesha kuwa *TANCOAL* imechangia jumla ya shilingi milioni 993 katika shughuli za maendeleo ya jamii katika maeneo ya Ngaka na Songea kama sehemu ya wajibu wake kwa jamii (*CSR*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo uchunguzi na taarifa kutoka vyanzo mbalimbali vimebaini kuwa ni kiasi cha shilingi milioni 75 tu na wastani wa milioni 15 kwa mwaka ndicho kilichotolewa na Kampuni ya *TANCOAL* kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya jamii, badala ya wastani wa shilingi milioni 198 kwa mwaka. Upo ushahidi wa kuthibitisha jambo hili, hivyo Kampuni ya *TANCOAL* ilitumia kiasi cha shilingi milioni 917.06 kwa matumizi mengineyo kwa udanganyifu kuwa inasaidia jamii ya jirani na mgodi. Kambi Rasmi ya Upinzani haioni kama kitendo kinachofanywa na kampuni hiyo kina utofauti na utakatishaji wa fedha na au uhujumu uchumi kwa Taifa hili. Kwa mantiki hii sasa, tunaitaka Serikali kiliarifu Bunge hili Tukufu hatua ambazo imechukua dhidi ya kampuni hii na mstakabali wa ubia huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu dosari katika umiliki wa hisa ya *Intra Energy Tanzania Limited* na *NDC*. Kifungu cha 3.2.1 cha Makubaliano ya Ubia kati ya *Intra Energy Tanzania Limited* na *NDC* kinabainisha kuwa, wabia watachangia mtaji kwa uwiano wa asilimia 50 kwa 50. Aidha, Kifungu 3.2.1 kinaainisha kuwa katika hatua ya upembuzi yakinifu, *PCEA* na *NDC* watakuwa na uwiano wa hisa 70 kwa 30 ambapo *PCEA* na *NDC* wanapaswa kutoa fedha.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, rasilimali husika ya makaa ya mawe haikizingatiwa kuwa sehemu ya mchango wa Kampuni ya *NDC* kwa ubia huo. Kuzingatia thamani ya rasilimali za makaa ya mawe kama mchango wa *NDC* kulisababisha *PCEA* kuwa na 70 licha ya kuchangia fedha ya mtaji kiasi cha milioni 1.7 pekee za Kitanzania ambacho tunaamini kilikuwa ndani ya uwezo wa *NDC* hivyo kukosekana mantiki ya ubia huo.

Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2013 hadi 2017, yalifanyika malipo ambayo hayakuwa sahihi kwa *Intra Energy Tanzania Limited* kama malipo ya menejimenti jumla ya shilingi bilioni 1.4 ambazo zililipwa kama ada ya menejimenti kwenda kwa Kampuni ya *Intra Energy Corporation* ya Australia. Matumizi hayo yalionyeshwa kama mkopo unaopaswa kulipwa na *TANCOAL*. Hata hivyo, mapitio ya maamuzi ya Bodi ya *TANCOAL* ya tarehe 15 Novemba, 2012 yalibainisha kuwa Bodi iliamua kusiwepo na makubaliano ya huduma za usimamizi (*Management Service*) na badala yake Kampuni ya *Intra Energy* ilipwe gharama halisi zilizoagizwa. Ni kwa msingi huo, gharama za shilingi bilioni 1.4 zililipwa kimakosa na zinastahili kurejeshwa *TANCOAL*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali hii imekuwa ikijinasibu kutetea maslahi ya Taifa hili na kwa kuwa moja ya taarifa za Kamati ya Bunge lako Tukufu zinaonesha ujisadi mkubwa, ukwepaji wa kodi pamoja na jitihada zinazofanywa kuikosesha mapato Serikali au kupitia ukosefu wa gawio au kodi; na kwa kuwa Ripoti ya Mkaguza na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali katika ripoti ya mwaka 2016/2017 unaonekana ujisadi wa shilingi milioni 800, ujisadi wa shilingi milioni 940 na dola za kimarekani milioni 3.3 ambazo ni fedha Serikali imezipoteza na nyingine zinapaswa kureshwa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kauli ya Serikali kuhusu mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, moja, ni lini gharama za shilingi bilioni 1.4 zilizolipwa kimakosa zitarejeshwa na *TANCOAL*? Mbili, Serikali inachukua hatua gani dhidi ya watendaji wa *TANCOAL* ambao wanashiriki kuhujumu uchumi wa Taifa kupitia kampuni hii wakishirikiana na wabia mwenza?; Tatu, ni lini fedha za mrahaba zaidi ya dola za Marekani milioni 3.3 ambazo zimepotea kutokana na usimamizi dhaifu zitapatikana na hatua gani Serikali inachukua dhidi ya wasimamizi hao dhaifu?; Nne, Serikali ina mpango gani dhidi ya mkataba huo wa ubia unaoendelea kuandikisha hasara kila mwaka na ikiwa hakuna uhakika wa kuendelea na biashara siku zijazo?; na Tano, ni lini sasa Serikali itaunda upya

Shirika la *National Development Corporation* na kupitia mikata yake yote ili kufikia lengo kuanzisha *NDC?* (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Chuma wa Mchuchuma na Liganga, nitaomba mambo yote hayo yaingie na yasomeka kama yalivyo na nitaomba Mheshimiwa Waziri ayatolee ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, naenda 60, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kupata majibu kutoka Serikalini, ni lini urasimu unaokwamisha mradi huo utakwisha ikiwa ni pamoja na kuangalia masharti mapya ya uwekezaji chini ya Sheria ya Madini ya mwaka 2017? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Sekta ya wachimbaji wadogo; wachimbaji wadogo wa madini ni wadau muhimu sana kwa ustawi wa Taifa letu. Pamoja na umuhimu huo kwa uchumi wa Taifa hili, wanakumbwa na matatizo mengi ambayo yanahitaji jitihada za Serikali ili kuweza kuwasaidia. Taarifa ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayo, inaonesha kuwa hadi kufikia Juni 30, 2018, kulikuwa na bakaa ya dola za Kimarekani 622,117 na shilingi milioni 130 katika Benki ya Uwekezaji Tanzania (*TIB*) zilizobaki kutoka sehemu ya ruzuku ya dola za Marekani 3,000,000 ambazo zilitolewa na Benki ya Dunia kwa Wizara ya Nishati na Madini mwaka 2015/2016 kwa ajili ya uendelezaji rasilimali madini nchini ili zitolewe kama ruzuku kwa ajili ya kuendeleza wachimbaji wadogo. Kwa hiyo hapa tunataka kujua ni lini Serikali itatoa fedha hizo kwa ajili ya wachimbaji wadogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, faini ya bilioni 5.6 ya mgodi wa dhahabu wa *ACACIA, North Mara*. Siku chache zilizopita Serikali kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) ilipiga faini ya shilingi bilioni 5.6 mgodi wa dhahabu wa *North Mara, ACACIA* uliopo Nyamongo wilayani Tarime, kwa kushindwa kuthibiti bwawa la maji yenye sumu na hivyo kuhatarisha afya za wakazi wanaozunguka mgodi. Kitendo hiki cha Serikali kupiga faini Kampuni ya *Accacia* inayomiliki mgodi wa North Mara kinathibitisha malalamiko ya muda mrefu ya wananchi wa Tarime wanaozunguka

mgodi huo. Malalamiko ya wananchi hawa yamewahi kuchunguzwa na Kamati mbalimbali za Bunge ikiwemo Kamati ambayo Mheshimiwa Spika uliongoza wewe. Kamati hiyo katika maazimio yake iliagiza Serikali ichukue hatua haraka kuchunguza suala hilo na kutoa malipo ya fidia.

Mheshimiwa Spika, madhara yaliyotokana na mgodi wa Nyamongo, *North Mara* kutiririsha maji yenyе sumu kwenye makazi ya raia; wakati iliyokuwa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira chini ya Mwenyekiti wake sasa ni Spika wa Bunge hili ikiagiza Serikali kuchunguza suala hilo, kutoa malipo ya fidia kwa waathirika, ni bora kufahamu athari ambazo ziliwapata wakazi wanaozunguka Mgodi wa Nyamongo. Tumeainisha athari mbalimbali ikiwemo wananchi kuchubuka ngozi, wengine kufariki, ng'ombe zaidi ya 500 kufa na maeneo ambayo ya Kwinyunyi na Kwimange kuharibika kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa nakuja kwenye hatma ya waathirika wa maji yenyе sumu; baada ya kueleza kwa kina athari hizo ambazo zimewakumba wananchi hawa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kauli ya Serikali kuhusu kiasi ambacho wananchi wanaozunguka Mgodi wa *North Mara* watalipwa kama fidia kutokana na madhara waliyoyapata yanayotokana na Mgodi wa *North Mara* kutiririsha maji yenyе sumu kuanzia mwaka 2007 kwenye makazi ya watu na kuwasababishia magonjwa ya ngozi, kupoteza mifugo na maeneo yao ya kilimo. Naomba pia hatma ya fidia ya wananchi wa Tarime Waziri aje aijibu hapa ingawaje kwenye swali asubuhi alijibu, lakini nahitaji majibu zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ahadi katika sakata la makinikia na majadiliano yasiyofikia kikomo; mnamo mwezi Machi 2017, Wizara ya Nishati na Madini iliandika barua kwa umma kuwajulisha wafanyabiashara na makampuni yanayojishuhulisha na shughuli za uvunaji madini kuacha mara moja shughuli za usafirishaji wa makinikia (*concentrates*) na mawe yenyе madini ya metaliki kama vile dhahabu, shaba, nikeli na fedha. Pamoja na katazo hilo, Mheshimiwa

Rais aliunda Kamati mbili za uchunguzi wa usafirishaji wa makinikia nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine, ripoti zote zilizungumzia hasara kubwa tunayoipata kama Taifa kutokana na Sheria mbovu za madini, mikataba mibovu iliyoingiwa baina ya Serikali ya CCM na wawekezaji. Ripoti zote mbili zilijikita zaidi katika kubaini viwango vya madini vilivyopo katika makinikia na mikataba ya uchenjuaji ambayo haikuwa wazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, udhaifu katika sakata zima la makinikia; sakata la makinikia lilikuwa ni sakata la kisiasa liliojawa na ahadi nyingi ambapo mpaka sasa inaigharimu Serikali kutokana na maamuzi hayo ya kukurupuka.

Kwa takribani miaka zaidi ya 20 Wabunge kutoka vyama vya upinzani walikuwa wakidai uwepo wa uwazi katika mikataba ya madini na ubovu wa mikataba mingi ikiwemo mkataba wa Buzwagi, Resolute, Bulyanhulu na kadhalika. Katika awamu tofauti tofauti za Serikali Mawaziri ambao ndio Watendaji Wakuu wa Serikali walikuwa wakifumbia macho pamoja na kupigwa kelele nyingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunakumbuka mwaka 2017, kampuni hii ilituhumiwa kukwepa kodi na hivyo kuzua mtafaruku mkubwa na Serikali wakati huo. Katika makubaliano Barrick iliahidi kulipa Serikali kishika uchumba cha shilingi milioni 700 wakati mazungumzo zaidi yakiendelea ili kuona ni namna gani nchi itanufaika lakini hadi sasa hata hicho kishika uchumba chenyewe hakijalipwa, huku ACACIA wakiendelea kuchimba dhahabu katika migodi wanayomiliki hapa Tanzania. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Heche, hapo aliyeokuwa anachumbiwa ni Serikali inachumbiwa. Sijui Kiswahili hicho kama ni sawasawa. (*Kicheko*)

MHE. JOHN W. HECHE - MSEM AJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MADINI: Mheshimiwa Spika, ndivyo alivyokiita Mheshimiwa Profesa Kabudi, kishika uchumba. (*Makofi*)

SPIKA: *Okay!*

MHE. JOHN W. HECHE - - MSEM AJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MADINI: Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kufahamu, kwa nini kishika uchumba hicho hakijalipwa hadi sasa, ikiwa *Accacia* kweli walipaswa kulipa malimbikizo ya kodi na tozo na hadi sasa.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi nimekuona, Mheshimiwa Waziri wa Nchi nimekuona. Mheshimiwa Heche kwa muda kidogo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(g) na Kanuni ya (f) kwa kweli lugha nydingine hata kama ni lugha ambazo zilizungumzwa nje ya ukumbi huu, lakini tunapoingia kwenye ukumbi wetu tuna lugha zetu za Kibunge ambazo zinaweza zikaleta *message* ambayo inalingana na hadhi yetu ya Kibunge. Kwa hiyo, hiyo lugha ambayo inatumika kwenye taarifa hii, mambo ya kishika uchumba kwenye ripoti ambazo ni ripoti rasmi za Bunge, nadhani angetofautisha lugha ambayo ilikuwa inatumika kuelezea huko nje na lugha rasmi ya Bunge ambayo inatumika kwenye ripoti.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba lugha hii kwa kweli ni ya kudhalilisha dhalilisha, siyo lugha rafiki, haipendezi. Kwa hiyo, naomba kwa madaraka uliyonayo kwa kweli iondolewe tu katika mjadala wetu wa leo na katika taarifa yetu ambayo ni taarifa yenye hadhi, ambayo ni taarifa ya Kibunge, lugha hii iondoke. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Ester.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, namheshimu sana dada yangu, kwanza wala hakuwa na mpango wa kusimama, huo ndiyo ukweli. Mheshimiwa Heche ame-*quote* maneno aliyosema Waziri, kwa hiyo, kama suala la udhalilishaji alilianza Mheshimiwa Waziri Kabudi na siyo Mheshimiwa Heche. Sasa tusiwe na *double standard* kama Bunge, ikitoka upande wenu ni sawa, ikitoka upande huu si sawa, hakuna cha kutoa hapo imetoka kwenu. (*Mkofi*)

SPIKA: Ambacho ningependa kukielekeza, Mheshimiwa Heche utaona hotuba yako hatujaigusia meza, hatujaiingilia popote wala nini, haya maneno mimi leo ndiyo nasikia kwa mara ya kwanza. Nasema ukweli wangu, kama yalisemwa huko, yalisemwa huko lakini kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano lugha hiyo siyo lugha sahihi. Tutoe lugha ya kwamba Kampuni inayoitwa *Acacia* inatoa kitoa uchumba kwa Serikali, kwa hiyo Serikali inaoleta na Kampuni ya wazungu? Yaani sisi wengine Kiswahili kidogo kinatupa shida, kwa hiyo kwa ajili yetu sisi na kwa ajili ya Bunge tafuta tu neno lingine hata kama la Kiingereza linalomaanisha hicho kitu lakini hili neno kishika uchumba hili kidogo lina ukakasi.

Kwa hiyo endelea Mheshimiwa kwa sababu muda wetu ni mdogo lakini tafuta neno la ku-*substitute* huo ujumbe wako ubakie uleule, lakini lile neno linatupa shida kidogo, kwamba yaani sisi wote tuolewe na wazungu mbona haiwezekani, na wewe Mheshimiwa Heche ukiwemo ndani yake. (*Makofi/Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Profesa ametupotosha.

MHE. JOHN W. HECHE - - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MADINI: Mheshimiwa Spika, nakuheshimiwa sana na nisingependa kutoa neno lolote kwenye maelekezo uliyonipa lakini mimi narudia ku-*insist* kwamba fedha ambazo tuliahidiwa kutangulizwa wakati mazungumzo yanaendelea zilitamkwa humu ndani ya Bunge na jina lililotumika ni hilo hilo kwamba kishika uchumba wakati majadiliano yanaendelea. Kwa hiyo naliondoa lakini ni fedha ambazo tunataka tujue kwa nini

hazijalipwa mpaka sasa wakati majadiliano yakiwa yanaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile katika ripoti ya makinikia illainisha takriban aina 11 za madini yaliyopo katika makinikia. Serikali ilikubaliana na ACACIA kulipa asilimia 4 ya mrahaba tu bila kuangalia aina nyingine za madini yaliyomo katika makinikia. Hii yote ni kutokana na mikataba mibovu na utendaji kazi uliokosa ufanisi katika taasisi mbalimbali za Serikali zinazojishughulisha na madini.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho. Napenda kumalizia hotuba yangu kwa kusisitiza mambo yafuatayo; Serikali iwaambie Watanzania hatma ya majadiliano ya kampuni ya Acacia na fedha ambazo ilipaswa kulipa, ni kwanini fedha hizo hazijalipwa. Ikiwa makampuni haya yalikwepa kodi zaidi ya trillioni 400 na kitu ambazo Watanzania tuliambiwa, ni kwanini hadi sasa bado hayajalipa fedha hizo; na ikiwa Serikali iliudanganya umma, ni lini sasa Serikali itatoa taarifa sahihi kuhusu fedha hizo. Mbili, je, ni lini sheria zilizopitishwa kwa msukumo mkubwa wa aliyekuwa Waziri wa Sheria Profesa Kabudi kuhusu ulinzi wa rasilimali, *The Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty Act*, 2007 pamoja na marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2017 ambazo kwa pamoja zinaathiri Sekta ya Uwekezaji kwa kutumia mashauri ya kibiashara ya makampuni makubwa...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Dakika moja umalizie.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, tatu, wananchi walioathirika na maji ya sumu kutoka Mgodi wa North Mara watalipwa kiasi cha fedha kama sehemu ya fidia ya madhara waliyoyapata.

Mheshimiwa Spika, nne ni nini kauli ya Serikali kuhusu bakaa ya Dola za Marekani 617,000 na shilingi 130,000,000 zilizobaki kutoka sehemu ya ruzuku ya Dola za Marekani

3,000,000 zilizotolewa na Benki ya Dunia zitatolewa kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, tano, Serikali inachukua hatua gani dhidi ya watendajiw aliohujumu uchumi wa taifa katika kampuni ya migodi ambayo Serikali inamiliki hisa, migodi ambayo Serikali mara zote imekuwa ikipata hasara kwa uzembe wa watendaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. Naomba hotuba yangu yote kwa sababu nimesoma *summary* iingie kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge. Nashukuru sana. (*Makofii*)

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI KATIKA WIZARA YA MADINI, MHESHIMIWA JOHN
HECHE (MB), AKIWASILISHA MAPITIO YA BAJETI YA WIZARA
KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 PAMOJA MAONI YA
KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO
NA MATUMIZI YA FEDHA, KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020
– KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*Yanatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu
za Bunge, Toleo la Januari, 2016*

A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kunijalia uhai, afya njema na kunipa nguvu na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako tukufu ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Madini pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

2. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Hati Idhini Na.144 ya tarehe 22 Aprili, 2016 iliyofanyiwa marekebisho tarehe 15 Oktoba, 2017 majukumu ya Wizara ya Madini ni kubuni, kuandaa na kusimamia Sera, Mikakati na Mipango ya kuendeleza sekta ya Madini, kusimamia migodi na

kuhamasisha shughuli za uchimbaji pamoja na utafutaji wa madini kwa kutumia tafiti za kijofizikia na kijiolojia, kuratibu na kusimamia uongezaji thamani madini kwenye biashara ya madini, kukuza ushiriki wa wazawa kwenye shughuli za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini nchini, kusimamia na kuratibu shughuli na maendeleo ya wachimbaji wadogo, kusimamia taasisi na mamlaka zilizoko chini ya Wizara pamoja na kuratibu na kusimamia maendeleo na utekelezaji majukumu kwa watumishi wa Wizara. Wizara pia inasimamia taasisi sita ambazo ni Tume ya Madini Tanzania, Chuo cha Madini, Kituo cha Jemolojia Tanzania, na Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative-TEITI).

3. Mheshimiwa Spika, Napenda pia kurejea Sera mbadala za CHADEMA, Toleo la Julai, 2018 kuhusu usimamizi madhubuti na endelevu wa Sekta ya Madini. Ili kuhakikisha sekta ya Madini inasimamiwa kwa maslahi mapana ya Taifa na wananchi, CHADEMA tutahakikisha tunarekebisha sheria zote zinazosimamia madini, tutahakikisha tunakuwa na Mfuko wa Taifa wa Maendeleo, tutahakikisha kunakuwepo na fursa za mikopo kwa wachimbaji wadogo na wa kati, pamoja na kurudisha mazingira katika hali yake ya kawaida baada ya shughuli za uchimbaji.

4. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kwamba madini ni kwa ajili ya vizazi vyote vya sasa na vijavyo na kuwa, itahakikisha kwamba uwepo wa madini unatumika kama dhamana kwa ajili ya Serikali kupata fedha za kuwekeza kwenye miradi ya maendeleo ambayo ni endelevu, na hivyo CHADEMA hatutashindwa kupeleka fedha za miradi ya maendeleo. Uwezo wetu wa kupeleka fedha za Bajeti utakuwa mkubwa kuliko uwezo wa Serikali ya sasa wa kupeleka 0.5% ya bajeti ya miradi ya maendeleo kwa wananchi, katika mwaka wa fedha 2018/2019.

5. Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo CHADEMA tunaamini kwamba madini yanasaidia kukabiliana na changamoto za kiuchumi kama vile mfumuko wa bei,

kuyumba kwa soko la hisa na mitaji na pia rasilimali hizo ni muhimu kukabiliana na m dororo wa uchumi kwa ujumla. Wananchi watanufaika kwa kuwa na fursa ya mikopo yenye masharti nafuu kwa wachimbaji wadogo na wa kati na pia fursa za ajira zenye kipato zitapanuka. Pamoja na hayo huduma za kijamii zitaboreshwa kwa sababu Serikali itapata mapato kutoka kwenye makampuni ya uwekezaji na kuititia utaratibu wa makampuni ya uwekezaji kusaidia jamii.

6. Mheshimiwa Spika, Nimeona ni vyema kuanza na utangulizi wa Sera Mbadala kutokana na Sera zilizopo kushindwa kuwanufaisha wananchi kama walivyotarajia, Maoni ya Kambi ya Upinzani Bungeni yamejielekeza kuonesha namna ambavyo Wizara imeshindwa kutekeleza majukumu yake kulingana na Bajeti iliyopata na kwa kufanya hivyo hotuba yetu imeonesha mbadala wa sera zilizoshindwa za Chama Cha Mapinduzi.

B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

7. Mheshimiwa Spika, Wizara katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 iliidhinishiwa jumla ya shilingi bil. 58,908,481,992. Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 19,620,964,000 zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli Miradi ya Maendeleo na shilingi 20,958,262,992 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

I. Fedha za Maendeleo Zilizopokelewa

8. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara iliomba na kuidhinishiwa jumla ya shilingi Bilioni 19,620,964,000 hadi kufikia Februari, 2019 Wizara ilikuwa imeshapokea jumla ya shilingi milioni 100 tu, **sawa na 0.5%** ya bajeti yote ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Kwa uwezo huu wa Serikali kushindwa kutoa hata asilimia moja ya fedha za miradi ya maendeleo, ni kushindwa kwa Serikali hii kutekeleza miradi ya maendeleo, kwa maneno mengine Serikali imefikia kikomo cha uwezo wa kugharamia miradi ya maendeleo, na ushahidi wake ni

namna ambavyo Serikali inaweza kukusanya na kutumia fedha. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua sababu za Serikali kutoa fedha ambazo hazifiki hata 1% ya bajeti ya maendeleo ya Wizara.

9. Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha miaka miwili sasa Serikali ya Chama Cha Mapinduzi imeshindwa kupeleka fedha kwenye miradi ya maendeleo ya Wizara hii. Mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali ilitoa fedha za kugharamia Miradi ya Maendeleo kwa Wizara ya Madini kwa 3.83%, mwaka wa fedha 2018/2019 hali ni mbaya zaidi kwa kuwa Serikali sasa imetoa fedha za kugharamia Miradi ya Maendeleo kwa asilimia 0.5%. ya bajeti yote ya Miradi ya Maendeleo iliyopangwa na kuitishwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka majibu kutoka Serikalini sababu hasa za kushindwa kupeleka fedha za maendeleo kwenye Wizara hii kwa miaka miwili mfululizo?

10. Mheshimiwa Spika, kushindwa kwa Serikali kupeleka fedha za Miradi ya Maendeleo kama ilivyoidhinishiwa na Bunge lako tukufu ni matokeo ya sera mbaya za Serikali ya CCM ambazo zinasababisha Serikali hii kukosa fedha na hivyo kushindwa kupeleka fedha kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Ndiyo sababu CHADEMA katika sera mbadala tunasema, tutaanzisha Mfuko Maalumu wa fedha zinazotokana na uwekezaji wa madini ili zitumike katika miradi mikubwa yenye manufaa kwa nchi na kutoa huduma za kijamii kwa wananchi, Sera hii itaondoa tatizo la Serikali kushindwa kupeleka Fedha za Miradi ya Maendeleo kama ilivyo sasa.

11. Mheshimiwa Spika, Ni dhahiri kwamba miradi yote ambayo Wizara ilitarajia kutekeleza katika mwaka wa fedha 2018/2019 haijatekelezwa kwa sababu Serikali hii haina fedha za kutekeleza Miradi hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kufahamu ukiacha Sera za Serikali ya CCM ambazo zimetufikisha hapa tulipo, Serikali inakwama wapi? Ni muhimu kufahamu ili Bunge liweze kuishauri na kuvisimamia Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

II. Fedha zilizotolewa bila Idhini ya Bunge

12. Mheshimiwa Spika, taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019 zinaonesha kwamba Wizara ilipokea shilingi bilioni moja (**1,000,000,000.00**) kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Wizara eneo la Ihumwa, Dodoma. Pamoja na malengo mazuri ya ujenzi wa Ofisi, Kambi Rasmi ya Upinzani tunaona siyo sawa Wizara ya Fedha na Serikali kutoa fedha ambazo hazikuwa kwenye bajeti, ikiwa Serikali ilikusudia kujenga Ofisi hiyo, kwa nini haikuomba bajeti yake ndani ya Bunge hili ili kuidhinishiwa na Bunge hili? Na ikiwa Serikali ilipata wazo hilo baadaye kwa nini Serikali haikuafuta utaratibu wa kisheria wa Bajeti ya Nyongeza kwa matakwa ya sheria za Nchi? Utaratibu huu, ambao ni kinyume na kifungu cha 43 cha sheria ya Bajeti, Sura ya 439 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2015 umeanza kuota mizizi katika Serikali hii ya Awamu ya Tano kuvunja na kudharau sheria za nchi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuacha mazoea ya kuvunja sheria za nchi ambazo walikula viapo kuzilinda.

13. Mheshimiwa Spika, Mara zote utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa miaka yote tunaambiwa unazingatia pamoja na mambo mengine; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2015 - 2020; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21); Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; Sera ya Madini ya Mwaka 2009; Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Marekebisho yake ya Mwaka 2017 na Kanuni zake. Vilevile, umezingatia maoni na ushauri wa Kamati Maalum ya Mheshimiwa Rais ya kuchunguza aina, wengi na thamani ya madini, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kujua je, utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, na maelekezo ya Serikali maana yake ni kupeleka fedha za Miradi ya maendeleo kwa kiwango cha 0.5%?

C. HATMA YA SEKTA YA MADINI NCHINI

14. Mheshimiwa Spika, Sekta ya madini imekuwa haifanyi vizuri tofauti na matarajio ya walio wengi nchini. Utajiri mkubwa wa madini yaliyoko nchini, hauendani kabisa na hali ya umaskini mkubwa wa wananchi. Mpaka sasa **45% tu ya**

mauzo ya nje ya nchi yanategemea madini huku nchi yetu ikiwa ni ya 4 Barani Afrika kwa uzalishaji wa madini hususani ya dhahabu. Ni wazi kuwa bado wananchi walio wengi hawanufaiki na sekta hii na taifa halipati mapato stahiki kutokana na madini.

15. Mheshimiwa Spika, sekta ya madini imeshindwa kutoa mchango wenye manufaa katika bajeti ya serikali. Kwa mujibu wa hotuba ya Naibu Waziri aliyoitoa tarehe 15 Januari 2018 akizungumza na Wakuu wa Idara na Vitengo vya Wizara ya Madini Ofisi Kuu Dodoma alisema mpaka sasa sekta ya madini huchangia 3.5% katika pato la taifa.

16. Mheshimiwa Spika, ni fedheha kwa nchi yetu iliyozungukwa na madini na miamba ya aina mbalimbali kushindwa kukusanya kodi na maduhuli kiasi cha kutosheleza angalau mahitaji ya bajeti ya Wizara nne. Mfano, kwa mujibu wa ripoti ya Jiolojia ya Mwaka 2007 kuhusu aina za madini na kiwango cha madini nchini inasema nchi yetu ina aina 5 kuu za madini yakiwemo madini ya metali inayojumuisha madini ya **dhahabu takribani tani 2,222**, chuma (**iron ore takribani tani milioni 103**,**nikeli takribani tani milioni 209**, kobalti na fedha. Aina ya pili ya madini ni yale ya vito inayojumuisha madini ya almasi ambapo nchi yetu ina **takribani karati milioni 50.9**,**tanzanite takribani tani 12.60**, yakuti, garnets na lulu. Aina ya tatu ni madini ya viwandani kama vile chokaa,**magadi soda takribani tani mil 109 (soda ash)**, jasi (**gypsum**) ambapo tuna takribani tani mil 3, chumvi na **fosfet(phosphet) takribani tani mil 577.4** Aina ya nne ni madini yanayozalisha nishati kama vile **makaa ya mawe takribani tani mil 911**, na uranium. Aina ya tano ni madini ya ujenzi kama vile kokoto, mchanga na madini kwa ajili ya tarazo.

17. Mheshimiwa Spika, mpaka sasa katika soko la dunia mathalani soko la dhahabu kwa wastani aunce **1 huuzwa kati ya dola 1,296**, na kilo moja ya dhahabu huuzwa mpaka dola **41,696 sawa na shilingi milioni 96,528,700** kwa **exchange rate ya shilingi 2,300**. Pamoja na gharama nydingine nydingi kuanzia kwenye uchimbaji mpaka kwenda sokoni bado nchi yetu ina uwezo wa kukusanya fedha nydingi kupitia sekta ya

madini ambayo kwa sasa imekuwa mzigo mkubwa kwa wananchi kwa kuwa wengi wao hawanufaiki.

18. Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo sekta hii imeshindwa kuwa kipaumbele cha kutoa ajira kama ambavyo kwa nchi nyingine imekuwa ikichangia kiasi kikubwa cha ajira hususani kwa vijana. Mfano, katika **nchi ya Afrika ya Kusini**, sekta hii **inatoa ajira takribani 30,000** kwa mwaka ikilinganishwa na hapa nchini. Kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa na Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania ya Mwaka 2015 inaonyesha kuwa sekta rasmi ya uchimbaji madini **ilitoa ajira 7,355 ambazo** ni za moja kwa moja na takribani ajira 3,000 za wakandarasi tu. Mathalani, kwa mwaka 2015, sekta hii ya madini ilipunguza wafanyakazi **kutoka 7,335** hadi kufikia **6,205** wenye ajira za moja kwa moja kwa kipindi cha mwaka 2011 pekee.

19. Mheshimiwa Spika, hii ni sawa na **punguzo la takribani 15%** ya punguzo la ajira katika sekta ya madini. Mwaka 2017, takribani ajira za wafanyakazi wapatao 2,000 walipunguzwa kutoka kampuni ya Acacia pekee. Kati yao wafanyakazi 1,200 kutoka mgodi wa Bulyanhulu na wakandarasi wapatao 800 kutoka kwenye kampuni zenyenye zabuni kwenye mgodi.¹ Hili ni anguko kubwa la ajira nchini kwa kampuni moja kusimamisha idadi kubwa ya wafanyakazi kiasi hicho. Maana yake ni kuwa familia zilizokuwa zikitegemea kupata riziki kuititia mgodi huo zimeachwa katika lindi kubwa la umaskini. Vilevile, Serikali kuititia mifuko ya hifadhi nayo imekosa kodi na hivyo kupunguza patola serikali. Hizo ni baadhi tu ya athari ambazo zimejitokeza kutokana na kuperomoka kwa sekta hii ya madini.

D. MAPITIO YA TAASISI ZILIZOCHINI YA WIZARA YA MADINI

i. Tume ya Madini

20. Mheshimiwa Spika, Tume ya Madini iliundwa kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 2010, Sheria ya Marekabisho

¹ Gazeti la Mwananchi; Bulyanhulu yapunguza wafanyakazi 2,000

Anuai Na. 7 ya Mwaka, 2017. Mamlaka ya kuianzisha Tume na majukumu yake yameainishwa katika kifungu cha 21 na kifungu cha 22, ambapo, mionganini mwa majukumu ya Tume hiyo ni kusimamia, kuratibu, kupanga, kudhibiti na kutekeleza masuala na shughuli zote zinazohusu madini na pia kuishauri Serikali kuhusiana na shughuli zote zinazohusu Sekta ya Madini nchini.

21. Mheshimiwa Spika, Tume ya madini ni chombo chenye mamlaka kamili ya kushitaki au kushitakiwa pale inapobidi. Changamoto kubwa ambayo inaikabili tume ni kutokueleweka kwa sheria ya madini kwa wadau wa madini na hivyo kusababisha ugumu kwa Tume kukusanya baadhi ya tozo mbalimbali zinazotakiwa kwa mujibu wa Sheria ya Madini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri Tume ya Madini kuwa na mkakati kabambe wa kutoa elimu kwa umma mara kwa mara na kutumia njia mbalimbali kama vile televisheni, redio za kitaifa na kijamii pamoja na mitando ya kijamii ili umma wa watanzania uelimike kuhusu Sheria ya Madini , kazi na mamlaka ya Tume ya Madini.

**ii. Taasisi ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali
Madini, Mafuta na Gesi Asilia Tanzania (TEITI)**

22. Mheshimiwa Spika, Mpango wa Uwazi na Uwajibikaji Tanzania katika sekta ya Mafuta, gasi na madini, ulianzishwa chini ya Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji ya Mwaka 2015 kwa lengo la kukuza na kuboresha Uwazi na uwajibikaji katika uvunaji wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia. Mpango huu unaratibiwa chini ya Wizara ya Madini.

23. Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwake, taasisi hii imekuwa ikikabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo kutokuwa na vyanzo vya uhakika vya fedha katika kutekeleza mipango na shughuli zake mbalimbali. Katika mapitio ya taarifa ya shughuli zilizotekelizwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019, taasisi hii imeshindwa kutekeleza shughuli nyingi zilizopagwa kutekelezwa kwa mwaka husika kutohana na uhaba wa rasilimali fedha. Kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019 jumla ya shilingi 1, 3385,964,000 zilizopitishwa na Bunge, hazikutolewa.

24. Mheshimiwa Spika, Taarifa ya TEITI haioneshi na au kufafanua kwa kina kuhusu matumizi mengineyo katika bajeti yaani (OC) yalitumika katika matumizi gani hasa kutokana na kwamba taasisi haikupokea kiasi chochote cha fedha kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Pamoja na hilo, taarifa kuu ya TEITI ya utekelezaji kwa mwaka 2016/17 na 2017/18 hazijatolewa hadi leo, ingawa, kuna maelezo ya kuanza kwa utaratibu wa kumtafuta mtaalamu mshauri wa kuanda taarifa husika. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kwamba TEITI inapaswa kutoa mrejesho wa hatua zilizofanyika katika kutekeleza jukumu la utolewaji wa taarifa tajwa.

25. Mheshimiwa Spika, Miongoni mwa majukumu ya TEITI ni pamoja na kuanzishwa kwa rejista ya taarifa kwa Umma kuhusu wamiliki wa hisa katika kampuni za madini, mafuta na gesi asilia, ila hakuna maelezo yoyote katika taarifa kuhusu hatua za utekelezaji wa uanzishwaji wa rejista hiyo kama ilivyositisizwa na aliyekuwa Waziri wa Madini, Mh. Angella Kairuki tarehe 25/10/2018, jijini Dodoma wakati akizindua kamati ya tatu ya TEITI. Rejista ina umuhimu mkubwa katika kuboresha uwazi katika sekta hii na pia itasaidia kuzuia upotevu wa rasilimali na mapato yatokanayo na rasilimali madini, mafuta na gesi asilia. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia TEITI kutoa mrejesho kwa Umma kuhusu hatua iliyofikiwa ya uanzishwaji wa rejista.

26. Mheshimiwa Spika, Taarifa ya TEITI imeonesha mionganoni mwa mafanikio kwa mwaka 2018/19 ilikuwa ni kuongezeka kwa uwazi wa matumizi ya mapato ya halmashauri yanayotokana na tozo kutoka kampuni za uchimbaji madini, mafuta na gesi asilia. Hata hivyo hakuna maelezo ya kutosha kuonesha ni halmashauri zipi na iwapo ongezeko hilo ni kwa kiasi gani ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita.

27. Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka TEITI kutoa taarifa zenye maelezo ya kutosha ili kusaidia watumiaji wa taarifa kuelewa kwa kina.

28. Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza na kushauri

kwamba Serikali ifanye marekebisho ya Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia ya Mwaka 2015 ili kuiwezesha TEITI kuwa Taasisi ilio huru na yenye muundo na mfumo mpana unaoiwezesha kuwa na mamlaka katika kukusanya rasilimali fedha na kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati.

29. Mheshimiwa Spika, Pamoja na kutumia televisheni na redio, kuwafikia wadau mbalimbali, TEITI inapaswa kutumia njia mbadala katika kuhabarisha na kutaarifu Umma na wadau mbalimbali kuhusu kazi, wajibu na shughuli za TEITI, ingekuwa vyema kuanza kutumia mitandao ya kijamii na redio za kijamii (social media and community radio) ambazo zipo karibu na watu wa rika tofauti na pia hutumiwa na watu wengi zaidi.

30. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Madini iharakishe mchakato wa upatikanaji wa **Taarifa na Uwazi wa Mikataba ya Madini**, na **rasilimali zingine** kwa kuzingatia kwamba, msingi mkuu wa kuanzishwa TEITI ni kwa ajili ya kukuza na kuboresha Uwazi na uwajibikaji katika uvunaji wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia.

31. Mheshimiwa Spika, TEITI itoe taarifa kuhusu maendeleo ya uchunguzi wa ukaguzi maalum wa Shilingi bilioni 30.5 kama ilivyojitokeza katika taarifa ya mshauri mwelekezi, pamoja na hilo TEITI iharakishe upatikanaji wa watumishi wenye uwezo na sifa zinazohitajika katika kutekeleza majukumu ya TEITI katika ngazi tofauti lakini pia, Wizara ya Madini iwajibike ipasavyo kufanikisha upatikanaji wa rasilimali fedha ili TEITI iweze kuwa na fedha zinazohitajika kutekeleza shughuli za maendeleo kama ilivyopangwa.

iii. SHIRIKA LA MADINI LA TAIFA – STAMICO

32. Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa STAMICO ni moja kati ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini. Hili ni shirikia linalomilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja, ambalo lilianzishwa rasmi mwaka 1972 chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma (1969). Mwaka 2015 Shirika liliifanyiwa marekebisho

makubwa ya kimuundo (restructuring) chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma (mabadiliko ya uanzishwaji wa mashirika ya Umma) 2015.

33. Mheshimiwa Spika, STAMICO inamiliki makampuni kadhaa ya madini yakiwemo STAMIGOLD, Buhemba Gold, Makaa ya Mawe Kiwira kwa lengo la kuyaendesha kifaida. Miongoni mwa changamoto zinazoikabili STAMICO ni uhaba wa rasilimali fedha zinazohitajika kuendesha shirika.

34. Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa taarifa ya ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa nyakati mbalimbali, STAMIGOLD kampuni tanzu ya STAMICO, imekuwa inajиendesha kwa hasara takribani miaka 3 iliopita kutokana na madeni, uwekezaji mdogo na kampuni kutofanya shughuli za uzalishaji.

35. Mheshimiwa Spika, Kifungu namba 9 cha marekebisho ya Sheria ya Madini 2010, kuititia Sheria ya Marekebisho Anuai Sheria Na. 7, 2017, Sheria inaelekeza umiliki wa Serikali usiopungua asilimia 16 katika makampuni ya madini, hata hivyo kutokana na mapungufu ya kisheria na kikanuni, sheria na kanuni zake hazitoi mwongozo kuhusu mamlaka ipi ya Serikali itahusika na jukumu la kusimamia umiliki huo. Mapungufu kama haya ndiyo yanapelekea CHADEMA katika sera zake inakusudia kuititia sheria zinazosimamia madini ili kuwa na manufaa kwa wawekezaji na kwa uchumi wa nchi yetu.

36. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Bajeti, Katika makadirio ya mwaka wa fedha wa 2018/2019, jumla ya shilingi bilioni 13.6 ziliombwa kuititia Wizara ya Madini kwa ajili ya maendeleo, ambapo takribani shilingi bilillion 9 zikiwa kwa ajili ya maendeleo ya miradi ya Kiwira na Buhemba na shilingi bilioni 4 na zaidi zikiwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hata hivyo, hadi kufikia Februari, 2019, STAMICO ilipokea shilingi bilioni 2.7 tu ambazo zilikuwa ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na matumizi mengineyo na ndiyo maana Sera za CHADEMA ni kuanzisha mfuko maalum wa fedha zinazotokana na uwekezaji wa madini ili zitumike katika miradi

mikubwa yenyе manufaa kwa nchi kama hii iliyo chini ya STAMICO na kutoa huduma za kijamii kwa wananchi.

37. Mheshimiwa Spika, kutokana na kwamba Serikali haifanyi vizuri kuhusu STAMICO, pamoja na changamoto zinazozikabili Shirika la Madini la Taifa, na ikizingatiwa kwamba shirika linajidhesha kwa hasara, Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza mambo yafutayo:-

38. Mheshimiwa Spika, kwanza tunapendekeza Serikali ifanye uwekezaji mkubwa kwa STAMICO ikiwa ni pamoja na kuipa ruzuku na pia kuchukua dhamana ya madeni yanayoikabili ili iweze kuwa na uwezo wa kujimarisha kifedha ili kumudu gharama za uzalishaji.

39. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunapendekeza kuwa STAMICO ifanyiwe mabadiliko makubwa ya kumuundo na kimfumo ili iwe kampuni hodhi (Holding company) inayoweza kumiliki hisa au sehemu ya umiliki katika makampuni mengine ya migodi na pia iweze kukuza mtaji kwa kuingia makubaliano ya kimkakati na yakiwekezaji, ikiwezekana, kukopa na hata kukaribisha wadau (hasa wananchi) wenye nia ya kuwekeza katika vipaumbele vya Shirika.

40. Mheshimiwa Spika, iwapo STAMICO itabdalishwa na kuwa kampuni hodhi, itasaidia kukuza mtaji wake kwa haraka, pia itamwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali kufanya ukaguzi katika mashirika ya Umma na makampuni binafsi kwenye sekta ya madini, mafuta na gesi asilia na hatimaye kuweza kujiridhisha na mwenendo wa mapato na matumizi ya makampuni hayo ambayo kwa sasa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali hana uwezo wa kuyakagua kwa mujibu wa sheria.

41. Mheshimiwa Spika, tunapendekeza kuwa, STAMICO ifanyiwe mabadiliko na ipewe jukumu la kusimamia na kuratibu umiliki wa asilimia 16 za Serikali katika makampuni ya madini kwa niaba ya Serikali. Aidha STAMICO ijitanue na kufanya utafiti na uwekezaji katika aina tofauti za madini

kama vile "graphite", coal" na mengineyo kuliko kujielekeza zaidi katika dhahabu

E. UKIMYA NA UFISADI TANCOAL

42. Mheshimiwa Spika, National Development Cooperation waliingia ubia na Kampuni ya Pacific Corporation East Africa Limited kwa kifupi (PCEA)ya Australia, mnamo tarehe 03 Aprili, 2008 katika umiliki wa asilimia 30 (Tanzania)kwa 70 (PCEA) kwenye Kampuni ya TANCOAL Energy Limited (TEL), kwa malengo ya kuendeleza uchimbaji wa makaa ya mawe, uzalishaji na usambazaji wa umeme katika mradi wa Mhukuru, Ngaka, Kusini mwa Tanzania. Hata hivyo, mnamo tarehe 28 Aprili, 2011 Kampuni ya PCEA ilibadili jina na kuwa Intra Energy Corporation (IEC) Australia. Kampuni ya IEC ndiyo inamiliki hisa za Kampuni ya Intra Energy Tanzania Limited (IETL) kwa asilimia 100. Kampuni ya IETL ndiyo inasimamia shughuli za uendeshaji wa Kampuni ya TANCOAL Energy Limited (TEL).

43. Mheshimiwa Spika, taarifa zinaonesha kwamba TANCOAL Energy Limited (Kampuni msimamizi wa ubia) haikutekeleza majukumu ya uendeshaji wa ubia huo kulingana na matakwa ya mkataba. Gharama kubwa za ukodishaji magari na mitambo mgodini zilizotokana na TANCOAL kushindwa kuwekeza kiasi cha Dola za Marekani milioni 20.49 kwa ajili ya ununuzi wa mitambo na kiasi cha Dola za Marekani milioni 1.41 kwa ajili ya ununuzi wa magari. Kushindwa huko kwa TANCOAL kumesababisha Kampuni hiyo kutumia Dola za Marekani milioni 42.7 kwa ajili ya kukodisha mitambo na magari, gharama ambazo ni mara mbili zaidi ya kiasi kilichotakiwa kuwekezwa kwenye ununuzi wa mitambo na magari kati ya mwaka 2012 hadi 2016, Jambo hili linaongeza gharama za uendeshaji na kuitia Serikali hasara.

44. Mheshimiwa Spika, Kampuni hii pia imeshindwa kujenga barabara ya kwenda mgodini kwa kiasi cha Dola za Marekani milioni 14.49 kati ya mwaka 2012 hadi Julai 2016 hivyo kuongeza gharama za uzalishaji, gharama hizo ziliongezeka baada ya kampuni kutumia jumla ya Dola za Marekani milioni

2.843 kwa ajili ya kukodi magari kutoka mgodini hadi sehemu ya mauzo ya, umbali wa kilometra 40.

45. Mheshimiwa Spika, kutojengwa kwa barabara hiyo, kumeongeza gharama za uendeshaji na kuondoa fursa ya Kampuni kupata faida ambayo ndio chanzo cha Serikali kupata gawio.

46. Mheshimiwa Spika, nchi yetu sasa imekuwa ni shamba la Bibi, taarifa za fedha za TANCOAL kwa miaka sita kati ya mwaka 2011 hadi 2016 zinaonesha kuwa gharama za utafutaji madini za shilingi bilioni 6.5 zilijumuisha kiasi cha shilingi milioni 880.7 isivyostahili. Gharama hizo ziliainishwa katika taarifa za fedha za mwaka 2013 hadi 2016 isivyostahili kwani utafiti wa madini ulikuwa umekamilika tangu mwaka 2012.

47. Mheshimiwa Spika, Kuingizwa kwa gharama hizo katika taarifa za fedha za TANCOAL kuliathiri upatikanaji wa faida na kuonyesha hasara ambapo Serikali haikuweza kupokea gawio wala kukusanya kodi stahiki.

48. Mheshimiwa Spika, Mwaka 2014 hadi 2016, TANCOAL walitumia jumla ya shilingi milioni 940.3 kwa shughuli zisizohusiana na uchimbaji wa madini kinyume na mkataba wa ubia. Hali kadhalika, jumla ya Dola za Marekani milioni 3.3 zililipwa kama gharama za shughuli za madini kwa kampuni Tanzu ya Intra Energy inayojulikana kama TANZCOAL ya nchini Malawi.

49. Mheshimiwa Spika, Matumizi hayo tajwa ni kinyume na mkataba, na yamesababisha TANCOAL kutoripoti faida, hivyo kushindwa kutoa gawio kwa mbia, pia kutolipa kodi stahiki kwa Serikali.

50. Mheshimiwa Spika, Mapitio ya taarifa za fedha za TANCOAL kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2014 yalionyesha kuwa TANCOAL imechangia jumla ya shilingi milioni 993 katika shughuli za maendeleo ya jamii katika maeneo ya Ngaka na Songea kama sehemu ya wajibu wake kwa jamii (CSR).

51. Mheshimiwa Spika, Hata hivyo uchunguzi na taarifa kutoka vyanzo mbalimbali vimebaini kuwa ni kiasi cha shilingi milioni 75, sawa na wastani wa shilingi milioni 15 kwa mwaka ndicho kilichotolewa na Kampuni ya TANCOAL kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya jamii, badala ya wastani wa shilingi milioni 198 kwa mwaka. Upo ushahidi wa kuthibitisha jambo hili. Hivyo Kampuni ya TANCOAL ilitumia kiasi cha shilingi milioni 917.6 kwa matumizi mengineyo kwa udanganyifu kuwa inasaidia jamii ya jirani na Mgodi. Kambi Rasmi haioni kama kitendo kinachofanya na kampuni hii kinautofauti na utakatishaji wa fedha na au uhujumu uchumi wa Taifa hili, kwa mantiki hii sasa, tunaitaka Serikali kuliarifu Bunge hili tukufu hatua ambazo imechukua dhidi ya kampuni hii na mstakabali wa ubia huo.

52. Mheshimiwa Spika, kuhusu dosari katika umiliki wa Hisa kati ya IETL na NDC Kifungu cha 3.2.1 cha Makubaliano ya Ubia kati ya IETL na NDC kinabainisha kuwa wabia watachangia mtaji kwa uwiano wa asilimia 50 kwa 50. Aidha, Kifungu 3.2.1 kinaainisha kuwa katika hatua ya upembuzi yakinifu, PCEA na NDC watakuwa na uwiano wa hisa 70:30 ambapo PCEA na NDC wanapaswa kutoa fedha.

53. Mheshimiwa Spika, Hata hivyo rasilimali husika ya makaa ya mawe haikuzingatiwa kuwa sehemu ya mchango wa Kampuni ya NDC kwenye ubia huo. Kutozingatia thamani ya rasilimali za makaa ya mawe kama mchango wa NDC kulisababisha PCEA kuwa na hisa asilimia 70 licha ya kuchangia fedha ndogo ya mtaji wa kiasi cha shilingi milioni 1.7 ambacho tunaamini kilikuwa ndani ya uwezo wa NDC hivyo kukosekana mantiki ya ubia huo.

54. Mheshimiwa Spika, Kati ya mwaka 2013 hadi 2017, yalifanyika malipo ambayo hayakuwa sahihi kwa IETL kama malipo ya Menejimenti jumla ya shilingi bilioni 1.4 ambazo zililipwa kama Ada ya Menejimenti kwenda kwa Kampuni ya Intra Energy Corporation ya Australia. Matumizi hayo yalionyeshwa kama mkopo unaopaswa kulipwa na TANCOAL.

55. Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mapitio ya maamuzi ya bodi ya TANCOAL ya tarehe 15 Novemba, 2012 yalibaini kuwa Bodii iliamaa kusiwepo na makubaliano ya huduma za usimamizi (Management service)na badala yake Kampuni ya IEC ilipwe gharama halisi zinazoingiwa (Reimbursable). Ni kwa msingi huo, gharama za shilingi bilioni 1.4 zillipwa kimakosa na zinastahili kurejeshwa TANCOAL.

56. Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa Serikali hii imekuwa ikijinasibu kutetea maslahi ya Taifa hili, na kwa kuwa moja ya taarifa za Kamati ya Bunge lako tukufu zinaonesha ujisadi mkubwa, ukwepaji wa kodi pamoja na jitihada zilizofanywa kuikosesha mapato Serikali au kuititia ukosefu wa gawio au kodi. Na kwa kuwa Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali katika Ripoti yake ya mwaka 2016/2017 unaonekana ujisadi wa Shilingi, Milioni 880,940 na Dola za Marekani Millions 3.3 ambazo ni fedha Serikali imezipoteza na nyingine zikipaswa kureshwaa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kauli ya Serikali kuhusu mambo yafuatayo:-

- a. Ni lini gharama za shilingi bilioni 1.4 zilizolipwa kimakosa zitarejeshwa na TANCOAL?
- b. Serikali inachukua hatua gani dhidi ya watendaji wa TANCOAL ambao wanashiriki kuhujumu uchumi wa Taifa kuititia kampuni hii wakishirikiana na wabia wenza?
- c. Ni lini fedha za mrahaba zaidi ya Dola za Marekani Mil 3.3 ambazo zimepotea kutoptana na usimamizi dhaifu zitapatikana na hatua gani Serikali inachukua dhidi ya wasimamizi hao dhaifu?
- d. Serikali ina mpango gani dhidi ya mkataba huo wa ubia unaendelea kuandikisha hasara kila mwaka na ikiwa hakuna uhakika wa kuendelea na biashara kwa siku zijazo?
- e. Ni lini sasa Serikali itaunda upya Shirika la National Development Cooperation na kuititia mikata yake yote ili kufikia lengo la kuanzishwa NDC?

F. MRADI WA CHUMA WA MCHUCHUMA LIGANGA

57. Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Sichuan Hongda Group ya China ilishinda tender ya kimataifa kuendeleza Mradi wa Mchuchuma na Liganga mwaka 2009 lakini hadi sasa Mradi huo umekwama. Ikumbukwe kwamba Serikali iliingia ubia na kampuni hiyo ikaunda kampuni ya Ubia ya Tanzania China International Mineral Resources Company Limited (TCIMRCL) kuendesha mradi huo kwa ubia wa 20% Serikali na 80% Sichuan Hongda.

58. Mheshimiwa Spika, uwekezaji wa mradi huo amba ni Dola za Marekani Bilioni 3 sawa na Shilingi (trillioni 6.8) ulitarajiwu kuajiri wafanyakazi wa moja kwa moja wapatao 5,000 na ajira zingine kama kandarasi na jamii inayozunguka watu. Hata hivyo mradi ultiakiwa uwe umeanza tangu mwaka 2010, lakini hadi sasa miaka 9 baadaye mradi huo umekwama bado hauzaanza kutekelezwa.

59. Mheshimiwa Spika, Mradi una rasilimali (Mashapo) ya makaa ya mawe kiasi cha tani milioni 428 kwenye eneo la Mchuchuma na tani milioni 128 za chuma iliyochanganyika na titanium na vanadium kwenye eneo la Liganga. Aidha manufaa mengine ya mradi wa Liganga na Mchuchuma ni Kodi na Tozo Dola milioni 10 (shs bilioni 23), mchango kwenye pato la taifa (GDP) kati ya 3% na 4%, kuhifadhi fedha za kigeni kiasi cha Dola milioni 320 (shs bilioni 640) kwenye hazina ya Taifa kutokana na kutokuagiza chuma kutoka nje ya nchi na Dola milioni 240 (bilioni 480) kutokana na kutokuagiza makaa ya mawe kutoka nje ya nchi na kwa kutumia chuma chetu kwenye viwanda vyote vya chuma, yaani viwanda vya nondo, mabati, vyuma vya ujenzi wa madaraja na reli vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi kwa sasa. Kubwa zaidi teknolojia ya chuma ingebaki hapa nchini kwa manufaa ya watanzania walio wengi.

60. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kupata majibu kutoka Serikalini lini urasimu unaokwamisha mradi huu utakwisha ikiwa ni pamoja na kuangalia masharti mapya ya uwekezaji chini ya sheria ya madini ya mwaka 2017?

G. SEKTA YA MADINI NA WACHIMBAJI WADOGO

61. Mheshimiwa Spika, inaonekana kuna mkanganyiko wa tafsiri ya wachimbaji wadogo wa madini kati ya Serikali na tafsiri ya wachimbaji wadogo wa madini ambao Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawakusudia. Kwa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, tunapozungumzia wachimbaji wadogo wa madini ni ambao wanafanya shughuli za uchimbaji kwa kutumia masururu bila zana zozote za uchimbaji. Tunazungumzia wale wachimbaji ambao hawana leseni ya uchimbaji na ambao hawafahamu hata utaratibu wa kupata leseni hizo.

62. Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wa madini ni wadau muhimu sana kwa ustawi wa Taifa letu, pamoja na umuhimu huo kwa uchumi wa Taifa hili, wanakumbwa na matatizo mengi ambayo yanahitaji jitihada za Serikali ili kuweza kuwasaidia.

63. Mheshimiwa Spika, taarifa ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayo, inaonesha kuwa, hadi kufikia Juni 30, 2018, kulikuwa na bakaa ya Dola za Marekani 622,175 na Shilingi 130,331,274.45 katika Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) zilizobaki kutoka sehemu ya ruzuku ya Dola za Marekani 3,000,000, ambazo zilitolewa na Benki ya Dunia kwa Wizara ya Nishati na Madini (2015/16) kwa ajili ya kuendeleza rasilimali madini nchini ili zitolewe kama ruzuku kwa ajili ya kuendeleza wachimbaji wadogo.

64. Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hakukuwa na maelezo yoyote kutoka Wizarani kuhusu fedha hizo ambazo zingeweza kuwa msaada kwa wachimbaji wadogo. Wakati haya yakiendelea kutokea hakuna fedha iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya mikopo ya wachimbaji wadogo wa madini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwaeleza wachimbaji wadogo ni kwa nini inashindwa kutenga fedha kwa ajili ya mikopo ya wachimbaji wadogo. Aidha wachimbaji wadogo wanapenda kufahamu nini hatima ya bakaa ya fedha ambazo zilitolewa kama rukuzu kwa wachimaji wadogo wa madini na ni wachimbaji wangapi wamenufaika na fedha hizo.

65. Mheshimiwa Spika, Pamoja na hatua ya Serikali ya kukutana na wadau na wachimbaji wadogo wa madini nchini kwa lengo la kusikiliza kero, changamoto na maoni yao kuhusu uendelezaji wa Sekta ya Madini na hatua zilizochukuliwa hadi za kufuta Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) 18% na Kodi ya Zuio (Withholding Tax 5%) kwa wachimbaji wadogo, kufungua na kujenga masoko ya madini katika mikoa yenye uzalishaji wa madini bila fursa za mikopo kwa wachimbaji wadogo na wakati, wachimbaji hawa hawawezi kunufaika kwa kuwa hawatakuwa na mtaji wa kuendesha shughuli zao za uchimbaji.

66. Mheshimiwa Spika, uwezeshaji wa wachimbaji wadogo ni moja kati ya maeneo muhimu na ya vipaumbele katika Sheria ya Madini ya mwaka 2010, (Kama ilivyofanyiwa marekebisho na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Anuai Na. 7, 2017). Uchimbaji mdogo umetengeneza ajira kwa watu wengi na unaweza kunufaisha zaidi wananchi wengi na nchi kupata mapato yatokanayo na kodi na tozo mbalimbali katika rasilimali madini.

67. Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Madini, kati ya Julai, 2018 hadi Februari, 2019, leseni za uchimbaji mdogo 4,497 zilitolewa na Tume ya Madini kwa wachimbaji wadogo. Hatua ya Serikali kupitia Wizara ya Madini ya kuanzisha utoaji wa ruzuku kwa wachimbaji wadogo na wa kati na pia kufuta Kodi ya Ongezeko la Thamani na Kodi ya Zuio kwa wachimbaji wadogo, ni hatua nzuri lakini kuna kero zinazowakabili wachimbaji wadogo ambazo ni pamoja na kutumia zana duni katika uchimbaji, ukosefu wa masoko ya uhakika ya madini, maeneo madogo, migogoro, ukosefu wa mitaji.

68. Mheshimiwa Spika, ni Rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Serikali kwamba ni vyema Wizara, Tume ya Madini na STAMICO, kuendelea kuwawezesha wachimbaji wadogo kwa kuwakopesha zana za uchimbaji, kuwapatia utaalamu na matumizi ya teknolojia katika uchimbaji na uchenjuaji wa madini, pia, kuwapatia mafunzo ya ujuzi, huduma za utafiti, teknolojia, mitaji na hasa kuanzisha benki

ya madini au kuwadhamini ili waweze kupata mikopo yenye masharti na riba zisizoumiza.

69. Mheshimiwa Spika, Pamoja na rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Serikali pia iwawezeshe wananchi kunufaika na maeneo yao dhidi ya wamiliki wa leseni ambao leseni zao ziko kwenye maeneo ambayo tayari ni makazi ya wananchi. Ni lazima utengenezwe utaratibu sasa ambao siyo tu utamfanya mumiliki wa leseni ya uchimbaji kumlipa mwenye eneo fidia, bali pia uwepo utaratibu wa kumfanya mmiliki wa leseni ya uchimbaji kuwa na hisa na umiliki wa ardhi katika mgodi husika, utaratibu huu utamnufaisha mwananchi wa kawaida kuliko hali ilivyo sasa ya kuondolewa kwenye maeneo yao kwa mitutu ya Bunduki.

H. MWELEKEO WA KISERA NA HATIMA YA RASILIMALI MADINI TANZANIA

70. Mheshimiwa Spika, ili kuweza kulinufaisha Taifa na watanzania kwa ujumla wake, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni bado kama ilivyo kwenye sera zetu kwamba ili kufikia usimamizi mathubutu na endelevu kwa sekta ya Madini, CHADEMA tutarekebisha Sheria zinazosimamia Madini na kwa mantiki hiyo hiyo tunaona umuhimu wa kuzidi kusisitiza na kushauri Serikali kufanyia marekebisho kwa baadhi ya Sheria zinazogusa maendeleo ya Sekta ya Madini.

71. Mheshimiwa Spika, Serikali lazima iweke msukumo zaidi katika uwezeshaji wa kifedha na kiufundi na pia usimamizi katika utekelezaji wa Sheria na Kanuni mbalimbali za Madini ili kutekeleza usimamizi madhubuti wa rasilimali madini kwa ajili ya kuwanufaisha wananchi na Nchi kwa ujumla kwa maamuzi na uelekeo wa kisera katika sekta ya madini na rasilimali nyingine kulenga kujenga mifumo imara na taasisi endelevu, inayotoa wigo mpana wa ushiriki wa wananchi kwa ujumla.

I. UKAGUZI WA FEDHA NA TAARIFA KWENYE SEKTA YA UZIDUAJI

72. Mheshimiwa Spika, Kwa nyakati tofauti, taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, imebaini

changamoto kwa ofisi yake kupata taarifa za kifedha na kimikataba kutoka katika mashirika na makampuni kwenye sekta ya madini, na sekta nyingine kama mafuta na gesi asilia.

73. Mheshimiwa Spika, Changamoto hizi zimesababisha ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kushindwa kufanya ukaguzi wake kwa mujibu wa sheria. Ili kuweza kuchochea ongezeko la uwazi na uwajibikaji kwenye sekta ya madini pamoja na sekta nyingine zinazogusa rasiliamali za Taifa hili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona na kushauri kwamba sheria zinazohusu rasiliamali za nchi hii kama Sekta ya Madini, mafuta na gesi asilia zipitiwe upya ili kumpa mamlaka ya moja kwa moja Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kupata taarifa zitakazosaidia ukaguzi wake kwa maslahi mapana ya nchi.

**J. UWEZESHAJI WAZAWA KATIKA SEKTA YA MADINI
(LOCAL CONTENT)**

74. Mheshimiwa Spika, kupitia Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na kanuni zake, kampuni za uchimbaji madini Tanzania zinapaswa kuandaa na kuwasilisha mpango wa uwezeshaji wazawa katika Kamati/ Tume ya Uwezeshaji Wazawa ambapo pamoja na masuala mengine, mpango huo utapaswa kuonesha namna kampuni za wananchi (wazawa) zitapata vipaumbele katika zabuni na bidhaa zinazopatikana nchini, upatikanaji wa ajira kwa watanzania na utoaji wa mafunzo ya kuwajengea uwezo zaidi waajiriwa wazawa.

75. Mheshimiwa Spika, Hata hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni bado inaona kuna changamoto ambazo ni pamoja na uwezo na umahiri/ushindani usioridhisha wa kampuni za wazawa kushiriki kikamilifu katika fursa hizo, na pia kukosekana kwa muunganiko wa mnyororo wa thamani baina ya kampuni za madini na sekta zingine za kiuchumi, kama kilimo, uvuvi, elimu, ufundi, pamoja na uelewa mdogo wa wananchi kuhusu uwepo wa fursa hizo.

76. Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto tajwa hapo juu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali

kuweka mifumo na mikakati inayotekelzeza kwa ajili ya kuwaandaa wananchi na kuwajengea uwezo ili washiriki kikamilifu katika sekta ya madini kwa kushirikiana na wadau na taasisi mbalimbali za maendeleo zikiwemo asasi za kiraia.

K. UWAJIBIKAJI WA MAKAMPUNI KWA JAMII

77. Mheshimiwa Spika, dhana ya uwajibikaji wa makampuni kwa jamii, yanaelezwa katika mifumo ya kisheria hapa Tanzania. Suala la uwajibikaji wa makampuni kwa jamii, linaelezwa katika kifungu cha 102 cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, (Kama ilivyofanyiwa marekebisho na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Anuai Na. 7, 2017). Kwa mujibu wa kifungu hicho, wajibu wa makampuni kujihusisha katika huduma za kijamii katika maeneo ambayo shughuli za uziduaji zinafanyika umefafanuliwa. Sheria pia inaelekeza kuwa, kila mwaka kampuni hizi zinapaswa kuandaa Mpango wa Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii (Plan for Corporate Social Responsibility), ambao utapelekwa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa/ Vijiji/ Halmashauri kwa ajili ya majadiliano na kupitishwa ili uanze kutekelezwa katika eneo husika.

78. Mheshimiwa Spika, Pamoja na matakwa haya ya kisheria baadhi ya makampuni hayatekelezi majukumu yao kama inavyotakiwa kisheria, hata hivyo, ipo pia migongano ya uelewa kwa baadhi ya makampuni na halmashauri, ambapo baadhi ya makampuni hudhani suala la mipango ya nini kifanyike ni suala lao pekee, ilihali baadhi ya Halmashauri zikiamini kuwa wao ndio wanaopaswa kupanga na kupeleka mipango yao katika kampuni husika ili zitoe fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mipango yao. Halikadhalika, hakuna ukomo wa kiwango (asilimia) cha kiwango kinachotakiwa kutumika katika shughuli za uwajibikaji wa makampuni kwa jamii na hili unufaisha makumpuni kwa kupunja jamii za maeneo husika kufaidika na rasilimali zao.

79. Mheshimiwa Spika, hata viongozi wa Serikali nao inaonekana hawatambui au kujua majukumu na ukomo wao katika majukumu, linapokuja suala la uwajibikaji wa Makampuni kwa jamii. Mfano ni Mkuu wa Mkoa wa Mara,

Mheshimiwa Adam Kighoma Malima ambaye anataka kuwa mlipaji mkuu wa fedha zinazotolewa na Mgodi wa North Mara. Fedha zinazotokana na uwajibikaji wa makampuni kwa jamii haziwezi kuwa ni fedha za mkoa mzima isipokuwa zinalenga kunufaisha eneo ambalo Kampuni husika inatekeleza shughuli zake. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwapatia mwongozo viongozi wa Serikali akiwemo Mkuu wa Mkoa wa Mara juu ya matumizi sahihi ya fedha zinazotokana na Mgodi kama sehemu ya uwajibikaji wa mgodi husika kwa jamii inayozunguka Mgodi huo.

80. Mheshimiwa Spika, kutokana na madhaifu hayo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inapenda kuishauri Serikali, kuandaa kanuni na au Mwongozo wa ngazi ya Taifa utakaofafanua masuala kadhaa kuhusu majukumu na wajibu wa wadau mbalimbali katika jamii yakiwemo makampuni na halmashauri husika.

L. SEKTA YA MADINI NA UTUNZAJI WA MAZINGIRA

81. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa kutambua kuwa kuna baadhi ya migodi inatarajia kufungwa, mathalani, Bulyanhulu, na migodi mingine, Sera ya CHADEMA ni kuhakikisha kuwa shughuli za madini zinazingatia mipango ya athari za kimazingira zinazoweza kujitokeza kabla ya kuanza shughuli za uchimbaji na pia kuwa na mkakati wa namna ya kurudisha mazingira katika hali yake ya awali baada ya kumaliza shughuli za uchimbaji. Ili kufanikisha hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya tathmini ya athari za kimazingira katika meneo ya miradi mikubwa na taarifa za athari hizo ziwekwe bayana ili kuelimisha wananchi hasa wanaoishi kando kando ya miradi hiyo kuchukua tahadhari za kiafya na maisha yao.

82. Mheshimiwa Spika, Taasisi zingine kama Asasi za Kiraia (AZAKI) na Taasisi za kitaaluma pia wafanye tafiti sambamba zenye lengo la kubaini athari za kimazingira ili kuchangia katika juhudhi za Serikali katika utunzaji wa Mazingira. Aidha kwa kuzingatia Mwenendo wa mabadiliko ya tabianchi

(trends of climate change), na jitihada za Serikali kufufua na kuwekeza katika eneo la madini ya makaa ya Mawe, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia upya Sheria za usimamizi wa mazingira ili kuepusha madhara/ athari hasi zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi.

83. Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 pamoja na Marekebisho yake ya Mwaka 2017 na Kanuni zake zinasisitiza umuhimu wa utunzaji wa mazingira, shughuli za utafiti, uchimbaji na uchenjuaji wa madini zinapaswa kuhakikisha usalama wa watu na mazingira katika maeneo wanayofanya kazi. Kwa mujibu wa Kifungu cha 60 cha Sheria ya Madini, moja ya masharti ya leseni zitolewazo kwa wachimbaji madini ni kutoa tamko la utunzaji wa mazingira ambapo kwa mchimbaji mdogo hutakiwa kuwasilisha Mpango wa Utunzaji wa Mazingira (*Environmental Protection Plan*) kwa Afisa Madini Mkazi. Kwa upande wa uchimbaji wa kati na mkubwa, wamiliki hutakiwa kuandaa Tathmini ya Athari za Mazingira na Mpango wa Kutunza Mazingira (*Environmental Impact Assessment (EIA) and Environmental Management Plan (EMP)*). Lengo kuu la kuwa na maandiko haya ni kuhakikisha mwenye mradi anatambua kuwa shughuli anazofanya zina athari kwa mazingira na kufahamu maandalizi yake kwenye utunzaji na uhuishaji wa mazingira ili kuwa rafiki kwa matumizi ya binadamu akiwa bado anaendelea kuwekeza au anapomaliza uchimbaji katika eneo husika.

84. Mheshimiwa Spika, wakati akiwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yake, aliyekuwa Waziri wa Madini kwa kipindi hicho aliliambia Bunge lako tukufu kwamba Wizara ya Madini ilikuwa inaendelea kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Kanuni ya 177– 184 za Mwaka 2010 za Uchimbaji Salama, Afya na Utunzaji wa Mazingira zinazoelekeza migodi kuwa na miundombinu muhimu ya kutupa mabaki ya miamba, mabwawa ya kutunzia maji na mabaki yenye kemikali yatokanayo na uchenjuaji wa madini (*Waste Rocks Dumps and Tailings Storage Facilities*).

85. Mheshimiwa Spika, Serikali ilisema katika aya ya 39 ya hotuba ya Waziri wa Madini ya mwaka wa fedha 2018/2019 kwamba "Katika mwaka wa fedha wa 2017/18, kwamba Wizara ya Madini ilimuelekeza mmiliki wa Mgodi wa Dhahabu wa Nyarugusu kulipa fidia kwa waathirika kutokana na bwawa la kuhifadhi maji yenyе kemikali zilizotumika kuchenjua madini ya dhahabu kumwaga maji hayo katika mashamba na kuathiri mazao ya wakulima kutokana na mvua kubwa kunyesha ndani ya muda mfupi. Licha ya kulipa fidia kwa waathirika,mmiliki alielekezwa kufanya usanifu mpya wa bwawa hilo ili liweze kuhimili mvua kubwa pamoja na kuandaa mpango wa dharura wa ukusanyaji maji hayo wakati wa mvua

M. FAINI YA BILIONI 5.6 YA MGODI WA DHAHABU WA ACACIA - NORTH MARA

86. Mheshimiwa Spika, Siku chache zilizopita Serikali kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) iliupiga faini ya shilingi bilioni 5.6 mgodi wa dhahabu wa Acacia North Mara uliopo Nyamongo wilayani Tarime, kwa kushindwa kuthibiti bwawa la maji yenyе sumu na hivyo kuhatarisha afya za wakazi wanaozunguka mgodi huo.

87. Mheshimiwa Spika, Kitendo cha Serikali kuipiga faini Kampuni ya Acacia inayomiliki mgodi wa North Mara kunathibitisha malalamiko ya muda mrefu ya wananchi wa Tarime wanaozunguka mgodi huo. Malalamiko ya wananchi hawa yamewahi kuchunguzwa na kamati mbalimbali za Bunge hili tukufu kwa nyakati tofauti tofauti bila mafanikio. Mathalani iliyokuwa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira chini ya Mwenyekiti wake Mhe. James Lembele iliwahi kufanya ziara Nyamongo kwa kile kilichoelezwa kuwa ni kukagua utekelezaji wa maelekezo ya Kamati hiyo iliyoyatao mwaka 2010 kuhusu athari za mazingira zilizosababisha baadhi ya wakazi wanaozunguka Mgodi huo kupata athari za kiafya, Kitu cha kusikitisha ni kwamba kamati hiyo ilifika mgodini hapo kwa ndege za kukodishiwa na wamiliki wa mgodi huu.

88. Mheshimiwa Spika, Hata hivyo wakati Kamati hiyo ikiwa mgodini Nyamongo waliokuwa Wenyeviti wa Vijiji

vinavyozunguka mgodi huo wa Nyamongo walizuiwa kuingia ndani ya mgodi kwenda kushiriki katika mazungumzo baina ya uongozi wa Barrick na sasa Acacia, na Wajumbe wa Kamati ya Bunge.

89. Mheshimiwa Spika, Mapema Februari, 2010 Kamati hiyo chini ya aliyekuwa Mwenyekiti wake na sasa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Job Ndugai ilifanya uchunguzi wa taarifa za athari za sumu kwa wananchi wanaoishi pembezoni mwa mgodi huo na kutoa taarifa iliyoweka wazi kwamba kulikuwa na udhaifu katika ufuatiliaji wa malalamiko ya wananchi.

90. Mheshimiwa Spika, Kamati hiyo katika maazimio yake iliagiza Serikali ichukue hatua za haraka kulichunguza suala hilo na kutoa malipo ya fidia kwa waathirika.

a) **Madhara yaliyotokana na Mgodi wa Nyamongo-North Mara kutirishwa Maji yenye Sumu kwenye makazi ya Watu**

91. Mheshimiwa Spika, Wakati iliyokuwa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira chini ya Mwenyekiti wake, ambaye sasa ni Spika wa Bunge hili ikiagiza Serikali kuchunguza suala hilo na kutoa malipo ya fidia kwa waathirika, ni bora kufahamu athari ambazo ziliwapata wakazi wanaozunguka mgodi huo.

92. Mheshimiwa Spika, athari hizo, ambazo iliyokuwa Kamati yako ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ilishuhudia na au kusikia ilipotembelea mgodi huo ni pamoja na binadamu kubabuka ngozi, wanyama kuathirika ngozi na kufa, kuharibika kwa mazingira yanayozunguka mgodi, kuathirika kwa Mto Tighithe. Kutirishwa kwa sumu itokayo Mgodini katika Mto Tighite kumeathiri visima vya maji vikubwa na vya asili, ambavyo ni kwa matumizi ya binadamu katika kata ya Matongo na hasa vitongoji vya Kegonga, Kwimange na Kwinyunyi.

93. Mheshimiwa Spika, athari nyingine zinatokana na shughuli za mgodi hasa telling, pit ya Nyabirama na bwawa la maji

machafu vimeharibu ardhi pale. Ardhi iliyokuwa inatoa mavuno ya gunia takribani 100 kabla ya uharibifu huo, sasa baada ya madhara hayo wananchi hawawezi kuvuna hata gunia 2. Zaidi ya hayo watu zaidi ya 500 kutoka Kegonga A na B, Kwinyunyi watu zaidi ya 340 wameathirika, eneo la centre shule watu zaidi ya 200 wote hawa hawana visima vyta maji, mashamba yao hawalimi kutokana na ardhi yao sasa kuathirika ma sumu inayotoka mgodini na uoto wa maeneo haya sasa ni madini tembo.

94. Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyokuwa yanaitwa Kwinyunyi sasa yamebadilika na yanaitwa Telling Dump (Eneo la Taka) wako wakazi walikufa kwa sababu ya maji machafu, mathalani Mwikabe Mwita Waigama aliyefariki mwaka 2018. Maji ambayo sasa Serikali imedai ni machafu na yanaharibu mazingira yamewaathiri kwa kuwa babua ngozi, Mzee Marwa Range Isaroche, Maguku Chacha Tekele, Keraka Magebo, Mama Nchama Mgusi Mwita, Mama Chaina Mwita Bhoke na Mwita Waigama ni baadhi ya waliobabuka ngozi kutokana na maji hayo yenye sumu.

95. Mheshimiwa Spika, ng'ombe 900 katika Kijiji cha Matongo walikufa kutokana na kunywa maji hayo yenye sumu, huku Mzee Ryoba Irondo peke yake akibakiza zizi tupu baada ya ng'ombe wake zaidi ya 100 kufa.

b) Hatima ya waathirika wa maji yenye sumu

96. Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza kwa kina athari hizi ambazo zimewakumba wananchi hawa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kauli ya Serikali kuhusu kiasi ambacho wananchi wanaozunguka Mgodi wa Nyamongo, North Mara watalipwa kama fidia kutokana na madhara waliyopata yatokanayo na Mgodi wa North Mara kutiririsha maji machafu yenye sumu kwenye makazi ya watu na kuwasababishia magonjwa ya ngozi, kupoteza mifugo na maeneo yao ya kilimo.

97. Mheshimiwa Spika, Kama ilivyokuwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa Mgodi wa Dhahabu wa Nyarugusu

kutakiwa kulipa fidia wakazi wa Nyarugusu wanaozunguka mgodi huo kwa kutiririsha maji yenyе sumu na kuathiri wakazi wanaozunguka mgodi huo, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu wakazi wanaozunguka Mgodi wa Dhahabu wa North Mara watanufaika na shilingi ngapi kutokana na faini hiyo ya Bilioni 5.6 ambazo mgodi umepigwa faini. Ikiwa wananchi hawatafaidi fedha hizo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua Serikali ina mpango gani wa kuiagiza sasa Mgodi wa North Mara kuwalipa fidia wananchi wanaozunguka Mgodi huo kutokana na athari walizopata kufuatia mgodi huo kutiririsha maji yenyе sumu kwenye maeneo yao na kuwasababishia athari kubwa.

N. HATIMA YA FIDIA KWA WANANCHI WA TARIME

98. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani kwa nyakati mbalimbali, tangu mwaka 2010, tumekuwa tukiuliza na kufuatalia hatima ya wananchi wa kata za Kemambo, Nyamwanga na Matongo wanaoishi kuzunguka Mgodi wa Nyamongo walifanyiwa tathimini ya kulipwa fidia lakini hadi sasa hawajalipwa fidia hiyo. Mawaziri kadhaa wa Serikali, akiwemo aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini, Prof. Sosthenes Mhongo, Mheshimiwa Kairuki na Waziri wa sasa, kwa nyakati tofauti wameagiza Mgodi uwalipe wananchi fidia lakini.

99. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali sasa kutoa kauli ni kwanini wananchi hao hawajalipwa fidia pamoja na Serikali kuelekeza kwa nyakati mbalimbali, Serikali inachukua hatua gani dhidi ya Mgodi wa North Mara ambao umekaidi agizo la Serikali kulipa fidia na kumaliza mgogoro na wananchi.

O. MUUNDO WA WIZARA YA MADINI

100. Mheshimiwa Spika, Kuna haja ya kupitia upya muundo wa Wizara ya Madini na kufanya marekebisho katika Idara au Taasisi ambazo zinaonekana kuwa na majukumu yanayofanana. Mathalani, kuanzishwa kwa Tume ya Madini kwa mujibu wa Marekebisho ya Sheria ya Madini 2010,

inapokonya mamlaka na kazi ambazo Idara ya Madini chini ya Kamishna wa Madini alikuwa nazo. Kwa mantiki hiyo, kuendelea kuwa na Idara na Taasisi ambazo zinafanya kazi zinazofanana siyo tu kwamba zinatoa taarifa ya utendaji unaofanana ila pia ni kuingia gharama zisizo na tija kitu ambacho Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona ni matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi.

P. MATAMKO YA KISIASA NA UTEKELEZAJI WA BAJETI

101. Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia utawala wa Sheria, taratibu na kanuni za nchi, matumizi yote ya Bajeti ya Serikali yanapaswa kupitishwa na Bunge kwa niaba ya Wananchi. Katika utawala wa Awamu ya Tano kumekuwa na matamko mbalimbali ya kisiasa yenye athari katika Utekelezaji wa Bajeti kama zinavyopitishwa na Bunge. Madhara ya matamko hayo Mheshimiwa Spika ni kushindwa kutekelezeka kwa Bajeti elekezi na kufikia lengo husika. Kwa mantiki hiyo, na ili kuwepo na bajeti inayozingatia ukomo na uhalisia endelevu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kusitisha matamko ya kisiasa yanayoongeza gharama na bajeti ambazo hazikuwepo awali ili kufanya rasilimali fedha zitumike kwa vipaumbele vinavyotakiwa na siyo vinginevyo.

102. Mheshimiwa Spika, Viongozi Wakuu wa Serikali na watendaji wa Serikali hawana budi kuzingatia Sheria, taratibu na kanuni za nchi katika usimamizi na Utekelezaji wa Bajeti. Ukinzani wa uhalisia wa Bajeti na matamko ya kisiasa siyo tu husababisha hasara, lakini pia unadhihirisha kwa wananchi kwamba viongozi wao na Serikali kwa Ujumla wake hawaaminiki.

Q. MADINI YA VITO NCHINI NA FUNGAMANISHO KATIKA KUKUZA AJIRA

103. Mheshimiwa Spika, Tanzania imebahatika kuwa mzalishaji wa madini ya vito ya aina mbalimbali, ambayo ni kama ifuatavyo; amethyst, aquamarine, cordierite, emerald, garnet, ruby, sapphire, spinel, tanzanite, and tourmaline.

104. Mheshimiwa Spika, Maeneo ambayo yamebahatika kuwa na madini ya vito ni pamoja na yafuatayo; Winza Wilaya ya Mpwapwa Dodoma na Milima ya Uluguru yamejaliwa kuwa na ruby na sapphire ambapo uchimbaji unafanyika maeneo ya Matombo, Ngongolo, Mwaraze, na Kibuko. Wilaya ya Mahenge ni maarufu kwa madini ya spinel na ruby Tunduru maeneo ya Muhuvesi, Lumesule, na Mto Ruvuma hadi maeneo ya juu ya Ngapa na Kitowelo, ni maarufu kwa uchimbaji wa blue, yellow, green, pink, and purple sapphires, na rubby. Wilaya ya Kilindi eneo la Loolera ni maarufu kwa uchimbaji wa ruby.

105. Mheshimiwa Spika, Faida mojawapo kubwa ya Madini ya Vito ni kwamba mara baada ya kuchimbwa yanaweza kuuzwa moja kwa moja (*direct to the market like harvested crops*). Madini haya hayahitaji hatua nyine kama dhahabu inayohitaji uchakataji na uchomajili kupata zao la mwisho kwa ajili ya kuuza. Endapo dhahabu isipopitia hatua hiyo hujulikana kama'ghafi' ambapo hata bei yake sokoni inabidi ipungue.

106. Mheshimiwa Spika, Kwa mantiki hii, uwekezaji katika shughuli ya biashara ya Madini ya vito si wa gharama kubwa ikilinganishwa na Madini ya metali. Mbali ya faida hiyo, Madini ya vito huuzwa bei kubwa zaidi ya Madini ya metali. Kwa ujumla, uwekezaji katika Madini ya vito ni njia mahususi katika kuondoa umaskini kwa wananchi na kuongeza mapato kwa serikali. Aidha suala la uharibifu wa mazingira hasa vyanzo vya maji, ni mdogo kwa sababu madini ya vito hayahitaji kemikali maana hayahitajiuchakatajii kama madini ya metali.

107. Mheshimiwa Spika, kwa takwimu zilizotolewa na Kamati ya Jaji Bomani inaonesha kwamba Tanzania ina hazina ya Almasi karati milioni 50.9, Tanzanite tani 12.60. na madini mengine ya vito ambayo tumeyaonesha hapo juu bado hatujafahamu tuna hazina kiasi gani. Lakini tunaamini hazina ni kubwa pia.

108. Mheshimiwa Spika, Ni muhimu pia kufahamu kuwa Serikali ilishaweka katazo la kusafirisha nje ya nchi madini ya

vito ghafi kwa lengo la kuongeza faida kwa wazawa katika biashara nzima ya madini ya vito.

(i) Mchakato Mzima wa Mnyororo wa Kuongeza Thamani

109. Mheshimiwa Spika, huu ni mchakato mzima wa mnyororo wa uongezaji wa thamani wa madini ya vito unaohusu ukataji na uchongajji wa madini kwa sura (shape) na ukubwa (size) kwa kusafisha na kung'arisha madini kulingana na mahitaji ya soko, hapa kunahitaji uwekezaji mkubwa wa rasilimali watu na vifaa. Kwa njia hiyo ni dhahiri fungamanisho la madini ya vito na utoaji wa ajira vitaenda sambamba na hivyo sekta hii ndogo inaweza kuwa ni mojawapo ya vivutio vya watalii wengi kutembelea eneo letu la Tanzania. Hivyo ni muhimu kuwa na eneo maalum nchini kwa "*Beneficiation of gemstones*"

(ii) Kitengo cha Uchambuzi na Uthamini wa Madini ya Almasi na Vito (Tansort)

110. Mheshimiwa Spika, TANSORT ni Kitengo cha Uchambuzi na Uthamini wa Madini ya Almasi na Vito cha Wizara ya Madini ambapo uthamini unalenga ukokotoaji sahihi wa mrabaha wa Serikali kama ilivyoelekezwa na Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, Kitengo hiki kilichoanzishwa mwaka 1966 kina ofisi tano sehemu tofauti tofauti ikiwa ni pamoja na Antwerp nchini Ubelgiji, Kanda ya Mashariki (Dar es Salaam), Kanda ya Kati-Magharibi (Shinyanga) Kanda ya Kaskazini (Arusha) na Kanda ya Kusini (Songea).

111. Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana ni kuwa TANSORT haina Ofisi nchini India au Thailand nchi ambazo ndizo zinasifikasi kwa biashara ya madini ya vito duniani. Aidha, TANSORT haioneshi kuwa na mkakati wa kuhakikisha Tanzania inakuwa na uwezo wa kufanya 'Beneficiation' kwa madini ya vito yanayopatikana hapa Tanzania.

(iii) Uonevu kwa wataalamu wa uthamini wa madini

112. Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini inataka madini yote kuthaminishwa ili kukokotoa mrahaba wa awali (provisional

royalty) ili ulipwe hapohapo. Katika utaratibu wa kawaida, baada ya kulipwa mrahaba wa awali, madini hupelekwa sokoni kuuzwa na inapotokea yakauzwa kwa bei ya juu zaidi ya iliyothaminishwa mchimbaji hutakiwa kulipa tofauti ya mrahaba. Na ikitokea yameuzwa kwa bei ya chini ya iliyothaminishwa Serikali inamrudishia mchimbaji. Aidha lengo la uthaminishaji wa madini ni kujihakikishia malipo ya mrahaba mapema zaidi.

113. Mheshimiwa Spika, yapo madini ambayo taratibu za uuzwaji kwenye soko la Dunia ni mzuri kwa kuwa yanauzwa kwenye mnada wa wazi kwenye soko la kimataifa, eneo la mnada ambalo halina udanganyifu. Pamoja na utaratibu huo, wataalamu wa uthaminishaji kwa nyakati tofauti wanakumbwa na changamoto zikiwemo kubambikiziwa mashitaka ya uhujumu uchumi. Katika mazingira ambayo taaluma ya uthaminishaji haisababishi hasara yoyote kutokana na utaratibu wa kulipwa na au kulipa tofauti ya mrahaba, dhana ya uhujumu uchumi inatoka wapi? Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba, kama Serikali haipendi utaratibu wa uthaminishaji ni bora ikafanya marekebisho ya sheria ili kuondoa utaratibu huo na uonevu kwa wathaminishaji.

(iv) Uzoefu wa nchi ya Thailand kuhusu madini ya vito

114. Mheshimiwa Spika, Thailand ni nchi iliyoenedlea ikilinganishwa na nchi nyingine zinazoizunguka. Serikali ya Thailand ilitunga sheria; shughuli zote za uchimbaji na biashara ya madini vito itakuwa chini ya wazawa na kupiga marufuku usafirishaji wa madini vito ghafi nje ya Thailand bali ina ruhusu uingizwaji wa madini ghafi ya aina yoyote ndani ya Thailand bila kibali. Hatua iliyofuata ni kutengwa kwa mji wa CHANTHABURI kama kitovu cha biashara ya madini hususan madini ya Vito. Serikali ya Thailand kwa kushirikiana na taasisi za elimu walianzisha mafunzo ya utengenezaji na uvumbuzi wa mashine za bei nafuu zitakazotumika kukata, kuchonga na kung'arisha madini vito ili kuyaongeza thamani.

115. Mheshimiwa Spika, Zoezi hili lilianza kwa kuwatumia Wahunzi wa Jadi. Kwa kuwatumia hao, ilikuwa rahisi kuweza

kutengeneza mashine kwa kutumia teknolojia ya ndani. Zoezi hilo lilipata mwitikio mkubwa na mashine mbalimbali na ujuzi tofauti wa kukata madini ya vito vilivumbuliwa zaidi. Nchi ya India pia ilifuata mfano huu kwa kuwachukua baadhi ya Wahanzi wa mashine za kutengeneza nguo na kuwapeleka nchini Thailand kujifunza namna ya kutengeneza mashine za kuchonga na kung'arisha madini ya vito ikiwa ni pamoja na kujifunza kukata.

116. Mheshimiwa Spika, Baada ya mafunzo husika walirudi na Serikali ya India ikatenga mji wa Jaipur kuwa eneo la kuanzia shughuli husika.Ndani ya muda mfupi Jaipur ukawa mji maarufu kwa uuzaaji na ukataji wa madini ya vito.ltalkumbukwa madini ya Tanzanite hukatwa kwa wingi na kuuzwa katika mji huu sababu kuu ikiwa ni hizo zilizotajwa – Manguli wa Kukata,kuchonga na kung'arisha Madini ya Vito kwa ustadi wa hali ya juu pamoja na Gharama nafuu.Thailand imeendelea kuboresha biashara ya madini ya vito kwa kuanzisha huduma fungamano; vyuo vinavyotengeneza bidhaa (mapambo) zinazotumia madini ya vito, uanzishwaji wa maeneo rasmi ya uuzaaji na ununuvi wa madini (Minerals Bourses), maonesho ya biashara ya madini ya vito mwaka mzima katika vipindi tofauti.

117. Mheshimiwa Spika, Katika nchi zote zinazojishughulisha na madini ya vito, 'Bourses' imekuwa ndiyo suluhisho la makusanyo badala ya 'Individual Broker and Dealers''. Masharti yamewekwa ya kuongeza kodi zaidi kwa 'Individual Broker and Dealers' na kuondoa au kupunguza kodi kwa wafanyabiashara katika 'Bourses'.Bourses ni eneo linalotengwa na kujengwa na Serikali na kuandaa meza ambazo wafanyabiashara huruhusiwa kufanya mauzo na manunuvi ya madini na watumishi wa Serikali kutoza kodi na kutoa vibali vyote katika eneo hilo.

R. AHADI HEWA KATIKA SAKATA LA MAKINIKIA NA MAJADILIANO YASIYOFIKIA KIKOMO

118. Mheshimiwa Spika, Mnamo mwezi Machi 2, 2017, Wizara ya Nishati na Madini iliandika barua kwa umma

kuwajulisha wafanyabiashara na makampuni yanayojishuhulisha na shughuli za uvunaji wa madini kuacha mara moja shughuli za usafirishaji wa makinikia (concentrates) na mawe yenyewe madini ya metaliki kama vile dhahabu, shaba, nikeli na fedha.

119. Mheshimiwa Spika, pamoja na katazo hili Rais aliunda Kamati mbili za uchunguzi wa usafirishaji wa makinikia nje ya nchi. Pamoja na mambo mengine ripoti zote zilizungumzia hasara kubwa tunayoipata kama taifa kutokana na sheria mbovu za madini na mikataba mibovu ilioingiwa baina ya Serikali ya CCM na wawekezaji. Ripoti zote mbili zilijikita zaidi katika kubaini viwango vya madini vilivyopo katika makinikia na mikataba ya uchenjuaji ambayo haikuwa wazi.

a) **Madhaifu katika sakata zima la makinikia**

120. Mheshimiwa Spika, sakata la makinikia lilikuwa ni sakata la kisasa liliojawa na ahadi nydingi hewa ambapo mpaka sasa linaigharimu Serikali kutokana na maamuzi hayo ya kukurupuka. Kwa takribani miaka zaidi ya 20 Wabunge kutoka vyama vya upinzani walikuwa wakidai uwepo wa uwazi katika mikataba ya madini na ubovu wa mikataba mingi ikiwemo mkataba wa Buzwagi, Resolute, Bulyanhulu n.k. Katika awamu tofauti za Serikali Mawaziri ambao ndio watendaji wakuu wa Serikali walikuwa walilifumbia macho pamoja na kupigiwa sana kelele.

121. Mheshimiwa Spika, katika Tume ya Jaji Bomani, iliainisha mapungufu makubwa katika mikataba ya madini ambayo iliruhusu upenyo wa ukwepajji kodi ikiwemo ukwepajji wa mrabaha, usiri katika uendeshaji wa biashara ya madini nchini na rushwa. Japokuwa Sheria zilikuwepo, tatizo kubwa lilikuwa katika mikataba ambayo Serikali iliingia na makampuni ya madini. Mfano Mwaka 1997 mpaka 2009 hakuna kampuni hata moja iliyolipa kodi ya mapato. *Mathalani kampuni ya Resolute iliyojukwa inachimba dhahabu katika mgodi wa Lusu iliyochimba dhahabu kwa takribani miaka 14 ililipa kodi kwa kipindi cha miaka 2 tu kabla ya kufunga mgodi.* Pamoja na hilo katika ripoti ya Makinikia ya mgodi wa Bulyanhulu na

Buzwagwi unaonyesha kuwa kampuni ya Acacia ambayo ndiyo mmiliki wa migodi hiyo ilikuwa ilkidaiwa na Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) kiasi cha dola za Marekani 190 bilioni sawa na zaidi ya trillioni 424 ambayo ni kodi iliyokuwa ikikwepwa pamoja na riba

122. Mheshimiwa Spika, hata hivyo kiasi hiki cha fedha kiliwafanya watanzania kuwa na matumaini makubwa wengi wao wakiamini kila Mtanzania ataweza kumiliki gari aina ya Noah na wengine wakiamini huduma za kijamii zitapatikana bure. Katika sakata zima la makinikia lilioliohusisha kampuni ya Acacia Serikali imeendelea kuyafanya yale yale ambayo iliifanya mwaka 2007. Hii ni kutokana na kwamba **Acacia waliihana taarifa iliyotolewa na Serikali kuwa haijawahi kukwepa kodi na huilipa Serikali 4% ya mirahaba ya dhahabu, shaba na fedha kwenye makinikia** kama ilivyo kwenye makubalino baina ya Serikali na Acacia.

123. Mheshimiwa Spika, tutakumbuka mwaka 2007, kampuni hii ilituhumiwa kukwepa kodi na hivyo kuzua mtafaruku mkubwa na Serikali wakati huo. Katika makubaliano Barrick iliahidi kulipa Serikali kishika uchumba cha dola **milioni 700 kama kishika uchumba** wakati mazungumzo zaidi yakiendelea ili kuona ni namna gani nchi itanufaika lakini hadi sasa hata hicho kishika uchumba chenyewe hakijalipwa, huku ACCACIA wakiendelea kuchimba dhahabu katika migodi wanayomiliki hapa Tanzania.

124. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatakufahamu kwanini kishika uchumba hicho hakijalipwa hadi sasa? Ikiwa ACCACIA kweli walipaswa kulipa malimbikizo ya Kodi na tozo na hadi sasa kwa nini bado wanaendelea na shughuli za uchimbaji madini hapa nchini wakati tuliambiwa ni wezi wa rasilimali za nchi yetu? Na ikiwa Serikali iliwayanganya watanzania, ni lini sasa Serikali itajitokeza hadharani kufafanua jambo hili ambalo limegubikwa na sintofahamu, wakati watanzania wakiendelea kusubiria magari ya Noah kama walivyoahidiwa na Serikali.

125. Mheshimiwa Spika, vilevile, katika ripoti ya makinikia iliainisha takribani aina 11 za madini yaliyopo katika makinikia, Serikali ilikubalina na Acacia kulipa asilimia 4 ya mrabaha tu bila kuangalia aina nyingine za madini yaliyo katika makinikia. Hii yote ni kutokana na mikataba mibovu na utendaji kazi uliokosa ufanisi katika taasisi mbalimbali za Serikali zinazojishughulisha na madini. Mpaka sasa Serikali inazungumzia madini ya dhahabu, fedha na shaba pekee. Kamati ya makinikia iliainisha aina nyingine za madini kutoka kwenye nyaraka za usafirishaji wa makontena yaliyokamatwa bandari ikiwa ni pamoja na Sulphur, Chuma na madini mkakati (strategic metals) yaani Iridium, Rhodium, Ytterbium, Beryllium, Tantalum na Lithium)

126. Mheshimiwa Spika, kabla ya Serikali kutoa zuio la kusafirisha makinikia nje ya nchi, kulikuwa na mazungumzo yanayoendela baina ya Kampuni ya Acacia na Kampuni ya Endeavour Mining kutoka nchini Canada. Mazungumzo hayo yaliyoanza mwezi Januari 2017, yalikuwa kuhusu kuuza kampuni ya Acacia inayomiliki Migodi ya Bulyanhulu, Buzwagi na North Mara. Katika hatua za awali za majadiliano hayo Kampuni ya Endeavour ilitaka kuinunua Acacia kwa takribani paundi bilioni 3, sawa na dola bilioni 4.4.

127. Mheshimiwa Spika, Kutokana na mauziano hayo (**Transfer of shares**) Tanzania **ingeweza kupata capital gain tax**. Kutokana na zuio lillilowekwa na Serikali ya Tanzania dhidi ya Kampuni ya Acacia ililazimu kampuni ya Endeavour kusitisha majadiliano. Hivyo nchi **ilipoteza takribani dola 880 mil sawa na shiling trillioni 1.8 ambayo ni 20%** ya mauziano kama mpango huo wa mauziano ungefaniwa. Hivyo kauli za kisiasa na maamuzi yasiyo pimwa yamelisababishia taifa kukosa 1.8 trillioni ambayo ni zaidi ya bajeti ya Wizara kilimo pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2019/2020.

128. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji wa GST 2018, wakati Mgodi wa Buzwagi ukiwa unazalisha makinikia mgodi huo ulikuwa unazalisha **dhahabu kilo 28, fedha kilo 5 na shaba tani 18.9 kwa siku**. Baada ya kubadili mfumo wa uchenjuaji kwa sasa **unazalisha dhahabu kilo 23.5,**

fedha kilo 0.24 na shaba kilo 1.6 pekee kwa siku. Baada ya kutumia mfumo huu mpya uzalishaji wa dhahabu umepungua **kutoka asilimia 97 mpaka asilimia 87 kwa siku.**

129. Mheshimiwa Spika, mfumo huu mpya wa uchenjuaji unasababisha kupotea kwa madini ya fedha na shaba. Hivyo kwa mfumo huu Serikali inapata hasara kubwa tofauti hapo awali. Mauzo ya dhahabu hapo awali ilikuwa ni **95% ya mapato ya jumla, na 70% ni kutoka kwenye mauzo ya tofali za dhahabu, na 25% hutoka kwenye dhahabu iliyomo ndani ya makinikia.** Iliyobaki **5% ya mapato ni kutokana na shaba iliyomo katika makinikia na kiasi kidogo tu cha fedha.** Kwa maana hiyo kwa sasa kampuni inapoteza **30% ya jumla ya mapato.** Na karibia **50% ya mapato ya pamoja ya Bulyanhulu na Buzwagi.** Kwa katazo la kusafirisha makinikia tunapoteza mapato ya zaidi dola mil 1 kwa siku.

130. Mheshimiwa Spika, kwa mfumo huu mpya wa uchenjuaji unasababisha pia mabaki ya fedha na shaba kuchanganywa na mabaki ya zamani ambayo hayakuwa yanasaferishwa kwa kuwa hayakuwa na madini yoyote au kiwango kidogo sana cha madini. Mchanganyiko huo (dilution) unasababisha Serikali kupata hasara kwa kuwa mali iliyopo katika makinikia inapotea.

b) Mchakato wa kujenga kiwanda cha uchenjuaji (smelting)

131. Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo Bunge lilipitisha Sheria mpya ya Mamlaka ya Nchi kuhusu umiliki wa Maliasili (The Natural Wealth and Resources –Permanent Sovereignty 2017), ilyoletwa kwa hati ya dharura ndani ya Bunge na kujadiliwa kwa dharura katika kifungu cha 9(1) kimeweka masharti kuwa shughuli zote za uzinduaji, uchimbaji na upatikanaji au utumiaji wa rasilimali utahakikisha kuwa hakuna rasilimali ghafi itakayosafirishwa nje ya Tanzania. Maana yake ni kuwa hata makinikia yasisafirishwe nje ya nchi.

132. Mheshimiwa Spika, maana yake ni kuwa nchi inapaswa kuwa na uwezo wa kufanya uchenjuaji hapa hapa nchini. Kuanzia mwaka 2011 Serikali kuitia TMAA ilifanya upembuzi

yakinifu (visibility study) ya uwezekano wa kujenga kinu cha uchenjuaji (smelter) hapa nchini. Baada ya upembuzi huo Serikali ilitoa ripoti kuwa kujenga kinu cha uchenjuaji hakina faida ya kibiashara kwa nchi. Mwaka juzi (2017) Waziri Mkuu alipofanya ziara ya kikazi mkoani Mbeya, alitembelea Mgodi wa Sunshine Group uliopo Chunya. Waziri Mkuu alisema kuwa Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na wawekezaji ili kuona namna ya kujenga mitambo ya kuchenjulia makinkia.

133. Mheshimiwa Spika, jambo la kushangaza ni kuwa, kama Serikali ilifanya tathimini mwaka 2011 na ikaja na majibu kuwa makinkia hayana faida hivyo hakukuwa na sababu ya kujenga kiwanda hapa nchini na kwa sasa tunaona Serikali inaweza kupata faida kupitia makinkia, Je, Serikali imechukua hatua gani ya kuwawajibisha wataalamu wale waliosababishia hasara mwaka 2011 kwa kuishauri Serikali vibaya na kusababisha uhujumu uchumi zikiwemo kuapeleka mahakamni? Vilevile, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua iwapo Serikali imefanya tena upembevu yakinifu juu ya kujenga kiwanda cha uchenjuaji nchini na ripoti ya upembuzi huo inasemaje. Pamoja na hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua mazungumzo baina ya Serikali na Kampuni ya Sunshine Group yamefikia wapi?

134. Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Tanzania ina uwezo wa kuzalisha takribani tani 60,000 za makinkia. Kwa kawaida viwanda vyta uchenjuaji *refinery* huitaji takribani tani 150,000 za makinkia. Hivyo, mpaka sasa bado hatujawa na utoshelevu wa malighafi ya makinkia kama ambavyo wataalamu mbalimbali wameainisha. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua ni aina gani mbadala ya teknolojia mbayo Serikali itaitumia ili kuweza kufanya uchenjuaji wa kiwango hicho ambacho kinazalishwa nchini. Vilevile, ni muhimu kutambua kwamba uchenjuaji hufanyika kutohana na aina ya miamba. Kila aina ya miamba hutegemea aina fulani ya uchenjuaji. Mfano, uchenjuaji unaofanyika mkoani Mara na maeneo ya Geita hatua zote huweza kufanyika mgodini na kuzalisha matofali ya dhahabu hii ni tofauti na Buzwagi na Bulyanhulu ambapo dhahabu yenyewe ndio bidhaa muhimu.

135. Mheshimiwa Spika, vilevile, ili kuweza kuendesha mitambo ya uchenjuaji ni lazima nchi iwe na umeme wa uhakika. Mpaka sasa tuna takribani megawati 1,500 ambazo hazitoshelezi mahitaji hususani mahitaji ya viwandani. Mpaka sasa Serikali haina mbinu mbadala ya uzalishaji wa umeme, na bado tunategemea umeme unatokana na maji (Hydro Power)na sasa Serikali ikijikita kutekeleza Mradi wa Rufiji Hydropower Plant.

136. Mheshimiwa Spika, Ili kupata umeme wa uhakika lazima Serikali iwekeze kwenye vyanzo vingine vya nishati vikiwemo umeme wa upepo na jua (*solar power*). Zipo taarifa kwamba maeneo ya Same, Singida na Makambako tunaweza kuzalisha takribani megawati 5,000 ambazo zitatusaidia katika viwanda. Hata hivyo, ni muhimu pia kuwekeza katika umeme wa jua (*solar power*) ili kuweza kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya hali ya hewa ambapo vyanzo vingi vya maji vinakauka kutokana na kukata miti na kuongezeka kwa hewa ya ukaa na hivyo kujikuta tukizalisha matatizo mengine kama ya Richmond.

S. MRADI WA MADINI YA BATI (KYERWA TIN COMPANY LIMITED)

137. Mheshimiwa Spika, kwa takribani miaka minne sasa kampuni tanzu ya Kyerwa Tin Company Limited (KTCL) ambayo hisa zake zinamilikiwa na **STAMICO kwa 99% ya 1% inamilikiwa na Msajili wa Hazina** imekuwa ikishindwa kununua madini hayo kutoka kwa wananchi.

138. Mheshimiwa Spika, kutoka mwaka 2014 mpaka 2017 kampuni iliweza kununua jumla ya **tani ya 106.267** tu kwa gharama ya **shilingi 1,570,996,000**. Mpaka sasa STAMICO wameshindwa kuendelea na shughuli za kununua kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo ukosefu wa fedha.

139. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi wamewekeza fedha nyingi katika kuchimba madini haya na sasa Serikali inashindwa kununua na hakuna soko jingine ni kwa nini Serikali isitafute wadau wengine wenye uwezo wa kuyanunua madini

hayo? Mpaka sasa wananchi wengi wa maeneo hayo wamekopa fedha ili kuwekeza katika uchimbaji huo. Hivyo hawana fedha za kurudisha mikopo kitendo kinachowapelekea wengi kuishi maisha magumu na wengine hata kujitoa uhai kutokana na hofu ya kudhalilika kwa wingi wa madeni.

140. Mheshimiwa Spika, kuna taarifa zisizo rasmi kuwa baadhi ya walanguzi wameanza kujipenyeza baada ya kuona Serikali haina uwezo wa kufanya manunzi na hivyo kununua madini hayo kwa fedha ndogo na kuyapeleka nchini Rwanda kwa bei rahisi ambapo Serikali inakosa mapato. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua hatua ambazo Serikali inachukua ili kuwanusuru wananchi hawa na madeni na hali ngumu ya kiuchumi. Serikali ieleze Bunge lako ni lini hasa Serikali itaanza ununuzi wa madini hayo ya bati.

T. MRADI WA DHAHABU BUHEMBA UWEKEZAJI WENYE SHAKA

141. Mheshimiwa Spika, mgodi wa Buhemba ni moja ya mgodi ulioacha historia mbaya kwa wananchi wanaoishi Musoma Vijiji. Mradi huu uliachwa na Kampuni ya Meremeta ambayo ilifunga uzalishaji katika mgodi huu na kuacha mashimo makubwa na uharibifu mkubwa wa mazingira. Katika ripoti ya ukaguzi wa mazingira iliyofanywa na TMAA 2007-2009 iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini 2010, ilainisha uharibifu mkubwa wa mazingira na hivyo kuitaarifu Serikali kuwa inahitaji takribani Dola milioni 1.1 ili kufukia mashimo yaliyoachwa wazi na Kampuni ya Meremeta iliyofunga shughuli zake za uchimbaji katika Mgodi wa Buhemba.

142. Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, mapema mwaka huu (2018) Serikali ilitangaza kuufungua tena mgodi huu ili kuanza kuangalia kiwango cha mashapo ya dhahabu (mabaki) yaliyosalia baada ya Kampuni ya Meremeta kufunga mgodi. Hivyo, STAMICO ilitangaza zabuni ya kumpata mbia wa kushirikiana naye katika kuendesha mradi

huo kwa njia ya ushindani ili kujiridhisha na uwepo wa mashapo hayo ya dhahabu.

143. Mheshimiwa Spika, mradi huo unakadiriwa kutoa takribani wakia 600,000 za dhahabu japo jambo hilo halijathibitishwa kwa kuwa tathimini bado inaendelea. Mabaki hayo yaliachwa tangu wakati wa ukoloni, na vilevile unahuisha uchimbaji wa dhahabu katika miamba migumu (hard rocks mining).

144. Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 8.6 kwa ajili ya mradi. Pamoja na Serikali kutenga fedha hii ni dhahiri kabisa mradi huu hauwezi kufanya vizuri kutokana na madeni makubwa yanayoukabili mradi huu yaliyoachwa kipindi cha nyuma. Wafanyakazi waliokuwa wakifanya kazi katika mgodi huu mpaka leo wanadai fedha zao. Wananchi waliohamishwa kupisha shughuli za mgodi hawakulipwa fedha zao ambapo takribani nyumba 100 zilivunjwa, zahanati na shule, Kambi ya Jeshi JKT iliyoitwa Buhemba nayo ilivunjwa.

145. Mheshimiwa Spika, Jambo la kusikitisha zaidi ni kuwa mashimo yaliyoachwa baada ya Kampuni ya Meremeta kuondoka yanajaa maji jambo ambalo ni hatari kwa mazingira, na hata wachimbaji wadogo ambao wameendelea na shughuli za kujipatia riziki ndogo ndogo kutoka kwenye mabaki hayo. Mgodi huo umekuwa sababu kubwa ya kupungua kwa maji katika Bwawa la Kiarano na kwa sasa maeneo hayo yanakabiliwa na shida kubwa ya maji hasa wakati wa ukame. Pamoja na kuwepo kwa malalamiko makubwa kutoka kwa wananchi dhidi ya Kampuni ya Meremeta iliyoikuwa inaedesha mgodi bado kampuni hii ilikuwa ni moja ya makamuni yaliyotajwa kukwepa kodi.

146. Mheshimiwa Spika, Sheria za kimataifa za migodi na miamba inatambua kuwa kabla kampuni yoyote hajafunga mgodi ni lazima ifanye miradi ya utunzaji wa mazingira angalau miaka miwili kabla ya kufunga mgodi ikiwa ni pamoja na kufukia mashimo, kuvunja mabanda, kuondoa

mitambo na kupanda miti. Endapo kampuni itashindwa kufanya hivyo basi Serikali ina uwezo wa kuinyang'anya mitambo ya uchimbaji au kufungua kesi ya madai.

147. Mheshimiwa Spika, hivyo basi, Kambi Rasmi inataka kujuu ni kwa nini Kampuni ya Meremeta iliacha mashimo hatari wazi huku sheria na matakwa ya leseni yakifahamika! Je, ni kiasi gani cha fedha kilicholipwa kwa Serikali kutoka kampuni ya Meremeta katika shughuli ya kufukia mashimo? Je, endapo fedha hizo zilitolewa zilikwenda wapi au kufanyia shughuli gani? Mpaka sasa Serikali ituambie, je, iliwhahi kufungua kesi yoyote kwa Kampuni ya Meremeta kushindwa kufukia mashimo na kuchukua hatua za kulinda mazingira? Pamoja na hilo, Serikali ilieleze Bunge ni mbia gani aliyeshindwa tender ya kushirikiana na STAMICO katika kuendesha mradi wa kutafuta mabaki ya dhahabu na taratibu gani zilifuatwa kumpata mbia huyo?

U. MWENENDO WA MRADI WA TANZANITE ONE

148. Mheshimiwa Spika, Mgodi wa TanzaniteOne unamilikiwa na ubia baina STAMICO na Kampuni ya TanzaniteOne kwa usawa wa 50/50. Mpaka sasa shughuli za uzalishaji katika mgodi huu zimesimama tangu Mwezi Desemba 2017. Hii ni kutokana na mapendekezo ya Kamati Maalum ya Spika katika kuchunguza mwenendo wa biashara. Hata hivyo mgodi huu unakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo ukosefu wa wataalamu wa kuthaminisha madini, mitobozano na madeni makubwa yanayotokana na madai ya wafanyakazi. Mpaka sasa ni takribani miaka miwili wafanyakazi wa Kampuni ya TanzaniteOne zaidi ya 442 hawajalipwa mishahara yao takribani shilingi 3,094,756,320.

149. Mheshimiwa Spika, Mwezi Desemba 2017, kampuni iliiza madini ya vito yenye thamani ya shilingi bilioni 1.8 huku Serikali ikipokea mrahaba wa shilingi milioni 126. Kiasi kingine cha takribani kilo 159.34 kimehifadhiwa kwenye maghala ya mgodi. Bado wafanyakazi wanasota kwa kukosa mishahara, familia zao zinateseka lakini hatuoni hatua stahiki zikichukuliwa na Serikali kuhakikisha wafanyakazi hao

wanapata fedha zao. Ikumbukwe kwamba Mgodi ulisitisha uzalishaji kupisha majadiliano ambayo yalikuwa yanaongozwa na Mheshimiwa Prof. Kabudi Waziri wa Sheria na Katiba kwa kipindi hicho na sasa, Wazi wa Mambo ya Nje.

150. Mheshimiwa Spika, hadi sasa Serikali haijatoa tamko lolote kuhusu mwendelezo wa majadiliano ya mkataba, kwa zaidi ya miaka miwili wakati. Serikali inafanya haya huku ikifahamu kwamba inaendelea kupata hasara. Wakati Serikali ikipata hasara, familia za wafanyakazi nazo zinaendelea kupata shida kutokana na maamuzi haya ya Serikali, utadhani kufanya kazi katika mgodi huo ilikuwa ni laana kwao. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali kuliambia Bunge hili tukufu ni lini majadiliano na Mgodi wa TanzaniaOne yatahitimishwa na lini wafanyakazi wa mgodi huo, zaidi ya 442 watalipwa fedha zao za mishahara wanazodai kwa zaidi ya miaka miwili hadi sasa!

V. HATIMA YA MAONI YA RIPOTI ZA KAMATI ZILIZOUNDWA KATIKA SEKTA YA MADINI NCHINI

151. Mheshimiwa Spika, kutokana na malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu sekta hii ya madini kuwa hainufaishi wananchi ipasavyo, Serikali illamua kwa nyakati tofauti kuunda kamati mbalimbali ili kuwa sehemu ya ufumbuzi wa changamoto katika sekta ya madini nchini.

152. Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2002 hadi sasa zimeundwa Kamati mbalimbali kushughulikia changamoto za sekta ya madini hapa nchini, hadi sasa bado Taifa halijanufaika na rasilimali kutokana na mikataba mibovu ambayo ililingiwa na watendaji wa Serikali. Mapendekezo ya Kamati mbalimbali yanapendekeza kufanyiwa marekebisho mikataba hiyo ili kuweza kulinufaisha Taifa.

153. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kupata kauli ya Serikali, ni lini Serikali itawafikisha watendaji wake wote ambao walihusika kusaini hiyo mikataba mahakamani na kushitakiwa kwa makosa ya

kuhujumu uchumi? Pili, ni lini sasa mikataba hiyo itafikishwa Bungeni, ili Bunge kwa niaba ya wananchi na kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liweze kuishauri Serikali kuhusu mikataba hiyo na kuisimamia katika utekelezaji wa Mikataba hiyo?

W. KAMATI MAALUM ZA BUNGE KUHUSU MADINI

154. Mheshimiwa Spika, hata hivyo ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ziliundwa kamati mbalimbali, ikiwemo **Kamati ya Spika** ili kuchunguza Madini ya Almasi na Tanzanite japo ripoti ile haikuwasilishwa ndani ya Ukumbi ya Bunge.

155. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kufahamu sababu hasa za ripoti hizo kutowasilishwa ndani ya Bunge hilli tukufu na kujadiliwa na Bunge kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni za Bunge lako tukufu.

156. Mheshimiwa Spika, Pamoja na kuwa Serikali ilichukua hatua kadhaa ikiwa ni pamoja na kuwasimamisha kazi watendaji wakuu wa Wizara wakiwemo Mawaziri, kuvunjwa kwa Bodi ya TMAA na baadhi ya watendaji kubadilishiwa kazi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona jambo hilo halitoshi hata kidogo kwani bado kuna mambo mengi hayajafanyiwa kazi, na Serikali haionyeshi dalili za kuchukua hatua za kimkakati na za kisayansi za kuinusuru sekta hii. Maana yake ni kuwa bado mambo katika sekta hii ya madini yanafanyika kwa mtindo ule ule, walolilettea taifa hasara kubwa bado wengine wanaendelea na majukumu yao kama kawaida na hivyo kufanya zoezi zima kuwa la kisia na lenye kukosa tija.

a. Ripoti ya Almasi na Kiasi cha Madini ya Almasi

157. Mheshimiwa Spika, katika ripoti ya Almasi, Kamati ilibaini kuwa Serikali haina takwimu sahihi kuhusu kiwango cha madini kilichopo katika migodi mbalimbali hapa nchini kwa sasa. Hili linajihidhirisha kwa kuwa katika Ripoti ya Wakala wa Jiolojia (GST) ya mwaka 2007 ilionyesha kuwa Tanzania ina

hazina ya madini ya Almasi takribani karati milioni 50, katika taarifa ya Wakala wa Jiolojia Tanzania mwaka 2009 ilionyesha Tanzania ina hazina ya almasi takribani karati milioni 40.4, na kwa mujibu wa taarifa za maafisa wa Serikali walitoa takwimu waliifahamisha kamati kuwa nchi inahazina ya almasi takribani karati milioni 38.0

158. Mheshimiwa Spika, Mkanganyiko huu wa takwimu hautokei kwa bahati mbaya. Kukosekana kwa takwimu sahihi katika hazina ya madini maana yake ni kuruhusu mwanya wa kuibwa na Serikali kushindwa kudhibiti mwenendo wa rasilimali madini pamoja na mapato. Jambo la kusikitisha ni kuwa takwimu zilizopo zimetolewa kutoka upande wa mwekezaji.

159. Mheshimiwa Spika, Jambo hili linashtua sana. Wakala wa Jiolojia nchini kamwe hataweza kufanya kazi zake za utafiti vizuri ikiwa Serikali haiwekezi ipasavyo katika tafiti na vifaa vya kisasa na vya kisayansi vya kufanyia tafiti. Kwa kuwa katika utekelezaji wa mpango kazi wa GST fedha zinazotengwa ni fedha za matumizi (OC) na fedha za mishahara (PE) pekee. Hivyo utendaji kazi unakosa ufanisi kutokana na uhaba wa fedha.

160. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia namna bora ya kuiwezesha GST ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi. Ni muhimu sana madini yote nchini yakafanyiwa utafiti upya ili kujua kiwango cha hazina ya madini iliyopo ardhini badala ya kuwaachia wawekezaji kufanya kazi za namna hiyo.

X. **MABADILIKO YA SHERIA ZA MADINI NA MIKATABA MIKUBWA**

161. Mheshimiwa Spika, Mwaka 2017, Bunge lilipitisha Mabadiliko ya Sheria ya Madini yaliyofanyika mwaka 2017 ambayo yameleta changamoto kubwa katika sekta ya madini hususani kwa wawekezaji, wachimbaji na watafiti. Hii ni kutokana na baadhi ya vifungu kutokupata tafsiri (vinaleta mkanganyiko), baadhi ya vifungu havina afya kwa

wawekezaji na haviwezi kuwa na tija kwenye maendeleo ya taifa.

162. Mheshimiwa spika, Sheria mpya za Ulinzi wa Rasilimali (The Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty, Act 2017) na Sheria ya Madini ya mwaka 2017 ni sheria zinazoleta masharti mapya ya uwekezaji ambayo ni changamoto. Changamoto hizo ni pamoja na kufanya utafutaji wa madini katika sekta ya madini umekufa kwa mfano, kutokana na sheria hii. Kwa mfano kifungu namba 5(2) cha sheria ya Madini iliyoreshkebishwa mwaka 2017 kinaneleza kuwa madini yoyote yaliyochimbwa ni mali ya Serikali bila kujali kama yamechimbwa na kampuni kwa gharama zake. Kutokana na kifungu hiki ni wazi kwamba makampuni hayapo tayari kuichimbia Serikali madini ila yapo tayari kushirikiana na Serikali kama mbia anayetoa fedha kugharamia uchimbaji. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kauli ya Serikali, ni lini sheria hii ambayo inavifungu kama hivi, italetwa Bungeni ili kufanyiwa marekebisho.

163. Mheshimiwa Spika, hadi sasa ni miaka miwili imepita sasa na lengo la mabadiliko hayo ilikuwa ni kuleta ahueni kati ya Serikali na wawekezaji. Miaka miwili baada ya Bunge hili kupitisha mabadiliko ya sheria, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu kutoka kwa Serikali mambo yafuatayo; Mosi, Serikali imepata mapato kiasi gani ambayo ni matokeo ya mabadiliko ya sheria hii, na Bunge kwa niaba ya wananchi linajulishwaje Tatu, ni makampuni mangapi ya uchimbaji ambayo yameshafanya mabadariko ili kwenda sambamba na matakwa ya mabadiliko ya Sheria mpya ya Madini?

164. Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 5(3) cha Sheria kinatamka kwamba Serikali itakuwa na haki ya umiliki wa madini yote yatakayovunwa. Kifungu hiki kimezia mkanganyiko katika utekelezaji. Hii ni changamoto kubwa hususani kwa wawekezaji kutokana na masharti ya taasisi nyingi za fedha hususani pale wanapotafuta mikopo ya kuendeleza uchimbaji.

165. Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 9(1) cha Sheria kimeweka masharti kuwa shughuli zote za uzinduaji, uchimbaji na upatikanaji au utumiaji wa rasilimali utahakikisha kuwa hakuna rasilimali ghafi itakayosafirishwa nje ya Tanzania. Kifungu hiki kimezua mkanganyiko kutokana na kutoeleza wazi ni aina gani ya rasilimali ambazo hazitasafirishwa nje ya nchi zikiwa ghafi (Raw Minerals/Rough Minerals). Baadhi ya rasilimali ambazo zimetajwa katika rasilimali asili haziwezi kuchakatwa na pengine uchakataji wake unaweza kuwa na athari kwa mazingira, afya za watumiaji na hata kuharibu thamani ya bidhaa husika. Mfano, Madini kama Uranium ambayo yana athari za moja kwa moja za kimazingira na pia ni hatari kwa viumbi hai watakaozunguka jirani na maeneo hayo ya uchimbaji, baadhi ya maliasili ambazo ni viumbi vidogo vidogo (micro-organisms), viumbi wa baharini nk. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza maana halisi ya rasilimali ghafi (raw resources).

166. Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 10(1) na (2) ni muhimu vifungu hivi vikawa na maelezo ya ziada. Kifungu cha 10(1) kinapaswa kueleza bayana ni asilimia ngapi ya mapato inapaswa kubaki katika benki zetu au taasisi za fedha. Vilevile, kifungu cha 10(2) kinalenga kukataza uhamishaji wa mapato yatokanayo na mauzo ya rasilimali na kwa kusema kuwa kitendo hicho ni kinyume na sheria. Pamoja na hiyo Sheria hii inakinzana na baadhi ya vipengele katika Sheria ya Fedha (Finance Act 2016) kuhusu utaratibu wa Ring fencing ambayo inaleta changamoto katika sekta ya madini japo inailettea Serikali mapato, pia vifungu 56(1) kuhusu 'Change in Control'. Kifungu hiki kina changamoto kwa kampuni zinazofanya tafiti.

167. Mheshimiwa Spika, katika maoni ya wadau kupitia Chemba ya Madini, wamebaini kuwa katika kanuni zilizosainiwa hakuna sehemu inayozungumzia namna ya kuendesha maghala ya kuhifadhia madini ghafi. Kanuni hazizungumzii ni nani namna ya uendeshaji wa maghala hayo wala bima endapo jambo lolote litatokea.

168. Mheshimiwa Spika, katika maoni ya wadau katika sekta ya madini yaliyo katika ripoti ya Tanzania Chamber of Mines, wanahitaji Chemba ya Madini ambayo wanachama wake wanachangia 95% ya makusanyo wa kodi na mrahaba iingizwe katika Kamisheni ya Madini. Pamoja na hilo ni wakati muafaka sasa wa Serikali kushiriki katika makongamano mbalimbali ya kimataifa kuhusu madini kama vile Mining Indaba. Hivyo basi Kambi Rasmi inaitaka Serikali kutoa ufanuzi katika maeneo yote yanayoleta mkanganyiko katika Sheria.

169. Mheshimiwa Spika, Taifa hili limeingia mikataba mingi mikubwa na Makampuni ya Madini. Kwa kuwa Bunge ndicho chombo kikuu cha kuismamia na kuishauri Serikali kwa niaba ya wananchi, na ili kuongeza wigo wa uwazi katika rasilimali za Taifa, ni lini sasa mikataba yote ambayo Serikali illingia na Makampuni ya Uchimbaji Madini italetwa hapa Bungeni ili Bunge liweze kuipitia na kuishauri Serikali kwa niaba ya Watanzania wote?

Y. HITIMISHO

170. Mheshimiwa Spika, Napenda kumalizia hotuba yangu kwa kusitiza mambo yafuatayo:-

i. Serikali iwaambie watanzania hatima ya majadiliano na Kampuni ya ACACIA na fedha ambazo ilipaswa kulipwa ni kwa nini fedha hizo hazijalipwa. Ikiwa Makampuni haya yalikwepa kodi kama ambavyo watanzania tuliambiwa ni kwa nini hadi sasa bado hayajalipa fedha hizo. Na ikiwa Serikali iliudanganya umma, ni lini sasa Serikali itatoa taarifa sahihi kuhusu fedha hizo.

ii. Je, ni lini sheria zilizopitishwa kwa msukumo mkubwa na alliyekuwa waziri wa sheria, Prof. Kabudi kuhusu ulinzi wa rasilimali "The Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty, Act 2017 pamoja na Marekebisho ya Sheria ya Madini ya mwaka 2017 ambazo kwa pamoja zinaathiri sekta ya uwekezaji kwa kutaka mashauri ya kibiashara kati ya makampuni makubwa na nchi kufanyika ndani ya nchi

kinyume na Mkataba wa Kimataifa wa MIGA wa kulinda uwekezaji mkubwa Duniani ambazo Tanzania iliridhia zitafanyiwa marekebisho ili kuliondoa Taifa katika mkwamo wa sasa?

iii. Wananchi walioathirika na maji ya sumu kutoka Mgodi wa North Mara watalipwa kiasi gani cha fedha kama sehemu ya fidia ya madhara waliyopata kwa kipindi kirefu.

iv. Nini kauli ya Serikali kuhusu bakaa ya Dola za Marekani 622,175 na shilingi 130,331,274.45 zilizobaki kutoka sehemu ya ruzuku ya Dola za Marekani 3,000,000 zilizotolewa na Benki ya Dunia ili zitolewe kama ruzuku kwa wachimbaji wadogo, fedha ambazo wachimbaji wadogo walipaswa kupata ambazo hadi sasa hawajapewa, ni linii wachimbaji wadogo watapewa ruzuku hiyo toka Benki ya Dunia, ambayo Serikali hajaitoa kwa zaidi ya mlaka minne sasa?

v. Serikali inachukua hatua gani dhidi ya watendaji wanaohujumu uchumi wa Taifa katika Kampuni ya Migodi ambayo Serikali inamiliki hisa, migodi ambayo Serikali mara zote imekuwa ikipata hasara kwa uzembe wa watendaji wake?

171. Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha.

.....
John W. Heche, (Mb)

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI
KATIKA WIZARA YA MADINI**

27 Mei, 2019

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Heche, tunakushukuru sana kwa kupitia hotuba yako kama Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara hii ya Madini. Tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa wachangiaji wetu kwakweli ni wachache, ni sita tu; lakini muda ulivyo nitawaomba niongeze nusu saa. Tuvumiliane, tutakwenda haraka haraka wote watapata nafasi ili angalau basi jioni anaporudi Mheshimiwa Waziri badala ya wengine kuchangia jioni halafu majibu anakuwa hajayatafuta, ni vizuri tukachangia asubuhi hii ili jioni tukirudi Mheshimiwa Waziri awe katika wakati wa kuweza kujibu. Wale ambao hatuna nafasi ya kuchangia nawaomba basi tuandike mambo yetu, maoni, ushauri wetu tuweze kumpelekea Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri wako hapa wachukue maoni yetu ili waweze kujiblu baadaye.

Kwa hiyo, CCM wana nafasi zao nne lakini wamekubaliana watachangia kwa dakika tano, tano; kwa hiyo watakuwa nane katika zile nne na upinzani wana nafasi zao mbili wameamua dakika 10 kila mmoja kwa hiyo tunaendelea.

Tunaanza wa kwanza Neema Mgaya dakika tano, jielekezeni moja kwa moja maana dakika tano ni chache sana.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kuweza kusimama na kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kazi nzuri ya kuamua kujenga ukuta Mererani. Nilipongeze Jeshi, nimpongeze Mkuu wa Majeshi, *General Venance Mabeyo*, kwa usimamizi mzuri wa ujenzi huu wa ukuta wa Mererani. Tumeona ndani ya miezi mitatu Jeshi limeweza kujenga kilometra 24.5 na kutumia gharama ndogo ya bilioni 5.2 ambazo kwa mkandarasi wa kawaida Serikali ingeweza kutumia zaidi ya bilioni nane na kutumia muda mrefu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pongezi hizi si bure tu, tumeweza kuona matunda ya ukuta huu wa Mererani na tumeona

kwamba mapato ya Tanzanite yameongezeka kutoka milioni 700 kwa mwaka, na katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri amesema mpaka kufika Machi, mapato ya Tanzanite yameongezeka mpaka bilioni 1.43 na hivi sasa ninavyozungumza mapato ya Tanzanite yameongezeka mpaka bilioni 2.3. Hongera sana Wizara ya Madini kwa kazi nzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niendelee pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Madini kwa kazi nzuri anayoifanya ya kusimamia uanzishwaji wa masoko ya madini. Ndani ya muda mchache wa miezi miwili tumeona kwamba wameshawea kufungua masoko 13 ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuanzishwa kwa masoko haya, nilikuwa na ushauri katika Wizara hii ya Madini.

Mheshimiwa Spika, kwanza; Mheshimiwa Waziri na timu yako mhakikishe kwamba mnasimamia vizuri masoko haya ya madini ya kuhakikisha kwamba yanatimiza lengo lilokusudiwa na yasiende kugeuka kuwa kichaka cha wafanyabiashara haramu wa madini. Vile vile niwashauri Wizara hii muendeleee kuwafanyia utafiti wa madini wachimbaji wadogo ili kuweza kuwapunguzia gharama ya uchimbaji. Vilevile endeleeni kuwatengea maeneo mengi wachimbaji hawa wadogo wa madini na ambayo yameshafanyiwa utafiti ili kuweza pia kuwapunguzia gharama za utafiti wachimbajia hawa wadogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia nniombe Serikali iwasaidie wachimbaji wadogo katika suala zima la *environmental impact assessment* kule kwenye maeneo yao ambayo wanachimba madini. Muhakikishe kwamba mnawaelekeza namna bora ya kuchimba madini lakini wakati huo huo wakiwa wanatunza mazingira.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie sua la mradi wa Liganga na Mchuchuma. Mimi na Watanzania wengine hususan wakazi wa Mkoa wa Njombe Wilaya ya Ludewa tungependa sana kujua hatma ya mradi huu wa Liganga na

Mchuchuma, kwani tumeweza kusikia mambo mengi mazuri yanayotokana na mradi huu lakini vilevile mradi huu umekuwa ni kichocheo kikubwa katika uchumi. Kwa sababu mradi huu endapo kama utamalizika utatoa ajira za moja kwa moja kwa watu 5,000 lakini ajira ambazo *indirect* kwa maana ya kwamba ya wakandarasi na jamii ambayo inazunguka mradi ule watu 30,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile mradi huu kama utakamilika utaenda kuchangia Pato la Taifa (*GDP*) asilimia tatu mpaka asilimia nne. Hivyo basi na sisi wananchi wa Mkoa wa Njombe tuna hamu ya kuyaona mafanikio hayo na hivyo tunaiomba Seri kali iweze kutuambia *status* ya mradi huu iko vipi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kusema, huu ni mradi wa kielelezo wa mpango wa miaka mitano kuanzia mwaka 2015 mpaka 2016 na 2020 mpaka 2021; lakini mpaka sasa ninavyozungumza hapa takriban miaka minne imeshapita na umebakia m wak ammoja tu hivyo basi kilio chetu wananchi wa Mkoa wa Njombe hususana Wilaya ya Ludewa tunaomba kujuu *status* ya mradi huu Mheshimiwa Waziri ukija kufanya *wind up*, na kinyume cha hapo kwakweli utanisamehe Mheshimiwa naweza nikaja kushika shilingi.

SPIKA: Ahsante sana kwa kutumia muda wako vizuri sana

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Neema, umetumia muda vizuri mno. Mheshimiwa Catherine Magige, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein amar dakika tano tano.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Dotto Biteko na Naibu wake Mheshimiwa Stanslaus Nyongo kwa kazi nzuri wanayoifanya. Mheshimiwa Dotto, tunajua mti wenye matunda ndio unaopigwa mawe;

hayo mawe endelea kuyapokea, piga kazi kama unavyopiga msaidieni Rais. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 22 Januari, Mheshimiwa Rais alitiisha kikao cha wadau wa madini wote Tanzania pale Dar es Salaam; na wadau wale walifurahi sana na kumshukuru Mheshimiwa Rais wa wanyonge kwa kuwajali na kuwaona na kuona umuhimu wao na kuwaita.

Mheshimiwa Spika, mionganoni mwa changamoto ambazo wadau wa madini walizomba kwa Mheshimiwa Rais; changamoto kubwa ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) ambayo ilikuwa asilimia 18 na kodi ya zuio asilimia 5. Mheshimiwa Rais aliyapokea na akaahidi atayafanyia kazi. Serikali sikivu ya Awamu ya Tano ililetu Bungeni tarehe 9 Februari kufanya marekebisho Muswada wa Sheria wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) na hii ya zuio la asilimia tano, ilipitishwa na Mheshimiwa Rais alisaini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini mpaka sasahivi zuio ndilo ambali limepita lakini mpaka asasahivi wachimbaji wanateseka. *TRA* bado wanachaji ongezeko la *VAT*la asilimia 18, sasa mimi najiuliza, kama Bungeni tulipitisha, Mheshimiwa Rais alisaini, wao ni nani? Najua Waziri wa Fedha ananisikia, jamani hawa wafanyabiashara wa madini wanateseka, na mnawachonganisha na Mheshimiwa Rais, alipitisha na Bunge tulipitisha, nani mwingine zaidi wa kuacha kutekeleza haya maagizo? Waziri wa Fedha unanisikia, Waziri wa Madini unanisikia na leo nashika shilingi kwa sababu Bunge tulishapitisha. Hawa wafanyabiashara wazawa wana mitaji midogo ukilinganisha na wageni ambao hii asilimia 18 ya *VAT* haiwahu, inawahusu hawa hawa wafanyabiashara wetu wadogo.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali uangalie na Mheshimiwa Rais huko ulipo unisikie, ulichokisaini mpaka sasa hivi wafanyabiashara wa madini hawajatendewa haki. kwa hiyo Mheshimiwa Rais siku ile ni kama siku nzima amekaa na wale wafanyabiashara umepoteza muda kwa sababu

hawajatekeleza. Tunaomba watekeleze haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze moja kwa moja mchango wangu katika *export permit*, kibali cha kusafirisha madini. Sheria ya Madini inatamka kuwa Katibu Mtendaji wa Tume ndiye mwenye mamlaka ya kusaini vibali vya kusafirisha madini. Katibu Mtendaji wa Tume yupo Dodoma. Wafanyabiashara wengi nchini wako sehemu mbalimbali. Inachukua muda mrefu Katibu huyu kuletewa hapa Dodoma mpaka kusaini madini yaweze kusafirishwa nje. Hapa Tanzania inachukua hata wiki ilhali wenzenetu Kenya wanachukua dakika 10.

Naomba kila mkoa angeteuliwa mtu ambaye mnamuona anafaa aweze k ufanya hii kazi kuliko kukaa kusubiri huyu Katibu Mtendaji wa Tume, akiwa hayuko, akiumwa, kazi zinasimama. Hivi jamani, hii Serikali ya Awamu ya Tano kuna kitu kama hiki? Kazi zisimame kwa ajili ya mtu mmoja? Haiwezekani! Mheshimiwa Waziri, naomba uliangalie hili, wawepo watu ambao wanaweza kufanya hii kazi, sio mtu mmoja tu wamtegemee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumeona Wizara ya Mazingira imepiga marufuku mifuko ya plastiki. Nawapongeza sana kwa sababu ni katika suala zima la kuhifadhi mazingira; lakini wafanyabiashara wa madini hasa ya *Tanzanite* wanasafirisha madini yao kwenda nje kwa mifuko ya aina hii ambayo kama imepigwa marufuku madini haya ambayo yanakuwa yamesafishwa, yameshawekwa katika ubora yataharibika. Kwa hiyo wenyewe bila kutumia mifuko kama hii tutaharibu biashara yao. Naomba, najua hii Serikali ni sikuvi na iko radhi kuongea na hawa wafanyabiashara, iangalie ni jinsi gani wao waruhusiwe hata kutumia mifuko ambayo wamekuwa wakitumia bila kuathiri mazingira kwa sababu kwanza mifuko wenyewe inaenda nje haikai hapa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Arusha kulikuwa na maonesho ya madini tangu mwaka 1992, yalikuwa yanaitwa *Arusha Game Fair* lakini cha kusikitisha...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Bahati mbaya dakika tano zimeisha Mheshimiwa Catherine.

MHE. CATHERINE V. M AGIGE: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia 100. (*Makofi*)

SPIKA: Hayo ya mwisho yaandikie Mheshimiwa Catherine. Mheshimiwa Hussein Amar, dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Sebastian Kapufi.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia. Kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu na Watendaji wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nauelekeza upande wa wachimbaji wadogo hususan wa Wilaya ya Nyang'wale. Wachimbaji hawa mapato yanazidi kupotea, huwa nasema kila mara, lakini pia niipongeze Serikali ya Wilaya ya Geita ama Mkoa wa Geita kwa kuvuka malengo ya ukusanyaji asilimia 109. Hata hivyo asilimia hizo bado mimi nasema kuwa ni ndogo kwa sababu wachimbaji walio wengi mpaka sasahivi hawajatambuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuna wachimbaji katika maeneo ya Isekeli, Bululu, Ifugandi, Shibalanga, Rubando, Iyenze, Nyamalapa, Iyulu, Ibalangulu na Kasue. Maeneo yote yale, uchimbaji madogo mdogo unaendelea na ile dhahabu inapotea. Kwanini Serikali isichukue hatua ya haraka ya kwenda kuyapima yale maeneo ya kuwapa leseni wale wachimbaji wadogo ili tuweze kuwatambua na kuweza kupata yale mapato? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili ni kwamba kuna changamoto kwa wachimbaji wadogo wadogo wadogo na wadau wa madini katika Wilaya ya

Nyang'wale kwa sababu tumeuwa hatuna Afisa Madini maeneo hayo na wachenjuaji wamekuwa wakipata gharama kubwa kwa kufuatilia vibali kutoka Wilayani Nyang'wale kwenda Geita. Kibali hicho unakifuata kwa gharama ya kilometra 180 kw akutumia *trip* mbili za gari. *Trip* ya kwanza ni kufuata kibali kwa ajili ya kuchukua *carbon* kuzipeleka Geita, na kibali cha pili ni kutoka pale Madini kwenda *illusion*, gharama zote hizo zinakuwa ni za mwenye *carbon*. Kwa hiyo ninakuomba Mheshimiwa Waziri, tufungulie ofisi ndogo ya Madini pale Nyang'wale tuweze kuепusha zile gharama kwa sababu gharama zinakuwa ni kubwa sana. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, pia bado tuna changamoto nyingine, tuna *illusion* zetu pale katika Wilaya ya Nyang'wale. Maafisa Madini wanakaa Mkoani Geita, ukitaka kuwafuata inabidi utumie gharama zako wewe mwenyewe kwenda kuwafuata. Hizo gharama tunaomba mtuepushie kwa kuwasogeza karibu hao Maafisa Madini pale Wilayani Nyang'wale. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, pia kuna urasimu mkubwa sana; Ofisi ya Madini Geita kuna urasimu. Unapofuatilia vibali ukifika pale unachukua zaidi ya masaa matatu kupewa kile kibali. Hicho kibali ni cha kwenda kuchukua *carbon* kutoka kwenye maeneo yako, kibali hicho ni cha kupeleka *carbon* pale madini. Lakini pia kibali kile cha kutoka madini kwenda *illusion* nacho unachukua zaidi ya masaa matatu kukipata kile kibali. Mimi nadhani utaratibu huu sio mzuri, jaribuni kuangalia utaratibu huo, haupendezi.

Mheshimiwa Spika, pia bado kuna urasimu mwingine. Unapomaliza kuchoma dhahabu yako pale kwenye *illusion*, TMA yuko pale, madini yuko pale na maafisa wengine wako pale wanakuandikia kibali hicho cha kubeba dhahabu yako kupeleka kwenye soko; lakini bado utakapoibeba ile dhahabu ambayo labda umeipata gramu 100, utakapokwenda kwenye lile soko unakuta ofisi ya Tume ya Madini wanaipima tena ile dhahabu pale, ile dhahabu bahati mbaya ikitokea imepungua ilikuwa gramu 100 lakini

wakaipima ikawa gramu 99 wanakusumbua kwamba gramu moja imekwenda wapi, ilhali kule kwenye *illusion* wamekuandikia gharama ya mrahaba na *service levy* iko kwenye karatasi. Kama imepungua si ni gharama yangu mimi acha ipotee hiyo? Lakini wana usumbufu na wanatisha watu, kwamba wameipeleka wapi.

Mheshimiwa Spika, suala hili sio zuri, urasimu huo sio mzuri. Dhahabu si *cocaine*, hii ni biashara. Jiulize huyu amepitaje hiyo dhahabu mpaka gramu 100 leo hii imepungua gramu moja, ni kipimo, vipimo vinatofautiana; lakini pamekuwa na usumbufu na vitisho. Kwa hiyo nakuambia Mheshimiwa Waziri, jaribu kuliangalia kwa Mkoa wa Geita, usumbufu huo upo. Kwa haya machache nakushukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasiya kuweza kuchangia. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Amar. Mheshimiwa Sebastian Kapufi atafuatiwa na Mheshimiwa Maftaha na Mheshimiwa Heche ajiandae.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, na mimi nimpongeze Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, na mimi pia nakumbuka hiyo tarehe 22 na 23 Januari nilikuwepo pale Dar es Salaam wakati akiwepo Mheshimiwa Rais akikaa na wachimbaji wadogo. Kati ya mambo aliyoaongea Mheshimiwa Rais ilikuwa ni pamoja na haya yafuatayo; Aliwaomba watendaji akiwepo Waziri kwamba yeye kama amefunga mlango wao waangalie hata namna ya kufungua dirisha. Alipolisema hilo alikuwa anamaanisha haiwezekani yeye Mheshimiwa Rais akafanya mambo yote, kuna baadhi ya mambo wamsaidie, watendaji hawa.

Mheshimiwa Spika, nikilisema hilo namaanisha mimi ninafsi kwanza nikiri mbele yako ni moja kati ya wachimbaji wadogo wa madini, nchimba madini ya dhahabu. Limekuwepo tatizo moja la kitu wanaita makinikia. Naomba

nikiri, katika mgodi wangu pale Mpanga tunayo makinikia ya kutosha ambapo naamini Serikali hii ilikuwa na uwezo wa kupata kiwango kikubwa cha fedha. Makinikia yale yamekuwepo kutokana na sheria ya zamani kabla ya sheri ampya kupitishwa hapa Bungeni. Sasa anapokuja kuadhibiwa mtu kwa sheria ya zamani ambayo ilimpa nafasi ya kufanya hiyo kazi nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri utusaidie katika hili na najua Mheshimiwa Waziri nimekuwa nikipita kwako kwa muda mwingi nikikueleza kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Spika, katika hili niseme, katika mgodi kwa mfano huu wa Katavi-Kapufi, kuna makinikia ya kutosha ambayo hayo, mbali ya makinikia hayo, kuna ajira za Watanzania wenzangu, zaidi ya Watanzania 400, wameajiriwa pale, lakini suala ambalo linatukabili sasa hivi ni hiyo kuzuua kuyasafirisha makinikia haya ambayo yalikuwepo kutokana na sheria ya zamani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hilo namwomba sana Mheshimiwa Waziri, atusaidie na hata pale ambapo anaonyeshwa kwamba mchango wa dhahabu ni asilimia 86.07, bado mchango wa dhahabu ungeweza kuwa mkubwa zaidi. Nikilisema hili, niendelee kusema, kwa wale wote ambao hata wana makinikia ya kopa ya sheria ya zamani, ndiyo maana Mheshimiwa Rais alisema hivi, kiwepo kipindi cha mpito, wakati ambapo watu wanajipanga kwa ajili ya kuja na *smelter na refinery*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, siyo suala la mara moja, ni uwekezaji mwingine mkubwa, kwa hiyo, kama kuna watu wamefanya uwekezaji mkubwa, wengine wakishirikiana na watu wa nchi za nje, leo unapomwambia ashughulikie suala la *smelter na refinery*, hakuna mtu anakataa hilo, lakini siyo suala la usiku mmoja, *it takes time*, vipi watu hao wasipewe kipindi hiki cha mpito? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitoke hapo, nije katika suala llingine, ni kweli tunazungumzia wachimbaji wadogo, lakini naomba sana jitihada ambazo zinaendelea kufanywa

na Wizara, kuendeleza tafiti nyingine na kuhakikisha tunaendelea kujenga uchimbaji wa kati na uchimbaji mkubwa pia. Kwa sababu mchimbaji mdogo, ukimfanya mazingira mazuri, atakua, akishakua anaweza kwenda kuwa mchimbaji wa kati na baadaye akaja kuwa mchimbaji mkubwa, kwa hiyo, maeneo yote hayo na bila kuacha tafiti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, madini yanakuwa na thamani ukiyatoa ardhini, lakini wakati yakiwa bado yako ardhini, ni mwamba kama mwamba mwingine wowote ule. Kwa hiyo, Watanzania kwa ujumla wake, Baba wa Taifa alifanya kazi nzuri ya kusema kwamba, hatuchimbi mpaka Watanzania watakapokuwa tayari. Wasiwasi wangu, tusipojitahidi tukachimba, kwa Baraka hizi alizotupa Mwenyezi Mungu, tutajisifu tuna dhahabu tuna nini, lakini kama bado iko chini ya ardhi, haina thamani, thamani yake ni pale itakapotoka ardhini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niseme, kwa nini *tusi-take advantage* ya madini haya tuliyonayo kuhakikisha yanachimbwa kwa kadri tutakavyoweza, halafu tunakwenda kwenye uwekezaji mwingine tofauti. Nchi zenyе mafuta na gesi, wanahakikisha kwa sababu ina *under go law of diminishing return*, madini yanakwisha. Kwa hiyo, kabla ya hayajakwisha, tuhakikishe yametusaidia katika maeneo mengine, huo ndiyo ushauri wangu kwa Serikali yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kapufi kwa ushauri mzuri sana. Nilishakutaja Mheshimiwa Maftah, wewe ni dakika 10 na Mheshimiwa Heche dakika 10 na Mheshimiwa Musukuma ajiandae.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu. Pia nikushukuru wewe kwa

kunipa nafasi hii. Naomba nami nichangie mchango wangu kwenye Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, mwaka 2017 uliunda Kamati ya Kuchunguza Madini ya *Tanzanite* na Madini ya Almasi na nilikuwa mionganoni mwa wajumbe kwenye Kamati ile. Naomba nizungumze yale mapendekezo ambayo Kamati ilipendekeza utekelezaji wake umekuwa kwa kiasi gani. Nimshukuru Mheshimiwa Dotto Biteko, Waziri wa Wizara hii kwa sababu ndiye aliyekuwa Mwenyekiti wa ile Kamati ya *Tanzanite* na kwa kiasi kikubwa hotuba yake imagusagusa mambo hapa nimeweza kuyasikia, lakini nataka niweze kufahamu utekelezaji hasa ukoje.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, jambo la kwanza, tuliona pale Mererani pale ambapo kuna Mgodi wa *Tanzanite* kwamba kumekuwa na mrundikano wa leseni nyingi sana za wachimbaji hawa wadogowadogo ambaao amewataja na tuliweza kubaini kwamba kuna leseni zaidi ya 900 pale ambazo zimetolewa na Serikali na Wizara na kukawa na changamoto kubwa kule chini, wale wachimbaji wadogowadogo wanavyochimba, kwamba wanafikia sehemu inaitwa mtobozano, wanatobozana kule chini wanakutana wanaauana huko chini, watanzania wengi wanakufa.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua je, pendekezo lile Mheshimiwa Waziri limetekelezwa kwa kiasi gani kwamba, wale Watanzania wanaokufa kutokana na idadi kubwa ya leseni ndogondogo zilizotolewa pale Mererani na kule chini wanaauana kwa sababu wanakutana kule chini na wakati mwingine wanakutana na ule mgodi wa *TML* na wanaauawa kule chini, Watanzania wengi sana. Suala hili limefikia wapi na utekelezaji wake ukoje? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine naomba kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri hapa, kwamba amezungumza suala la *one stop center* kwamba itajengwa katika ule ukuta wa Mererani pake Arusha. Utaratibu wa hii *one stop center* ukoje, unakwenda kujenga kwa ajili ya kuza

yale madini yetu kwa sababu ya wanunuzi ambao wanakuja kununua kutoka nje ya nchi au tunakwenda kujenga zile *smelters* za kuchenjua yale madini. Kwa sababu tatizo limekuwa ni kubwa sana kwamba uchenjuaji unafanyika India kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, hili jambo Kamati ilizungumza sana, kwamba Watanzania wanakosa ajira sana kwa sababu yake madini yetu hayachenjuliwi hapa Tanzania, hasa madini ya *Tanzanite* na kwa kiasi kikubwa yanachenjuliwa kule India na taarifa zinaeleza kwamba India kuna watu zaidi ya laki sita wamepata ajira kutokana na uchenjuaji wa madini ya *Tanzanite* ambayo yanatoka Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kujua *seriousness* ya Serikali juu ya kuchenjua madini haya pale Mererani Arusha. Kwa hiyo, hlio *smelter one stop center* inakwenda kutoa suruhisho la kudumu, kwamba Watanzania sasa tuweze kuchenjua wenyewe na kule India kuwe hakuna tena ajira ya kuchenjua haya madini ya *tanzanite*.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine naomba kufahamu, Mheshimiwa Waziri atueleze, wakati tunapitia zile taarifa mbalimbali za watoa taarifa mbalimbali tulielezwa kwamba kutokana na utoroshwaji wa madini ya *tanzanite* ambao unafanyika kwenye Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, kuna njia za panya zaidi ya 400 ambazo madini haya yanapita kuelekea kule Kenya na hili limepelekea Watanzania wenyewe tuwe ni watu wa mwisho kunufaika na madini haya ambayo yanapatikana Tanzania tu duniani, sisi wenyewe tukawa watu wa mwisho. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wa kwanza ni kule yanakokwenda Marekani, ambako ni *Tucson* kule Marekani ndiko yanakouzwa na wanaopeleka kule ni Wahindi, ambao wanakwenda kuuza kwa kiasi kikubwa sana haya madini! (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hao ndiyo wanufaikaji wa pili, wanufaikaji wa tatu ni watu wa Afrika Kusini, ambako hii

kampuni ya *TML* ndiyo inaonyesha kwamba uhusiano wake mkubwa na nchi ya *South Africa* ndiko wanakotoka kule, lakini wengine ni Wakenya, wa nne, na sisi wenyewe ni wa mwisho watu Watanzania. Sasa hili limepelekea kwa sababu kuna njia nydingi za panya, haya madini yanatoroshwa katika nchi ya Tanzania kuelekea nchi ya Kenya na taarifa zinasema, Kenya imeendelea baadhi ya miji imekuwa ni mikubwa, imekuwa na maendeleo ukiwemo Mji wa Naivasha kwa sababu ya madini ya *tanzanite* yanayotoroshwa kutoka Mererani Arusha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kujua, hizi njia 400, kwa sababu imeelezwa hapa kwenye na taarifa ya Kamati na ya Upinzani imezungumzwa pia kwamba *personnels* wenyewe hawatoshi. Mpango wa Wizara ukoje wa kuajiri *personnel* ya kuweza kuhakikisha kwamba tunadhiliti hizi njia za panya, njia 400 zillizopo pale Arusha na kule Mkao wa Kilimanjaro. Mheshimiwa Waziri naomba atupe maelezo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, kulikuwa na suala hili la *STAMICO*, kwamba, *STAMICO* tumekuwa tunazungumza kwa muda mrefu sana, kwamba ni taasisi ya Serikali ambayo imekosa nguvu, aidha nguvu ya kifedha ama nguvu ya kiusimamizi, kwamba hata wale watendaji wake wamekuwa ni watu ambao tulivyoenda kuangalia wizi ambaulikuwa unafanywa na watu wa *TML*, pale Mererani Arusha, yaani zinaibiwa ndoo sita za madini, yule mtu wa *STAMICO* yuko palepale ndani, ukiangalia ile *clip* inaonesha kabisa mtu wa *STAMICO* amewekwa pembeni kule, watu wanafanya *sorting* ya madini, ndoo sita zinaibiwa, ye ye yuko palepale, ambaye ndiyo tegemeo la Serikali, tegemeo la Watanzania kwamba aweze kusimamia madini yetu pale ili Serikali iweze kupaya gawio, iweze kupata tozo, iweze kupata kila kitu, ye ye yuko palepale, ndoo sita za madini zinaibiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atuambie, kwamba Watanzania hawa tunaowapeleka kwenye kampuni hii ya Serikali, ambayo sisi tunaitegemea, sasa hivi wameweka mkakati gani wa kuweka *personnel*

ambao wana uwezo wa kusimamia madini yetu ili Serikali isikose mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi *STAMICO* tuna asilimia pale 49 katika ile kampuni ya *TML*, kwamba ushirikiano wa Serikali tunategemea kampuni hiyo, kwa hiyo ni lazima tuwe na watendaji ambao wana *capacity* kubwa ya kuweza kuwazuia wale wageni, wale akina Rizwani Ulaa, na wengine wale wenza ambao walikuwa wanaiba yale madini yetu takribani ndoo sita na Serikali kukosa kabisa gawio na kukosa kabisa mapato.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kuna hisa moja ambayo ilikuwa imezungumzwa sana katika ile kampuni ya *TML*, tunaita hisa kivuli, ya mtu mmoja anaitwa Amy Mpungwe, hii hisa imekuwa haielewekieleweki, kwamba hiyo hisa hata gawio nalo halipatikani kwa huyo Amy Mpungwe, ambaye ni Mtanzania, alilingia kwenye ile *TML*. Sasa Mheshimiwa Waziri tunaomba atupe taarifa, tumezungumza suala la *local content* hapa, kwamba kuwawezesha watanzania waweze kujihusisha na rasilimali za Tanzania na sheria hii inaeleza asilimia 25 Watanzania waweze kuhusishwa katika ajira na katika kumiliki rasilimali za Watanzania. Ile hisa moja iliyopo kwenye kampuni hii ya *TML*, ya Amy Mpungwe ambaye ni Mtanzania, bado inaendelea kuwa hisa kivuli, hisa hewa au namna gani. Tunaomba atupe maelezo Mheshimiwa Dotto Biteko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, naomba kuzungumza, mwaka jana nilieleza hapa suala la madini ya *blue sapphire*, ambayo kwa kiasi kikubwa duniani sasa hivi yanaonekana kwamba yanazalishwa kutoka nchi ya Sri Lanka, lakini ukija kule kusini, Ruvuma pale Tunduru, madini ya *blue sapphire* yanapatikana kwa kiasi kikubwa sana na wanunuzi wa madini haya hapa Tanzania ni watu wa Sri Lanka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa niiombe Serikali, kwa sababu hajjaweka utaratibu mzuri, hajjaweka utaratibu wa kuwa wa *certificate of origin*, yaani kuoesha kwamba madini haya

yanatoka Tanzania, kwa sababu yakinunuliwa na wale wa Sri Lanka, wanapeleka kule Sri Lanka, wanajumuisha na ya kwao, halafu ni madini yenye thamani sana duniani, *blue sapphire*, halafu wanasesma haya madini yote yanatoka Sri Lanka, wakati mengi yake yanatoka kwetu Tanzania na hajilikani kama yanatoka Tanzania na yanatoka Tunduru Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri, mwaka jana nilizungumza hapa hili suala kwamba aende Tunduru akaweke utaratibu mzuri, yale madini yetu yanayotoka pale Tunduru, yaweze kuonyeshwa kweli yanatoka Tanzania na yanatoka Tunduru badala ya kwamba yanajumuishwa kule dunia nzima inafahamu *blue sapphire* inatoka Sri Lanka pekee, kumbe siyo kweli. Namwomba Mheshimiwa Waziri na Wizara, hili suala waliangalie kwa jicho la kipekee kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, kuna suala hili Mheshimiwa Waziri amezungumza hapa, kwamba tunahitaji kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo waweze kupata manufaa na hawa ni Watanzania na hawa ndiyo maskini ambao tunawazungumzia hapa, lakini ukienda Tanga leo hii hawa wachimbaji wadogo wamepewa leseni, lakini bado wanasumbuliwa sana na Askari wetu. Yaani wale wachimbaji wakubwa kwa mfano, ukienda kwenye maeneo ya *Umba River*, eneo la Kalalani, Mgombeni, Kigwase, Mwakijembe, wanatumwa wale watu polisi Askari wa....

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Maftah, nakushukuru sana.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie, kidogo tu.

SPIKA: Haya haya.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, nilichokuwa nasema, kwamba ukienda kule Tanga kwenye maeneo hayo niliyoyataja, wale wachimbaji wakubwa,

wanawatuma Askari, kwenda kuwabugudha hawa wachimbaji wadogo ambao ni Watanzania kwenye maeneo yetu hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana Serikali kwamba hawa watu wana haki na wamepewa leseni zile za kisheria kabisa, waachiwe ili tuweze kuondokana na umaskini hapa nchini Tanzania. Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Maftaha, umeitetea sana *blue sapphire* kutoka kule Mto Msanjesi, Tunduru kule.

Mheshimiwa Heche, una dakika 10, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Musukuma.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hi ya kuchangia. Kwanza napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Kapufi, nimemsikiliza vizuri sana, amezungumza kwa kweli mambo mazuri kwa ajili ya nchi yetu na nilipokuwa namsikiliza nilifikiri anarejea Sera ya CHADEMA ya Julai, mwaka 2018 inayozungumza kuhusu madini.

Mheshimiwa Spika, wenzetu kule Norway wanapochimba gesi yao na mambo ya madini, wameweke benki, wanaweka akiba kwa ajili ya vizazi vijavyo na sisi kuendelea kuwa na kauli hizi kwamba madini yabaki chini hayaozi hayafanyi nini, siafiki utaratibu huo, ninachokubaliana nacho, ni kwamba, madini haya yanayochimbwa, yachimbwe vizuri na fedha zinazotokana na madini haya zitunzwe kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi almasi duniani, 40% ya almasi inayovaliwa duniani ni almasi ya kutengenezwa. Sasa tunapokwenda kuendelea kusema sijui tuna almasi, wao watu wanaonunua haya madude baadaye wakija waka, hasa haya ya mapambo, wanaweza kuja kuyabadilisha wakaanza kutumia vitu vingine ukabaki na *tanzanite* na almasi ambazo hazina thamani yoyote. Kwa hiyo, nafikiri tuangalie lakini tuna-*insist* kwamba, kila tunapotoa rasilimali

hizi zibaki kwa ajili ya vizazi vingine, tusitumie sisi wenyewe na tukamaliza.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo nahitaji maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, wachimbaji wadogo, wanalipia *environmental impact assessment*, milioni tatu mpaka milioni sita, lakini kuna mtu wa mazingira yuko halmashauri, kazi yake ni nini yule mtu wa halmashauri pale, mpaka hawa watu wanalipia hizo fedha. Mbona mtu wa kilimo tunapokwenda kuomba *consults* hatulipi na tusipofanya *environmental impact assessment*, ambayo nakubali ifanyike, unapigwa faini. Kwa hiyo, nataka kujua kwa nini wachimbaji wadogo wanalipia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, swalii la tatu, sumu iliyotiririka kwenye Mgodi wa Nyamongo, nimeizungumza vizuri kwenye hotuba na ningependa hotuba yangu nzima Mheshimiwa Waziri ajitahidi kuisoma na aijibu. Kuanzia mwaka 2017, watu wamekufa, mali za watu zimepotea, Mto Tigite uliharibika na huu mto unatiririka mpaka Mto Mara, pote kwenye maeneo karibu ya kata sita. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, miaka yote hii, tumekuwa tukiambia Serikali, kwa ushahidi, kwamba kuna watu wanababuka ngozi kwa kuoga maji, viumbe vinakufa, nyasi zinakauka, wakati wote huo Serikali ilikuwa ikitisema, hakuna kitu, hakuna kitu, hakuna kitu. Mheshimiwa Waziri alikuja pale akaona maji yanavyotiririsha, eneo la Kwinyunyi, Kwimange na kule Kegonga, kitongoji kizima watu wamehama, wameacha maeneo yao, hayazalishi chochote kwenye kilimo. Eneo ambalo ulikuwa unalima unapata labda gunia 100, leo ukilima hupati hata gunia 10 kutokana na madini, tembo kuathiri lile eneo.

Mheshimiwa Spika, asa nataka, Mheshimiwa Waziri, kwanza, Serikali wamepiga faini pale, hivi wao wameathirika nini? Kwa sababu walioathirika ni wananchi wanaoishi yale maeneo. Tunataka hizo fedha walizopiga faini, ziende kulipa wananchi ambao wameathirika, wananchi wa Tarime ambao wamekunywa maji ya sumu, ndiyo wakalipwe fidia.

Ng'ombe waliopotea, watu waliokufa na tunataka ifanyie *assessment* mpya, kujua madhara ni kiasi gani na wale wananchi wapate fidia inayostahiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Waziri ni rafiki yangu, nimekuwa nikimshauri kufuata sheria, Sera ya Madini ya Mwaka 2009, inasema, unapohamisha watu kutoka eneo la mgodi, unawalipa fidia, *compensation*, unawajengea makazi, yaani unafanya *reallocation* na unawalipa gharama za kuwahamisha. Hakuna, watu wote waliolipwa fidia Tarime, imekuwa ni kidogo na mgodi umekuwa ukisema, ooh ni kubwa sana, lakini hakuna mtu ambaye amewahi kufanyiwa *resettlement* kwa kujengewa nyumba na kupewa makazi, watu wachache tu waliofanyiwa *resettlement*, halafu hawakulipwa fidia, wakajengewa vinyumba tu, Waziri aliviona na Kamati ya Waziri Muhongo ilisema, vibomolewe na vijengwe upya, ukipiga teke kanadondoka. Sasa tunataka kujua ni kwa nini, hawa watu hawafanyi hivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala la Mchuchuma na Liganga, amelizungumza vizuri sana ndugu yangu hapa Neema. Kampuni ya *Hongda Sichuan*, mwaka 2019 ilisaini mkataba na Serikali na mkataba wa zaidi ya dola bilioni tatu, ambazo ni trillioni 6.8, ambazo zilikuwa zimekuja kufanyiwa *investment* hapa, Watanzania zaidi ya elfu tano walikuwa wanakwenda kupata ajira za moja kwa moja kwenye huu mgodi. Mpaka sasa imekuwa ni kizungumkuti, Serikali ime-*delay* fedha hizi zote ambazo zingekuja kusaidia uchumi wa nchi yetu, nataka Waziri atuambie, ni kwa nini kumekuwa na *delay* tangu mkataba huu usainiwe na Wachina na tukaunda kampuni. Kwa nini mpaka sasa *investment* hii haija-*take off!* Tunataka kujua. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, *service levy*; makampuni yanayofanya kazi pale kwenye mgodi na mgodi wenyewe, umekuwa ukilipa 0.03% ya *service levy* kwenye halmashauri, lakini kampuni ambazo zinalipwa fedha nyingi sana ni kampuni za *insurance*. *Insurance* wanachukua fedha nyingi, wana-*insure* kuanzia dhahabu, mitambo yote mbayo ni ya gharama kubwa na migodi yenyewe, lakini kampuni zote za

insurance, hazilipi hata senti moja ya *service levy* kwenye maeneo ambayo halmashauri zinatoka.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka Waziri aje atuambie, kuna vikampuni vya Watanzania, mtu anafanya kazi ya kujenga kadaraja pale kwenye mgodi, kazi ya milioni 100, analipa 0.03% na siku hizi halmashauri kwa sababu hazina mapato, hata kwenye maduka tu, haya ya wananchi, mtu ana kioski cha milioni mbili, anafukuziwa na 0.03% ya *service levy*. Ni kwa nini makampuni makubwa ya *insurance* ambayo yanachukua matrillioni ya fedha kutoka Tanzania, hayalipi *service levy* kwenye migodi! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ni kuhusu *smelter*. Kwa nia njema kabisa sisi tulizungumza hapa wakati sakata la makenikia linakuja mnatuambia mtatuletea Noah, na Watanzania hawajasahau na tunataka mjibu Noah ziko wapi? Kwa sababu tuliambiwa mambo mengi hapa tukaambiwa na *smelter* inajengwa, mwaka 2017 hakuna *smelter*. Amezungumza Mheshimiwa Kafupi pale, watu wanazidi kupata hasara; 2018 hakuna *smelter*, 2019 hakuna dalili, 2020 hakuna dalili; *smelter* mtajenga lini hapa? Kwa sababu tuliambiwa hapa tumeibiwa sana makenikia haziendi na sisi tunasema *thank you very much, now we want a smelter here*, tunataka *smelter* na watu waanze kufanya uchenjuaji wa madini hayo hapa tuone faida kwenye nchi yetu hii. Kwa sababu hizi kauli za kisiasa ambazo zimekuwa zikifanyika kila siku kufanya kuwahadaa Watanzania sisi ni wazalendo kuliko watu waliokuwepo sijui na nini, tunataka sasa uzalendo huo uonekane kwa vitendo, na tunataka wananchi waanze kunufaika na madini hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na nazungumza hivi kwa sababu watu wanaotoka kwenye maeneo ya madini wameathirika sana. Jana tulikuwa kwenye semina fulani hivi na mtu mmoja akaanza kusema pale, sitaki kumtaja, ni Mbunge na alikuwa Waziri hapa anasema eti tuambiwe *benchmark* ya faida ni nini, kama hatujanufaika tumepata sijui kodi ya trillioni moja. Hivi mzee Ryoba Ilondo ambaye ng'ombe wake zaidi ya 500 wamekufa unamwambia mgodi unafaida gani kwakwe?

Kwa sababu yeye alizoea ng'ombe wale asubuhi anafunga kwenye jembe anakwenda kulima pale Matongo, anavuna, anakamua maziwa watoto wake wanakula; maisha yanaendelea. Alikuwa kwenye nyumba ambazo zimeezekwa kwa majani *fine*, lakini yeye maisha yake yalikuwa yanaendelea, hawajawahi kulala njaa; lakini leo ng'ombe wake wamekufa analala njaa; unamwambiaje mgodi una ufaida, na madini haya yanafaida? kwa hiyo Mheshimiwa Waziri hayo ni mambo *serious* tunaomba majibu kwa ajili ya watanzania, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Heche, Mheshimiwa Joseph Musukuma atafuatia na Mheshimiwa James Milly.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia...

SPIKA: Dakika tano tano.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa sisi jamii tunaotoka kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo ni dhahiri kabisa tumepata Waziri ambaye Ofisi yako inaingilita kirahisi. Tulyaona, kabla ya wewe kulikuwa na Mawaziri Maprofesa hapa siku unataka kukutana naye yaani inabidi uende kwa dobi ukafue hata suluari kwanza, lakini tunakuombea Mungu na uendelee na moyo huo kwa sababu unamsikiliza kila mtu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kwa kweli Wizara hii inafanya vizuri na sisi wapiga kura wetu ambao ni wachimbaji sidhani kama ukimsema vibaya Waziri Dotto atakuelewa; tunahitaji tu kukushauri kwa machache ambayo pengine tunaona ukiyafanya utakuwa rafiki mzuri zaidi ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, kama alivyoeleza Mheshimiwa Kasu, tunaona kwenye maeneo yetu ya wachimbaji kuna shida kubwa sana ya watendaji, shida kubwa sana. Wachimbaji wadogo wengi wameitikia wito wa kulipa kodi

Iakini pale ambapo mtu anapotaka sasa afuate zile *procedure* za kulipa kodi kuwapata watendaji wa Wizara yako ni shughuli; inabidi mtu akae na *carbon* saa nyingine mpaka siku tatu *risk* wezi wako kule wanajua *carbon* imeshaiva. Sasa nikuombe Mheshimiwa Waziri, kama Serikali hajakupa kibali cha kuajiri tunaweza kutumia njia ya dharura tu kama tuliweza kuchukua Wanajeshi wakaenda kuchukua kangomba kule Mtware tunashida gani? Tumuombe Mheshimiwa Raisakupe Wanajeshi waende wakasimamie ni shida kubwa sana unakuta kwa mfano Geita kuna *erosion plant* labda 30 mpaka 50 watumishi wanane inawezekana vipi? Ni mateso makubwa. Mimi nikuombe Mheshimiwa Waziri nimeona hata makusanyo ya Wilaya yangu ya Geita tuna kilo karibu 600 sasa hivi kwa miezi mitatu. Mheshimiwa Waziri mimi naangalia kabisa kwa macho yangu na uzoefu wangu hata theluthi bado hujakusanya dhahabu bado inaibiwa.

Mheshimiwa Spika, hebu nikushauri kwa sababu mimi ukikusanya sana wewe na mimi kwenye halmashauri napata pesa nyngi hebu jaribu hata miezi miwili chukua Wanajeshi tusambazie kule uone dhahabu itakayokuja, kuna dhahabu nyngi. Lakini nikuambie kingine ni kwamba watu wako pia si waaminifu ubovu unaanza kwenye Ofisi yako humo humo kwa wasimamizi na nikuombe Mheshimiwa Waziri ushauri wangu tu pengine unapotaka kuajiri hawa wasimamizi wako Mikoani na Wilayani kuna chuo kile cha Jeshi kiko Kunduchi, nilizungumza hapa, kile cha *NDC*, hebu wachukue kwanza wakafundishwe uzalendo wa kuyalinda haya madini yetu pengine nakuona kila siku mara unafukuza mara unahamisha utaumiza kichwa unazofukuza ni hela dhahabu ni pesa watafutie utaratibu waende wakafundishwe pale miezi mitatu wakirudi hapo hawataiba, hawatashiriki huo wizi unoaoendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine kuna kitu inaitwa *inspection fee* inachukuliwa kule kwetu kwenye migodi yetu kule asilimia moja. Sasa nilikuwa tu nakushauri hii asilimia moja hebu jaribuni kuangalia hata theluthi ibaki kule mikoani. Leo Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya na Kamati ya Ulinzi na Usalama ndiyo tumemkabidhi majukumu yote; tukishafungua maduka

tu tunawaachia walinzi wao kufukuzana na wezi wao halafu hawana kitu unampigia Mkuu wa Mkoa njoo kuna watu wanaiba madini anaanza kuomba mafuta kwa Mkurugenzi, hiki kitu si sawa, turudishieni hata kidogo ili Wakuu wetu wa Wilaya na Wakurugenzi na Wakuu wa Mikoa wale na fungu la kuwapa hata motisha wale watu wanaoenda kufukuzana na wezi kule kwenye machimbo usiku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, linguine, Geita hatujalipwa hela zetu, na wewe mwenyewe unafahamu. Mheshimiwa Nyongo amekuja Geita Mjini Nyamarembo, Magema na Katoma, kuna watu wamefanyiwa *compensation* miaka minane; na ninapata taarifa kwamba wanaanza kulipwa lakini hizo fidia wanazolipwa ni wamepunjwa nataka njue kama mdhamini mkuu wa Serikali alishirikishwa kwenda kuhakikisha kwamba watu wetu wanapata pesa inayostahili na maeneo yao au na nyumba zao? Si vibaya Mheshimiwa Waziri mimi nikumvie na yeye wenyewe ulikuwa mjumbe wangu wa Kamati ya Siasa, nilivalia njuga kipindi kile 2013, mama Tibaijuka Mungu amsaidie sana alitusaidia watu walilipwa mabilioni ya pesa si vibaya mkachukua uzoefu wake alitumia njia gani watu wetu wakalipwa, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa James Millya dakika tano.

MHE. JAMES K. MILLYA: Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze sana Wizara kwa ujumla wake kwa kazi kubwa wanayofanya.

Mimi ni Mjumbe wa Kamati hii najua kazi mnayofanya ni kubwa na kubwa na hongereni sana. Mheshimiwa Maftaha ameongelea wizi wa Mererani hapa ni kabla ya ukuta kujengwa. Mheshimiwa Rais baada ya kuona kwamba kuna wizi mkubwa ukuta ukajengwa kazi hii inafanyika vizuri ukuta umedhibiti uimarisaji wa kodi na ndiyo maana unaona kwenye takwimu ya Wizara baada ya ku-*collect* milioni 700 tu tuna-*collect* sasa *almost two point three billion*. Kwa hiyo hii ni kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya CCM, hilo ni moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile na mimi nishukuru kwa ajili ya ujenzi wa Mererani, ule ukuta umesaidia nchi sana watu wetu wamenufaika, utajili unaongezeka. Hapo awali tulikuwa tunabezwa Mheshimiwa Rais kafanya kitu gani bwana, CCM inafanya kazi gani; lakini niwaambieni kitu kimoja mimi kama Mbunge wa Jimbo linalotokana na *Tanzanite* utajiri wa watu wetu mionganoni mwa watu wetu unaongezeka kwa kiasi kikubwa sana, Serikali imenufaika. Hata hivyo Mheshimiwa anajua changamoto mbili tatu ambazo nitazitaja, muda hautoshi.

Mheshimiwa Spika, pale kuna milolongo mikubwa sana, Mheshimiwa Waziri unakumbuka mwezi wa nne tulikuwa wote na Katibu Mkuu, naomba msaidie kuwepo na wafanyakazi wa kuongezeka pale ili ile milolongo ya watanzania waliokuwa tayari kulipa kodi basi ipungue. Ninaomba suala la maji, unakumbuka siku ile tuliongelea.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Upinzani kidogo mimi nawashangaa. Ukurasa wa 14 wa hotuba yao ukiona, hawa watu wanasema nchi hii imekuwa shamba la bibi, ukurasa wa 14 ile aya ya kwanza. Lakini baada ya kurasa 13 baadae wanajisahau wanaanza kusema, ukurasa wa 27, Kampuni ya ACACIA iliyomiliki mgodi wa North Mara kunadhibitisha malalamiko ya muda mrefu ya wananchi na kwamba wamepigwa faini kubwa sana Mheshimiwa Waziri na Wizara ya Mazingira. Sasa watu hawa huku mnasema Serikali haya madini yameachwa kama shamba la bibi lakini huku mnaona Serikali inafanya kitu gani, ninyi tuwaamini kwa kitu gani? Niwaambie kwa awamu hii ya Tano, mara ya kwanza Mheshimiwa Rais; na wewe unajua mmesimamia haya madini umeunda Kamati mbili ya *Tanzanite* na *Diamond* unakumbuka umesimamia kwa hiyo awamu hii kipekee kwa kweli ni awamu ya kipekee mmeamua kulinda rasillimali za nchi yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lingine, kuna Kamati iliyochunguza mambo ya *Tanzanite*, kuna madeni ya ajabu ambayo yamelimbikiziwa watu wangu ma-Broker halafu wachimbaji wakubwa na wale ambao wanafanya masuala ya *Tanzanite*.

Kamati hii imeamua kuchukua *almost* miaka kumi iliyopita kuwalipisha watu wangu madeni ambayo hayapo kabisa. Watu hawa wamekuwa ni maskini wengine hawana hata chochote. Mbali na uchunguzi uliofanyika kwenye *Gold*, mbali na uchunguzi uliofanyika kwenye masuala ya *Diamond* wameshikwa watu wa *Tanzanite* peke yake nchi ndiyo wanaosumbuliwa na Kamati fulani ambayo naomba nisiitaje na Mheshimiwa Waziri unajua na malalamiko yangu kama Mbunge nimeshakuambia niombeni mshughulikie kwa sababu uonevu huu haukulaliki hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naunga mkono hoja, ahsante sana.(*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Ezekiel Maige, na mwisho atamalizia Profesa Jumanne Kishimba; Mheshimiwa Maige hayupo?

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi bahati mbaya ukunitaja kabla kidogo nijipange. Naomba kwanza niipongeze sana Serikali na hasa Mheshimiwa Rais kwa mabadiliko makubwa, marekebisho makubwa sana yaliyofanyika kwenye sekta hii. Kama mnavyofahamu Waheshimiwa wenzangu mimi natoka mgodi wa Bulyanghulu; nimekuwa na matatizo na kero nyingi ambazo nimekuwa nikizilalamikia hapa lakini kwa kweli awamu hii tumeona kazi kubwa nampongeza sana Mheshimiwa Rais. Nimpongeze sana pia Mheshimiwa Waziri na Nibu pamoja nawatendaji wote wa Wizara pia mnafanya kazi kubwa kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais, pia kusimamia mifumo mipya ya sheria za madini ambayo inanufaisha sana wananchi hasa wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, nina mambo kama mawili tu ambayo nilitaka kuyazungumzia; kwanza kwa wachimbaji wakubwa. Kama nilivyo sema mgodi wa Bulyanghulu una changamoto zake kwa sasa hivi tunafahamu kwamba walishasimamisha uzalishaji na wanaendelea na mazungumzo na Serikali kuhusu migogoro yao ya kule nyuma.

Sisi kama wananchi wa pale tumekuwa tukisema tuna matatizo yetu ambayo tumekuwa nayo kwa muda mrefu; la kwanza ambalo nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri utusaidie; tumekuwa tukidai *service levy* mapunjo kabla hawajaanza kulipa *zero point three percent*, walikuwa wanalipa dola 200,000 jumla yake ni kama dola milioni 8.6 ambazo ni takriban shilingi bilioni 16. Tulishaomba kupertia Wizara ya TAMISEMI kwa sababu ni suala liko chini ya halamashauri kwamba Waziri Jafo pamoja na Wizara ya Madini mtusaidie kumbana huyu mwekezaji ili haki yetu tuweze kulipwa. Nilikuwa naomba suala hilo lilwe mezani kwako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilitaka vilevile nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, tulishamweleza kuhusu matatizo ya migogo ya wananchi ambayo imekuwepo pale; kubwa zaidi ni fidia mgodi wa Bulyanghulu ulipoanzishwa mwaka 1996 wananchi waliokuwepo pale ni kaya 4,600, waliolipwa ni kaya 34 tu, na hili suala nimekuwa nikilieleza na Wizara inalifahamu. Tunaomba tuendelee kulifuatilia, suala la fidia kwa wananchi wa Bulyanghulu bado halijawa *settled.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni wachimbaji wadogo wadogo, tuna matatizo ya maeneo kule kwetu tulikuwa tulishaunda vikundi kuna kikundi kinaitwa *Kasi Mpya Gold Mining Cooperative Society*, kiliomba leseni eneo la Mwazimba; na kikundi kinaitwa *Bushimangila and Masabi and Segese Gold Mining Cooperative Society (BMS)* waliombwa eneo la Bushimangila, Mheshimiwa Waziri ulifika; walishaomba leseni kwa taratibu zote. Kwa bahati mbaya sana utoaji wa leseni katika maeneo haya umekuwa na matatizo; na Mheshimiwa Waziri ulishaagiza amesema Mheshimiwa Musukuma hapa; katika vita tuliyonayo ya kupambana na ujisadi na rushwa moja ya maeneo ambayo tunayo bado ni kwenye Maafisa wetu wa madini. Afisa Madini Mkaazi wa Kahama, baada ya kuwa umeshaagiza siku mbili baadaye aliondolewa; akaja Afisa Madini mwengine, kazi yake ya kwanza aliyoifanya ni kutoa leseni kwa mtu mwengine ambaye wala hakuwa katika maombi ambayo tulikuwa tumeshakuomba na ulishaelekeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kwa sasa hivi tayari pale kuna mgogoro, kwa sababu kuna leseni ambayo imeshatolewa na ulishaagiza kwamba wale watu wapewe leseni lakini hamna kilichofanyika. Nilikuwa naomba sana, mgogoro wa leseni wa Mwazimba, mgogoro wa leseni wa Bushimangila leo utusaidie angalau kauli itoke kwa sababu kule tunategemea wananchi wangu watafurahi wakisikia kauli yako na msimamo wa mwisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni la kuomba wachimbaji hawa wadogo wadogo ambao wamewezeshwa kwa kiasi kikubwa sana wanamatatizo ya kupata hasara kwa sababu wanachimba kwa kubahatisha sana. Mbinu tunzozitumia sisi za kienyeji hizi za kupiga ramli hazitusaidii kujua mahala ambapo dhahabu ipo. Kwa bahati nzuri maeneo mengi ambayo sasa hivi wanaachiwa ni yale yaliyofanyiwa *exploration* na makampuni makubwa na *data zimetunzwa* na makampuni lakini *copyziko* Wizarani. Tulikuwa tunaomba takwimu hizi ziwe *shared* na hawa wachimbaji wadogo wadogo ambao wanapewa leseni ili waweze kujua *exactly* mashapo yako wapi na waweze kuchimba *with a focus* kuliko huu uchimbaji wa kubahatisha bahatisha; tutaweza kuokoa hasara wanazopata, lakini tutaongeza tija katika shughuli zao. (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, naomba kusema naunga mkono jitihada za Serikali, naunga mkono bajeti hii, ahsante sana kwa nafasi. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige. Sasa Mheshimiwa Kishimba utufungie uchangiaji wetu.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Spika, *yeah*, ahsante sana; na mimi niungane na Wabunge wenzangu

kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na Watendaji wote Idara ya Madini kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, mimi ninayo shida kubwa sana kwenye Mgodi wangu wa Buzwagi. Mgodi huu unaenda kufungwa au kufukiwa; mgodi huu juzi kwenye ziara ya Makamu wa Rais Mheshimiwa Naibu Waziri Nyongo alikuwepo na Mawaziri wengine; Meneja wa mgodi alituhalifu kwamba mgodi ule bado una *balance* ya dhahabu *ounce* audhi milioni moja, ni sawa sawa na kilo 31 za dhahabu. Anachodai Meneja wa mgodi ni kwamba gharama zao za uzalishaji ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, kilo 31 ni sawa sawa na dola bilioni 1,200,000 ambazo ni sawa na triliuni 28. Kinachonishangaza hapa; ni kweli tukubali kwenda kufukia mgodi wenyе dhahabu ya triliuni 28 ilhali sisi tunauwezo wa kufunga mto Rufiji tukapata umeme?

Mheshimiwa Spika, lawama lazima tuitupe tu kwa wataalamu ukweli ni wavivu kwa kufikiri, hauwezi ukaletewa ripoti na mtu mmoja mwenye mgodi akafukia mgodi wako wenyе thamani ya triliuni 28 na wewe unashida ya kujenga *Standard Gouge* wewe uko tayari kuziba mto Rufiji, haiwezekani, ni kitu ambacho kinazunisha sana. Serikali kwenye Sheria yetu mpya ana asilima 16 mle ndani ina maana na Serikali atapoteza na kodi tutapoteza. Lakini alichosema Meneja wa mgodi ni kwamba gharama zao ni kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa mimi niombe kwa Mheshimiwa Waziri au wewe utusaidie. lundwe tume ndogo iende ikaangalie gharama za uzalishaji za mgodi huo; zile ambazo zinaweza kuondolewa ziondolewe. Lakini Serikali upande wake pia ifikirie; maana *TANESCO* anapata bilioni mbili kwa mwezi, *TRA* anapata na yeye zaidi bilioni 20 Idara ya Maji tunapata zaidi ya bilioni nne. Hawa kama wanaweza na wao kupunguza *tariffs* zao wapunguze maana kama mgodi utafungwa hata hizi *tariffs* zao hazitafanya kazi popote. Ikiwezekana wapunguze ili tuunusuru mgodi huu.

Mheshimiwa Waziri tumekuwa tukiongea mara kwa mara lakini bado mimi nawasiwasi kwamba wataalam wetu ni wavivu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili ni suala zima la madini. Utajiri wa Warabu ni mafuta, na Warabu wamepata utajiri wa mafuta pale bei ya mafuta inapopanda. Sisi tunayo dhahabu, wahasibu wetu wanachanganya kati ya hesabu ya kiwanda na hesabu *mining*. Dhahabu haipandi kwa ajili ya gharama ya uzalishaji, dhahabu inapanda kwa hali inayoendelea duniani. Kama kuna hofu au tatizo lolote dhahabu itapanda.

Mheshimiwa Spika, sasa nachojaribu kujuliza hapa; na nafikiri Mheshimiwa Waziri itabidi hapa nishike shilingi ili tupate ufumbuzi. Bei ya dhahabu mwaka 2008 ilikuwa *gram* moja ni dola 40, ambapo ni kama ounce moja dola 800; leo ni dola 60; lakini gharama za uzalishaji hazikupanda, maana *raw material* ya dhahabu ni mawe ambayo ni asilimia 70, kilichoongezeka hapa hakikuongezeka kwa sababu ya gharama ya uzalishaji, kimeongezeka kwa sababu ya *demand* duniani tofauti na kiwanda. Serikali ya Tanzania kama wahasibu au wataalam wetu watakubali, tunakuwa na utajiri mkubwa sana pale bei ya dhahabu inapopanda; ile pesa si pesa ya mweye mgodi wala mwenye mgodi hawezi kuidai, kwa sababu hata dhahabu isipopanda yeye anaendelea na uzalishaji na faida anapata. Warabu wametajirika ni pale bei ya mafuta inapopanda duniani, ile tofauti inatakiwa kuwa yote ni mali ya Serikali siyo mali ya mwenye mgodi. Maana yake hiki ni *reserve* ya ile nchi ndiyo faida yake iko hapo; wataalam naona bado linawapa shida sana suala hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya muda naomba niungane kwenye suala moja na Mheshimiwa Heche. Mheshimiwa Heche amesema, ni kweli ile migodi haijawahi kutulipa *service levy* yetu mpaka sasa hivi. *Service levy* hiyo anayoisema inahitaji ufanuzi kidogo; ni kwamba hizi *mining* zote zilizoko Tanzania zina bima tatu, zina bima ndani ya dhahabu inapokaa, zina bima ya mgodi mzima, zina bima

zinapotaka kwenda kukopa benki maana yake zote zimekopa benki lazima ziweke bima; kwa hiyo zina bima tatu. Bima hizi ni zimeliipiwa Ulaya kweli, lakini kwenye *tariffya TRA* wame-deduct kama *cost*. Kwa hiyo zile pesa tunatakiwa sisi tulipwe *service levy* yetu ambayo ni *zero point three*.

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo hii pesa siyo ya mgodi ni ya yule mtu wa *insurance* ambaye yupo; ni watu wa mgodi tu kutuambia kwamba ni huyu hapa na *invoice* tumpelekee, si mali ya mgodi hata siku moja na hawa watu wa *insurance* hawajawahi kujulishwa mimi ninavyojuua; na watakataa kwa sababu hawajawahi kulipa kitu chochote wana *benefit* wao. Ingetusaidia sana, kama alivyosema Mheshimiwa Heche na Mheshimiwa Musukuma kwamba ni vizuri watusaidie.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Jumanne Kishimba. Nafikiri niliwahi kuwaambieni wakati fulani na mtakubaliana na mimi kwamba Mheshimiwa Kishimba akisimama huwa ni mtu aliyejipanga na ana *a lot of knowledge* ambayo ni *practical* kabisa. Kwa hiyo tunakushukuru sana; na ndiyo maana kwa maksudi kabisa nilimteua awe Mjumbe wa Kamati ya bajeti ili kupeleka maneo haya kule kwenye Kamati ya bajeti na kuweka sawa mambo haya.

Waheshimiwa Wabunge nawashukuruni sana wale Wajumbe sita niliowaombea wote mmepata kuwasikiliza vizuri nawashukuru kwa uvumilivu wenu kwa dakika hizi zilizoongezeka.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia Wizara hii ya Madini kulingana na umuhimu wake kwa vizazi vilivyopo na vijavyo katika kulinda rasilimali zetu za nchi yetu kwa kuzingatia mambo muhimu katika kuhifadhi rasilimali zetu.

Mheshimiwa Spika, Wachimbaji Wadogo. Kumekuwa na malalamiko makubwa kwa wachimbaji wadogo nchini. Nashauri Serikali kubadilisha utaratibu wa kuwatia moyo kwa kutatua changamoto zao kwa wakati kwani nao ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, mikataba inayolalamikiwa ifanyiwe marekebisho. Kumekuwa na malalamiko kuwa kuna baadhi ya mikataba ambayo pia inafanya baadhi ya wawekezaji kuona kwao ni kikwazo kuja kuwekeza nchini. Ninashauri Serikali mikataba hiyo ipitiwe upya.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Madini. Nashauri Serikali itimize wajibu wake kikamilifu kwani Tume hii ikitimiza wajibu wake kwa uhakika na kwa muda mwafaka kutaleta matokeo chanya kiutendaji na pia kulipatia taifa letu mapato kwani wataweza kutatua kero nyingi na baada ya kutatua tutaweka mazingira rafiki kwa wawekezaji wa ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utafiti ya Madini. Tume hizi ni vyema zikawa zinaleta matokeo yanayotokana na tafiti wanazozifanya kwenye maeneo mbalimbali nchini ili wananchi ambao si wataalam lakini wamekuwa wakigundua madini mbalimbali nchini. Ni vyema pia kuwatia moyo wananchi hawa kwenye maeneo mbalimbali hata kwa kuwapa maeneo ili kujua na kutambua michango yao.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na vifo mbalimbali kwenye maeneo ya uchimbaji kwenye maeneo au machimbo ambayo yamekuwa yakiathiri nguvu kazi ya Taifa. Nashauri Serikali kufuatilia kwa ukaribu mambo yanayopelekea vifo vya kila wakati kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, kutoa elimu maeneo yanayopatikana na uchimbaji wa madini. Kuna maeneo mengi ambayo wananchi wanaozunguka migodi. Serikali itoe elimu kwa wananchi juu ya athari ambazo wanaweza kupata kutokana na vifaa au sumu zinazoweza kutumika katika uchimbaji wa madini kwenye maeneo ambayo yanachimbwa popote nchini.

Mheshimiwa Spika, Soko la Madini. Nashauri Serikali itumie Umoja wetu wa Afrika Mashariki kama fursa kwa kufanya tafiti la soko kulingana na aina ya madini tuliyonayo nchini kwetu ili kuwasaidia wachimbaji wetu na kulisaidia taifa kwa ujumla. Hii itawanufaisha wananchi wanaozunguka maeneo yote ya uchimbaji madini nchini.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Wizara hii kwenye maeneo makuu mawili; mosi, ulipaji wa fidia kwa wakati na kwa wananchi wote waliopo kwenye maeneo yaliyochukuliwana na Mgodi wa *Acacia North Mara*. Maana kuna baadhi ya nyumba hazijafanyiwa tathmini kabisa na yapo maeneo ya operesheni za mgodi. Hivyo, Waziri anapokuja kuhitimisha atueleze hatua zilizochukuliwa kwa hizi familia na lini wanalipwa sanjari na wengine wanaosubiri malipo tangu mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya hizo familia zilizopatwa na madhara kutoptana na operesheni kama vile vumbi, mishtuko wakati wa *blasting*, kubomoka kwa nyumba; mfano ni Simon Mikulabe, Max, Ibrahim, Max, Prisca Chacha, Chacha Ihande, Abel Max, Mwita *Tall*, Amos Atendo, Mwita Nyamhanga, Chacha *Tall*/John, Mwikabe Bina, Amos Atendo Nyankobe, Mhere Wagi na wengine.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi waliachwa kwenye zoezi la uthamini No. 20 ndani ya *buffer zone* kwa sababu mbalimbali kama vile kutokuwepo wakati wa tathmini (safarini), wengine walikuwa gerezani. Raia hawa wameshafika mgodini na kuongea na uongozi wa mgodi juu ya uthamini. Hata hivyo mgodi wanasema Serikali inasitisha uthamini hadi itakapotoa kibali tena. Tunaomba kauli ya Serikali juu ya hatua ya hizi familia zilizopo ndani ya *buffer zone*.

Mheshimiwa Spika, vilevile ninataka kujua, katika ile faini waliyotozwa *Acacia* dhidi ya uchafuzi wa mazingira Wananyamongo wanafaidika vipi kwa kupewa fidia hasa wale walioathirika na uchafuzi wa mazingira?

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu Mgodi wa Kabanga ulioko katika Mji wa Tarime ambao wachimbaji wadogowadogo wamekuwa wakipata matatizo mengi kwa kunyanyaswa na watu wenye fedha (kama Mzungu) na hata wengine kupelekwa gerezani wakati wanachimba kwenye maeneo yao halali.

Mheshimiwa Spika, hili jambo nilishalifikisha Wizarani kipindi Mheshimiwa Kairuki akiwa Waziri na hata kwa Kamishna wa Madini wa Kanda yetu na mkoani wanajua. Hili eneo la Kabanga inasemekana leseni ni ya Barrick, kwa muda mrefu tumeomba iweze kufutwa na leseni zipewe kwa wachimbaji wadogowadogo ili wafanye uchimbaji wao kwa uhuru zaidi bila kubugudhiwa. Pale kuna wajane wananyanyasika sana. Pale kuna mkandarasi tu ndiye ana leseni na hiyo ya Barrick. Wanakabanga tunapenda kujua kama leseni ya Barrick imeshafutwa ama bado na kama imefutwa kwa nini leseni hawajagaiwa wale wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, pili, mkishawapa leseni watakuwa wmaepata sifa ya kupewa ruzuku ili wajie ndeleze kwenye Sekta ya Uchimbaji na kufaidika na rasilimali zilizopo kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha.

MHE. LUCIA U. M. MLLOWE: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo; Mradi wa chuma wa Mchuchuma na Liganga. Nasikitika kwamba mradi wa Mchuchuma na Liganga uko kimia. Hata katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri haujatajwa. Mradi wa Mchuchuma na Liganga ungefani kiwa ungekuwa na manufaa makubwa sana. Kwanza ungewasaidia wananchi wa Mkoa wa Njombe kupata ajira pia pamoja na kuuza mazao yao. pia ingesaidia Serikali kuijingizia kipato chake. Lakini pia ingepnguza ghamama kwa Serikali kununua chuma nje na badala yake chuma hicho kingesaidia hata ujenzi wa reli inayojengwa (*Standard Gorge Railway*). Naomba Mheshimiwa Waziri

atakapohitimisha hoja yake alieleze Bunge ni kwa nini Mradi huo unasuasua?

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wana changangamoto nyingi. Moja ya changamoto hizo ni kutokuwa na elimu ya kutosha juu ya namna ya kuwa na bima ambayo angewasaidia wanapopata majanga kama vile kufukiwa na kifusi; hivyo kwa kuwa hawana bima wakipata majanga familia zao zinabaki katika hali ya umasikini. Naiomba Serikali itoe elimu kwa wachimbaji hao ili kila mchimbaji awe na bima.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Spika, na mimi nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibau Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara. Leo mimi nitajikita kuzungumzia *minerals (industries)*. Madini ya viwandani kama *gypsum*, *lime stone*, *coltan* na *kadhalika*. Madini ya viwandani yana soko zuri nje ya nchi hasa Afrika Mashariki. Kwa mfano limestone unaweza kusafirisha kwa kuiponda kuwa kokoto au ambayo imekuwa *processes* au wengine wanachoma zile kokoto na kusafirisha kwenye viloba.

Mheshimiwa Spika, tatizo ambalo wachimbaji wangine wanapata hasa wachimbaji wadogo ni pale wanapohitaji vibali vya kusafirisha madini ya viwandani inawawia vigumu. Kwa mfano wachimbaji wa Kigoma, Katavi na Rukwa, ili wapate vibali lazima wasafiri kuja Dodoma na inaweza kuchukua hata miezi 6 hadi mwaka bila kupata kibali.

Mheshimiwa Spika, natambua Serikali inapenda madini haya ya viwandani yauzwe hapa hapa nchini, lakini tatizo ni bei. Kwa mfano kokoto za limestone zinanunuliwa na wenye viwanda vya saruji na wanalipa 25,000 hadi 35,000 kwa tani ilhali ukipeleka nje ya nchi, kwa mfano Burundi na Rwanda unalipwa USD 150 *per tone*. Sasa unaweza kuona ni jinsi gani wafanyabiashara wakubwa wa viwanda wanavyowalilia

wafanyabiashara wadogo. Tunaomba Wizara iweke kanda za kutoa vibali vyta kusafirisha madini ili kurahisisha wafanyabiashara wa madini ya viwandani wasafirishe kwa wakati

Mheshimiwa Spika, la pili ni kuhusu uingizaji wa vifaa vyta viwandani kama *crusher machines, Grinding machines, processing machines etc.* Tunaomba Serikali itoe *exemption* ili wachimbaji wadogo waweze kuingiza mashine hizi na kuchimba kwa kisasa zaidi kuliko ilivyo sasa, ambapo wanagonga mawe ili yawe kokoto ndipo wapange kumi kwa ajili ya kuchoma. Mkitoa vibali vyta kuingiza hizi mashine utapunguza wachimbaji wadogo kuharibu mazingira kwa kukata miti.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kuhusu suala la *grants* najua kuna mikopo ya wachimbaji wadogo niombe Wizara iangalie na wachimbaji wa Kigoma kwani Jimbo langu lina wachimbaji wengi wa chokaa. Kwa leo mchango wangu ni huo.

Mheshimiwa Spika, mwisho niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri Doto Biteko na Naibu wake Mheshimiwa Nyongo kwa kazi kubwa wanayoifanya kwenye Wizara hii naunga mkono hoja.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru kwa fursa hii, sambamba na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa wasilisho zuri asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais John Pombe Joseph Magufuli kwa uamuzi wake wa busara wa kujenga ukuta wa Mererani; na matunda ya kazi hiyo tumeanza kuyaona kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 13 na 14. Kwa mujibu wa hotuba hii mapato yameongezeka kutoka milioni 71,861,970 mwaka 2016 mpaka kufikia shilingi 1,436,427,228. Haya ni mafanikio makubbwa sana na ya kuendelezwa ili taifa liendelee kunufaika na rasilimali zake.

Mheshimiwa Spika, kama hotuba ya Mheshimiwa ilivyoonyesha ukurasa wa 15 na 16 kuhusu mkakati wa kuongeza thamani ya madini yetu kwa kualika kampuni tisa zenye nia ya kujenga viwanda vyta uongezaji wa thamani ya madini ni jambo jema. Niombe Wizara iharakishe mchakato huu wenye manufaa makubwa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Matumizi Holela ya Baruti za Kulipulia Miamba. Suala hili limekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wanaoishi maeneo jirani na migodi mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usio na shaka matumizi haya ya baruti yameleta madhara ya kiafya. Ushauri wangu ni kuwa wananchi wanaoishi jirani na machimbo haya walipwe fidia stahiki na wahame, wakaishi maeneo ya mbali na machimbo.

Mheshimiwa Spika, jambo linguine ni kwamba baruti hizi zimekuwa zikitumika nje ya matumizi ya migodi, hususan kwenye uvuvi haramu, jambo hili liangaliwe na udhibiti ufanyike.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme; umeme wa *REA* katika Wilaya ya Rungwe, hasa *REA phase III* haijafanya maeneo mengine na hasa vijijiini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mgodi wa Kiwira. Ni lini mgodi huu utaendeshwa kwa faida ya nchi na Wanambeya? Kumbuka uliajiri vijana wengi hasa wanawake wa Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za *ACACIA*. Ni lini tunalipwa wananchi sawa na ahadi ya Waziri husika? Maana wananchi wa Mbeya tunasubiri gawio.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii mbele yetu. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Biteko, Naibu Waziri, Mheshimiwa Haroon Nyongo (Mb), Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri na kubwa wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina madini, vito na rasilimali nyingi za madini ya thamani na yasiyo na thamani lakini kwa umasikini uliopo hata maeneo yanayotoka madini au rasilimali hizi haziakisi utajiri huo. Hii inatokana zaidi na utekelezaji wa sheria na kanuni zetu katika kuwezesha mali hii kulisaidia taifa. Hatuna rafiki wa wazalishaji wa sekta hii kwa jinsi tunavyowanyanya kwa lugha, vitisho, kodi na tozo.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Makaa ya Mawe Kiwira na Kabulo. Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira umesima kwa zaidi ya miaka tisa sasa. Mwaka 2018 uchimbaji ulianza kidogo katika mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kabulo; tangu wakati huo hatujapata taarifa yoyote mpya ya mendeleo ya migodi hii miwili. Hotuba ya Waziri wa Madini ukurasa wa 53 una-report kuwa *STAMICO* wamechimba tani 22,119 za makaa ya mawe na kuuza tani 7,664.8 tu.

Mheshimiwa Spika, lakini taarifa hii ni ileile tuliyopewa kwenye hotuba mwaka jana. Ina maana hatuna maendeleo yoyote yaliyofanyika tangu Aprili, 2018? Serikali itufahamishe ina mpango gani wa kufufua mgodi wa Kiwira na kuendeleza mgodi wa Kabulo. Tangu mgodi wa Kiwira usitishe chini ya *Tanpower Resources Company Limited* kumekuwa na sintofahamu ya nani muhusika mkuu wa mgodi huu baada ya kuondolewa kwa muwekezaji huyu aliyekabidhiwa mgodi tangu mwaka 2005; walipewa silimia 70 ya hisa na Serikali kubaki na silimia 30.

Mheshimiwa Spika, tangu mgodi kurudishwa Serikalini mwaka 2009, NSSF waliliipa madeni ya mgodi shilingi bilioni 28.72, Benki ya CRDB nayo ina deni, *PPF*, *NSSF* wanaudai mgodi Dola milioni saba. NSSF ilitaka kuchukua mgodi huo na kuuendesha na kulipa madeni yote. Hii ingwezekana kwa sababu mgodi una mali nyingi zaidi ya madeni.

Mheshimiwa Spika, mgodi wa Kiwira ulilenga kutumia Makaa ya Mawe kuzalisha umeme na kuuza *TANESCO*. Mgodi huu ulikuwa unatoa ajira 7000 kwa wananchi wa lleje kwa uchache lakini kwa kiasi kikuba na Kyela na Rungwe. Mgodi ulikuwa unawezesha Halmashauri kupata mapato na vilevile kuchangamsha uchumi kupitia biashara na ajira zinazounganisha watoa huduma kwenye mgodi. Vilevile kwa familia za watumishi wa mgodi wanaonufaika na mgodi. Sasa hivi kusimama kwa mgodi huu kumezorotesha uchumi wa lleje na wilaya za jirani kwa zaidi ya miaka tisa sasa na hivyo ni athari hasi sana kwa wilaya yenye rasilimali muhimu na kubwa kama mgodi huu wa makaa ya mawe.

Mheshimiwa Spika, aidha, huu mgodi huzalisha umeme; hii pia imeleta athari kwasababu maeneo haya yamekosa hii *connection*. Katika bajeti ya Wizara ya TAMISEMI illitengwa bajeti ya kujenga daraja kwenye Mto Mwalisi linalouanganisha mgodi wa Kiwira na lleje. Je, hiyo fedha itatolewa lini ili kurahisisha usafirishaji wa makaa ya mawe?

Mheshimiwa Spika, Wana lleje tunaomba sana Mgodi wa Kiwira na wenyewe uanze kazi; na vilevile na ule wa Kabulo uendelee kwa kasi zaidi kwa kutafuta masoko zaidi kwa mwe yanayochimbwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, napongeza juhudzi za Serikali kurekebisha sekta ya madini. Naunga mkono juhudzi hizo na mipango ya Serikali kupitia bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali irekebishe na kusaidia wachimbaji kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, urasimu na mazingira ya rushwa katika utoaji wa leseni za uchimbaji; wachimbaji wadogo wa Msalala kupitia vikundi vyao vya *KAGOMCO (Kasi Mya Gold Mining Cooperative Society)* na *BMS (Bushimangila, Masabi na Segese Coperative Society)* waliomba leseni maeneo ya

Mwazimba na Bushimangila. Mheshimiwa Waziri Biteko alikuja Msalala na kuwahakikishia kuwa watapata leseni.

Mheshimiwa Spika, akiwa Bushamangila aliagiza hivyo, cha ajabu baada ya muda mfupi Afisa Madini Mkazi wa Kahama alihamishwa, afisa madini aliyeletwa alitoa leseni kwa mtu mwingine siku moja tu baada ya kufika Kahama, kinyume kabisa na maagizo ya Waziri; hiyo siyo rushwa? Naomba afisa huyo aliyetoa leseni Bushimangila kwa kampuni tofauti na *BMS* katika mazingira hayo ya rushwa achukuliwe hatua na leseni zitolewe kwa *BMS*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *KAGOMCO* waliomba leseni Mwagimba tangi 2008 na leseni yao kuingia kwenye mgogoro, naomba mno wapewe leseni yao kama Waziri, Mheshimiwa Biteko alivyoagiza.

Mheshimiwa Spika, kusiadia wachimbaji wadogo kupata *exploration data* za maeneo wanayofanyia kazi ili kupunguza hasara kwani maeneo mengi yalishafanyiwa *exploration* na *GST*na Sekta Binafsi na data hizo Serikali inazo au inaweza kuzipata.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Msalala tunadai *Acacia* ushuru wa huduma miaka toka 2000 hadi 2014. Jumla ya madai ni dola 8,500, sawa na shilingi 16 bn. Naomba Wizara ya Madini kwa kushirikiana na *TAMISEMI* isaidie halmashauri yetu ilipwe haki yake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri kwa Mheshimiwa Waziri, moja; ufunguzi wa masoko ya madini katika maeneo imejikita zaidi kufanya uzinduzi huu katika kila mkoa ambao kuna uchimbaji wa madini. Uzinduzi huu wa masoko ya madini uendane sambamba na utaratibu mzuri wenye kukidhi vigezo vyote vya usalama katika maeneo yote yenye machimbo husika nchini. Kwani maeneo mengi hayana wasimamizi au watumishi wa madini na askari ili

kulinda madini hayo kwa ajili ya wachimbaji wengi kutokuwa waaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, utoaji wa elimu kwa wachimbaji mbalimbali juu ya umuhimu wa kutumia masoko ya madini yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, tozo za madini; watendaji wa mamlaka za kiserikali wanatoza kodi za tozo zilizofutwa. Inaaminika tozo hizi zote zinafanyika kwa maslahi binafsi ya wakusanya tozo hizo. Tozo hizo zinawalenga wachimbaji wadogo wadogo wa madini wenye uelewa mdogo wa sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na Wizara ya Madini pamoja na Tume ya Madini. Tozo mbalimbali zinazotozwa ni ushuru wa mawe, ushuru wa karasha, ushuru wa duara, ushuru wa mwalo na ushuru wa *compressor*. Tozo zinazotambulika na Serikali ni kama zifuatayo:-

Moja, *royalty*(mrabaha), ada ya ukaguzi (*service and clearance*) na *service levy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati sasa Serikali kusimamia sheria zilizotungwa ili kuwanufaisha pande zote za Sekta hii ya Madini hasa wachimbaji wadogo wadogo kukatwa tozo/kodi kwenye viroba vyaa mchanga au mawe.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuweza kuchangia. Pia, nachukua fursa hii kuwatachia Waislam wote Tanzania na duniani kote mfungo mwema wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Madini Tanzania, madini ni sekta muhimu katika uchumi wa nchi yetu Tanzania na inachangia katika Pato la Taifa kwa kiasi kikubwa hususan tangu imeingia madarakani Serikali ya Awamu ya Tano. Cha kushangaza katika bajeti ya mwaka jana taarifa zinasema fedha ya miradi ya maendeleo iliyopokelewa na Wizara ni chini ya asilimia moja. Hili ni jambo la aibu kwa kuwa sekta hii inaingiza fedha nyingine katika Hazina ya Serikali. Sasa

ikiwa Wizara imeomba Sh.19,620,964,000.00 badala yake, hadi Februari, 2019 Wizara ilipatiwa 100,000,000 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonesha ni jinsi gani Serikali yetu haijawa tayari kuendeleza Sekta ya Madini ukilinganisha na nchi za Botswana, Malawi, South Africa, Rwanda na Burundi ambao tumewazidi kwa rasilimali ya madini tuliyonayo Tanzania. Miongoni mwa nchi nilizozitaja zina aina chache mno ama aina moja tu ya madini. Tanzania tunayo aina mbalimbali zikiwemo, almasi, dhahabu, *tanzanite*, *ruby radolite*, *alexanderlite*, *blue sapphire*, *pink sapphire*, *red sapphire*, *white sapphire*, *red gainet*, *green tomoline*, *green gainet*, *rose acquamarine*, chuma (*iron*) shaba, *uranium*. Aina hizi za madini ni ushahidi tosha kuwa Tanzania yetu ina utajiri wa kutosha na mkubwa katika Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, Serikali ihakikishe Sekta ya Madini inaboreshwu kwa kutoa fedha za miradi ya maendeleo na fedha za matumizi ya kawaida angalau kwa asilimia 80 badala ya kupeleka asilimia 0.5, tuoneshe *seriousness* katika madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wachimbaji wadogo, ni ukweli usiofichika kuwa wachimbaji wadogo ndio chanzo/waanzilishi wa machimbo ya madini ya aina zote hapa Tanzania na maeneo mengine katika nchi mbalimbali. Nchini kwetu Tanzania wachimbaji wadogo wakishagundua madini, Serikali inawaita wavamizi na wanapelekewa Jeshi la Polisi (*FFU*) na kupigiwa, kunyanyaswa na kubambikiwa kesi za uvamizi au uhujumu uchumi, mahali pengine wachimbaji wanapigwa risasi na kufa ama kujeruhiwa. Mfano, ni maeneo ya Kalalani, Korogwe, Tanga; Dalini, Korogwe, Tanga; Ngombeni, Korogwe, Tanga; Mwakijembe, Mkinga; Kigwase, Mkinga na Uimba *River* Mkinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya Serikali kuwaita wachimbaji wadogo, wavamizi, wangepatiwa elimu ya kutosha mitaji ya mitambo ya kuchimbia kama *iggers* na

excavators, pamoja na kuwawezesha kupata mikopo ya masharti nafuu kutoka katika taasisi zetu za fedha.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Spika, masuala nyeti ya uwazi kwenye tasnia ya uziduaji yanayohitaji majibu ya Serikali; mchango wangu wa hotuba hii ya Wizara ya Madini mimi ni mdaa wa madini natoka katika maeneo yenye machimbo, hivyo mchango wangu unajikita katika hatua kadhaa zinazochukuliwa katika utekelezaji wa Sheria ya Uwazi katika Tasnia ya Uziduaji ya mwaka 2015. Uwazi unasaidia kuzuia makandokando ya rushwa, matumizi mabaya ya madaraka, utakatishaji wa fedha haramu na utoroshwaji haramu wa fedha kutoka kwenye Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi. Hivyo, nitazungumzia mambo manne muhimu kuhusu uwazi katika tasnia ya uziduaji (madini, mafuta na gesi asilia).

Mheshimiwa Spika, nitaeleza athari za uwazi kuhusu kampuni 23 za uziduaji kutoorodheshwa katika Soko la Hisa Dar-es-Salaam. Katika mchango wangu nitaomba Serikali ituambie hatua za utekelezaji wa kanuni za mwaka 2019 zilizotungwa ili kuweka wazi majina ya watu watatu ambao ni wanufaika wa umiliki wa makampuni ya uziduaji.

Mheshimiwa Spika, nitawataja wanasiasa na wenye maslahi yenye kutia shaka katika kampuni za uziduaji (*political exposed personalities*). Sheria hizi za makampuni zinaiweka Tanzania katika nchi zilizo hatarini kutumiwa na wahuni kuficha mali za wizi kwenye tasnia ya madini, mafuta na gesi.

Mheshimiwa Spika, Kampuni 23 za Uziduaji Kutoorodheshwa katika Soko la Hisa Dar-es-Salaam. Kati ya kampuni 54 za tasnia ya uziduaji ni kampuni nne tu ndio zilizoorodheshwa katika soko la hisa la Dar-es-Salaam (*Dar es Salaam Stock Exchange*). *Establishment Maurel et Prom Swala Oil & Gas (Tanzania) Public Limited Company. The Tanzania Cement Company Limited* na *TOL Gases Limited*.

Mheshimiwa Spika, kampuni 23 za uziduaji kutoorodheshwa soko la hisa. Kampuni 23 kati ya 54 ni

kampuni zinazomilikiwa na umma huku kampuni zao kuu zikiwa zimesajiliwa nchi za Canada, Kenya, Norway, *South Africa* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia leo kwenye soko la hisa (Dar es Salaam) ni kampuni 28 za sekta mbalimbali zinazouza hisa zake katika soko hilo huku Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi zikiwa kampuni nne pekee. Endapo kampuni hizi za gesi na madini zikiorodheshwa katika Soko la Hisa Dar es Salaam fursa ya uwazi itafunguliwa kutokana na kanuni za uendeshaji wa soko hilo zilivyo, wamiliki halisi wa kampuni watakuwa wazi hivyo kuondoa dhana ya rushwa, matumizi mabaya ya madaraka na utakatishaji wa fedha haramu.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri akija hapa kuhitimisha hoja yake aseme ni kwa nini wasilet marekebisho ya Sheria ya Uwazi katika Tasnia ya Uziduaji ili kiwepo kipengele kinachowalazimisha kampuni zote za uziduaji kuorodheshwa katika Soko la Hisa Dar-es-Salaam. Waziri Biteko alitunga sheria Februari, 2019 kuhusu uwazi na uwajibikaji kwenye tasnia ya uziduaji, hivyo zielekezwe.

Mheshimiwa Spika, tungeweza kuwabaini hawa wanasiasa na watumishi wenyе maslahi katika madini, lakini tunashindwa kubaini kwa sababu Sheria ya Maadili inazuia kuweka wazi. Hapa hakuna uwazi. Majibu nahitaji?

Mheshimiwa Spika, Waziri akija hapa kuhitimisha aseme ni kwa nini Serikali isilete sheria ya makampuni au sheria ya uwazi katika tasnia ya uziduaji, ili kuzuia uhuni.

MHE. SONIA J. MAGOGO: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri na jitihada kubwa tunazoziona katika kuiendeleza hii tasnia. Pamoja na pongezi hizi niombe Wizara izingatie sana changamoto zinazowakabili hasa wachimbaji wadogo. Mojawapo ikiwa ni ufahamu mdogo wa Sera ya Madini inayopelekea kushindwa kukuza shughuli zao na wengi kuishia kupata hasara.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la mitaji; wachimbaji hawa wadogo hasa wanawake wapewe mitaji hata mikopo toka katika mabenki kwa kutumia leseni zao na hata madini ambayo wanayo.

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto nyingine ya masoko ya uhakika kwa madini yanyopatikana wengi hawajui *exactly* masoko watapata wapi na hata bei zinazoendana na ile wanachokipata hivyo kupelekea kuuza bidhaa zao chini ya bei. Wachimbaji hawa wangepewa elimujuu ya madini mbalimbali na hata dalili za kuwa sehemu fulani kuna madini ya aina fulani ili kupunguza tatizo la kuhama hama linalochangia kuleta hasara.

Mheshimiwa Spika, pia manyanyaso dhidi ya wachimbaji hasa wadogo wadogo yadhibitiwe ili kuwajengea mazingira mazuri ya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. ZAINAB M. AMIR: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya katika Wizara hii kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ifuatavyo:-

Kwanza, fedha zinazotengwa katika bajeti zitolewe kwa wakati ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kwa wakati.

Pili, itoe elimu ya kutosha hususani kwa wachimbaji wadogo wadogo jinsi ya utunzaji wa mazingira ukizingatia wakati wachimbaji madini huacha mashimo makubwa ambayo huharibu mazingira yetu. Elimu itolewe ili baada ya kuchimba wayafukie mashimo hayo.

Tatu, iwapatie wachimbaji wadogo wadogo zana/vifaa vya kufanyia shughuli zao za uchimbaji ili waweze

kupata madini kwa urahisi pia kuweza kupata mapato kwa Taifa.

Nne, iandae vifaa vyta uokoaji vyta kutosha katika migodi yetu ili pindi zikitokea ajali za kufukiwa wachimbaji ndani ya migodi iwe rahisi kuwaokoa.

Tano, ili kukuza soko la ndani la madini kwa kuvutia wawekezaji, Serikali iendelee kuwatafutia wachimbaji wadogo masoko ya uhakika ili kuuza madini yao ndani ya nchi na kuepusha utoroshwaji wa madini nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, namwomba Mungu ampe afya njema na umri mrefu Mheshimiwa Waziri wa Madini pamoja na Naibu Waziri ili kuweza kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

MHE. NURU A. BAFADHILI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na afya aliyonipa. Napenda kuipongeza Wizara kwa kufungua maduka mbalimbali ya kuuza madini.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha ufunguzi wa maduka haya kitasaidia kapatikana madini yetu kwa wingi badala ya madini yetu kusafirishwa kwa njia za panya kwenda nje. Vilevile ufunguzi wa maduka haya utawasaidia wachimbaji wadogo kuweza kuuza madini yao na kupata fedha katika njia za usalama badala ya hapo awali baadhi walikuwa wanadhulumiwa haki zao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wachimbaji wadogo wadogo, wahamasishwe kuwa na vifaa vyta uchimbaji siyo wachimbe kiholela. Wachimbaji hawa wadogo wahamasishwe kuuza madini yao katika masoko yaliyoanzishwa ili kuepuka kudhulumiwa haki zao. Serikali ihakikishe wenye maduka ya kuuza vitu vyta dhahabu (sonara) wasichanganye madini wakati wanapotengeneza vitu hivyo mfano pete, vipuli (hereni), mikufu, vikuku na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja na kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote kwa kazi nzuri zinazoonekana kufanyika.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua hatma ya maeneo ya Jimbo langu ambalo kuna dhahabu. Eneo hilo lipo Sakale, Amani na Mheshimiwa Waziri amefika eneo hilo na kuzungumza na wananchi. Nakushukuru ulituma wataalam wa sekta zote ambazo walifika eneo hilo, lakini bado hawajatoa taarifa yao. Namhakikishia Mheshimiwa Waziri pamoja na madini hayo kuwa karibu na chanzo cha maji ya Mto Zigi, lakini naamini tunaweza kukubaliana njia bora na ya kisasa kuweza kuchimba utajiri huo kitaalam. Naomba alipe umuhimu suala hili ambalo linanipa tabu sana Jimboni.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Spika, nipende kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nishauri Serikali kushughulikia miradi ambayo ikitekelezwa inachangia pato kubwa kwa Taifa na kwa uchumi wa mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kujizatiti kwenye Mchuchuma na Liganga mahali ambapo tungakuza uchumi wa nchi wa urahisi kuliko miradi ambayo yenye we inakuwa mlaji na si mtoa faida ya haraka na haitengenezi ajira kwa wananchi wengi kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Ludewa, mahali ambapo kuna Liganga na Mchuchuma wamechoka kusikia maelezo hayo hayo huku uwekezaji ukiwa sifuri. Waziri anapokuja kuhitimisha aje atueleze Serikali imekwama wapi kwenye Mradi wa Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuishauri Serikali kufuatilia migodi inayofungwa na kuacha mashimo makubwa yakiwa wazi na yamekuwa hatari kwa jamii

yanapojaa maji. Nishauri Serikali kuhakikisha kuwa kabla migodi hajifungwa wanatakiwa kuhakikisha Mikataba yao inasomeka kutokufunga mpaka mashimo yote yamefunkwa.

Mheshimiwa Spika, ningependa kushauri Serikali kuhakikisha inapiga marufuku Wawekezaji wakubwa kuwakandamiza wachimbaji wadogo pale wanapogundua mahali kuna madini.

Mheshimiwa Spika, niishauri Serikali kuhakikisha wachimbaji wanakuwa na bima za maisha kwani wengi wamekuwa wakipata madhila kwa wachimbaji ambapo huishia kufa na kuacha familia ikiwa haina walezi.

Mheshimiwa Spika, nishauri Wizara kuangalia jinsi uchimbaji wa mchanga pia unaacha mashimo makubwa na kuharibu mazingira.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Spika, kwanza natoa shukrani zangu kwake kwa kunipatia fursa hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuandika na hatimaye kuiwakilisha kwa ufasaha wa hali ya juu. Katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mchango wa Sekta ya Madini kwenye pato la Taifa; napenda kuipongeza Serikali pamoja na Wizara kwa kuweka mikakati mizuri katika Sekta ya Madini. Sekta hii ni mionganini mwa sekta muhimu sana katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu katika suala hili, ni kwamba Serikali iendelee kuweka mikakati ya kuimarishe sekta hii ili kuweza kuongeza pato la Taifa, ni vyema Wizara ikaweka wafanyakazi waaminifu katika sekta hii ambao watasisimamia vyema mapato kwa uhakika na kwa uaminifu mkubwa. Mikakati hii iwe ya uhakika na kitaalam zaidi.

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa uchimbaji mdogo wa madini, naipongeza Wizara kwa kuendeleza jambo hili katika maeneo husika. Hii ni sehemu moja kubwa ambayo itaweza kuongeza ajira kwa wananchi wa maeneo husika na kuweza kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu katika suala hili ni kwamba Wizara iendelee kuwasahihisha wananchi kwa kuwapa elimu na vitendea kazi vya kisasa ili waweze kumudu kazi zao na kuleta ufanisi zaidi. Aidha, Wizara iendelee kuwashirikisha wananchi wa maeneo husika kwenye sekta hii ili na wao wajihisi kama ni sehemu ya kuchochea maendeleo katika sekta hii. Wizara itakapowashirikisha kikamilifu wataweza kulinda na kuithamini sekta hii muhimu katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. YOSEPHER F. KOMBA: Mheshimiwa Spika, machimbo ya dhahabu ya Amani yapo maeneo katika Tarafa ya Amani, Wilayani Muheza ambapo wananchi wa kawaida wamegundua madini katika eneo lile. Ni kwa bahati mbaya sana baada ya kuanza kuchimba Serikali kupitia Halmashauri walisitisha uchimbaji, kukamata watu na kuwaumiza. Mpaka sasa hakuna utaratibu wowote ulioandaliwa kwa wananchi wanaozunguka mradi/mgodi ule. Je Wizara iko tayari kuweka utaratibu mzuri kwa wachimbaji wadogo ili waweze kujipatia kipato? Pia Wizara wana utaratibu gani wa kuwapa mtaji wachimbaji wadogo ili waweze kujikwamua?

Mheshimiwa Spika, *Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative* Taasisi hii imepewa jukumu kubwa la kusimamia uwazi na uwajibikaji, lakini kwa bahati mbaya haipati fedha za kutosha kufanya shughuli zake. Napenda kufahamu ni kwa nini *Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative* haipati fedha zilizotengwa kwa wakati na kwa ukamilifu. Je Kanuni zinazoongoza utendaji wa *TEITI* zimeshatoka na zimeanza kutumika?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Naomba basi kwa uvumilivu huo huo saa kumi Kamili jioni turudi mapema ili sasa Mheshimiwa Naibu Waziri anze Mheshimiwa Waziri tuweze kuhitimisha hoja yetu kwa wakati. Sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi Saa Kumi Kamili ya leo.

(Saa 7:00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10:00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae.

Tunaendelea, sasa tutaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara dakika tano, atafuata Mwanasheria Mkuu wa Serikali halafu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kumshukuru Mungu kwa siku hii ya leo, lakini vilevile nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Madini pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri ambayo wamefanya na hivyo kuifanya Tanzania kufaidika na madini kama ambavyo imekuwa ikitarajiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika maeneo machache kama ifuatavyo na ikizingatiwa kuwa hayo maeneo pia yanahu suala la Mgodi wa *TANCOL*; ni kweli katika maneno ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge kwamba Tanzania tunawekeza na tunawaleta wawekezaji kwa lengo la kuhakikisha kwamba kunakuwa na tija na mafanikio ya kifedha, lakini vilevile mafanikio mapana katika uwekezaji unaofanyika. Katika mradi wa *TANCOL*, mafanikio tuliyoyapata ni kwamba mpaka sasa makaa ya mawe ambayo yanatumika katika viwanda vyetu hususan vya *cement* yote yanatoka Tanzania na

mengine tumekuwa tukiwa hata nje ya nchi, kwa hiyo yameleta faida katika kuwezesha kupata malighafi katika viwanda vyetu vya *cement*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, nikiri tu kwamba taarifa ambayo ilikuwa inazungumzwa ambayo imetokana na taarifa ya *CAG*, sisi kama Wizara tunayo na hatujaifumbia macho. Tayari tulishaunda Kamati ya kufuatilia namna gani tunatekeleza maoni ya *CAG* na kupata ni namna gani au kwa kiasi gani yashughulikiwe. Kwa hiyo, kuna mambo ambayo yanatakiwa yashughulikiwe katika mpango wa muda mfupi lakini mengine yalikuwa yanahitaji tafakari pana zaidi kwa muda mrefu. Suala hilo lipo katika mikono salama na niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge pale tutakapokuwa tumekamilisha hayo tunayoyafuatilia watapata taarifa ambayo inakusudiwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile niseme tu kwamba, wao wenyewe *TANCOL* pamoja na kampuni zile ambazo walikuwa wanazitumia katika kuwezesha kutoa huduma wamekuwa na migogoro. Kwa mfano, katika Kampuni ya *Caspian* walipelekana mpaka mahakamani lakini wakaamua kufanya makubaliano nje ya mahakama na hivyo wakakubaliana kulipa zaidi ya shilingi millioni nane kwa ajili ya hayo makubaliano yao na hasa katika lengo la kuvunja mkatuba wa kuendelea kuchukua huduma kwa hao *Caspian*. Kwa hiyo hayo ni mambo tu ambayo yalikuwa yanajitokeza katika migogoro iliyokuwa inaendelea. Niwahakikishie tu Wabunge kwamba kwa hali iliyopo sasa kwa Serikali hii ya Awamu ya Tano hatutakubali uwekezaji wowote usio na tija na hivi wote tunaangalia Taifa letu katika mtazamo huo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mchuchuma na Liganga ni kwamba kweli huyo mwekezaji alipatikana na makubaliano ya awali yalikuwepo na hata kwa upande wa nchi kama Serikali tayari tulianza hata kuwekeza katika miundombinu kama ya barabara ili kuwezesha mradi huo uweze kuanza, lakini kama ambavyo nimezungumza na sheria ambazo tulikuwa tumetunga za kusaidia nchi inufaikie

zaidi na rasilimali zake, tulikuja kuangalia na tukaona kwamba katika baadhi ya taarifa ambazo mwekezaji alikuwa amezitoa hasa kuhusiana na madini zilizokuwepo zinaonekana haziendani na uhalisia kulingana na taarifa zingine tulizozipata kupitia utafiti wetu wa *source* nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo, vilevile hata katika upande wa kuchukua mikopo, mwekezaji alizungumza kwamba ili apate mikopo kwa kupitia dhamana ya mashapo yaliyopo, sasa kama ndivyo yeye amekuja na nini? Kama dhamana inatokana bado na rasilimali ile ile ambayo tunayo sisi wenyewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna mambo ambayo inabidi tuendelee kuongea na mwekezaji, tuweze kutafakari kama tutakuwa tumekubaliana basi ataendelea na kazi, lakini kama tutakuwa hatujakubaliana na pale Serikali inapoona kwamba hapa hakuna tija ya huo uwekezaji, basi sisi tuwaambie tu kwamba hatutakubali kuendelea nae kwa sababu msiiimamo wa nchi utabakia vilevile kwamba kila uwekezaji lazima uwe na tija na manufaa mapana ya wananchi lakini pia na upande wa muwekezaji kuwe na *win win situation*. Kwa hiyo, hiyo ndiyo hali halisi na sisi hatutakubali kuja kuwajibika hapa kwa sababu eti tuliwekeza tu kwa ajili ya kuwafurahisha watu. Lazima tujipange kwa kupata ufumbuzi wenyewe tija.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, *Engineer Stella Manyanya*. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali dakika tano pia.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye hoja iliyoko mezani. Mchango wangu nitajielekeza zaidi hasa katika kutoa ufanuzi kwenye mojawapo ya masuala yaliyoibuka wakati wa mjadala. Nielezee zaidi *position* ya kisheria iko namna gani na hili ni suala la fidia kwa

walioathiriwa na uchafuzi wa mazingira uliotokea katika mgodi wa *North Mara Gold Mine* unaoendeshwa na Kampuni ya *Acacia* kule Nyamongo.

Mheshimiwa Spika, pendekezo lilitolewa ilikuwa ni kwamba *fine* ile ambayo imetozwa kampuni hii basi ingefaa *fine* hiyo igawanywe kwa wale waathirika wa uchafuzi wa mazingira, lakini basi kama hili haliwezekani, labda itafutwe namna yoyote ya kuwafidia hao walioathirika na uchafuzi wa mazingira uliosababishwa na huo Mgodi wa *North Mara* unaoendeshwa na Kampuni ya *ACACIA*.

Mheshimiwa Spika, katika hilo nataka kusema kwamba kuigawa ile *fine* iliyotozwa kwa waathirika wa mazingira kuna ugumu kidogo kwa sababu hakuna Sheria inayoweza kuruhusu kufanyika jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo lile suala la kuichukua ile *fine* iliyotozwa na *NEMC* halafu kuigawa kwa wale wananchi walioathirika hilo jambo lina ugumu kwa sababu hakuna Sheria inayoruhusu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fidia kwa walioathrika na uchafuzi wa mazingira sheria ipo. Ni hii Sheria inayohusiana na ulinzi wa mazingira (*Environmental Management Act*) na napenda hapa nisome tu kwa haraka hiki kifungu kwa sababu ni kifungu cha 110(1)(3). Kifungu cha 110 cha hii Sheria ya *Environmental Management Act* tukianza na kifungu cha kwanza kinasema:

"No person shall discharge any hazardous substance, chemical oil or mixture containing oil in any waters or any segment of the environment"

Hicho ndiyo kinachoanza kuweka zuio na katazo la uchafuzi na kifungu cha 110(3) kinasema:

"Apart from the general punishment provided for under this Act, the person convicted of an offence under this section may be ordered by the court"

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kifungu kidogo cha 110(3)(b) kinasema:

"To pay the cost of third parties in the form of reparation, restoration, restitution or the compensation as may be determined by the court".

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo katika msimamo wa kisheria kuna uwezekano wa hawa watu walioathiriwa na uchafuzi wa mazingira kulipwa ama *reparation* au *compensation* au kwa namna yoyote itakayowezekana, lakini ni lazima tuangalie kitu kimoja hapo kwamba hii amri inatolewa na Mahakama na kwa sababu hiyo ni lazima pawe pamefunguliwa kesi ya jinai na Mahakama baada ya kupata ile kesi na uthibitisho ukatolewa inaweza kutoa maelekezo ya kulipa fidia.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira tuliyonayo tuna changamoto kidogo, kwa sababu ukienda kifungu cha 194(2) cha Sheria hii hii kinasema, mahali ambapo kosa limekuwa *compounded* kwa ajili ya yule aliyetenda kosa kutoa *fine*, basi kesi ya jinai au kesi nyingine yoyote ya kimahakama haiwezi kuendelea kwa sababu itakuwa ni kama umetoa adhabu mara mbili.

Mheshimiwa Spika, sasa lakini hiyo haiondoi ukweli kwamba suala la fidia kwa watu walioathiriwa na uchafuzi wa mazingira ni la muhimu kuangaliwa. Kwa hiyo pengine labda baada ya hatua hii ya kulipa *fine* labda inaweza ikaangaliwa pia hiyo hatua nyingine hapo baadaye ya kulipeleka shauri hilo Mahakamani ili Mahakama itumie mamlaka yake kutoa maelekezo ya kuwalipa fidia walioathrika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali tunakushukuru sana kwa maelezo hayo. Mheshimiwa Naibu Waziri robo saa.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuhitimisha hoja hii ya Wizara yetu hii ya Madini.

Mheshimiwa Spika, nianze ka kutoa pongezi kubwa kwa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya katika kusimamia Sekta hii ya Madini lakini vilevile nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uteuzi alioufanya kwa kuweza kumteua Waziri wangu Mheshimiwa Dotto Biteko mimi na ye ye kusimamia sekta hii muhimu ya madini kwa kweli namshukuru sana na tunapenda kumwahidi kwamba hatutamwangusha, tutaendelea kufanyakazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, niendelee kumshukuru vilevile tena Mheshimiwa Rais wka kumteua dada yetu Angella Kairuki kushika nafasi ya kuwa Waziri wa Mambo ya Uwekezaji ambayo itakuwa chini ya Waziri Mkuu. Ni hatua kubwa sana mbapo hata sisi kwa upande wa madini ina tija kubwa na itatusaidia sana katika masuala yote ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuishukuru Wizara ya Madini ikiongozwa na Katibu Mkuu, Profesa Msanjila kwa kazi kubwa anayoifanya tunasaidiana nae lakini vilevile niendelee kuwashukuru sana Wabunge kwa michango yao ambayo kwa kweli leo wamechangia hapa tumeona Kamati ambayo nayo imeweza kutoa maoni yake. Nipende kusema kwamba tunashirikiana vizuri sana na Kamati ya Nishati na Madini na tunafanya kazi bega kwa bega kuhakikisha kwamba tunapeleka sekta hii ya madini kule ambapo kunastahili.

Mheshimiwa Spika, vilevile niendelee kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Maswa Mashariki kwa kuendelea kunivumilia kwa kazi kubwa ninayoifanya maana muda mwangi nakuwa niko nao mbali lakini kwa kweli wamezidi kunipa ushirikiano mzuri, tunaendelea kushirikiana nao kuhakikisha kwamba naendelea kusimamia Jimbo langu la Maswa Mashariki kupeleka maendeleo ambayo tulikuwa tumewaahidi wananchi, lakini vilevile wanaendelea kuwa na uvumilivu wa kunivumilia mimi muda mwangi ninapokuwa sipo

Jimboni. Vilevile bila kusahau niishukuru sana familia yangu ambayo inanipa nguvu katika kufanya kazi zangu za Wizara.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niendelee sasa vilevile na kuchangia hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitungumza hapa.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nipende kusema kwamba tunaendelea kupongeza, kumpongeza Mheshimiwa Rais na kupongeza Bunge lako Tukufu kwa kukubali kuitisha au kubadilisha Sheria yetu ya Madini ya Mwaka 2010 na hayo mabadiliko ambayo tumeyafanya mwaka 2017. Kwa kweli kwa muda ambaao tumeanza kutumia sheria hii tumeweza kuona mabadiliko makubwa ambayo yameweza kusaidiwa na sheria hii baada ya kufanya haya mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, cha kwanza kabisa ni ile Serikali kumiliki asilimia 16 kwenye miradi yote ya migodi ya madini. Kwa kweli imeonekana kuwa na tija kubwa na watu wote, wawekezaji wote wa upande wa madini wako tayari kutoa asilimia 16 ambayo Serikali itakuwa inazimiliki japokuwa Kambi ya Upinzani walikuwa na wasiwasi kuona kwamba labda inamiliikiwa na nani, lakini niwatoe tu wasiwasi Kambi ya Upinzani kwamba hii asilimia 16 sasa hivi iko chini ya *Treasury* kwa maana ya Hazina. Vilevile mapendekezo yao walikuwa wanayatoa kwamba iwe *STAMICO, ok fine*, inaweza ikawa *STAMICO* lakini inaweza ikawa kwa upande wa *Treasury*, lakini bado iko upande ule ule wa Serikali. Ile *ownership* ya 16 percent bado inamiliikiwa na Serikali na Serikali inapopata gawiwo basi itapeleka maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa mabadiliko haya haya tunashukuru na kuona tija kubwa ambayo imekwenda hasa katika kubadilisha kiwango cha mrabaha kutoka asilimia nne na asilimia tano sasa hivi tunatoza asilimia sita kwenye madini ya metali na asilimia sita hiyo kwenye madini ya vito. Tumeona jinsi ilivyoweza kupandisha mapato na kuweza kupata maduhuli makubwa kutokana na ku-*charge* asilimia hiyo sita ikiwa ni pamoja na tozo jipya la asilimia moja kwa maana ya

clearance fee. Kwa kweli niwashukuru wachimbaji wamejitolea na wame-complyvizuri na sheria hii na wanatoa hiyo tozo na kwa kweli hawana malalamiko yoyote.

Mheshimiwa Spika, isipokuwa tu niendelee kumshukuru tena Mheshimiwa Rais pale tarehe 21 Januari, 2019 baada ya kukaa na wachimbaji akaongea nao kwa kweli walitoa malalamiko mengi na hasa katika kodi ambazo ziliikuwa zinatozwa katika sekta hii ya madini. Nishukuru kwamba baada ya kuondoa hiyo VAT pamoja na *withholding tax* kwa kweli unafuu umeonekana mkubwa na sasa hivi wengi wa wachimbaji wanaonekana kutoa ushirikiano katika kufanya biashara kwa sababu tumepunguza kodo hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwamba kuititia Shera hii ya madini amekuwa na msisitizo mkubwa katika kuanzisha masoko ya madini. Kwa kweli uanzishwaji wa masoko ya madini imeonekana kuwa na tija kubwa. Mfano mzuri, soko moja tu la kule Chunya, siku ya kwanza ambapo tumefungua soko la madini tuliweza kupata zaidi ya kilo 13 za dhahabu na kupata zile kilo 13 za dhahabu tulipata zaidi ya shilingi milioni 68 kwa siku moja tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ina tija kubwa na sasa tumefungua masoko 22 na kwa kweli ni kwamba ukusanyaji wa fedha umekuwa ni wa hali ya juu, tumeona jinsi fedha ilivyokusanywa kwa sababu dhahabu iliyopita kwenye masoko mpaka hivi sasa ninavyozungumza ni zaidi ya kilo 578 ambapo zina thamani zaidi ya bilioni 48 na sisi kama Serikali kuititia huo mrabaha tumeweza kupata zaidi ya bilioni 3.6.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tukiendelea na kusimamia vizuri masoko haya basi tunaweza tuakajikuta tunakusanya vizuri zaidi na nipende tu kuishukuru Kamati ya Nishati na Madini imetoa mapendekezo yake na niseme tu kwamba tumeyachukua mapendekezo hayo, tunakwenda kuyatumia mapendekezo hayo katika kuboresha masoko haya na kuhakikisha kwamba masoko haya yanaendesha vizuri shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, niendele kuwaasa wachimbaji, walete madini kwenye masoko haya kwa sababu ukileta madini kwenye masoko haya unapata uhalali wa Serikali, utaingia kwenye ule utaratibu sahihi wa Kisheria ambapo madini yako sasa yatatambulika Kiserikali na wee utalipa kodi yako lakini vilevile Serikali itapata kipato chake na Serikali itakulinda, itakupa usalama wa madini hayo na itakupa usalama wa soko.

Mheshimiwa Spika, vilevile niwaase wanunuzi; bado wanakwenda kununua madini katika masoko ya pemberi au ya uchochoroni. Tuwaase na kuwashauri kwamba waje katika masoko ya madini kwa sababu masoko haya tumeyatengeneza kukutanisha wauzaji na wanunuzi wa madini. Wakifika katika soko utaratibu wote unachukuliwa na wataalam wetu wako pale, wanapima madini hayo na kuhakikisha madini siyo feki, madini ni sawasawa, kipimo utatolewa sawa sawa lakini vilevile ni kwamba utakuwa na uhakika na kile ambacho wewe umekinunua.

Mheshimiwa Spika, niendele kushukuru katika marekebisho haya haya ya Sheria ambayo tuliweza kuyafanya, kuna suala la *local content*; wafanyabiashara wengi au wachimbaji wengi wame-comply na Sheria ya *Local Content*, mpaka sasa hivi tuna uhakika kampuni nyingi sasa hivi wanaajiri Watanzania, lakini Kampuni nyingi vilevile sasa hivi zinakwenda kutumia bidhaa za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pia tushukuru kwamba kwa kweli hata wafanyabiashara wa Kitanzania wameonekana kuwa na kufanya biashara ambayo iko katika viango ambavyo wenye migodi wanahitaji. Zamani ilikuwa ni shida kupeleka bidhaa au wafanyakazi ambao wana ile *quality* au ule ubora ambao wachimbaji wanautaka, lakini kwa kutumia Sheria hii, Watanzania wamekuwa tayari kufanya biashara na migodi mikubwa na kuhakikisha kwamba wanakidhi yale mahitaji na ubora ambao wachimbaji wetu wanataka.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika sheria hii tuliona suala la *CSR* na Wabunge wengi wameliongelea. Katika

suala hili la *CSR* kuna Halmashauri nyingi ambazo sasa hivi wameanza kuona matunda yake ikiwepo Halmashauri ya Manispaa ya Geita. Geita sasa hivi wanakwenda kupata zaidi ya bilioni tisa na bilioni tisa hiyo itakwenda kufanya maendeleo katika Mji wa Geita. Hapo awali ni kwamba hii *CSR* ilikuwa ikitoka unakuta wanatueleza tu kwamba leo wamejenga shule, ukiuliza bei ya shule wanakwambia tumejenga kwa bilioni moja. Ukiangalia thamani ya shule hiyo haiendani na bilioni moja hatu milioni 200 haifiki.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa hivi Madiwani watasimamia fungu hili na wanaposimamia fungu hili watahakikisha kwamba *value of money* ipo kuhakikisha kwamba miradi hiyo sasa inakuwa na tija na ubora lakini inalingana na kiwango cha fedha ambayo imetengwa.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la *service levy*; niendelee tu kutoa ushauri kwa halmashauri zote, watu wote wanaotoa huduma kwenye migodi watupe ushirikiano kwa kushirikiana na halmashauri. Mtu yoyote ambaye hayuko tayari kutoa *service levy* katika Sekta hii ya Madini sisi tutambana. Tuhakikishe kabisa kwamba watu wote wana *complyna* sheria ya ya kulipa *service levy* ambayo ni asilimia 0.3 na waweze kutoa kwa halmashauri husika. Mfano mzuri juzi nilikuwa Shinyanga, yule mchimbaji mmoja ambaye alipata almasi kubwa kabisa ambayo hajawahi kutokea hapa Tanzania yenye *carat* zaidi ya 512, palepale tumemchaji katika soko la madini amelipa mrabaha wetu zaidi ya milioni mia moja na themanini na kitu; lakini vilevile katoa fedha kwa ajili ya *clearance fee* na palepale tukatoa fedha ambayo ni 0.3 percent kwa ajili ya Halmashauri ya Kishapu; na halmashauri imepata fedha. Huo ndio mfano mzuri kwa wachimbaji wote waweze kuhakikisha wanafuata taratibu na sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile nishukuru kwamba katika Wizara yetu tumeendelea kusimamia masuala ya uongezaji wa thamani ya madini (*value addition*), sasa hivi katika kituo chetu cha *TGC* cha pale Arusha tunaendelea kutoa mafunzo kuhakikisha kwamba vijana wetu wanajifunza namna ya

kukata madini na kuweza kuongeza thamani katika madini hayo.

Mheshimiwa Spika, tuna Taasisi ya *GST* ambayo ni muhimu sana kwa wachimbaji Waheshimiwa Wabunge wameiongelea. Nipende kukuhakikishia katika Bunge lako kwamba tunaendelea kufanya tafiti mbalimbali na kuchora ramani ambazo zinaonesha uwepo wa madini kwa kila mkoa na kwa kila Wilaya. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wangu imeeleza, kwamba tumeshatengeneza ramani hiyo na wachimbaji wote wanawenza wakaja *GST*kuweza kupata taarifa mbalimbali za uwepo wa madini mbalimbali katika yale maeneo tuliyonayo.

Mheshimiwa Spika, *STAMICO*; kwa mara ya kwanza sasa hivi *STAMICO* imefufuka na hapa tunavyozungumza mgodi wa *STAMIGOLD* ambao ulikuwa unatengeneza hasara tulikuta hasara ya zaidi ya bilioni 64. Sasa hivi mgodi wa *STAMIGOLD* unatengeneza faida tumeshapata faida zaidi ya bilioni moja; ni kwa sababu ya usimamizi mzuri na tulibadilisha pale menejimenti sasa hivi wanachimba kwa faida. Nipende tu kuwahakikishia ile *STAMICO* iliyokuwa inazungumzwa zamani vibaya na Bunge lako hili Tukufu, kwa sababu Waheshimiwa Wabunge kweli ilikuwa inawachefua sasa hivi tunakwenda kuongelea faida katika uchimbaji au katika miradi ya *STAMICO*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuzungumzia *issue* ya Mheshimiwa Kishimba. Amezungumzia katika ufungaji wa Mgodi wa Buzwagi; ni kweli kuna shimo kubwa pale ambalo liko pale na ndani ya shimo hilo au tuseme chini bado kuonaonekana kuna chembechembe au kuna uwepo wa dhahabu zaidi ya *ounce* milioni moja. Ni kweli, lakini katika masuala ya uchimbaji dhahabu inaweza ikawa chini haina tatizo lakini namna ya kuichukua dhahabu hiyo chini kuna gharama, gharama inapokuwa kubwa; kwa mfano sasa hivi *ounce* moja iko kwenye dola 1200, ukaweza kuchimba kwa gharama ya dola 1100, 1200, bado kuna wasiwasi inawezekana ukatengeneza hasara kubwa. Lakini kama unaweza ukachimba, sasa hivi pale Buzwagi mpaka

wanafikia mwisho walikuwa wanachimba ounce moja kwa gharama ya dola 900, kwa hiyo ukienda kuuza kwa dola 1200 unapata faida.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa hivi ni kwamba wana mitambo mikubwa, ukisema uchimbe dhahabu iliyoko pale kwao hawataweza kutengeneza faida; labda aje mchimbaji ambaye anaweza kuchimba kwa gharama ndogo, akichimba kwa gharama ndogo kwa hali iliyoko pale anaweza akatengeneza faida. Lakiini kinachotokea shimo lile ni kubwa kuna matetemeko yanapita yanahatarisha usalama wa wananchi wanaoishi maeneo yale. Tuna mfano mzuri pale katika mgodi wa Lisolute pale Nzega mashimo yameachwa, ni hatari kweli kweli. Sasa katika uchimbaji sheria inasema unapotaka kuanza kuchimba lazima utupe *mining plan* yako lakini lazima utupe *mining closure* yako *plan* ikoje na Kamati ya *mining closure* lazima ione na iridhie. Sasa hivi wameshawasilisha *mining closure plan* yao na ni lazima wafukie shimo hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini kama Mheshimiwa Mbunge anaendelea kutushawishi kwamba inawezekana mtu anaweza akachimba kwa gharama nafuu atuhakikishie ufunikaji wa shimo hilo; kitu ambacho tunaona ni kitu kigumu. Kwa hiyo bado majadiliano yanaendelea ya kuona namna ya kufanya.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile niendelee kumueleza Mheshimiwa Kishimba, amezungumzia hoja ambayo hata sisi tunakubaliana nayo; kuhusu *service levy* kwa yale makampuni yalikuwa yanatoa huduma ya bima katika migodi hiyo. Huduma ya bima ilikuwa inatolewa katika migodi hiyo, wale waliokuwa wanatoa huduma hiyo ni makampuni ya nje. Niliwahi kuzungumza tukiwa na Mheshimiwa Mbunge, tukiwa Kahama tukiwa katika msafara wa Mheshimiwa Makamu wa Rais Mama Samia Suluhu; nikasemaje; hatuna shida sisi kuwabana makampuni haya yatoe ushirikiano wa kutambua yale makampuni ambayo yalitoa huduma na kutueleza walioweza kuwalipa shilingi

ngapi ili tuweze ku-*charge* asilimia 0.3 ambayo ni *service levy* kwa halmashauri ya Kahama.

Mheshimiwa Spika, niliwaeleza kwamba halmashauri hiyo ifanye ufuatiliasi huo lakini mpaka sasa tunavyozungumza hawajatuletea kutueleza ni nani wamewasiliana naye, je amekubali au amekataa? Nimshauri tu Mheshimiwa Mbunge kwamba atuletee taarifa hiyo ili tuweze kufanya mawasiliano na hawa watu waliohusika. Lakini vilevile tutambue kwamba wale wote waliokuwa wanatoa *service kwenye* migodi kila mmoja ana wajibu wa kulipa *service levy* ambayo ni asilimia 0.3

Mheshimiwa Spika, kuna hoja nyininge ambayo imezungumziwa hapa na Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusiana na mradi wa *Tancoal*. Kuna mengine yataelezwa na Mheshimiwa Waziri atazungumzia na wahusika, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara amezungumza. Lakini nipende tu kuongelea mambo mawili kuna suala la barabara kilomita 40 kutoka pale Ngaka kwenda Kitai; kwa kweli hili suala linaongeza gharama ya uendeshaji au uzalishaji wa makaa ya mawe kwa sababu gani, kutoka Ngaka kwenda Kitai...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante malizia Mheshimiwa Waziri dakika moja.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, ahsante kutoka Ngaka kwenda Kitai ni kilomita 40 na madaraja yaliyopo pale katikati ni madaraja 12 na kila daraja lina uwezo wa kupitisha tani 15 tu za makaa ya mawe na wakati magari yale ambayo yanabeba makaa ya mawe kwenda Rwanda na Burundi yanatakiwa yabebe tani 30, kwa hiyo inabidi magari madogo yaliyo chini ya tani 15 yapitishe kwenye yale madaraja mpaka Kitai halafu Kitai pale ndipo yapakiwe sasa kuingia kwenye magari makubwa ambayo ni *Semi trailer*. Kwa kweli hii inasababisha ongezeko kubwa la uzalishaji,

nikubaliane na tumeshakuongea na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma pamoja na watu wa utengenezaji wa barabara (*TARURA*) ambao wamesema watakwenda kujenga madaraja hayo na kuhakikisha kwamba sasa baada ya muda wakishajenga madaraja hayo usafirishaji pale utakuwa wa bei nafuu kwa sababu magari ya tani 30 yataweza kufika kule Ngaka.

Mheshiimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ahsante sana. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshiimiwa Naibu Waziri Stanslaus Nyongo sasa naomba nimuite mtoa hoja Mheshiimiwa Waziri Doto Biteko Waziri wa Madini tafadhali karibu sana utajitahidi maksimamu tutakupa dakika 40. (*Makof!*)

WAZIRI WA MADINI: Mheshiimiwa Spika, kabla ya kuanza kujibu hoja mbalimbali zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa tumefarijika sana kama Wizara kutokana na michango mbalimbali ambayo Waheshimiwa Wabunge wameitoa kwa kusema na kwa kuandika. Tumepata ushauri na maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, ushauri na maoni hayo yalikuwa ya msingi na sisi tunaamini ushauri huu ni muhimu sana kwetu katika kutekeleza majukumu yetu.

Mheshiimiwa Spika, lakini vilevile tumesikia hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ambao nao wametoa ushauri mbalimbali ambao kwa kiasi kikubwa Serikali kwa hatua mbalimbali imekuwa ikiufanya kazi. Pia Waheshimiwa Wabunge wapatao 10 wametoa michango yao kwa kusema; michango yao hiyo yenye maoni na ushauri tunayachukua kwa uzito wake na itatusaidia sana katika kuboresha utendaji wa kazi Wizarani. Aidha, Waheshimiwa Wabunge 18 wamechangia kwa maandishi ambao pia michango yao hiyo tumeichukua kwa umuhimu wa kipekee na itatusaidia sana katika kuboresha utendaji wetu.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba hoja zote zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge sisi kama Wizara tunazichukulia kwa uzito wa kipekee na mimi nimesimama hapa kutolea ufanuzi baadhi ya hoja zilizotolewa. Hata hivyo kutokana na ufinyu wa muda tulionao yawezekana hoja zote hizi nisipate nafasi ya kuzieleza moja baada ya nyingine. Itoshe tu kusema kwamba tutaziwasilisha kwa maandishi kwa Waheshimiwa Wabunge ili pamoja na mambo mengine majibu yetu yawe rejea kwa siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, Kabla sijaanza kujibu naomba na mimi nirudie tena kumshukuru tena na tena Mheshimiwa Rais kwa imani kubwa aliyotupa kwa kuanzisha Wizara hii ya Madini, na kwa kweli Wizara hii pamoja na kwamba inaweza ikaonekana inazo Taasisi chache ina mambo mengi ya kufanya kwa sababu shughuli zake zinasaidia sana ukuaji wa uchumi. Mheshimiwa Rais msukumo alioutoa ni wa kusababisha Wizara hii mchango wake utoke kwenye asilimia 4.8 ya kuchangia Pato la Taifa sasa uwe mchango wa walau asilimia 10 ifikapo 2020. Lakini namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa ye ye mwenyewe amekuwa kinara mkubwa sana wa kutusimamia na kutupa maelekezo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, utakumbuka wakati tunaanzisha utaratibu wa kuanzisha masoko hapa nchini Mheshimiwa Waziri Mkuu ye ye mwenyewe ndiye alitisha kikao cha Wakuu wa Mikoa wote nchini lakini soko la kwanza la masoko tuliyolianzisha ye ye mwenyewe wala hakutuma mtu wa kufanya kazi hiyo kwa niaba yake alifanya mwenyewe. Kwa kweli tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa msukumo wake huo na sisi Wizara ya Madini tunapata imani kubwa na nguvu kutoka kwake.

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru pia Naibu Waziri wa Madini Mheshimiwa Nyongo kwa ushirikiano mkubwa anaonipa, ye ye pamoja na wenzangu Wizarani, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine.

Mheshimiwa Spika, lakini nitakuwa mchoyo wa fadhila kabisa kama sitakushukuru wewe mwenyewe binafsi. Tulifanya semina moja hapa Bungeni kwa ajili ya kuangalia masuala la madini na wewe ulikuwa mgeni rasmi nakumbuka kwenye hotuba yako maneno uliyoyazungumza, ni kwamba Wizara ya Madini lazima mtuondolee aibu ambayo imezunguka sekta ya madini. Maneno haya ni nyongeza tu ya msukumo mkubwa ambao wewe mwenyewe umekuwa ukiutoa kwenye kusimamia sekta hii. Uliunda Kamati mbili kama Waheshimiwa Wabunge watakavyokumbuka na zote hizi zilikuwa na nia ya kuhakikisha kwamba tunasimamia vizuri sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, ninaweza kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, Kamati yetu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa michango yao, ushauri wao lakini sana kwa kufuatilia kwa karibu mambo mbalimbali yallyoko. Mwisho lakini si kwa muhimu niwashukuru Wakuu wa Mikoa wote, vyombo vyaya habari na wadu wa madini; na wengine umewaona wako hapo wamekuja kutuunga mkono. Baada ya kusema shukurani hizo naomba sasa nijielekeze kwenye hoja chache ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezieleza.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja hapa imezungumzwa juu ya wananchi wa Tarime; na hoja hii imezungumzwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwenye eneo la madini na ambaye pia ndiye Mbunge wa Tarime. Lakini mimi nilikuwa najaribu kutafakari, jambo hili tumelifanyia kazi kwa karibu sana. Mheshimiwa mtoa hoja atakumbuka jambo hili mgogoro wake haujaanza leo umeanza mwaka 2009, 2012. Mimi nimekwenda na Mheshimiwa Heche Jimbo kwa kwake tumekwenda kushughulikia jambo hili la fidia ambalo limekuwa la muda mrefu. Mheshimiwa Heche nilitamani sana leo asimame hapa asema kwa kweli Serikali mnajitahidi kwa kuchukua hatua kwa sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumekuta wananchi waliofanyiwa uthamini kwenye awamu ya 47 walio kwenye hati ya kulipwa na mgodi wako 66. Tumekwenda na *Chief valuer* kuangalia nyaraka mbalimbali tumekuta wananchi ambao walikuwa

wamefanyiwa uthamini ni zaidi ya 117 wengine wamekatwa kwa hila; na fedha walizokuwa wametengewa kulipwa zilikuwa ni shilingi milioni 224 peke yake; tukakataa tukiwa na Mheshimiwa Heche tukasema hapana Watanzania hawa walichagua Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ili iwasemee, haiwezekani atokee mtu tena kwenye ardhi yao wakatiwe maeneo na wengine wapunguzwe na fedha waliupwe kidogo. Tumeamuru uthamini urudiwe upya. Hili jambo Mheshimiwa Heche nilidhani leo kwa niaba ya watu wa Nyamongo angeweza kufika hapa akapongeza Serikali kwa kufanya jambo hili kwa faida ya watu wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa mbunge anafaamu, jambo la utirishaji wa maji kwenye mgodi wa *North Mara* limeanza kwa muda wa miaka 10 iliyopita. Tumeanza kwa awamu ya kwanza, huu ni mgodi mkubwa, ni kweli tunahitaji fedha kutoka nje, ni kweli tunahitaji ajira kutoka kwa watu wetu kwa ajili ya watu wetu lakini afya za watu ni muhimu kuliko jambo lolote. Nimekwenda mwenyewe na Mheshimiwa Mbunge pamoja na Mheshimiwa Mbunge mwingine aliyenialika Mheshimiwa Agness Marwa, tukafanya mkutano na wananchi wa Nyamongo tukawaambia warekebishe kasoro ifikapo tarehe 30 Machi hawakurekebisha kasoro; hatua ya kwanza kwa mujibu wa sheria tunapiga faini; na tumewapa wiki tatu baada ya wiki tatu kama kasoro hizo hazijarekebishiwa tutachukua hatua inayofuata ambayo imetajwa kwenye sharia. Nilitarajia Mheshimiwa Heche angefika akapongeza walau kwa faida hiyo, kwa sababu sisi wenyewe ndio tumeamua sasa kuwasimamia wananchi wa Nyamongo bila kupepesa macho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, limezunguzwa jambo lingine hapa kwenye eneo hili, kwamba je, haya mambo fedha mlizotoza faini warudishiwe wananchi? AG amelieleza vizuri sana na nilitamani sana Mheshimiwa Heche pamoja na sisi Waheshimiwa Wabunge ambao ni wawakilishi wa wananchi tuchukue nafasi hii ya kuwaelimisha wananchi utaratibu ulivyo. Inawezekana kabisa tunatamani walipwe fidia ya fedha walizotoza faini, lakini unalipa *against* kitu gani kwa

sababu tathimini ya madhara hayo haijawahi kufanyika? Lazima ikishafanyika tukajua ndio tunaweza kwenda kwenye hatua nyingina kama AG alivyozunguzma.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nikuhakikishie wewe pamoja Bunge lako, Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi chini ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kipaumbele chake cha kwanza ni watu wake na maisha bora ya watu wake waweze kunufaika na rasilimali hizi, tutasimama kidete kulinda uhai wa watu wetu kwa gharma yoyote ile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ameelze hapa Mheshimiwa Neema Mgaya juu ya taarifa ya *GST* na kuwafanyia utafiti wachimbaji wadogo. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu, Wizara ya Madini baada ya marekebisho makubwa ya sheria na kufanya *GST*sasa kuwa taasisi inayojitegemea na si wakalaa, tunaenda kufanya utafiti kwa ajili ya maeneo ya wachimbaji wadogo. Na hatua ya kwanza ili uweze kufanya utafiti ni lazima ununue hivyo vifaa vya kufanya utafiti; tumenunua mtambo maalum kwa ajili ya kuwafanya utafiti wachimbaji wetu. Niwaombe wachimbaji wa Tanzania wawe na subira tunapoendelea kufanya kazi mambo haya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Magige ameeleza vizuri sana na ameeleza kwa uchungu tabia ya baadhi ya watu kuendelea kutoza tozo ambazo Bunge hili limezifuta. Nilieleza hapo wakati najibu swali na naomba nirudie tena. Bunge hili halifanyi maigizo hapa, linatunga sheria na sheria hizo lazima zifuatwe, mtu yoyote anayetoza tozo ambazo Bunge hili limezifuta kwa mujibu wa sheria anatenda kosa. Ninaomba Mheshimiwa Magige atuletee mfano wa watu waliozwa sisi tutachukua hatua. Nimewasiliana na Wizara ya Fedha wamesema hakuna maelekezo hayo.

Mheshimiwa Spika, wakati mwengine ni tabia ya mtu mmoja tu, huyo mtu mmoja kwa vitendo vyake anavyofanya inaonekana Serikali nzima inanyanyasa watu. Nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Catherine Magige hakuna mtu

atatozwa tozo hizo ambazo Serikali imeshaziondoa, na mimi nikuhakikishie kwamba tutaendelea kulifanya kazi kwa nguvu zetu zote.

Mheshimiwa Spika, limeelezwa jambo la urasimu kwenye baadhi ya ofisi zetu na ikatajwa *specific* ofisi ya Geita, na Mheshimiwa Mbunge Ammar. Inawezekana ukaonekana urasimu, lakini tukubali kazi ya kusimamia Sekta ya Madini ndugu zangu imejaa mambo mengine, usipokuwa makini kosa moja la dakika moja unaweza ukaisababishia Serikali hasara ya mabilioni ya shilingi. Hawa vijana tulionao ni wachache lakini jambo la msingi sana; tumefanya kazi Wizara nzima ya kupruni watu wengine ambaa tulikuwa tunaona sio waaminifu tumebakiza watu ambaa wanafanya kazi .
(Makof)

Mheshimiwa Spika, ninawaomba waheshimiwa Wabunge hawa ni vijana wenu, hawa ni watoto wenu, hawa ni wanadamu pia wanahitaji kutiwa moyo; wamefanya kazi kubwa sana. Tunaangalia *trend* ya mapato inavyokwenda kwa sasa ni tofauti sana na miezi mitatu iliyopita, kazi hii wanafanya vijana hawa. Nkuombe sana Mheshimiwa Ammar, kama kuna *specific case*, ya mtu mmoja anayesababisa urasimu kwenye ofisi zetu sisi tutachukua hatua. Hata hivyo ombi lako la kuomba ofisi pale Nyang'wale naomba nikuhakikishie kwamba tunaendelea kufanya tathimini kwenye maeneo mbalimbali. Si tu Nyang'wale yako na maeneo ya Mbogwe kuna shughuli nyingi zinafanyika, tunaangalia kama tutapata uwezekano wa kupata *human resource* ya kutosha tutafungua ofisi ili watu wetu waweze kuhudumiwa kwa urahisi kuondoa mizunguko isiyokuwa na maana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, Mheshimiwa Amar anafahamu, maeneo mengi ambayo yalikuwa yameshikiliwa na makampuni makubwa yote tumeyapelekea *default note* na tuko kwenye utaratibu wa mwisho wa kuyafuta ili tuwapatie wachimbaji wadogo. Niwaombe wachimbaji wa Nyangh'wale na wachimbaji wa maeneo mengine Tanzania, wajunge kwenye vikundi, lakini niwaombe pia wachimbaji

wa Tanzania mfumo wa kuanza kuchimba wakianza kupata wanagombana hizo zilipendwa. Mheshimiwa Amar ni shahidi, wachimbaji hawatunawa-*mobilise* tunawaweka kwenye vikundi, wakianza tu kupata pesa migogoro inaanza. Niwaombe tushikamane tunapokuwa tunapata fedha kama ambavyo tunashikamana wakati tunatafuta leseni.

Mheshimiwa Spika, limeongelewa pia eneo hapa na Mheshimiwa Kapufi, juu ya makinikia na usafirishaji wake. Mheshimiwa Kapufi tumeshawahi kulizungumza hili jambo sio mara moja, sio mara mbili, tunayo changamoto ya kisheria, tunaiangalia changamoto hiyo; tunakisikia kilio chake na sisi tunatamani tumuondolee kero hiyo. Tunahitaji mapato kwenye mgodi wake, lakini tunahitaji pia na yeze fedha aliyowekeza iweze kurudi. Hii ni Serikali inayotaka kuona Mtanzania kwenye nchi yake anawekeza na anapata pesa anawekeza kwenye mambo mengine zaidi. Nmwombe Mheshimiwa Kapufi awe na subira tumalize hili jambo, ni jambo la kisheria, lakini kama nilivyomwambia mimi na yeze hapa ninavyozungumza moyo wangu na moyo wake inawasiliansa kwa sababu tulizungumza, anajua ni wapi tumekwama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hapa hata nikisimama nikasema kesho aanze kusafirisha atakutana na kikwazo ambacho kitampa hasara kubwa zaidi. Naomba awe na subira Mheshimiwa Kapufi, mimi naumia, nimekwenda mwenyewe kwenye mgodi wake na wenzangu Wizarani tunalfanyia kazi, likikamilika tutampa utaratibu utakaofanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Maftaha ameeleza hapa juu ya *One Stop Centre*, hii inafanyikaje. Naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge; *One Stop Centre* ni mfumo tuliouanzisha wa kufanya biashara ya madini kwenye dari moja. Tunataka kuwaondolea urasimu wachimbaji wetu wa kutoka *point* moja kwenda *point* nyingine kwa ajili ya kutafuta huduma. Kwenye *One Stop Centre* ni jengo kubwa ambalo ndani ya jengo hilo ofisi zote zinazohusika kwa ajili ya utoaji huduma kwenye madini zitakuwepo kwenye ukuta huo. Jengo hilo ni kubwa, Uhamiaji watakuwa hapo, *Valuers*

watakuwa hapo, watu wa kupima ubora wa madini watakuwa hapo, benki zitakuwa hapo, ukienda na madini yako vitu vyote unafanya kwenye eneo moja na kutoka na utaratibu wako unavyojua kwa ajili ya matumizi yako. Kwa hiyo, *One Stop Centre* sio *refinery* wala sio *smelter* wala sio kitu kinachofanya kazi ya kuchenjua, ni jengo kwa ajili ya kutolea huduma. Tutakapokwenda kulizindua nitamwomba Mheshimiwa Maftah tuandamane naye akaone *One Stop Centre* ilivyo ili aweze kujua tunafanya vitu vya namna gani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Musukuma amezungumzia habari ya watu wanaofanya kazi kwenye Ofisi ya Madini, uaminifu wao. Hilo tunalichukua, ni jambo ambalo tutaendelea kulifanyia kazi kila siku, lakini jambo la maana sana.

Mheshimiwa Spika, Mgodi wa *GGM*, toka mwaka 2017 tumekuwa na mgogoro na mipasuko kwenye maeneo ya Nyamalembo, nyumba 80 zilifanyiwa tathmini, lakini na sisi tukapeleka timu nyingine kwenda kuangalia. Tumetoka kwenye nyumba 800 tumekuta nyumba zilizoathirika ni zaidi ya nyumba 3,000 na mgodi umekubali baada ya timu ambayo tumeipeleka kule inayohusisha ofisi zote, mgodi walikuwemo, Halmashauri walikuwemo, Ofisi ya Ardhi walikuwemo, watu wa Madini walikuwemo, watu wa *RS* walikuwemo, ilikuwa timu kubwa imefanya kazi kwa muda ambao kwa kweli, ulizidi hata kiwango cha muda waliokuwa wamepewa.

Mheshimiwa Spika, wamekuja na ripoti nzuri sana juu ya fidia ya maeneo hayo. Nimwombe Mheshimiwa Musukuma, *GGM* wameanza kulipa fidia, inawezekana hiso fidia mtu mwingine anaweza kusema ndogo, lakini ndogo ukilinganisha na nini na ukilinganisha na tathmini gani? Sisi tunasema fidia hizi zimeanza kulipwa. Kama kuna mwananchi anadhani hajalipwa inavyostahili tuwasiliane na sisi tutampa vigezo.

Mheshimiwa Spika, wametokea watu wengine hapohapo Geita ambao walilipwa kipindi cha nyuma, wako

wananchi kama watatu mmoja amelipwa milioni 74. Pamoja na kulipwa milioni 74 kwenye orodha hii tena ya kulipwa upya jina lake limo. Pamoja na kwamba huu mgodi ni wa mwekezaji lakini lazima na sisi tumwonee huruma. Watu ambao wanafikiri wanaweza kupata fedha kwa ujanja ujanja, nashauri tu watafute shughuli nyingine ya kufanya.

Mheshimiwa Spika, tumewaaambia hata watu wa Nyamongo wale walotegesha hawawezi kulipwa hata iweje kwa sababu, wametegesha. Hata wale ambao Mheshimiwa Heche anawajua wa awamu ya 21 na wenzao waliokuwa wanadai fedha, watu 1,934 1,800 walichukua cheki, watu 134 wakaacha cheki, tuliwaambia na wao wakachukue cheki. Tunapokuwa tunawatetea Watanzania ni lazima pia tuwalinde wawekezaji na baadhi ya watu wachache ambao sio waaminifu kwa sababu, pia ni wajibu wa Serikali kuwalinda wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Millya ameeleza hapa juu ya foleni kubwa kwenye ukaguzi wakati watu wanaingia mgodini. Ushauri wake tunaupokea na tunaupokea kwa heshima kubwa na tunauzingatia. Namwomba awe na subira, tunatafuta kibali cha kuajiri watumishi wengine. Mara baada ya kukamilika, tukipata watu tutaongeza *workforce* pale kwa ajili ya kuangalia watu wanavyoingia pale mgodini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Maige ameeleza maeneo mbalimbali ambayo wachimbaji wake wana mgogoro. Ameeleza eneo la Bushimangira. Ni kweli mimi na ye ye tulikwenda. Eneo la Mwazimba ni kweli mimi na ye ye tulikwenda na kuna changamoto zilizokuwepo hapo za utoaji wa leseni. Wale waliohusika kwenye utoaji wa leseni hizo kwa kukiuka utaratibu walichukuliwa hatua na Wizara. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Maige wananchi wa Mwazimba na wananchi wa Bushimangila kwa Serikali hii wawe na amani, hawatapoteza leseni yao, watapewa leseni yao. Kwa sababu leseni ile ilitolewa katika mazingira ambayo ni tata, sisi Wizara tumechukua hatua moja kubwa zaidi kwa kufuata

utaratibu tumeiandikia *default notice* ili tuweze kuzifuta tuwapatie wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Maige kama ambavyo yeye anasema ni mtetezi wa wanyonge, aendelee kuwatetea wananchi wa Mwazimba na wa Bishimangila. Nataka nimhakikishie Wizara ya Madini tutam-*support* kwa mambo yote hayo. Ameeleza habari ya fidia, jambo hili tunalifanyia kazi tupewe muda, lakini baada ya muda tutalimaliza na watu wanaohusika.

Mheshimiwa Spika, yako maeneo mengine ambayo nataka nimalizie. Jambo lilirozungumzwa hapa ni habari ya Mgodi wa *TANCOL*, ameelieleza vizuri sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda. Tumeshapeleka barua kutoka *NDC*, Wizara ya Madini; *NDC* na yeye analalamika kwenye ubia ule anapunjwa. Tarehe 11 Mei, ametuletea barua na sisi baada ya bajeti hii tunapeleka timu ya wakaguzi maalum kutoka Tume ya Madini kwa ajili ya kwenda kujiridhisha na mambo yote yaliyomo kwenye barua iliyoletwa na *NDC*.

Mheshimiwa Spika, naomba nikuhakikishie hili jambo tumeanza kulifanyia kazi mapema. Hapa ninapozungumza *TANCOL* alikuwa analipa kodi kwa kutumia Sheria ya Madini ya mwaka 1998. Analipa kwa kutumia *Net Back Value*, kwa maana gani? Kwamba, yeye akishachimba makaa ya mawe, kodi anayotoza anatoza pale *site* kwa hiyo, wakati sisi tunachukua kodi kwa tani moja dola 53 yeye anasafirisha hayo makaa ya mawe anapeleka kwenye *destination* yake anauza tani moja dola 220. Sasa kodi tunachukua kwenye dola 53 badala ya dola 200 na kitu. Tumekuwa na ubishani mwingi wa kisheria, lakini hatimaye AG ametupa mwelekeo. Naomba niwahakikishie kwamba, jambo hili tunalifanyia kazi kabisa na Waheshimiwa Wabunge watapata matokeo baada ya taarifa yetu hii kwenda kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa niendelee tena kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge niwaombe kazi ya ulinzi wa rasilimali madini sio kazi ya Wizara ya Madini peke yake, ni kazi yetu wote. Niwaombe

tuungane wote na kwa kweli, wachimbaji wadogo wa Tanzania kama hatuwezi kuwapongeza kwa kipindi hiki hatutawapongeza tena, wamekuwa watu wema mno, ndio wanaotupa taarifa. Nimeeleza hapa watu ambao tumewakamata wakitorosha madini wanaotupa taarifa ni wachimbaji wenyewe.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa heshima na taadhima na kwa niaba ya Wizara ya Madini niwashukuru sana wachimbaji wa madini Tanzania kwa kuitikia wito, kwa kuona wivu na rasilimali zao. Nataka niwahakikishie Wizara ya Madini itawapa kila aina ya *support* watakayoihitaji.

Mheshimiwa Spika, pia niwashukuru sana vyombo vyaa habari nchini. Uelewa wa sekta ya madini hapa nchini unasaidiwa sana na vyombo vyaa habari, wamekuwa mstari wa mbele kueleza udhaifu uko wapi, wengine wameandika makala za kiuchunguzi ambazo zimetusaidia kujua ukweli. Kwa mfano kule Mahenge, ilianza makala ya gazeti moja, tulivyokwenda tukakuta mambo mengi yaliyokuwa yameelezwa kwenye makala ile yalikuwa ya kweli. Naomba nirudie tena kuwashukuru sana waandishi wa habari kwa uzalendo wao, kwa kuipenda nchi yao na kwa kweli kwa kuona sekta yetu hii ya madini inakua.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii na naomba nitoe hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Madini kwa kupitia ushauri mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge na kwa kweli umejitatihidi sana kujaribu kujibu kila eneo. (*Makofii*)

Sasa tunaendelea, Katibu.

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 100 – Wizara ya Madini

MWENYEKITI: Naomba tukae Waheshimiwa Wabunge. Tuendeleee, Katibu.

Kif. 1001 – *Administration and Human Resources Management.....Sh. 3,874,845,018*

MWENYEKITI: Mshahara wa Waziri. Tunaanza na Mheshimiwa Jumanne Kishimba.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimesikiliza majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu Mgodi wa Buzwagi,

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mgodi wa Buzwagi sio mali yangu binafsi kama Mheshimiwa Kapufi alivyo na *mine yake*. Huu Mgodi wa Buzwagi Serikali ina hisa asilimia 16. Serikali inapoteza triliuni 28, nashangaa Mheshimiwa Naibu Waziri anasema anaogopa tetemeko la ardhi litapita pale Buzwagi. Je, Mgodi wa Kahama *Mining* wenyewe kilometa nne *underground*, hilo tetemeko litakwepa ikiwa eneo moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea Naibu Waziri ashtuke au Waziri ashtuke kwamba, Serikali inaenda kupoteza hizi pesa kwa mawazo au barua ya mtaalam mmoja. Je, Serikali imewahi kutoa na yenyewe timu ya wataalam kwenda kujiridhisha na hayo? (*Makofj*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili suala la madini tumepata matatizo makubwa sana. Tumepoteza almasi nydingi sana wakati wa Mwalimu Nyerere, wakati huo Mwadui ripoti ilitoka ya wataalam ikionesa almasi zimekwisha na mgodi ukawa karibu kufungwa. Baada ya mgodi kuja

kufunguliwa ukaonekana kuna almasi nyingi mpaka Uwanja wa Ndege wa Mwadui ulichimbwa na unatoa almasi mpaka leo. Sasa ni kweli Mheshimiwa Waziri anataka kweli arudi akiwa ana imani kabisa tukafukie?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kutoa hoja, kama Wabunge wapo wa kuniunga mkono...

MBUNGE FULANI: Maelezo.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, watoe maelezo. Kama kuna maelezo ya kutosha aweze kunieleza, nisiporidhika nitashika shilingi. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ufafanuzi zaidi. Mheshimiwa Naibu Waziri Stanslaus Nyongo, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe tu Mheshimiwa Kishimba hakuna haja ya kuendelea kunishikia shilingi au kumshikia Mheshimiwa Waziri shilingi, kwa maelezo haya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchimbaji wa mgodi wowote kwa mujibu wa sheria ni lazima utele *mine plan* yako. Ueleze utachimba vipi na katika kuchimba huko ni lazima uoneshe mgodi wako utaufunga vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo *pit* anayoiongelea Mheshimiwa Kishimba ni *pit* kubwa, ni mita zaidi ya 100 na kitu kwenda chini na hapo ilipo ni hatari sana kwa maisha ya watu wanaozunguka eneo lile ni lazima uweke mazingira salama kwa kulinda mazingira na kuona namna bora ambapo shimo hili halitaleta madhara. Kuna kemikali nyingi ambazo zinazalishwa katika lile shimo ambazo zipo na kweli kama tetemeko litakuja bila shimo lile kuwa *maintained* vizuri kuna uwezekano mkubwa sana wa kupata zile kitu tunaita *rain slides* ambazo zinaweza zikahatarisha zaidi tena vilevile mazingira na viumbi vinavyoishi maeneo hayo. Hawa watu wa Buzwagi wako tayari na wameshakuja na *plan* yao na

kuna kitu wanaita *Mine Closure Plan Committee* ambayo nayo imepitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa dhahabu sio tatizo, isipokuwa gharama ya kuchimba dhahabu ile ndio tatizo. Nami nipende tu kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunapokea wazo lake, lakini linahitaji utafiti wa kutosha, linahitaji wakae wakae wa kutosha ili waweze kutupa namna, *plan bora* ya kuweza kuchimba pale. Kama ana mwekezaji ambaye yuko tayari kuja kuchimba pale aje *a-present* wataalam wetu wamsikilize waone namna anayoisema kama kweli inakubalika katika ulindaji wa mazingira na kuweza kuliweka lile shimo katika hali ya usalama kwa maisha ya baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tu Mheshimiwa atuachie shilingi tutaendelea kushughulikia hoja yake na tutaendelea kutafuta ufumbuzi wa eneo hilo. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kishimba.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba kutoa hoja kama kuna Wabunge watani-*support* wani-*support*, wasimame.

MWENYEKITI: Endeleeni kusimama ili Katibu aandike haraka-haraka.

Tuanze, Mheshimiwa Peter Serukamba, dakika tatu tatu.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Profesa Kishimba. Mheshimiwa Kishimba anaongelea dhahabu iliyobaki, Wizara *argument* yao wanaongelea tetemeko la ardhi, mazingira na gharama za kuichimba hiyo dhahabu iliyobaki. Sasa nadhani Serikali ama Wizara ingekaa na huyu mchimbaji waka-*negotiate* kwenye gharama kwa sababu, zile gharama ambazo atazionesha ndio zitakazoonesha kama je, kweli ni *viable*,

lakini ninachoona hapa, hapa kuna tetemeko la ardhi, ni gharama, tufunge; nadhani sio sawa.

MBUNGE FULANI: Kuna pesa.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, pale tumeambiwa kuna dhahabu ambayo ina *worth* trillioni 28, *unless* Serikali itwambie kwamba, hizo trillioni 28 ni za uwongo, lakini kama kuna dhahabu ya trillioni 28, wanataka Bunge hili tufanye maamuzi ya kufukia trillioni 28 *then* liko tatizo kubwa sana. Ningetamani, kama alivyoomba Mheshimiwa Kishimba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umefanya huko nyuma, Mheshimiwa Kishimba amekuomba asubuhi kwamba, kama inawezekana Bunge lichukue, aunde Tume iende ikaangalie hizo gharama tuishauri Serikali. Ninayo hakika tume hiyo itafanya kazi nzuri ambayo Serikali wataweza kutuelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Getere.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Mimi siungi mkono hoja ya Mheshimiwa Kishimba. Kwa professional yangu mimi ni mtu wa mazingira. Pale ambapo eneo lolote lile linalotoa production au faida likaonyesha kwamba lina hatari kwa maisha ya binadamu, hata kama kungekua na dhahabu bilioni mia ngapi lakini ili mradi kwamba yale maeneo yamekuwa yana hatari ya maisha ya binadamu lazima Serikali ichukue hatua ya kuyafunga kwa muda ili kunusuru watu na kuangalia gharama zitakavyokuwa zinatokea huko mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri kitendo cha Serikali kufunga pale, sina imani kwamba kinafungwa kwa jumla lakini inaweza kuwa kinatengeneza mazingira ya kuweka watu kwanza wawe huru na baadaye waje waone

kwamba hizo gharama zinakuwaje ili watu waweze kupona kuliko kuwaruhusu kuendelea kuwepo kwa sasa ambapo watu wanaweza kufa kwa sababu ya kulinganisha na gharama au dhahabu iliyopo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri kwamba Mheshimiwa Kishimba angeangalia kwamba hiii hoja, kama Serikali inaweza kwenda kufanya huko mbele kuangalia lakini ikiwa imeshaokoa watu, basi hili jambo litaendelea huku mbele lakini watu wameshaokoka, asante.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Ndassa.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga hoja ya Mheshimiwa Profesa Kishimba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulipoteua tume ya kuchunguza madini ya almasi, taarifa ambazo siku zile tulikuwa tukipewa ni kwamba mgodi ule unakwenda kufungwa kwa sababu madini yameisha. Na wenzetu hawa wa nje walichokuwa wanafanya, wanarundika gharama kwa Serikali ili ku-*declare* kwamba mgodi huu hauna faida. Mheshimiwa Kishimba ameeleza vizuri sana kuhusu suala la tetemeko; lakini ukitazama Bulyanhulu ni kilomita zaidi ya nne, huu unaosemwa ni mita 130. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ombi langu, na wewe bahati nzuri umekuwa mtu mwema sana wa kulinda na kusemea rasilimali za nchi yetu, mimi nilitegemea Serikali ushauri ambao umetolewa na Mheshimiwa Kishimba wangesema ngoja tuuchukue ushauri huu halafu twende tukaufanyie kazi kwa sababu hapa tunataka kulinda rasilimali za nchi yetu. Kufukia pale trilioni 28, bajeti yetu sisi inayokuja hii tunayokwenda nayo keshokutwa hii ni trilioni 33, sasa pale kuna mali. Tuangalie mimi nashauri Serikali iangalie ifungue... (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Asante sana, Mheshimiwa Salome Makamba

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo liliopo katika Mgodi wa Buzwagi ni kwamba ile biashara *is not commercially viable*, haitekelezeki kwa sababu ya kodi kubwa za Serikali na kuyumba kwa mkatuba kati ya Serikali na mwekezaji. Kitu ambacho naishauri Serikali ifanye, ifanye utafiti wake mwenyewe bila kutegemea ile *closure plan* ya mgodi, ifanye utafiti wake jje iseme ni kwa nini Mgodi wa Buzwagi unataka kufungwa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakueleza hii ni kwasababu Waziri anasema kutatokea *landslide* na *environmental* sijui matetemeko, Buzwagi ipo *seven kilometers* kutoka mjini, ukilinganisha Australia kuna mgodi upo katikati ya jiji lenye *high population*. Sasa hiyo *landslide* ya Mgodi wa Buzwagi itakayoenda ku-affect mazingira ya wananchi inatoka wapi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isitegemee ripoti ya mwekezaji, mwekezaji anatafuta *exit* kwa sababu ameona hawezи kuvumilia kufanya kazi kwenye mazingira ambayo hayana *stable laws* zinazomruhusu kufanya kazi. Kwa hiyo ninashauri Serikali ikae chini ifanye *research*, itafute watalaam wafanye *research* au Bunge lishirikishwe tufanye *research* kutafuta kwa nini Mgodi wa Buzwagi unataka kufungwa, nakushukuru. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, wa mwisho awe Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Na mimi naunga mkono hoja ya Mzee Mheshimiwa Kishimba. Nikuombe tu sisi tunaotoka kwenye maeneo yenye migodi hii mikubwa, ombi la Mheshimiwa Kishimba ni zuri sana na ningeomba tu na Waziri na meza

yako mkamkubalia kwamba pengine ukiunda tume ndiyo utaujua ukweli kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mawazo anayoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri si kweli, huo urefa anaosema Kahama ukija Geita ni mara mbili au mara tatu yake na huko chini kabisa ya mara mbili/tatu kumeanza kuchimbwa *underground*. Sasa hii ya Kahama pressure gani wakati matetemeko mengi Tanzania tunajua yanatokea Bukoba na sisi tupo Bukoba lakini kwetu ametoa leseni ya chini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nilikuwa nakuomba kama unaweza, najua Marerani ulifanya vizuri, uliunda tume, hebu unda iende kule; zipo shida. Kinachosababisha watu washindwe kufanya biashara ni kwamba wamekaa na wataalam wakatengeneza vitu feki. Unakuta *helmet* inauzwa shillingi laki tatu halafu mwisho kufaa wiki mbili inakuwa *expired*, utaendeshaje mgodi? Tujifunze kwa mzee huyu tuliyemkabidhi kule *TULAWAKA* dhahabu yake leo imeshuka kutoka 1,300 mpaka 800 kwa mzungu bado ipo 1400, utapataje faida? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri kama itakupendeza wazo la Mheshimiwa Kishimba ni zuri tulifanyie kazi; na anayekaa na mgonjwa ndiyo anajua mihemmo ya mgongwa, nakushukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa kishimba, hapana, ni Mheshimiwa Waziri kwanza.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi kama ambavyo nimetangulia kusema, *interest* yetu sisi tunachobishania hapa ni kwamba mgodi ule uwe *rehabilitated* au uachwe aje mwekezaji mwengine. Sisi hatuna tatizo, kama anakuja mtu ambaye anadhani anaweza kuurithi ule mgodi lakini mwishoni aka-*rehabilitate* kurudisha mazingira kwenye hali yake ya awali, hatuna matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linalozungumzwa hapa ni kwamba hawa wlaiokuwa na huu mgodi, *mining*

closure plan yao ilikuwa na udanganyifu mwingu, walisema lile *pit* wataliacha kama *pit lake* litajaa kwa muda wa miaka 100. Bunge hili linatoa mfano kila siku kwenye mgodi ulioachwa wazi wa Nzega ambapo shimo limebaki wazi kwa vigezo kwamba hilo eneo litatumika kwa ajili ya kufanya mafunzo ya awali. Tukiingia kwenye huu mtego, tutaacha lile shimo wazi, atakuja mtu ambaye ni *cosmetically* atakuja kusema anarithi huu mgodi, atakaa pale baada ya muda atakuja kutangaza matatizo yake mengine tutaachiwa shimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja iliyopo ni kwamba huu mgodi wamechimba *cart one, cat two* na *cat three; economically viable* inaleta faida. *Cart four* ili aweze kuichimba afike kwenye ore gharama zake za kiuchumi zinampa hasara; kwa hiyo anachofanya ni nini? anasema mimi ninarudisha huu mgodi ili nikatafute shughuli nyingine ya kufanya. Sasa wakati unarudisha kwa mujibu wa sheria lazima urudishe mazingira kwenye hali yake ya mwanzo, hatusemi tunafukia dhababu. Akitokea mtu mwingine hata kama *ACACA ame-rehabilitate* akataka kupata leseni kwenye eneo hilo, *well and good* tutampa. *TULAWAKA tumefanya hivyo, mchimbaji ameondoka amekuja mtu mwingine amesema mimi naweza kupata faida na kwa kweli amechimba amepata faida na sasa tumepata gawio.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Kishimba kama yeye anaye huyo mwekezaji, kwa sababu mimi huyo mwekezaji kwanza sijawahi kumuona wala Wizarani hajawahi kuja, kama yupo aje tuzungumze halafu tutamu-*engage third part* wetu atakuwa *ACACIA* atutachukua *rehabilitation bond* alioweka ya kurudisha mazingira yale kwenye hali yake. Kwa sasa *challenge* tuliyonayo na ule mgodi ni kwamba, *rehabilitation bond* alioweka ameweka Dola za Kimarekani milioni 23; kwa hesabu zetu ku-*rehabilitate* mazingira yale ile fedha ni kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na utaratibu ule alikuwa anasema mimi nimeweka *rehabilitation bond* kwa sababu

moja, bwawa hili nataka niliache muweze kufugia samaki, lile bwawa huwezi kuliacha *pit lake* kwa sababu ujaaji wa maji yake kwa hesabu zake litajaa kwa muda wa miaka 100. Yeye arudishie, kama ana mtu anadhani naweza ku-*take over* hatuna matatizo tutafanya *arrangement* na utaratibu utakwenda, nakushukuru. (*Makofij*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kishimba tafadhalii, turahisishie kazi kidogo, naona wameongea vizuri Wizara.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naungana na Wabunge wote waliochangia kwenye hili suala zima. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina tatizo na Mheshimiwa Waziri wala Mheshimiwa Naibu Waziri, mimi tatizo langu lilikuwa ni jepesi. Hawa watu kwanza kwa nini tunakataa kwenda kuwa-*audit* wao, zile gharama wanazodai ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utanipa kama dakika mbili; tukiwa pale kwenye Mgodi wa Buzwagi tukiwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais, meneja wa mgodi ambaye ni Mswahili alisema mgodi huu tuna gharama kubwa, hawezu kusema gharama zile kwa sababu anamuogopa tajiri yake. Sasa Serikali imepata dokezo, sasa ni Serikali gani ambayo imepata dokezo kwa *general manager* yenyewe haitaki kwenda ku-*audit* gharama ambazo meneja amezieleza? Kuna *helmet* inanunuliwa shilingi 250,000 imewekewa *expire date* ya miezi 3, mgodi utatengenezaje faida? (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona kwa *Major General* Mstaifu kule *TULAWAKA* kutoka 1300 imefika gharama ya shilingi dola 800, anauza 1300, mbona imewezekana? Kwa nini sisi hili haliwezekani kwenda kuwa-*audit* hawa, kuna nini? ili tupunguze gharama na zile gharama za Serikali ambazo tunazona si za lazima kama za *TANESCO* na *TRA* wanaweza kupunguza *tariff* zao kwa muda hali hali itakapokuwa im-schedule ya bei ya dhahabu na mgodi ukaendelea na *TRA* na Serikali ikapata faida. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana, natoa hoja.

MWENYEKITI: Unarudisha shilingi!

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudisha shilingi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, nakushukuru sana. Ushauri wako ni wa maana sana, mimi naamini Serikali imesikia na Waheshimiwa Mawaziri wamesikia, ni wa kufanya kazi. Nilikuwa na-*imagine* tu hapo kwenye hela nydingi namna hiyo halafu ukishafanya hiyo *closure exercise* yote halafu sijui uthalindaje maana kila mtu hayupo, sasa hawa Wasukuma ninaowajua mimi unawazuiaje kuwa wana-*dive* huko kama kule kwa Mheshimiwa Heche wanaingia na bunduki zipo, sasa huku *closure* imeshafanya kila mtu hayupo, itakuwa vurugu mechi huko lakini Serikali wamesikia. Mawazo yote haya ni mazuri kuyafanya kazi.

Tunakuja mchangiaji mwininge Richard Ndassa.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu mwaka 2015 humu ndani, na mimi wakati huo nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, tulianzisha Taasisi ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia, inaitwa *TEITI*. Sasa majukumu yake yanajulikana lakini kwa mujibu wa taarifa; kwanza sina sababu ya kuchukua shilingi ya Mheshimiwa Waziri; ila tu nilikuwa nataka nipate maelezo kwa sababu taasisi hii majukumu yake ni kuhakikisha makampuni yanayofanya shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta, madini na gesi asilia zinaweka wazi taarifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa taasisi hii kwa mujibu wa Taarifa ya Kamati ya Nishati, inasema tangu mwaka wa fedha uliopita mpaka leo, hakuna hata senti moja iliyotolewa ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna mkaguzi alitoa maelekezo kwa taasisi ile, kwamba kulikuwa na shilingi bilioni 30.5 wazitolee ufanuzi lakini wameshindwa kufanya hivyo kwa sababu taasisi ile haijapatiwa hela za maendeleo yoyote yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri, taasisi hii ni muhimu sana tulianzisha sisi humu ndani ili ikaangalie shughuli zetu za madini kwa ujumla zimekwendaje? Sasa nataka nipate maelezo, nini hasa tatizo kwa nini taasisi hii hamuipatii pesa ilhali tulianzisha rasmi kwa ajili ya kwenda kusimamia rasilimali zetu za madini na gesi?

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa *Senator Ndassa*. Ufanuzi wa jambo hilo, Mheshimiwa Waziri tafhadhali.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Ndassa pamoja na kwamba ame-raise hoja hii, hakusudii kushika shilingi na kwa sababu ni kaka yangu, namshukuru sana, anataka twende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachofanyika kwenye kazi hiz za *TEII* ni *reconciliation* kati ya kile kilicholipwa na kampuni kwa Serikali na kile kilichopokelewa Serikalini. Kilichotokea kwenye ripoti iliyopita ni kwamba kulikuwa na tofauti ya bilioni 30 hiyo anayoisema; na sheria inasema baada ya tofauti hiyo kutokea, sasa Waziri ana wajibu wa kumuomba *CAG* aende akakague kuona je, kwenye hii tofauti imesababishwa na nini, kwa sababu tofauti nyingine unakuta tu ni kwamba huyu amepokea pesa hakuna vocha fulani au huyu ame-double entry item fulani na kwa hiyo ime-raise ile thamani ya hicho kitu, kwa hiyo ni kitu kinachofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua tulioifikia sasa hivi ni kwamba tunapeleka hili jambo kwa *CAG* ili *CAG* atutafutie *clarification* ya jambo hilo, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Sebastian Kapufi.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru; na mimi pia awali nilikuwa nimekusudia kushika shilingi lakini baada ya ufanuzi mzuri wa Mheshimiwa Waziri kwa maelezo yake kwamba masuala yote yanayogusa makinikia bado atayaangalia kwa jicho la sharia. Na amesema Mheshimiwa Waziri kwamba miyo yetu inaongea kwa sura hiyo maana yake jambo hili si kwa maana ya mimi tu lakini kwa maana ya wachimbaji wote ambao masuala yao yalikuwa yapo katika sura ile kabla ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini wakati watakapokuwa wakienda kuyaangalia masuala haya kwa jicho la kisheria watazingatia maslahi mapana ya wachimbaji wote kwa ujumla wake. Nalisema hilo kwa sababu katika kikao kile muhimu ambacho mkuu wa nchi alikaa na sisi aliendelea kusema kwamba kama kuna watu wanaonyesha nia ya kuchangia kwenye mapato mbalimbali ya Serikali, kwa nini watu hawa wasipewe nafasi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana na mimi nirudi katika hili ambalo Mheshimiwa Waziri ameongea kwa maslahi mapana ya nchi, naamini tunapozungumzia mchango wa dhahabu hiki kilichopatikana ukiwaita wachimbaji ukakaa nao bado watakwambia nchi hii ina mapato makubwa sana. kwa hiyo ni kwenda tu kujirekebisha hapo katika suala la sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, natumaini Mwanasheria Mkuu wa Serikali umemsikia Mheshimiwa Kapufi na kilio ambacho amekuwa akiki-*present*. Sasa twende kwa Mheshimiwa Musa Mbarouk.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi. Mimi nimesikiliza kwa kina maelezo ya Mheshimiwa Waziri, amezungumzia kuhusu wachimbaji wadogo, lakini ukiangalia kwenye kitabu hiki ukurasa wa 67 imeelezwa kwa kifupi sana kuendelezwa

wachimbaji wadogo; na Mheshimiwa Waziri amegusia kwamba amewashauri waanzishe vikundi. Sasa mimi ninavyojua ni kwamba wanavyo vikundi vyao/vyama nya wachimbaji wadogo, hivi wanavyoviita *Regional Miners Association*. Sasa sikusikia Waziri akisema kwamba hivi navyo kwanza wanavitambua lakini navyo watavielimisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kwamba maeneo mengi ya madini yanagunduliwa na wachimbaji wadogo, lakini mara tu madini yanapoanza kupatikana basi wanabadilishwa jina wachimbaji wale na kuitwa wavamizi, majangili na kupelekewa vyombo nya usalama na kuondolewa. Sasa nataka Mheshimiwa Waziri anifafanulie, pamoja na hii aliyosema kwamba watawatafutia maeneo, watawapa elimu lakini mimi naona haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vyama vyao ambavyo wamevianzisha, mna mkakati gani sasa kwa sababu hawa wenye vyama ndiyo wanaowajua wale wachimbaji mmoja mmoja, wana mkakati gani sasa wa kuanza kuwaelimisha kwa kuwapa elimu ya hali ya juu kuhusiana na suala la madini lakini pia kuwatafutia hata mikopo ya vifaa nya kisasa nya kuchimbia lakini kubwa zaidi kuwapatia hata mitaji kwa maana ya Serikali kuzungumza na taasisi za fedha kuwawekea wachimbaji wadogo masharti nafuu ili waweze kuijendeleza kwa shughuli zao. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri anipe ufanuzi...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Asante sana, pale Tanga Mjini una wachimbaji wowote pale?

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Tanga Mjini tunao, wachimbaji wanaishi mjini wanakwenda kuchimba maeneo ya porini...

MWENYEKITI: Ufafanuzi Mheshimiwa Waziri, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Mussa Mbarouk asiendelee kutushikia shilingi wala nini kwa sababu Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri sana katika hotuba yake na wakati anamalizia hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tuna mikakati mikubwa sana kwa wachimbaji wadogo hasa katika kuhakikisha kwanza tunahakikisha tunawafanya tafiti za kutosha, tafiti ambazo zitawaondoa katika uchimbaji wa kubahatisha. Tuwape maeneo ambayo watakuwa na uhakika wa kupata madini, wachimbe waweze kupata faida, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tunawaweka kwenye makundi. Kwa kuwaunganisha kwenye makundi itakuwa ni rahisi, yaani tutawapa leseni wamiliki maeneo ya uchimbaji na ikiwezekana tuwatafutie maeneo mazuri. Mheshimiwa Waziri amekwisha toa *default notice* kwa wale wote ambao wana maeneo wanayamiliki hawayafanyii kazi, wale wenye leseni lakini bado vilevile kuna watu wana leseni za utafiti wamemiliki maeneo makubwa, mchimbaji mdogo akiomba kuititia *cadaster portal*, ule mtandao wetu wa kuombea leseni, unakuta maeneo yale yanamilikiwa na watu ambao wanafanya tafiti mbalimbali. Sasa hivi tumefuta hizo leseni za utafiti na kuhakikisha kwamba tunawapa wachimbaji wadogo waweze kuchimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto ya mitaji kwa wachimbaji wadogo. Wachimbaji wadogo tukiwafanya tafiti na kwa kuititia *STAMICO* tayari Mheshimiwa Waziri ameshazungumza, tumekwishakununua *rig machine* kwa ajili ya kufanya tafiti mbalimbali katika maeneo mbalimbali. Tukishafanya tafiti tutakuwa na uhakika wa *deposits* za yale madini ambayo yapo maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukishakuwa na uhakika wa taarifa hizo ni rahisi sana kwa taasisi za fedha kuweza kutoa

mikopo, hapo tutakuwa tumeweza kutatua changamoto ya mitaji. Kwa sababu wachimbaji wengi wadogo wanakosa vifaa, wanakosa taarifa, wanakosa utaalam wa uchimbaji salama. Hizi zote ni changamoto ambazo tunaziona, tumezunguka kwa wachimbaji wadogo wengi tumeona. Kwa kweli tunaendelea na mikakati mizuri kuhakikisha kwamba wachimbaji wadogo nao wanakuwa na sifa ya kuweza kukopeshwa na benki au hizi *financial institutes*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sasa hivi ukienda benki mchimbaji mdogo hawesi kupewa mtaji kwa sababu uchimbaji wake ni wa kubahatisha. Kwa hiyo tunataka hizi benki tutafute namna ya kuzipa taarifa ambazo zitakuwa na uaminifu kwa wachimbaji hawa kuwapa mikopo na wanakuwa na uhakika kwamba watakapochimba wataweza kulipa mikopo ile. Kwa kweli niseme tu kwamba kwa kipindi chote toka tumeshika Wizara hii ya Madini wachimbaji wadogo mpaka sasa hivi wanafurahi sana kuona namna gani tunawasaidia na kuwasimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna suala la ruzuku; ruzuku zilikuwa zinatolewa katika ule mradi wa *SMMRP* ambaao ulikuwa *financed* na *World Bank*, watu walikuwa wanapewa fedha, tulikuta kuna watu wameweza kuwapa fedha wachimbaji wadogo wengine hata sifa hawana, mwengine hata shimo, hata suluhu hana, lakini kapewa fedha millioni mia na kuendelea. Programu hiyo tumeisimamisha, sasa hivi tunaangalia namna bora ya kuwasaidia wachimbaji wadogo kuititia programu ile kuweza kugharamia tafiti mbalimbali na kuwapa maeneo waweze kuchimba. Hata hivyo, wale watu ambaao walipewa mikopo wengine mpaka sasa hivi wana kesi mahakamani na tunawadai fedha hiso wazirudishe ili ziweze kusaidia wachimbaji wengine wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nimwombe Mheshimiwa asitushikie shilingi, atupe shilingi yetu tukafanye kazi.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Labda niseme tu, si nia yangu kushika shilingi lakini

nina ushauri kidogo naomba wauzingatie Waheshimiwa Mawaziri kwa sababu sote tunajenga nyumba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewahi kuchimba madini miaka ya nyuma sana, najua adha, tabu na matatizo yanayowakuta wachimbaji na ndiyo maana leo najaribu kulizingumzia ili angalau na wao wawe na pa kuanzia. Sasa nishauri tu; pamoja na mikakati waliyokuwa nayo lakini isiwe mikakati ya kwamba wanaturidhisha tu kwa maelezo haya mafupi kwenye kitabu ili tupitishe bajeti waende wakafanye kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, twaomba wawe wakweli, wawasimamie wachimbaji wadogo kwa sababu Watanzania miaka nenda miaka rudi ni maskini hali ya kuwa madini yale yangetunufaisha sisi. Tuna madini ya aina nyingi, siyo dhahabu peke yake, tuna *red garnet*, tuna *green tourmaline*, tuna *sapphire* hiyo *blue, white, pink* na kadhalika, lakini ukintazama mchimbaji wa Tanzania ni maskini hohehahe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachowashauri Mawaziri wawasimamie, wawasaidie na hili la kupata mikopo kwa masharti nafuu iwe ndiyo kigezo namba moja. Namba mbili kama watu wana maeneo basi wanapokuja wawekezaji, huyu mchimbaji mdogo mtaji wake aingie ubia na yule mchimbaji mkubwa mwekezaji, mtaji wake uwe ni ardhi, yule mchimbaji mkubwa awe mtaji wake ni fedha na mitambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mussa Mbarouk. Ila ulipokuwa ukichangia badala ya kuwaangalia Waheshimiwa Mawaziri unamwangalia Mheshimiwa Ummy; kuna nini? (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Salome Makamba.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Dada yangu.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba niseme kabisa kama sitaridhishwa na majibu ya Mheshimiwa Waziri, basi nitashika shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Nchi ya Mazingira, Sera yetu ya Madini lakini pia Sera ya Uwekezaji inasisitiza *very clearly* kwamba usalama wa watu na mazingira unakuja kwanza. Tumeshuhudia, hata wewe katika Bunge lako hili Tukufu; Wabunge wengi wamekuwa wakilia kuhusu wawekezaji wa migodi, migodi mingi kuwa na madhara makubwa kwa mazingira na wananchi. Bunge lako hili Tukufu kwa kuona uzito wa jambo hilo liliwahi kuunda tume mbili na tume moja ilikuwa ya kwako wewe mwenyewe, tume nyininge ilikuwa Tume ya Mheshimiwa Lembeli, wakaenda kuchunguza ni kwa nini wananchi wanalamika kuathirika na uwepo wa migodi jirani yao katika maeneo yao, ikaenda mbali ikatoa mapendekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgodi wa Buzwagi wananchi wanalamika kwa sababu ya tetemeko linalotokana na migodi, wanalamika kutokana na kelele zinazotokana na migodi. *North Mara* Mheshimiwa Waziri amekiri hapa kwamba ni kweli mwekezaji alipatikana na hatia na wamewatoza faini ambayo mwisho wa siku imekwenda kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Geita, mjomba wangu, Mheshimiwa Musukuma pale amelalamika wananchi wanalamika na madhara ya kimazingira yanayotokana na mgodi. Naomba kauli ya Serikali; ni lini itafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa na Bunge lako Tukufu na ni lini itashughulikia malalamiko ya kimazingira, malalamiko yanayosababishwa na uwepo wa migodi? Hasa ikizingatiwa leo tunazungumzia kufungwa kwa baadhi ya migodi, yako kwenye *closure plan*; ni lini Serikali hii itakwenda kushughulika na matatizo yale *to the satisfaction* ya wananchi wanaozunguka migodi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Swali lako limekuwa *general* mno; Mheshimiwa Waziri tafadhali.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Makamba; niseme tu kwamba naona anachokisema ndiyo hiki tunachokifanya kwa sasa, tunachukua hatua mahali popote tunapokuta pana changamoto za kimazingira na usalama wa watu, tunachukua hatua. Hatua tunazochukua siyo hatua nyepesi kwa kiwango hicho, iko migodi tumeifunga kabisa, katika vitu ambavyo hatupendi Wizara ya Madini kufanya ni kufunga; tumekwenda kule Mangae tumeifunga migodi; tumekwenda Mahenge tumeifunga migodi; tumekwenda mahali pengi tunafunga, kwa sababu hiyo hiyo ya kulinda usalama na uhai wa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa *case* ya *North Mara* nimeeleza hapa ni jambo ambalo limekuwa likibishaniwa kwa muda mrefu, walau tumeifika hatua sisi tumepata hoja za kisheria za kuchukua hatua. Hatua ya mwanzo ni kupiga faini na faini tuliyopiga ni faini kubwa sana; bilioni 5.6, siyo pesa kidogo. Baada ya hapo tumewapa muda wa kufanya marekebisho kwa sababu humpi mtu faini tu ukamwambia nakupiga faini basi, unampa mtu faini kwa maana ya adhabu, unampa muda fulani wa kurekebisha hiyo kasoro asiporekebisha hiyo kasoro hatua inayofuata unawenza ukafunga mgodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nisingependa niingie kwenye mtego wa kusema hatua inayofuata wakati huyu *third party* hajatekeleza hiki ambacho ameshapewa. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mjumbe kwamba tunachukua hatua kali na naomba nimhakikishie kwamba wachimbaji; wawe wadogo, wa kati au wakubwa, wote wakiathiri mazingira tunachukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Buhemba leo ninavyozungumza wachimbaji wadogo zaidi ya 5,000 mgodi ule umesimama kwa sababu ya hatarisho la kimazingira. Nadhani Mheshimiwa Mbunge akubali twende mbele, atupe

nafasi tufanye kazi. Hili jambo tunahitaji kutiana moyo lakini muhimu sana kushauriana kama alivyoshauri, tutafanya kazi. Ninavyomwangalia sidhani kama ana dalili ya kuchukua shilingi, naomba tuendelee na hatua inayofuata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Nakushukuru. Nilifikiri... bado unamshikia shilingi kaka yako? Hawa Wasukuma wana matatizo kweli hawa; ehee, endelea Mheshimiwa Salome.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri asijisifie kwa kufunga migodi, kwa sababu kwa kufanya hivyo tu unakwenda kinyume na Sera ya Uwekezaji hapa Tanzania. Hoja yangu, hivi anajua kwamba kule Mwimbe, Mwakiryo, Mwazimba watu mpaka leo bado wanatumia *mercury* kuchenjua dhahabu na ina athari kubwa ya kimazingira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja Wajumbe wenzangu wanisaidie kumshauri Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja.

MWENYEKITI: Ni hoja ya nini sasa?

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi na ninaomba nitoe hoja Wajumbe wenzangu wanisaidie kuifahamisha Serikali kwamba athari ya mazingira na watu wanaoathirika kwa uwepo wa wawekezaji bado ni jukumu la Serikali na Serikali haijachukua hatua yoyote madhubuti katika kukabiliana na hii changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MHE. CATHERINE N. RUGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Iko vague kweli hii, lakini basi haya Katibu andika majina.

Haya, tuanze na mwathirika namba moja Mheshimiwa Heche.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kama alivyosema ndugu na rafiki yangu, Mheshimiwa Doto, ni kweli ni rafiki yangu na siyo kwamba sijatambua juhudhi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nazungumza wananchi wangu wamekufa tangia mwaka 2009, ng'ombe wamekufa, *I can mention them by names*, majina ya watu, ng'ombe waliokufa na mbuzi, ardhi imeharibika, eneo la Kwimange zima, Mheshimiwa Doto aliona, eneo kubwa unaweza kuangalia hapa mpaka kule stendi, eneo limeachwa wazi, Kwimange, Kwinyunyi na Mheshimiwa Doto tulikuwa naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo anaponiambia Serikali imechukua faini kwamba ndiyo mwisho wa hatua hizo mimi sielewi, sitaki kuelewa hilo, ninachotaka ni Waziri aniambie ni jinsi gani wananchi ambao wameathirika, akina mzee Ryoba Irondo, wanafidiwaje ng'ombe wao, wanafidiwaje maisha yao. Kuna watu wamebabuka wako pale, Waziri anajua, kuna mama amekwenda mpaka kwa Mheshimiwa Rais kuhusiana na hili tukio na mtoto wake wa miaka miwili alifariki, *he knows that*, tulikuwa na yeye pale Nyamongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa anapo jibu kwamba tumepiga faini, faini kupiga ni Serikali kukiri yale tuliyoyasema tangu mwaka 2009 kwamba kuna maji ya sumu. Sasa hatua za wananchi kufidiwa haziwezi kuja kufidiwa na Serikali baada ya kufidiwa Serikali, tunataka Waziri atoe kauli kuhusiana na mgodi kulipa fidia wananchi. Ndiyo hoja ninayozungumza hapo. (*Makofu*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sijui hali ya sasa, lakini kama mlivyosema niliwahi kuongoza Kamati enzi hizo iliyokwenda *North Mara*, tukafuatilia suala hili kwa sababu Kamati yetu ilikuwa ya mazingira, ya uchafuzi wa Mto Tigite, tulikuwa na Mheshimiwa Nsanzugwanko, mtakumbuka.

Moja ya *findings* zetu, wakati huo, sijui sasa, ilikuwa ni kwamba pamoja na uchafuzi wa mgodi ambaao ulikuwa na *controls* fulani za mabwawa na kadhalika lakini kulikuwa na kuvuja kwa aina fulani, lakini palikuwa na tatizo la pili ambalo wananchi wenyewe walikuwa na uchimbaji mdogo mdogo ambaao ulikuwa ukiendelea na wale wachimbaji wadogowadogo waliokuwa wakichimba katika maeneo yale wao walikuwa wanachenjua kwa *mercury* na kwa hiyo ule mwamba wa *North Mara* ulivyo na ile *mercury* inayotumika nayo ikawa ni sehemu kubwa sana ya *pollution* kwa mtu wa Tigite na kuji-*pollute* wenyewe. Sasa, ndiyo, unampiga faini huyu mwekezaji mkuu na hawa wengine sasa wapiga kura wa Mheshimiwa Heche ambaao nao wanachafua mazingira? (*Makof!*)

Mheshimiwa Dkt. Sware ulisimama.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeongea vizuri sana; hapa tunaangalia *end users*, wale walioathirika na yanayotoka mgodini. Serikali inaongelea kuwapa faini wale wachafuzi wa mazingira, je hawa waathirika wa mazingira wanachukuliwaje na Serikali? Ndilo swalii la msingi hapa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara yanayotokana na migodi madhara yake ni miaka mia na zaidi katika wanyama na katika binadamu na mazingira yenyewe. Sasa *commitment* ya Serikali ni nini katika sekta hii, kwamba tayari uchafuzi umeshafanywa, wale wananchi wanafidiwaje? Matibabu yanafidiwaje? Nafikiri hapo ndiyo tunatakiwa tutoke; *commitment* ya Serikali ikoje, siyo kumpa faini, fani

mimi bado tayari nimepata madhara sasa tunatokaje hapa, ndiyo swali la msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Umetuwekeea vizuri sana Mheshimiwa Dkt. Sware, ni mjadala na ni mjadala muhimu sana. Kuna wengine tupo Dodoma tumekula sato wa kutoka kule tumeathirika, sasa *surveyitakayofanyika* ya walioathirika kwa ujumla wake hiyo *surveyyake inafanananje*, yaani hiyo sayansi yake, labda Mheshimiwa Profesa Ndalichako anaweza kutuambia, maana yake ni pana sana, yaani ni pana. (*Makofi/Kicheko*)

Tunaendelea, nilikuona Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana. Namwomba mjomba wangu, Mheshimiwa Salome, amrudishie Mheshimiwa Waziri shilingi yake kwa sababu kiukweli wakati anachangia nimeshindwa kumwelewa. Wakati hoja ya Mheshimiwa mzee Kishimba inazungumwa kwa maana hiyohiyo alisimama akachangia akasema kufungwa kwa ule mgodi wa Buzwagi ni kutohana na mahusiano kati ya Serikali na mgodi, sasa hivi tena anasema mazingira. Sasa nimeshindwa kuelewa hoja ya msingi, pengine namwomba mjomba ajipange ili kipindi kijacho aweze kuweka hoja yake vizuri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Nami niungane na Mheshimiwa Waziri, ametoa maeleo mazuri sana ambayo nilitarajia dada yangu, Mheshimiwa Salome, atawezza kuyachukua. Hata hivyo, *commitment* ya Serikali ambayo Waziri wa Madini ameielezea sisi Wizara yetu ya Mazingira ndio tuliounda tume kwenda *North Mara* na imefanya kazi kubwa sana na matokeo ya tume hiyo ndiyo matokeo hayo tumehakikisha kutoa maelekezo kwenye migodi mingine yoyote na tunafanya *auditing* ya kila mwezi. Sasa sijajua hapa tunataka tufanye kitu gani kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwombe dada yangu; sisi kwenye Wizara ya Mazingira tunawajibika moja kwa moja kuhakikisha kwamba tunafanya *environmental auditing* ya haya mazingira yote na kuyaweka sawa...

MWENYEKITI: Yeye anataka walioathiriwa wapate fidia.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anachokihitaji na Mheshimiwa Waziri ameshaeleza. Katika suala ambalo *North Mara* pale tayari wameshatoza faini ya bilioni tano lakini bado Serikali inawajibika kuhakikisha hawa watu ambao wameathirika inawasimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana nani hajaongea leo. Mheshimiwa Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Nakumbuka Bunge lilitopita nilikuwa kwenye Kamati ya Mheshimiwa Lembeli na kama Kamati tulikwenda na tuliona jinsi ambavyo watu wengine walathirika moja kwa moja. Wananchi walikuwa wanatia huruma na kuna mapendekezo ambayo tulitoa Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nadhani hoja anyoongea Mheshimiwa Salome ni hoja ambayo iko wazi; ni kweli Serikali imechukua juhudhi lakini kuna watu ambao wameathirika moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa ni Serikali ya ajabu sana kuwaacha hawa watu walioathirika moja kwa moja wamepata maumivu, mifugo yao imekufa, wenyewe wameugua wengine wamekufa na wengine mpaka mimba zilitoka, halafu Serikali inyamaze. Ni wajibu wa Serikali kulinda raia na mali zao kwa hiyo ni wajibu wa Wizara kuji-comit ni namna gani itakwenda kuwafidia watu. Kuna watu waliorodheshwa majina... (*Makofii*)

MWENYEKITI: Unawezaje kutofautisha kati ya walioathirika moja kwa moja; mimba kutoka na ng'ombe, kutokana na uchimbaji mdogomdogo na kutokana na uchimbaji mkubwa; *how can you separate the two?*

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kitendo cha Serikali kupiga faini maana yake Serikali imethibitisha kwamba mgodi umeleta taabu. Kama vile haitoshi, kuna watu ambao wana majina moja kwa moja. Kama sisi watu wa Iringa tulikuwa hao samaki hatukujiorodhesha, wapo watu ambao wako kwenye eneo lile ambao waliathirika moja kwa moja na majina yao yapo, wanajulikana. Serikali haiwezi kukwepa mzigo huu. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mwisho Mheshimiwa Peneza.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama utakumbuka kwa kipindi cha nyuma kidogo tulikuwa na mabishano na watu waliokuwa wanaunga mkono magwangala na uzuri Serikali ikayazuia kwa sababu tungekuwa tunajadili madhara ya watu kufa kwa namna hii kwa sababu ya hizo sumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, sisi kwa kule Geita shida ni kwamba *commitment* ya Serikali kushughulikia matatizo ya wananchi kwa haraka pale yanapokuwa yametokea. Kama mfano katika maeneo ya Katongo na huko *Compound* kwa sisi kule Geita tumelalamika kwa muda mrefu kuhusu mgodi kufanya ulipuzi; wanawake mimba zimetoka, watu wamezimia, watu wamekufa kutokana na shughuli za mgodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelalamika muda mrefu mgodi anajitetea kwa namna yake, Waziri, Mheshimiwa Dkt. Kalemani, alikuja, wamekuja Mawaziri mbalimbali wanatoa maagizo, mgodi kesho yake wanaambiwa elekezeni huku wanafanya kilekile kesho yake asubuhi, madhara yaleyale. Yaani kile walichoambiwa wasifanye na Naibu Waziri, kile walichoambiwa wasifanye na Waziri ndicho kitu wanachokifanya kesho yake. Kwa hiyo maana yake ni kana

kwamba wao sasa wana mamlaka zaidi hata kuliko Serikali yenyewe inayoongoza wananchi wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na leo tukiwa pale nje nimeongea na watu GGM kule wamefanya uthamini wa wananchi kwa sababu nyumba zao zimepasuka anasema kwamba sisi tutalipa mipasuko tu yaani kile ule jinsi ukuta ulivyoachia ule ile ndiyo thamani... watu nyumba zao zimebomoka lakini wanalipwa fidia ufa. Siyo mambo mazuri

MWENYEKITI: Ahsante sana Kengele imeshalia naelekeea kwa Mheshimiwa Waziri lakini kabla Mheshimiwa Waziri hajasimama, nilikuwa nawaza kwa upana wake kwa sababu Serikalini kuna kitu kinaitwa *precedence*. Kwa mfano kuna hili tangazo la Serikali zuri sana la kuzuia mifuko ya plastic kuanzia tarehe moja mwezi ujao ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu allitufahamisha siku ya hotuba yake ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Sasa sisi hapa Dodoma mifugo yetu mingi sana imekufa kwa sababu ya kula mifuko ya *plastic* wakishalipwa hawa na sisi tutaidai Serikali mifugo yetu kwa kweli, ng'ombe wamekufa sana jamani. (*Kicheko/Makofi*)

Hata mimi zizini kwangu zaidi ya ng'ombe 10 wamekufa *plastic*. Kwa hiyo, majibu yako Waziri mazuri itatusaidia na sisi wengine tujipange vizuri kuidai Serikali. Mheshimiwa Waziri tafadhalii

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru lakini kabla sijajibu nilitamani sana niweke jambo hili vizuri na kwa sababu tunazungumza mbele ya watu wengi wanaskia isije ikachukuliwa hivyo kwamba, Wizara ya Madini tunajisifia kufunga Migodi. Nilikuwa najaribu kuonyesha ukubwa wa hatua tunazochukua, kwa sababu hatua ya juu ni kufunga mgodi na kama Mheshimiwa Mbunge anasema kwamba sasa tutakuwa tunaumiza uwekezaji huo uwekezaji huo huo ambaa unagharimu maisha ya watu kwetu sisi tunaona kwa kweli siyo sawa. Kwa hiyo aelewe tu kwamba tumetoa hiyo mifano kwa maana ya kwamba hatua ya juu kabisa pamoja na kupiga faini tunaweza tukafunga migodi na nikatoa huo mfano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo jingine nilichozungumza hapa na kama Mheshimiwa Heche alikuwa ananisikiliza na Mheshimiwa Salome alikuwa ananisikiliza hayo wanayoyazungumza niliyaeleza hapa nikasema hatua za kuchukua kwa mujibu wa sheria huamki tu asubuhi ukasema nafanya hivi kuna hatua za kuchukua hatua ya kwanza unampa mtu *order* ambayo wametoa watu wa NEMC, unapiga faini unampa muda wa kufanya marekebisho kama kuna malalamiko ya watu walioathirika yakaja hayo malalamiko unayachukua unakwenda tena kufanya tathmini ya kuona watu wameathirika kwa kiasi gani na una-*quantify* hizo athari maana yake ni kiasi gani cha fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko tutafika jambo la msingi ni kwamba tunazungumza *public* hapa kuna mambo mengine *internally* tunaya-*manage* tutakuwa tunatoa *advantage* kwa upande mwengine kuchukua hatua au kufanya *manipulation*. Nitampa mfano Mheshimiwa Heche tumesema awamu namba 47 irudiwe kufanyiwa uthamini *clearly* kabisa nia ni kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wametokea watu mle ndani wanazunguka wanawa-*lobby* wale wananchi kuna wananchi leo ninavyozungumza pale Nyamongo wamechukua hela kwa tathmini tuliyokataa kwamba wananchi wamepunjwa. Sasa tukiwa tunasema kila kitu hapa itafika mahali watu tutawapa nafasi ya ku-*manipulate procedure* tulizonazo na mwisho wa siku tutafeli kama nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Heche *to be specific* namtoa hoja Mheshimiwa Makamba Serikali raha yake ni kuona watu wake wanafuraha, Serikali raha yake ni kuona watu wanaishi maisha salama hakuna Serikali itakayofurahia wananchi kuumia, kufa ama kupata madhara mimi nimekwenda nimeona Heche tulifanya mkutano maneno anayoyasema ndiyo niliyasema kwenye mkutano kwamba haya maeneo yote yaliyoathirika lazima Serikali tuje na utaratibu na wewe ACCACIA tujua hawa wananchi wana fanywaje? Sasa mnataka mnataka nifanyeje siwezi kusema walipwe shilingi

mia leo nataka nikuhakikishie kwamba tunachukua hatua kama ambavyo tumekwisha kuzungumza. Nakushukuru. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Haya Salome rudisha shilingi kwa mjomba ako sasa.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namuelewa sana Mheshimiwa Waziri lakini tunaongelea kuhusu watu, faini anayoisema najiuliza hivi Serikali iko *busy inafanya nini?* Kama wameathirika tumezimeenda zimethibitisha watu wameathirika sasa hivi ni 10 years kutoka 2009 mpaka 2019 anasema anasubiri kwenda kufanya uthamini hivi hao watu wataendelea kuwepo kweli pale Mwendakulima Kahama Mgodi wa Buzuagi watu wanalamika nyumba zimepasuka tangu mgodi umekuwa pale mimi nimefanya kazi kwenye Mgodi wa Buzuagi ni *declare interest* nyumba zimepasuka watu wanataka walipwe fidia mgodi unafanya tathmini kwa viwango vyatimataifa unasema kwa viwango vyatimataifa hakuna madhara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizara inatakiwa iende kufanya tathmini kwa kuiwango cha nyumba za Tanzanai ndio tunachokisema hapa ilete ripoti yake kwamba kwa kiwango cha ujenzi na utaalam wa Tanzania umbali huu nyumba zinaweza zokapasuka wale watu wapewe fidia. Sasa *it takes a decade to do that a decade* watu wataishije ungekuwa ni wewe Mheshimiwa Waziri nyumba yako imepasuka inaufa unalamika unakuja kujibiwa kwamba Serikali inafanya tathmini miaka tisa ili kuja kuja ku-repair nyumba yako miaka 10.

MWENYEKITI: Sasa Dotto hajakuwepo miaka 10 ana mwaka tu

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iko muda mrefu iko muda mrefu ninachotaka niseme Serikali inatakiwa kuwajibika kwa wananchi wake, Serikali inatakiwa iwajibike kwenye mazingira yake iunde Tume

yenewe, itoe taarifa ndiyo kazi yake kuwasimamia wawekezaji na siyo kusubiri mwekezaji atoe ripoti kwa kiwango anachokitaka yeye ndiyo hicho ninachokisema ninachokisisitiza. Hapa kwa ruhusa yako mimi niko kwa niaba ya wananchi wa Tanzania naomba nikuruhusu uwaruhusu wajumbe wapige kura Serikali miaka 10 inasubiri kupata taarifa uhakiki kwa ajili ya...

MWENYEKITI: Kura ya nini sasa

MHE. SALOME W. MAKAMBA: ipige kura Serikali kuilazimisha Serikali iweze kuwajibika kusimamia usalama wa watu wake kwenye maeneo ya wawekezaji na usalama wa mazingira hasa wawekezaji wa migodi. Ahsante mwenyekiti.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Haya wanaoilazimisha Serikali, wanaomuunga mkono Mheshimiwa Salome waseme ndiyo, ambao hawakubaliani na hoja hiyo ya kulazimisha waseme siyo, Mheshimiwa Jacqueline Msongozi

(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mimi napenda nipate ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kumekuwa na suala la ucheleweshaji wa leseni kwa wachimbaji wadogo, wakati na wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inataka kufanya mageuzi makubwa sana katika sekta ya madini lakini pia tumekuwa tukitafuta wawekezaji usiku na mchana ili waweze kuwekeza kwenye sekta ya madini lakini tatizo limekuwa ni leseni. Sasa sijui kwamba tatizo hili la ucheleweshaji wa leseni linatokana na sera au na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka mchakato wa kwenda kukata risiti ya leseni inachukua zaidi ya miezi mitatu na baada ya mchimbaji kukata risiti inachukua tena miezi

mitano zaidi ili aweze kupata leseni sasa hili jambo limekuwa likirudisha sana maendeleo hayo katika sekta ya madini kiasi ambacho sasa mchimbaji anakaa na leseni anatembea nayo miezi sita inafika mahali sasa wale wachimbaji wanashindwa kuvumilia kwa mfano wachimbaji wadogo wadogo wanajikuta kwamba wanaenda kuvamia kwenye maeneo ya madini. Kwa hiyo, sasa mimi nilikuwa nataka nipate ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ni kwanini kumekuwa na ucheleweshaji wa leseni hizi za uchimbaji wa madini na kama sitapata maelezo mazuri ninakusudia kuondoa shilingi. Ahsante

MWENYEKITI: Uchelewefu wa leseni Mheshimiwa Naibu Waziri ufanuzi tafadhali

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Msongozi kwa hiyo hoja yake alioitoa ni kweli baada ya kufanya mabadiliko ya sheria ya madini ya mwaka 2010 na marekebisho tuliyoyafanya mwaka 2017 mamlaka ilikuwa ikitoa leseni ilibadilika na kuanzia sasa ni kwamba leseni hizo zinatolewa na Tume ya Madini. Ni kweli Tume ya Madini baada ya sheria kubadilika Tume ya Madini ilikuwa inatakiwa ianze kazi zake rasmi baada ya kuteuliwa Mwenyekiti wa Tume hiyo ya Madini. Kwa kipindi hicho tulikaa zaidi ya mwaka mmoja na ushee tukisubiri kupatikana kwa Mwenyekiti wa tume ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Mwenyekiti kuteuliwa na Mheshimiwa Rais Prof. Kikula tukaanza kutoa leseni kuitia Tume hii ya Madini, na leseni ndogo ambazo tunazitoa kwa maana ya PMLS tunazitoa na sasa hivi tumetoa leseni zaidi ya 12,000. Lakini vilevile kuna leseni ambazo tunazitoa katika ngazi ya tume yaani *mining license* tumekwisha kutoa leseni zaidi ya 5,000 na sasa hivi vile vile tunasubiri leseni kama mbili au tatu ambazo kwa mujibu wa sheria zinatolewa na Baraza la Mawaziri yaani *special mining license*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nimuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu zikifatwa kuitia ule

utaratibu wa *system* yetu ya *internet* yaani *portal cadastro* ambao iko katika Tume ya madini ambayo inatoa nafasi kwa mtu ambaye *ana-apply* leseni *aki-apply* leseni yake na akapewa ile *invoice* kulipia mara moja nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi tunakwenda kutoa kwa haraka sana leseni hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika Tume ya Madini kuna vile vikao ambavyo vinapitisha upitishaji wa leseni yaani zile *technical committee*, sasa hivi mwanzo zilikuwa zinakaa kila baada ya mwezi zinakaa mara moja sasa hivi tumeweke utaratibu watakuwa wanakaa zaidi ya mara moja yaani kwa maana ya mara mbili kwa mwezi kuona namna gani kuweza kuzitoa leseni hizo kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tatizo hilo kweli lilikuwepo lakini kwa mlakakati tullyonayo ndani ya Wizara na Tume ya Madini tunakwenda kutoa leseni hizo kwa haraka sana. Kwa hiyo, tumuombe tu Mheshimiwa dada angu Mheshimiwa Msongozi atuachie tu shilingi yetu tuendelee kufanya kazi tutampa ushirikiano wa kutosha.

MWENYEKITI:kabla sijarudi kwa Mheshimiwa Msongozi kama Mheshimiwa Naibu Waziri unaweza ukaunganisha na hoja ya Mheshimiwa Catherine alisema asubuhi kuhusiana na leseni kutolewa kwenye *source* moja peke yake, kama nilikuelewa Mheshimiwa Catherine kama lina ufanuzi kidogo kama linatolewa Katibu peke yake ndiye anayetoa akawa anasema kwamba...

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana alichokizungumza Mheshimiwa Catherine Magige ilikuwa ni suala la *export permit* kweli baada ya mabadiliko ya sheria, mtendaji pekee wa tume ya madini ndiyo anayesaini *export permit* ya madini yote nchini ndivyo sheria ilikuwa inasema na huyu alikuwa ame-base Dodoma peke yake. Sasa hivi nikueleze tu ni kwamba hilo tatizo tumeliona na hapa mpaka sasa hivi tunavyozungumza tumeshateua watu 12 ambao watakuwa wanatoa vibali vya *ku-export* na watu hao leo wanapata barua na wako hapa

Dodoma na kufikia Ijumaa ya wiki hii tutakuwa na watu zaidi ya 12 ambao wanasantini *export permit* kwa hiyo, tatizo hili linakwenda kwisha. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Msongozi kwa dakika mbili tu.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuwa maelezo ya Naibu Waziri yamelenga kusimamia tatizo hili na mwisho wa siku liweze kutatuliwa. Na kwa kuwa ni bajeti ya kwanza kabisa ya Mheshimiwa Waziri Dotto Biteko, basi niseme tu kwamba wacha tuwaache hawa vijana wakajipange vizuri na tunaimani nao kwamba watakwenda kutatua hili tatizo na litakuja sasa leseni hazitatolewa kwa muda mrefu kiasi hicho maana yake litatolewa kwa muda mfupi sana ili wawekezaji wa madini waweze kufanya uwekezaji wenye tija kwenye maeneo hayo. Ahsante sana

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa dakika moja Mheshimiwa Bashe.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nikuombe si hoja ya Mheshimiwa Jacqueline, nilitaka tu nikuombe mwongozo.

MWENYEKITI: Nimekuruhusu.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nikuombe mwongozo wako, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara wakati anachangia kuhitimisha hoja ya Waziri wa Viwanda na Biashara kuhusu hoja ya *TANCOL*. Waziri wa Viwanda na Biashara ameellezea *inefficiency* ya *TANCOL* akii-connect na mkandarasi anayeitwa *CASPIAN*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni-declare *interest* nina-interest ndani ya *CASPIAN*, lakini Bunge limepotoshwa. Ufisadi ulioko *TANCOL* ambaye *partner* wa Serikali anayeitwa *Intra energy* kwa ripoti ya *CAG* ya mwaka 2017 ndiyo iliyokuwa hoja mbele yetu Wabunge ikionyesha namna gani ameli-

patriot fedha bila idhini ya Bodi kupeleka Malawi; ikionesha ni namna gani ameli-*patriot* fedha kwa kudanganya kwa ajili ya *CSR*; akionesha ni namna gani Serikali imeibiwa *over 8 hundred billion shillings* na wakati anaituhumu Kampuni ya *CASPIAN* haikuwa mkandarasi wa *TANCOL* wakati huo; hoja iliyokuwepo ni ujisadi uliofanyika katika mwaka 2005 mpaka 2007 hii ndiyo iliyokuwa hoja mbele ya ripoti ya CAG.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *above all that* ujisadi uliofanywa na *Intra energy* ambao unaonyeshwa kwenye *stock exchange* ya Australia juu ya wizi anaofanya huku kuonesha miradi yake anayoifanya katika nchi ya Malawi bila kuwahusisha watu wa *NDC* hii ndiyo ilikuwa hoja, lakini Waziri kahamisha hoja kaipeleka kwa *local company* kuionyesha kwamba ndiyo *victim* na ndiye aliyesababisha ujisadi huo, ujisadi huu umefanywa na *Intraenergy* na ripoti ya CAG. Hii ndiyo ilikuwa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka tu mwongozo wako Waziri alivyoamua kulipotosha Bunge kutokana na hoja iliyokuwa mbele yetu, nashukuru.

MWENYEKITI: Tunachukua hilo jambo tutalifanyia baada ya *consultations* na *Chief Whip* tutaona namna gani na nini cha kufanya kwa sababu ya muda wetu ulivyo mkiangalia pale muda uko mdogo sana. Natamani nikupe nafasi Mheshimiwa dakika moja? Haya Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru Mheshimiwa Mbunge kwa mchango wake kimsingi niseme kwamba pengine hakunisikia vizuri.

Suala nililozungumza ni kwamba pamoja na hayo yaliyochangiwa na Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna hizo changamoto au matatizo makubwa yaliyozungumzwa nimesema kwamba tayari Wizara ilishaunda Kamati na imefanya kazi na siku yoyote tutaweza hata kuwapa taarifa

ya maendeleo ya masuala hayo jinsi ambavyo Mheshimiwa CAG alikuwa ameshauri.

Kuhusu *CASPIAN* nilisema kwamba pamoja na hayo kampuni ilikuwa ikizungumzia kwamba kulikuwa na ghamra kubwa za uendeshaji, nikasema pamoja na hayo kulikuwa na migogoro baina yao wale *TANCOL* pamoja na mto huduma waliyekuwa wameweka ambaye mmoja wapo ni *CASPIAN*. Na nikasema kwamba katika huo mgogoro wao walipelekana mahakamani, lakini baada ya hapo wame-settle nje ya mahakama kiasi kwamba wamekubaliana kulipana zaidi ya USD 8,000,000 na wamekubalina kulipana kwa awamu haya ndiyo maelezo yangu. Sasa kama kwamba *CASPIAN* na mwenzake *TANCOL* walikuwa hawajaenda mahakamani na wakafikia hiyo basi anieleze katika hili.

Kwa hiyo, sikuzungumza kwamba *CASPIAN* ndiyo namtuhumu ila nilisema hizo ni baadhi ya changamoto walizokuwa nazo na *Hansard* yangu naamini itakuwa inasoma hivyo.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa ni wakati wa *guillotine*. Katibu tafadhalii.

Fungu 100 – Wizara ya Madini

Kif. 1001 - <i>Administration & Human Resources Management</i>	Sh. 3,874,845,008
Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i>	Sh. 741,252,140
Kif. 1003 – <i>Policy and Planning Div</i>	Sh. 898,036,469
Kif. 1004 – <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 393,312,594
Kif. 1005 – <i>Legal Services Unit</i>	Sh. 453,286,637
Kif. 1006 – <i>Government Communication Unit</i> ..	Sh. 445,332,854
Kif. 1007 – <i>Procurement Management Unit</i>	Sh. 343,424,390
Kif. 1009 – <i>Management Information Unit</i>	Sh. 574,648,000
Kif. 2001 – <i>Minerals Division</i>	Sh. 34,702,909,898

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 100 – Wizara ya Madini

Kif. 2001 - Minerals Division.....Sh. 7,039,810,200

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Bunge Lilitrudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae.

Mheshimiwa Waziri taarifa tafadhali

TAARIFA

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni za Kudumu za Bunge Toleo ya Januari 2016 Kanuni ya 104, kanuni ndogo ya tatu (a) na (b) kwamba Bunge lako likikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake naomba taarifa ya kamati ya matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja illiamuliwa na Kuafikiwa)*

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2019/2020 – Wizara ya Madini yaliiidhinishwa na Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Bunge, Bunge hili limepitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Madini kwa mwaka 2019/2020. Nichukue nafasi hii kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote kuwashukuruni sana Wizara ya Madini, na kuwapongeza vijana wetu hawa Waziri, Naibu

Waziri lakini pia Katibu Mkuu, Profesa Msanjila Makamishna huko, Mwenyekiti wa Tume Profesa Kikula, na taasisi zote ambazo ziko chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri sana ambayo mmeendelea kuifanya. (*Makofii*)

Tulikuwa tumekata tamaa sana kwenye eneo la madini kama nchi tuligeuka kuwa kila mtu analalamika lakini tunashukuru sana chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Rais mwenyewe Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na ninyi Mawaziri mmejjipanga vizuri kwa kweli sasa malalamiko yetu yanazidi kupungua kadri tunavyoenda. (*Makofii*)

Jana wakati tunakagua mabanda hapa nikawakuta hata Mwadui nao wapo na wanazungumzia kuonyesha jinsi gani nchi yetu itazidi kupata faida kubwa zaidi kutokana na uchimbaji wa almasi pale. Maana swali langu la kwanza niliwaliza bado mpo? Si milisemaga mgodi hauna faida? Lakini unaona kila mmoja amejjipanga katika namna ambayo kwa kweli sasa somo linaanza kueleweka la kwamba unapochukua rasilimali za nchi yetu basi utuachie na sisi kidogo kwa ajili ya maendeleo ya watu wetu. Kwa sababu ni ukweli usiopingika tunahitaji hizo fedha kwenye elimu, kwenye afya, kwenye miundombinu, na maeneo mengine mengi ya maendeleo ya nchi yetu.

Kwa hiyo tunawapa moyo sana tunatumaini uchangiaji wa leo na wa maandishi na wa kusema umesaidia Wizara katika kujipanga upya katika mwaka huu wa fedha unaokuja tunajua fedha tulizowapa hazitoshii lakini mkajitahidi kujipanga na hizo ili mwakani tunapokutana hapa tuwe na hadithi inayoonyesha mafanikio zaidi na zaidi na zaidi, tunawapongezeni sana tunawatakitia kila la heri.

Basi Waheshimiwa Wabunge kwa hatua hii sasa naomba nahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 12.00 jioni Bunge lilahirishwa hadi siku ya Jumanne,
Tarehe 28 Mei, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*